Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

### Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 21 Julai, 2009

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na**:-**

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. JUMA SAID OMAR (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA)**:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA**):

Randama za Makadirio ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 249

#### Hali ya Soko Kuu la Tabora Mjini

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Kwa kuwa soko kuu la Mjini Tabora ni la siku nyingi na limepitwa na wakati; kwa maana ya kwamba halina huduma nzuri za kuhifadhia bidhaa za wachuuzi, halina mpangilio mzuri kulingana na biashara zinazofanywa sokoji hapo;

hakuna huduma za vyoo kulingana na wingi wa wafanyabiashara na wanunuzi wanaohudumiwa hapo; na kwa kuwa gharama za matengenezo zinazohitajika sokoni hapo ni kubwa sana kuliko uwezo wa kifedha wa Manispaa ya Tabora pekee yake:-

Je, kwa nini mradi huo usiingizwe kwenye orodha ya miradi inayostahili kufadhiliwa na Serikali Kuu ili soko hilo liweze kufanyiwa matengenezo yanayostahili na kulingana na mahitaji ya huduma zinazohitajika?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko Kuu la Mjini Tabora, lilianzishwa mwaka 1964 likiwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya idadi ya watu kwa wakati huo. Kutokana na ongezeko kubwa la watu, kwa sasa imekuwa vigumu kukidhi mahitaji kulingana na wingi wa wafanyabiashara waliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko hilo ambalo linamilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, kwa hivi sasa lina huduma ya choo kimoja ambacho kina matundu manane. Huduma hiyo haikidhi idadi ya wafanyabiashara 1,767 katika soko hilo na wanunuzi 30,000, ambao wanakadiriwa kuingia kwa siku katika soko hilo kutafuta mahitaji. Hivyo, Manispaa imepanga kujenga choo kingine chenye matundu 30 katika mwaka wa fedha 2010/2011. Hii ni kwa sababu, mwaka huu wa fedha bajeti ilikwishapitishwa. Hata hivyo, kwa sababu ni jukumu la Halmashauri kujenga masoko yake na mapato katika soko hilo ni wastani wa shilingi milioni 15 kwa mwezi, naishauri Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, iangaliwe uwezekano wa kuboresha huduma ya soko hilo kwa kutumia mapato hayo. Serikali Kuu haina utaratibu wa kujenga masoko ya Halmashauri.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyingeza. Kabla sijauliza, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa Majibu yake ambayo kwa kiasi fulani hayakuniridhisha. Majibu haya yamekuwa ya jumla jumla sana, wakati mimi nilikuwa na maswali *very specific.* Hata hivyo, naomba niuliuze maswali ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri amekiri kwamba, hali ya soko ni mbaya na ametuambia Manispaa ina mapato ya shilingi milioni 15 kwa mwezi. Kwa hiyo, itumie mapato hayo kurekebisha hali ya soko. Kwa hali ilivyo ukitaka kutengeneza lile soko, shilingi 15 milioni kwa mwezi hazitoshi. Kwa hiyo, naomba kuiuliza Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu; je, itakuwa tayari Manispaa ya Tabora kupata mkopo kutoka Mashirika ya Hifadhi ya Jamii kuzingatia kwamba pato letu kwa mwezi ni milioni 15 basi tupate mkopo mkubwa utakaotuwezesha kulijenga upya lile soko kwa kutumia mapato hayo ya milioni 15 kwa mwezi?

Swali la pili; Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba hali ni mbaya, choo kilichopo kina matundu manane. Watu ndiyo hao kama alivyosema katika hali ya dharura. Je, Serikali haiwezi ikaisaidia kwa ruzuku Manispaa ya Tabora ikajenga vyoo vyenye matundu 30 kama suala la dharura kwa sababu kusubiri mpaka 2010/2011 hali inaweza kuwa mbaya sana?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kaboyonga tulikuwa tunakaa pamoja na mimi sina mpango wa kujibu kitu chochote ambacho ni kinyume na unachotaka wewe. Hali ya soko

kutokuridhisha; ni kweli wakikaa mle ndani mvua zikinyesha wananyeshewa na jua likiwaka wanawakiwa.

Kwa hiyo, mimi nakubaliana na yeye kabisa kwamba, kweli hali ya soko ni mbaya. Ninampongeza Mbunge kwamba, yeye anawashughulikia watu wake ili waweze kuwa na masoko mazuri. Kuwa na masoko mazuri, ndiyo mtindo wa kisasa wa kuishi, maana yake ni kwamba, biashara za watu zitakwenda.

Mheshimiwa Kaboyonga ni Mwanauchumi na tunapozungumza hapa, anajua mambo ya uhasibu na anafahamu kila kitu. Ninachosema hapa ni kwamba, ninyi milioni 15 mnazipata kila mwezi na mimi nikitaka kukuletea takwimu hapa na nimezungumza na watu wa Tabora zote nimezipata ziko hapa. Wamelianzisha soko lile mwaka 1964. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, *business* inatakiwa i-*break even*, kama unaendesha biashara yoyote lazima uoneshe faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, umesema nisiongee sana; ninachotaka kusema hapa, tutasaidiana naye. Kuna LAPF, Loan's Board katika TAMISEMI, vyote hivi ni vyombo ambavyo vinatoa mikopo. Yote hii bado utakwenda kwa akina Mkulo tena na bado twende kwa mwenye dhamana ya jambo hili, tukae mimi na wewe tuzungumze, tukiona kwamba mkopo huu unaweza ukapatikana kwa maana hiyo, unayoyazungumza hapo tutakuwa tumesaidiana. Sasa ruzuku ya dharura, Bajeti imepita hapa, Spika akatuuliza mnaunga mkono; wote tukaitikia tukasema ndiyo. Sasa nikikukubalia hapa nikasema tutatoa ruzuku ya dharura itatoka wapi maana tulishapitisha? *(Kicheko)*

Na. 250

**Shule za Kata katika Maeneo ya Wafugaji kuwa na Hosteli**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuza:-

Kwa kuwa Shule za Kata katika maeneo ya Wafugaji zinatakiwa ziwe na hosteli badala ya kuwa za kutwa kutokana na umbali uliopo kati ya vijiji na shule zenyewe:-

Je, Serikali itachukua hatua gani kwa vile baadhi ya shule ziko mijini na zinafikika kwa shida sana?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitoa kipaumbele katika kuwapa elimu bora watoto wote nchini. Baada ya elimu ya msingi, wahitimu wanaofaulu hujiunga na elimu ya sekondari. Kwa kuwa wahitimu wa elimu ya msingi ni wengi, shule za sekondari za kutwa kwenye kata zilianzishwa nchini, ikiwa ni pamoja na kwenye maeneo ya wafugaji.

Changamoto iliyopo ni kwamba, katika maeneo ya wafugaji, shule za kutwa huchukua wanafunzi wachache kwa sababu ya umbali kutoka nyumbani hadi shuleni. Katika Wilaya ya Longido, kuna shule tano za sekondari zilizojengwa na wananchi na shule nne zimesajiliwa mwaka huu wa 2009. Watoto wa jamii ya wafugaji, ambao kwa kawaida ni wahamiaji, hawawezi kusoma wakitoka nyumbani kutokana na umbali ambao katika vijiji vingine ni

zaidi ya kilometa ishirini na hakuna usafiri wa aina yoyote. Shule za Sekondari katika maeneo ya wafugaji, zinapaswa kuwa na hosteli ambazo hujengwa na wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Longido ni dhahiri kwamba, hosteli zilizopo ni chache kulingana na wingi wa wanafunzi. Ujenzi wa Hosteli katika shule mpya haujakamilika. Halmashauri ya Wilaya ya Longido, inaendelea kukamilisha ujenzi wa Hosteli katika shule hizo na ujenzi wa mabwalo ya chakula.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni mazuri, napenda kuiambia Serikali kwamba, hali ya Wafugaji wa Longido kwa wakati huu ni mbaya sana, kutokana na ukame na kuna shule ambazo wanahitaji mabweni kwa haraka sana. Je, Serikali inaweze kusaidia kwa dharura kujenga mabweni hayo kutokana na hali halisi ya wafugaji kwa wakati huu ili wanafunzi waweze kupata mahali pa kulala?

Kwa kuwa katika shule hizo bado hakuna mabwalo wala vitanda katika baadhi ya mabweni; je, Serikali itachukua hatua gani kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Longido kwa sababu hali ya wafugaji wakati huu ni mbaya sana?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba ni-*declare interest* kwamba, mimi na Mheshimiwa Michael Laizer tunatoka mahali pamoja. Asilimilia 50 ya wapiga kura wangu ni hao anaowazungumza Mheshimiwa Laizer na wa Mheshimiwa Edward Lowassa tumepakana nao wote. Ninataka mjue hilo kwanza. Kwa hiyo, kumwambia mwezengu kwamba, hii habari haiwezekani na nini, najua itanidhuru mimi. *(Kicheko)*

Ninachotaka kusema hapa ni kweli kabisa kwamba, jamii hizi za wafugaji mpaka Ngorongoro na kule Longido na Siha, zina matatizo makubwa yanayotokana na ukame kama anavyozungumza Mheshimiwa Laizer. Hili halina ubishi na ndiyo maana analeta rai maalum kwa Serikali. Ninataka niseme msimamo wa Serikali; maeneo haya ya pembezoni ambayo yanaonekana yana matatizo, tumekuwa na mkakati maalum wa kuwasaidia na kama mnakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anapitisha bajeti yake hapa, pamoja na Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Waziri Mkuu, tulizungumzia maeneo ya Ngorongoro na Mheshimiwa Telele anafahamu hii habari.

Mheshimiwa Laizer tumekutajia mambo ambayo tutakufanyia kule ya kujenga nyumba za Walimu na kila kitu. Niwaambie kwamba, ninazo takwimu zinazoonesha jinsi ambavyo tunasaidia, lakini bado inabaki kwamba wenzetu hawa wa maeneo ya wafugaji wana matatizo. Kwa hiyo, yote mawili kwa pamoja kwa sababu yanahusu hela, sasa ni jambo ambalo itabidi tukakae tena upya, tulete kama ombi maalum kwamba, jamani hali ni hii. Kama nilivyojibu, bajeti ilishapita, hii ni hali ya dharura kwa sababu kuna ukame na hatukujua kama utatokea. Hili ni jambo ambalo tunaweza kuzungumza tukaangalia kwa sura hiyo. Niseme kwamba, Serikali ilishaweka *provision* maalum kwa ajili ya matatizo haya.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa nia ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni kuleta maendeleo yenye uwiano kwa nchi nzima na kwa kuzingatia historia na Jiografia ambayo imewaweka wafugaji katika mazingira ya kutokupata elimu; na kwa kuwa Waziri anakiri kabisa kwamba umbali kati ya kijiji kwa mfano kule Simanjiro ilivyo ni km 70 kati ya kijiji na kijiji; je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya

kutenga fungu maalum la kusaidia jamii hizi za wafugaji kama inavyotenga katika maeneo yanayodaiwa ya pembezoni kwa nia ya kuleta maendeleo yenye uwiano? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru sana Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Kama alivyoeleza kwamba, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba, sehemu zote zilizoko pembezoni zinapewa fungu maalum kwa ajili ya matatizo yaliyopo huko. Kwa hiyo, sehemu hizo za wafugaji zimetengewa fungu maalum kwa ajili ya upembezoni wake. Wilaya ya Simanjiro iko katika mkakati huo, lakini mwaka huu tuliona tuanze na Wilaya 34, ambazo zina matatizo zaidi. Kwa hiyo, katika kuleta uwiano, Wilaya ya Simanjiro nayo mbele ya safari itakuwemo ndani ya mpango huu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Ingawa mlisamama wengi, lakini maana yake ndiyo hiyo kwamba, Serikali inajiandaa. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba.

Na. 251

**Mgongano wa Kamati ya Ulinzi na Usalama**
**Kagunga na Wamiliki wa Maboti**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kijiji cha Kagunga katika Wilaya ya Kigoma Vijijini kuna Kamati ya Ulinzi na Usalama inayoshughulikia maisha ya wananchi wao kwa usafiri wa maboti; na kwa kuwa Kamati hiyo iliamua maboti yasafiri saa 12 asubuhi kutoka Kagunga hadi Kigoma lakini wamiliki hao wanapingana na Kamati hiyo na hatimaye kupewa kibali na Mkuu wa Wilaya kusafiri saa 11.00 usiku:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kibali hicho kinapingana na uamuzi wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kagunga?

(b) Je, kama boti zingesafiri saa 12 asubuhi, Serikali haioni kwamba yule mtoto aliyetumbukia Ziwani wakati wa safari ya Kagunga Kigoma angeweza kukolewa?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kijiji cha Kagunga, kwa kutoa kibali cha maboti kusafiri saa 12 asubuhi ilikuwa ni utekelezaji wa maamuzi ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya Kigoma, ambayo Mwenyekiti wake ni Mkuu wa Wilaya. Utaratibu wa maboti ya abiria yaendayo nje ya nchi mwisho wa kuondoka Bandari ya Kigoma ni saa 8.00 mchana na hayajaruhusiwa kupita Kagunga mpakani mwa Tanzania na Burundi, zaidi ya saa 12.00 jioni. Maboti ya abiria yanayosafiri ndani ya nchi mwisho wa kuondoka Bandari ya Kigoma ni saa 10.00 jioni. Kwa maboti katika vituo vilivyoko kandokando mwa Ziwa Tanganyika kuja Kigoma au kuelekea maeneo mengine muda wa kuondoka ni saa 12.00 asubuhi na siyo 11.00 alfajiri. Aidha, Mkuu wa Wilaya, hakutoa amri nyingine tofauti na maamuzi ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a); vyombo vyote vya usafiri hufuata ratiba iliyopangwa na si vinginevyo. Kuhusu ajali anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge; ajali za vyombo vya usafiri katika Ziwa Tanganyika, zimekuwa zikitokea kwa nyakati tofauti. Kuhusu mtoto aliyetumbukia, taarifa tulizonazo zinaonesha ajali iliyotokea katika Kijiji cha Kagunga ni ya mtu mzima, aliyetambuliwa kwa jina la Sembeye Ndaumenye, ambaye alikuwa anafanya shughuli za uvuvi kwenye muda wa saa nne za usiku. Ajali hii ilitokea tarehe 26 Agosti, 2008, saa nne usiku. Mara ajali inapotokea, Serikali hufanya juhudi kadiri inavyowezekana.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, sikubaliani nayo. Kwa kuwa mimi mwenyewe nilipata taarifa kuwa maboti yanatoka saa 11.00 alfajiri kule Kagunga, nilifanya utafiti na nilisafiri kutoka Kibirizi saa nane mchana nikafika Kagunga nikalala, siku ya tatu nikaondoka. Niliondoka saa 11 alfajili siyo saa 12. Sasa Naibu Waziri anasemaje?

Swali la pili, kwa kuwa sasa hivi usafiri wa maboti yanayosafirisha abiria kwenda Kagunga nauli imepanda kutoka Kagunga mpaka Kibirizi na kurudi ni shilingi 4,000; na kwa kuwa siku za nyuma mafuta yalikuwa yameshuka bei hata kama sasa hivi yamepanda kidogo, ninaomba Serikali ipunguzie kiwango cha nauli kiwe shilingi 2,000 kwenda na kurudi shilingi 2,000; jumla ziwe shilingi 4,000. Je, Serikali inaweza kutoa ruzuku?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka niseme hapa ni bahati mbaya dada yangu anaona kwamba, sijajibu swali kiufasaha. Katika swali ambalo lilinitesa na leo sikulala ni hili linaloulizwa hapa. *(Kicheko)*

Kule Kigoma OCD na DC hawajalala, nimewaambia waondoke waende mpaka Kagunga wakaangalie Mbunge anataka kupata majibu hapa. Kwamba, kwa vile huwa tunaondoa maboti saa 11 alfajiri, mtoto ametumbukia kwenye maji akidai kwamba, kama isingekuwa muda huo labda mtoto yule angeweza akaokolewa. Ndicho anachosema Mheshimiwa hapa. Mimi siwezi kushindana na Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu Mbunge ni mamlaka. Nimezungumza na nimemwambia Mkuu wa Wilaya, nataka utupe taarifa kuhusu mtoto huyu, tumeangalia orodha yote ile hatukuona jina la mtoto pale, tumeona jina la mtu mzima ndiye aliyefariki dunia. Sasa nikisema hapa mtu amekufa, inaonekana kwamba Serikali haijali. Nataka kusema kwamba, Serikali hii inajali sana maisha ya watu. Kwa hiyo, anachosema mwenzetu hapa kama ni kweli, yeye mwenyewe amewahi kuingia akasafiri, yeye kama Mbunge alitakiwa akatae kwa kusema kwamba, mimi sitaingia kwenye boti hii.(*Kicheko*)

Ndiyo maana Mbunge huyu ameapa hapa kwamba, mimi nitailinda Katiba. Sasa utaratibu unasema tutaondoka sasa 12, boti inaondoka saa 11 kwa vile alikuwa anafanya uchunguzi akaingia mle ndani, *which means* watu wengine wanaona si na Mbunge naye yumo ndani. Nataka tusaidiane hapa, tumemwambia Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Watendaji wote walioko Kigoma; ni marufuku kuondoa maboti yale nje ya muda ambao nimeutaja hapa. Ni marufuku kufanya hivyo na Mheshimiwa Nkayamba, Mheshimiwa Msambya na Mheshimiwa Zitto Kabwe, mkigundua kwamba utaratibu huo unakwenda, nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu nipande ndege niende mwenyewe mpaka Kigoma kulisimamia jambo hili. *(Kicheko)*

Namwomba Mheshimiwa Mbunge, tusaidiane hilo na nafikiri Viongozi walioko kule wamenisikia. Kuhusu suala la nauli, nalo nitapata shida kwa sababu nikisema sasa ondoa, ina maana Serikali ipeleke ruzuku pale. Jambo hili linazungumzika, mambo haya yanatakiwa yaanzie katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma wazungumze na wakifika mahali kwa kushirikiana na wahusika wakiona kuna haja ya kushusha, mjue kuna taratibu tumejiwekea hapa. Kuna watu wanaosimamia mambo ya nauli na mafuta kupanda na kushuka, taratibu za nchi zinafahamika. Kwa hiyo, nashauri tushirikiane na dada yangu Mheshimiwa Nkayamba, maswali unayouliza ni magumu sana. Tutashirikiana wote tuone kama hiyo nauli inaweza kupungua. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe usiende kupanda boti. Mheshimiwa Nkayamba ulikuwa unafanya utafiti? *(Kicheko)*

Swali linalofuata linaelekezwa Wizara ya Fedha, afadhali Mheshimiwa Naibu Waziri apumzike.

Na. 252

**Mashirika Yaliyodhaminiwa Kupata Mikopo ya BOT**

**MHE. MAULIDAH A. KOMU** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilidhamini mashirika ya watu binafsi kupata mikopo toka BOT: Je, ni mashirika gani yalidhaminiwa na dhamana yake ni kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maulidah Komu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Udhamini wa Mikopo ilianzishwa na Serikali, kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa vyama vya ushirika, makampuni na taasisi za kibiashara na kiuchumi, kwenye sekta mbalimbali za uchumi kwa kutoa udhamini kwa mabenki ya biashara yanayokopesha na taasisi za fedha zinazokopesha. Serikali imeikabidhi Benki Kuu ya Tanzania, jukumu la kusimamia Mifuko hii ya Dhamana kama wakala wake. Kwa hiyo, Benki Kuu haitoi mikopo bali hudhamini vyombo vya fedha, ambavyo vinakuwa vimekubali kukopesha katika misingi ya kawaida ya ubora wa miradi na taratibu nyingine za mikopo. Hadi sasa Serikali imeanzisha mifuko miwili ya udhamini: Mfuko wa Mauzo ya Nje ya Nchi *(Export Credit Guarantee scheme);* na Mfuko wa Miradi Midogo na ya Kati *(SME Credit Guarantee Scheme).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2003/2004 – 2008/2009, Mfuko wa Mauzo ya Nje ya Nchi, ulitoa dhamana kwa vyama vya ushirika, mashirika na makampuni. Thamani ya jumla ya dhamana zilizotolewa ni shilingi 290,687,000,000. Mikopo 45 kwenye Sekta za Kilimo, Viwanda na Ushirika ilihusika na dhamana zilizoidhinishwa na Benki Kuu. Mfuko wa Miradi Midogo na ya Kati, umetoa dhamana wenye Sekta za Elimu, Hoteli, Viwanda, Kilimo, Ujenzi, Afya na Biashara. Thamani ya dhamana hizo ni jumla ya shilingi 3,054,000,000 zilizotolewa kwa ajili ya mikopo 48.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa orodha ya waliopewa mikopo na kudhaminiwa na Mifuko hii ni ndefu na ndiyo sababu ya kutoisoma, naomba Mheshimiwa Komu na Mheshimiwa yeyote mwingine, atakayehitaji orodha hiyo atuambie ili tumpe.

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini sikuridhika kwa sababu nilikuwa nataka nipate orodha, hata kama ni ndefu namna gani mimi naitaka. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ndio hudhamini mikopo hiyo; na kwa kuwa mikopo hiyo inaposhindikana kulipwa wananchi hubeba mzigo huo kwa kulipa kutoka kwenye kodi zao:-

(a) Je, mashirika husika hupewa masharti gani ili wapatiwe mikopo kwa lengo la kuhakikisha hawashindwi kulipa mikopo hiyo?

(b) Je, hadi sasa ni Mashirika gani yameshindwa kulipa na yamechukuliwa hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu orodha. Orodha ya mikopo ambayo imepewa dhamana iko 93 na kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi kuwa, orodha ya waliopewa mikopo na kudhaminiwa na Mifuko hii ni ndefu na ndiyo sababu ya kutoisoma. Naomba Mheshimiwa Komu na Mheshimiwa Mbunge yeyote mwingine, anayehitaji orodha hiyo atuambie ili tumkabidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti ya dhamana zinazotolewa na Serikali kupitia Benki Kuu, yanategemeana sana na jinsi ambavyo Benki za Biashara ama Taasisi ya Fedha, itakavyokuwa imetathmini maombi ya mkopo ambao unaombewa dhamana. Kwa hiyo, masharti yanayotazamwa na Benki Kuu ni kuweza kijiridhisha kwamba, yale masharti ya chombo kile kitakachotoa mkopo yako kwenye misingi ya mikopo yenyewe, imefanya taratibu na kwamba, mkopo wenyewe unaoombewa dhamana, uwezekano mkubwa wa kutokufa au kwa kutoweza kurudisha ule mkopo unazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni Mashirika yaliyoshindwa kulipa yamechukuliwa hatua gani? Kwanza, niseme kwamba, kwa kawaida Benki Kuu chini ya dhamana hizi, inatoa dhamana kwa asilimia 50% tu ya jumla ya mkopo wenyewe. Kwa hiyo, baada ya kutathmini kwa ukaribu, kwa undani na kwa makini, si mikopo mingi ambayo imedhaminiwa na Benki Kuu, ambayo inashindwa kulipwa. Hata hivyo, pale ambapo mikopo hii inashindikana kulipwa ni dhahiri kwamba, ile dhamana nyingine ambayo mkopwaji atakuwa ametoa kwanza, inachukuliwa ndiyo adhabu yenyewe. Pili, kwa sababu hii ni dhamana ya Benki Kuu na ni ya Serikali, basi Serikali inalipa ule mkopo.

Na 255

**Kukamilika kwa Masoko ya Wakulima Igagula na Ilembula**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA (K.n.y. MHE. YONO S. KEVELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa masoko makubwa ya Kimataifa yako Igagula na pale Ilembula kama masoko ya wakulima:-

(a) Je, ni lini masoko haya yatakamilika?

(b) Je, Soko la Ilembula la Kimataifa limefadhiliwa na nani na kwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), naomba kufanya masahihisho kidogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Wakulima linaitwa Igagala sio Igagula, lipo katika Kijiji cha Igagala, Kata ya Imalinyi. Soko la wakulima la Igula sio Ilembula liko katika Kijiji cha Igula, Kata ya Ilembula, ambayo yote yapo katika Jimbo la Njombe Magharibi. Aidha, masoko hayo siyo ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya masahihisho hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Igagala lilishakamilika na kufunguliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 03 Agosti, 2008. Ujenzi wa Soko la Igula ulishakamilika na mkandarasi alishakabidhi soko hilo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, tarehe 30 Juni, 2009, tukiwa hapa hapa Bungeni.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Igula limejengwa kupitia Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (AMSDP) na limegharimu shilingi 434,200,000. Mchango wa Halmashauri ni asilimia tano, sawa na shilingi 21,710,000 na kiasi kilichobaki kilitolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB).

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Nadhani Mheshimiwa Kevela alitumia neno kimataifa kwa sababu ya *confusion* ya lile soko linalotarajiwa kujengwa Makambako, Njombe.

Je, ili kuondoa *confusion* ni lini Soko la Makambako litajengwa? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Makwetta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Kuendeleza Masoko ilianza tarehe 1 Januari, 2003 na inaisha tarehe 31 Desemba, 2009. Tulitegemea kujenga masoko 20, lakini yamejengwa masoko 24 kwa maana ya Wilaya 24 Tanzania na gharama yake ilikuwa shilingi bilioni 49. Fedha hizo tayari zimeshatolewa na kwa sasa hivi hakuna mpango wa kujenga tena kupitia Programu hiyo. Soko hilo linaweza likajengwa kupitia programu nyingine, kwa

sababu hata Serikali ya Ufaransa inatoa ufadhili huo wa masoko, kwa mfano, Soko la Kibaigwa na masoko mengine ya Morogoro.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu dogo la nyongeza. Ninaomba kujua ni vigezo gani vinatumika hadi soko kuitwa la kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aloyce Kimaro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vya kulifanya soko liwe la kimataifa; kwanza, eneo hilo liwe limezungukwa na maeneo ya uzalishaj. Pili, eneo hilo liwe na wakazi wanaozidi 15,000, kwa maana ya kwamba, watakuwa wananunua na kuuza mazao yao hapo. Eneo hilo liwe na miundombinu mingine kama vile barabara na mawasiliano. Vilevile Halmashauri iwe tayari kutoa asilimia tano ya mchango wa ujenzi wa soko hilo.

Na. 254

**Kupeleka Umeme Kijiji cha Kharumwa na Vijiji Jirani**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa ahadi ya Serikali ya kupeleka umeme Kijiji cha Kharumwa pamoja na Vijiji vya jirani ni ya muda mrefu; na kwa kuwa Wananchi na Mbunge wamekuwa wakifuatilia suala hili kwa zaidi ya miaka kumi sasa; na kwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini alipofanya mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Kharumwa mwezi Oktoba, 2008 aliahidi kuwa Mradi huo sasa utatekelezwa chini ya Miradi inayofadhiliwa na Mpango wa MCC na kwamba kufikia Desemba, 2008 utekelezaji wa mradi huo utakuwa umeanza:-

Je, hadi sasa utekelezaji wa Mradi ukoje?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang’hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa muda mrefu sasa imekuwa ikipanga kutekeleza ahadi ya kupeleka umeme kwenye Kijiji cha Kharumwa na vijiji vingine jirani vya Wilaya ya Geita. Ahadi hiyo imekosa utekelezaji kwa sababu mbalimbali zilizo nje ya uwezo kwa nyakati hizo. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa wakati wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara yangu, tarehe 8 Julai, 2008, Serikali itakamilisha utekelezaji wa Mradi wa Umeme katika vijiji hivi kwa kipindi hiki baada ya vijiji hivi kuingizwa katika vijiji vitakavyopatiwa umeme chini ya ufadhili wa MCC.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na mimi mwenyewe Naibu Waziri, kwa nyakati mbalimbali, tumekwenda kwenye maeneo ya Wilaya ya Geita na Majimbo yake yote ili kuwafahamisha wananchi, nia ya Serikali ya kupeleka umeme kama sehemu muhimu ya kuboresha shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wakati nikizungumza na Wananchi wa Nyang'hwale katika mkutano wa hadhara tarehe 15 Oktoba, 2008, Kijiji cha Kharumwa na vijiji vya jirani, vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa Umeme wa Nyang'hwale ulio chini ya Ufadhili wa MCC. Ni kweli kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, wakati wa mkutano huo wa hadhara, tuliwaahidi wananchi kwamba, Mradi huo utaanza kutekelezwa ifikapo Desemba, 2008. Kazi za Mshauri Mwelekezi zilianza Novemba, 2008 na kazi nyingine husika za TANESCO nazo pia zilianza kufanyiwa kazi kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za upimaji wa njia za umeme zimeshafanyika, kazi ya uthamini wa mali na mazao ya wananchi ambao itawalazimu kupisha miundombinu ya umeme kupita, itaanza kufanyika mwanzoni mwa mwezi Agosti, 2009. Utafiti wa mazingira na utayarishaji wa zabuni za ujenzi ulikamilika mwezi Mei, 2009, ujenzi wa miundombinu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2009 na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa njia ya umeme kwenda Kharumwa utahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 33, yenye urefu wa kilomita 16 kutoka kwenye kituo cha kupoza umeme kilichopo Bulyankulu. Jumla ya transfoma mbili zenye ukubwa wa kVa 200, zinatarajiwa kuwekwa na jumla ya wateja 250 wanatarajiwa kunufaika na Mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Nyang'hwale kuwa, kama tulivyoahidi wakati wa ziara, Serikali inafuatilia na itaendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mradi huo na tutampatia Mheshimiwa Mbunge, taarifa za mara kwa mara za maendeleo ya hatua za utekelezaji zinazofikiwa.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri, yenye matumaini yakitekelezwa kama yanavyotamkwa, napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wakati wa ku-*survey* njia wataalamu walipita kwenye Vijiji vya Ikangara, Kitongo, Nyarubere, Nyijundu, Nyaruguguna hadi Nyang'hwale; je, baada ya kuwa nguzo zimesimikwa, TANESCO wataunganishia wananchi wa vijiji hivyo umeme badala ya kupitisha nyaya juu tu na kwamba fidia ya mali italipwa kabla ya mradi kuanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri mwenyewe ajibu; Kwa kuwa *line* hii inaishia pale Nyang'hwale lakini kuna kituo cha afya na Shule ya Sekondari ya Nyang'hwale, ambayo iko kama kilomita nne kutoka Nyang'hwale itakuwa imeachwa na kijiji kikubwa sana cha Busolwa ambako kuna mgodi mdogo na Kijiji cha Ngoma ambacho kiko kwenye Jimbo la Waziri wa Nishati na Madini na kwamba alishaahidi kupeleka umeme pale na kuna mgodi mdogo:-

Je, Waziri mwenyewe anaweza kuwahakikishia wananchi hawa wapiga kura kwamba Mpango wa REA uunganishe sasa sehemu ambazo zilikuwa zimeachwa katika Mpango wa MCC kuanzia Nyang'hwale, Busolwa hadi Ngoma ambako hata yeye anategemea kura nyingi sana? Waziri anaweza kuhakikisha kwamba, atafanya hivyo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, kufuatia swali la msingi lililojibiwa vizuri sana na Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bahati mbaya kwamba, mimi naongea ikiwa ni sehemu ya watu wenye maslahi katika swali la nyongeza linaloulizwa. Kwa kuwa maslahi hayo ni sehemu ya maslahi ya Watanzania, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mipango ya REA inaendelea kufanyiwa kazi, kuhusu mradi wa maeneo aliyosema ya Busolwa kuunganisha na Kijiji cha Ngoma, ambacho kiko Jimbo la Sengerema. Haiishii hapo tu ni pamoja na miradi ya majimbo mengine mbalimbali, ambayo tumeshaanza kuwasiliana na wahusika.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Moja ya ahadi za Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2005 ni kwamba, katika kipindi chake cha utawala, atahakikisha Makao Makuu yote ya Wilaya yanapata umeme. Sasa nilitaka Mheshimiwa Naibu Waziri anisaidie; mpaka sasa hivi ahadi hiyo imetekelezeka kwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais anatoa ahadi ya utekelezaji huo wa kuepeleka umeme katika Makao Makuu yote ya Wilaya Tanzania nzima, ilikuwa ni sehemu ya utekelezaji ambao unakusudiwa wa Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika kipindi cha miaka mitatu hii, Serikali imepeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya kama ilivyopanga, isipokuwa nadhani bado hatujafikia Wilaya kama mbili hivi, ambazo nitampatia Mheshimiwa Mbunge maelezo ya kina ni Wilaya zipi hizo tutakapoonana. Naomba anitafute baadaye, nitampa maelezo hayo. *(Kicheko)*

Na. 255

**Umeme wa Nguvu za Jua na Upepo - Mbozi Magharibi**

**MHE. DKT. LUKA J. SIYAME** aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vyote 75 vya Jimbo la Mbozi Magharibi, Mji Mdogo wa Tunduma na Kijiji cha Mpemba, havina umeme; na kwa kuwa zaidi ya nusu ya eneo la Jimbo hili liko kwenye Bonde la Ufa lenye jua kali na upepo mkali:-

Je, ni lini Serikali itafanya utafiti wa kuwezesha eneo hili kupatiwa umeme wa nguvu ya jua *(Solar Electricity)* na umeme wa nguvu ya upepo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Luka Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kutathmini kasi ya upepo katika maeneo mbalimbali nchini ili kupata taarifa za kutosha kuandaa ramani ya upepo *(Wind Atlas)*, ambayo itasaidia kuelekeza maeneo ambayo yana kasi ya upepo unaofaa kwa ajili ya kuzalisha umeme. Hivyo, ili kuwa na uhakika kuwa maeneo ya Mbozi Magharibi yaliyo

katika Bonde la Ufa *(Rift Valley)*, yana kasi ya upepo inayoweza kuzalisha umeme, tathmini ya kina inapaswa kufanyika si chini ya mwaka mmoja ili kubaini mwenendo wa upepo na kasi muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Luka Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tulieleza hapa Bungeni wakati wa kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mbunge wa Hai, tarehe 15 Julai, 2009 kuwa, Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark na wahisasni wengine wakiwemo AfDB, imefanya utafiti wa kasi ya upepo maeneo mbalimbali ya nchi yetu, yakiwemo maeneo ya Kititimo Singida na Makambako Iringa. Vituo vya Makambako na Kititimo, vilionesha kuwa na upepo wenye kasi ya wastani wa mita nane kwa sekunde, ambao unafaa zaidi katika kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasimamia utekelezaji wa mradi wa miaka mitano wa ukuzaji wa maendeleo ya soko la umeme wa jua hapa nchini, unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA), ambao unatarajiwa kumalizika mwaka 2010. Lengo la mradi huo ni kujenga soko la umeme wa jua nchini, kwa kutoa mafunzo kwa Mafundi Sanifu na kusogeza upatikanaji wa teknolojia hiyo ya umeme wa jua karibu zaidi na wananchi. Mradi huo ulizinduliwa Mkoani Mbeya mwezi Juni, 2008 na umefika Wilayani Mbozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inafanya kila linalowezekana ili kukabiliana na matatizo ya umeme Mkoani Mbeya kwa sehemu zote za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji. Hata hivyo, ni vyema Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba, maamuzi ya Serikali yanategemea uwezo wa kifedha na ushauri wa kitalaamu kuhusu ufanisi wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii, kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na vyanzo vya nishati mbadala vya jua na upepo ambavyo ufanisi wake kwa Mkoa wa Mbeya haujathibitika, Serikali inaendelea na tafiti za vyanzo vya nishati Mkoani Mbeya, unaotokana na jotoardhi maeneo ya Songwe *(Geothermal Activity)* na ubora wa makaa ya mawe yanayopatikana Galula, kwa ajili ya kuzalishia umeme. Aidha, Serikali itazingatia umuhimu wa umeme huu kupatikana kwa gharama nafuu ili kukidhi malengo ya usambazaji wa nishati kwa Wananchi wa Mbozi na wa Mkoa wa Mbeya kwa ujumla.

**MHE. DKT. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa nina uhakika hadi sasa si Serikali yetu, Serikali ya Denmark wala *African Development Bank* ambao wamefika kufanya utafiti wa kasi ya upepo katika Jimbo la Mbozi Magharibi, napenda nikuhakikishie kwamba, kasi ya upepo katika Jimbo hilo ni kubwa mara mbili au hata mara tatu ya ile iliyopo Kititimo ama Makambako:-

(a) Je, Serikali inaweza kuwashauri hawa watafiti wa Denmark na AfDB kufika Mbozi Magharibi na kufanya utafiti huo wa kasi ya umeme kwani ile ya Kititimo na Makambako ni cha mtoto tu?

(b) Kama nilivyosema hapo awali kutokana na kwamba, Jimbo hilo halifikiki kwa urahisi, nguvu ya jua na hata jotoardhi lililopo pale Mbozi Magharibi, naweza kusema ni

mama wa jua ama ni mama wa joto. Je, serikali haioni umuhimu wa kwenda kufanya utafiti pale na pengine hata kuanzisha Gridi ya Taifa ya *solar energy* kutoka Mbozi Magharibi badala ya kutumia gharama kubwa kufanya utafiti wa *source* ya umeme sehemu nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Luka Siyame, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Dkt. Siyame kwamba, masuala ya upepo pamoja na kwamba unaweza ukakaa upepo ukawa unapiga mpaka nywele zinaruka, lakini kwa Tanzania hapa utafiti uliokuwa umefanywa kwa zaidi ya miaka kumi umebaini kwamba, upepo unaotakiwa ili kuzalisha umeme siyo upepo tu ambao unapuliza hapana; upepo wake ni maalum, unatakiwa uwe na *patern* na uwe na mfumo maalum, unaokwenda kwa zaidi ya mita nane kwa sekunde. Ukienda kwa mita tano kwa sekunde, unafaa pia kuzalishia umeme lakini ule wa mita nane kwa sekunde ndiyo unaofaa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upepo huo unatakiwa uwe unapiga kwa urefu zaidi. Sasa inawezekana kwamba, upepo ni mkali sana, lakini *patern y*ake kama tulivyosema juzi, inawezekana ule upepo hauna nidhamu, unapiga kushoto unapiga kulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ameniomba niwaombe wataalamu waende wakatazame, mimi sipingani na wazo hilo. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, REA wako kwenye kazi hiyo katika Wilaya ya Mafia, Wilaya ya Kilwa, maeneo ya Singida na kwingine. Nitamwomba Waziri wa Nishati na Madini, naye ananisikia, awaelekeze REA wafike Mbozi Magharibi ili waangalie kama upepo wake unaweza ukalingana na upepo wa Kititimo au Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili lingine la *source* ya nguvu ya jua, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, kusema kweli nguvu ya jua kama ilivyo kwa Tanzania nzima, kwa sasa utafiti umebaini kwamba, kwa Mbeya ukiondoa makaa ya mawe ambayo yako mengi, mfumo wa nishati ambao unaweza ukatusaidia ni kuendelea na utafiti wa jotoardhi, ambao kwa sasa hivi tunakadiria tunaweza kupata hata *Megawatt* 100 kama tutaendelea na utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi Shirika la Wajerumani linaendelea na utafiti, wamemaliza utafiti mwezi wa Januari, 2009. Tumeonana nao, wanaongea na GST ili kuweza kuendelea na utafiti huo, kubaini ngazi ya juu zaidi itakayoweza kukaribisha wawekezaji kuja kuwekeza kwenye jotoardhi.

**NAIBU SPIKA:** Siku ya kupeleka watafiti, Waheshimiwa Wabunge wa Mbozi muweko huko.

Na. 256

**Mpango wa Kuzalisha Twiga Katika Mapori ya
Wilaya ya Rufiji, Kilwa na Liwale**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI aliuliza:-**

Kwa kuwa mapori ya Wilaya za Rufiji, Kilwa na Liwale hayana wanyama aina ya Twiga kwa sababu Twiga waliopo upande mwingine wa Mto Rufiji hushindwa kuvuka Mto na kuingia kwenye mapori hayo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamisha baadhi ya Twiga kutoka upande ulio na Twiga na kuwapeleka kwenye mapori ya Wilaya ya Rufiji, Kilwa na Liwale ili wazaliane humo na kuongezeka?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mnyama Twiga hapatikani maeneo ya Rufiji, Kilwa na Liwale, kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo mifumo ya kiikolojia, hali ya malisho, mifumo ya ardhi, kina cha maji ya mto, ushirikiano wa Twiga na *species* nyingine za wanyamapori, hali ya ujangili na shughuli nyingine za binadamu. Kihistoria, tangu enzi za miaka ya 1800, wakati wa Mwindaji Bingwa Mwingereza, *Captain Selous*, haujawahi kufanyika utafiti wowote wa kisayansi wa kuelezea msingi wa mtawanyiko wa Twiga hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika miaka ya 1976 hadi 1987, watu wa aina mbalimbali ambao waliwahi kupitia au kukaa katika Pori la *Selous* ambao walikuwa ni marubani, waliwahi kuruka usawa wa chini sana *(low flying flight)* na kuruka kutokea eneo la Kaskazini mwa Mto kuelekea Kusini, kwa lengo la kuwahamisha Twiga upande mwingine wa Mto. Japokuwa kazi hii waliifanya mara kwa mara kwa vipindi tofauti, lakini Twiga hao waliendelea kughairi kuvuka mara walipofika upande wa ufuko wa Mto huo na kuamua kurudi upande wa Kaskazini walikotoka. Wahusika hao ni pamoja na Msimamizi wa Shirika la *Frankfurt Zoological Society (FZS),* Dkt. Bonner Fambae, ambaye kipindi hicho alikuwa anasimamia ufadhili wa utafiti wa Mbwa Mwitu katika Pori hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, aliyekuwa Mkuu wa Pori la Akiba Selous kipindi cha mwaka 1987 hadi 1991, kwa kutumia ndege aliwahi kuruka sana eneo hilo kwa nia ya kuwatawanya Twiga kuhamia eneo la Kusini mwa Mto Rufiji, lakini bila mafanikio kwa kuwa Twiga hao waliendelea kukaidi na kukaa Kaskazini mwa Mto huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uwepo wa Twiga kwenye eneo la Kaskazini la Mto Rufiji, limekuwa linazua hoja mbalimbali kwa wananchi, wataalam na viongozi wa wananchi; Wizara yangu imetoa maelekezo kwa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori *(TAWIRI),* kujumuisha utafiti wa mtawanyiko wa Twiga katika Pori la Selous katika mipango ya tafiti zao. Tafiti hizi pamoja na nyingine zitakazofanywa na watafiti wengine, zitasaidia kupata majibu ya kisayansi kwa nini Twiga hawako Selous Kusini mwa Mto Rufiji na hapo ndipo maamuzi ya kupeleka Twiga eneo la Kusini yatafanyika.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa idadi ya Tembo (Ndovu) imeongezeka sana katika Mapori ya Selous na kusababisha madhara makubwa kwenye mashamba ya wanakijiji pamoja na usalama wao; je, Serikali haiwezi kuwavuna Tembo hao ili ongezeko la Tembo lipungue kidogo na kuwanusuru wanakijiji?

(b) Kwa kuwa Twiga hawa wamekuwa wakaidi kuvuka Mto; Je, Serikali haiwezi kutumia magari makubwa kuwabeba na kuwapeleka upande wa pili wa Mto? *(Makofi/Kcheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, naomba ujibu swali la pili, kwa sababu swali la msingi halikuzungumzia Tembo, kwa hiyo jibu la Twiga, maana swali lake lilihusu Twiga.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama tulivyosema kwamba, Twiga wamekuwa wakikaidi au kutokufurahia kukaa upande wa Kusini mwa Mto Rufiji. Kwa sababu viumbe hawa wanaishi na kuna mazingira fulani ambayo wanayapendelea, sisi tukafikiri pengine kutumia nguvu zaidi ya zile zilizotumika, si kwamba wamekuwa hawavuki, hizi *low flying flights* ambazo nimezizungumzia ni kwamba, wamekuwa wakivushwa, lakini wamekuwa wakirudi upande mwingine.

Kwa hiyo, hakika hata tukiwavusha kwa malori watarudi. Ndiyo maana tukasema ni vizuri tufanye utafiti wa kisayansi na tayari tumeshawaelekeza TAWIRI wafanye utafiti huo, kujua ni sababu gani za msingi zinazofanya wasipende kuvuka. Baada ya kupata majibu ya utafiti huo, ndiyo yatakayoturahisishia kujua njia gani itumike ya kuweza kuwafanya waishi na yawezekana isiwe kutumia malori tu, tunaweza kutumia vivutio fulani, kwa mfano, tunaweza tukaweka chakula ambacho wanakipenda na wakavuka wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kwamba, tufanye utafiti, tupate majibu yake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Swali la Tembo halikuwepo kwenye swali la msingi.

Na. 257

**Mwongozo wa Kuvuna, Kusafirisha na Biashara ya Mazao ya Misitu**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii imeandaa Mwongozo wa Kuvuna, Kusafirisha na Kufanya Biashara ya Mazao ya Misitu kutokana na Sera ya Taifa ya Misitu; na kwa kuwa mwongozo huo unaainisha wazi kuwa ili uvunaji uwe endelevu ni sharti kuwe na mpango wa usimamizi misitu ambao utabainisha idadi ya miti iliyoruhusiwa kuvunwa katika kila eneo na idadi ya miti itakayopandwa:-

(a) Je, ni Wilaya ngapi hapa nchini mpaka sasa zimeanza kutumia Mwongozo huu?

(c) Je, ufanisi wake ukoje?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu unaotumika nchini kote ni ule ambao umeainishwa katika Mwongozo wa Uvunaji Endelevu na Biashara ya Mazao ya Misitu wa Mwaka 2007. Mpaka sasa Wilaya ambazo zina mipango ya usimamizi wa misitu ni 21, ambazo ni Uyui, Sikonge, Bagamoyo, Urambo, Kigoma, Songea, Morogoro, Ulanga, Geita, Biharamulo, Mkuranga, Kilwa, Nachingwea, Liwale, Tunduru, Rufiji, Kisarawe, Kilombero, Mvomero, Handeni na Mpanda. Wilaya hizo ziliandaa mipango ya usimamizi wa misitu na sasa inatumika baada ya kuidhinishwa na Wizara yangu. Aidha, mashamba ya miti ya Taifa yote 16 yanatekeleza maagizo yaliyomo kwenye Mwongozo wa Uvunaji Endelevu na Biashara ya Mazao ya Misitu. Wilaya zilizobakia ambazo zina rasilimali ya misitu, zimeagizwa kuacha uvunaji hadi hapo utayarishaji wa mipango yao ya usimamizi wa misitu itakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, hivi karibuni Wilara yangu itafanya tathmini ya misitu yote nchini, kwa ufadhili wa Serikali ya Finland na usimamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula *(FAO)*. Mradi huu wa kuhesabu miti kitaalam, utatekelezwa katika muda wa miaka mitatu kuanzia mwaka huu wa fedha wa 2008/2009. Tathmini hiyo itawezesha upatikanaji wa takwimu ambazo zitatumiwa kutengeneza mipango ya usimamizi ya misitu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ufanisi na mafanikio yaliyofikiwa tangu utekelezaji wa Mwongozo wa Uvunaji Endelevu na Biashara ya Mazao ya Misitu uanze kutumika ni kama ifuatavyo:-

(i) Uvunaji holela uliokuwepo awali umepungua katika Wilaya husika

(ii) Malalamiko yaliyokuwa yakiletwa Wilazarani juu ya tuhuma za ugawaji wa upendeleo wa mazao ya misitu kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu yamepungua. Hii ni kwa kuwa hivi sasa utoaji wa vibali unafanyika katika Wilaya kwa uwazi na kwa njia shirikishi ambazo zinawahusisha hata Wenyeviti wa Vijiji ambavyo misitu inavunwa.

(iii) Mapato ya Serikali yatokanayo na ushuru wa mazao ya misitu katika Wilaya yameongezeka kutoka shilingi 15,141,346,375 mwaka 2006/07 hadi shilingi 21,832,150,506 mwaka 2007/08. Hii ni kwa kuwa Wilaya zinakuwa na taarifa ya kiasi kinachotarajiwa kuvunwa kila mwaka.

(iv) Wilaya zilizoanza kutumia mwongozo wa uvunaji endelevu na biashara ya mazao ya misitu zimekuwa na orodha kamili ya wafanyabiashara wa aina tofauti ya mazao ya misitu. Hii imesaidia katika ufuatiliaji wa uvunaji wa mazao ya misitu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa sasa ni takriban miaka mitatu tangu Mwongozo huu umeanza kutumika na mpaka sasa Tanzania yenye zaidi ya Wilaya 120 ni Wilaya 21 tu zimeanza kutumia Mpango huu endelevu; na kwa kuwa kasi ya uvunaji ni kubwa wakati kasi ya upandaji miti ni ndogo:-

(i) Kwa kuwa Serikali inategemea Halmashauri zetu kwa ajili kutunza misitu; na kwa kuwa imekuwa haitoi fedha yoyote kwa ajili ya Idara za Misitu kwenye Wilaya zetu; je, haioni kwamba kwa mwendo huu misitu yote itateketea pamoja na rasilimali zilizokuwepo?

(ii) Kwa kutambua umuhimu wa misitu kwamba hata Kilimo Kwanza hakitafanikiwa kama misitu yetu haitatunzwa vizuri; je, Serikali ipo tayari sasa kutenga fedha kwa ajili ya Idara ya Misitu kwenye Halmashauri zote?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza si kweli kwamba, Wilaya zote zina rasilimali ya misitu; kuna Wilaya kama Ilala ama Kinondoni, sidhani kama zina rasilimali misitu. Kwa hiyo si Wilaya zote 120 zina rasilimali misitu na tumeshasema kwamba, zina rasilimali misitu ambazo hazina mpango wa usimamizi *(Management Plan),* tumezuia zisivune. Kwa hiyo, mazao yanayotoka kwenye Wiilaya hizo, yanatoka kinyume cha taratibu na tumekuwa tukiyakamata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi jitihada zinaongezwa za kuelimisha wananchi hasa katika Wilaya ili waweze kusimamia na kutekeleza Mpango huu kama Wilaya nyingine zilivyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha kupelekwa kwenye Wilaya, kuna mipango kadhaa inayofanyika ya kusaidia usimamizi wa misitu katika Wilaya, kuna Mradi wa *Participatory Forestry Management (PFM),* ambapo kuna Wilaya zinashiriki, lakini pia kwenye Wilaya ambazo zinavuna. Tumesema kwenye mwongozo, asilimia tano ya mapato yanayotokana na uvunaji yabaki Wilani kwa ajili ya kusimamia uvunaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwamba, kwa mikakati hii tuliyonayo, asilimia tano ni kiasi kikubwa sana zikitumika vizuri zinaweza zikasaidia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Mbunge mmoja ameniandikia hapa anasema; je, kuna uhusiano gani wa kitaalam kati ya baadhi ya Watumishi wanaokataa kwenda Kusini na Twiga wanaokaidi kwenda Kusini? *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, leo tuna wageni wengi na wengine wamekosa nafasi humu ndani, kuna ushauri mwingi wametoa Waheshimiwa Wabunge lakini ukweli unabaki kwamba kuhudhuria Bunge ni hiari ya wananchi, hatuwapangi ni nani waondoke na nani waingie na nani waende wapi. Kwa hiyo, wanaopata nafasi wanapata na wanaokosa wanakwenda *basement,* pengine baadaye mchana wanaweza wakaingia. Kwa hiyo, Ukumbi wa Bunge uko huru, hatupangi nani aje au nani afanye hivi hata kama Watumishi wanatakiwa saa nne wakae kwenye viti vyao, lakini wanapenda pia kusikiliza Bunge kama raia wengine. Kwa hiyo, hatuwezi kupanga hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni walioandikwa hapa kama ifuatavyo: Tuna wageni wa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira, ambao ni mke wake Bi. Florence; naomba asimame alipo, karibu sana tunashukuru kwa kuja. Wageni wengine wa Waziri ni Viongozi wa CCM Wilaya ya Bunda; yupo Katibu Kata mmoja, Madiwani watano, Makatibu wawili na Makada saba wa CCM Wilaya ya Bunda; tunaomba wasimame mahali walipo, kama wapo *basement* basi wataingia mchana.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige, ambao ni Mheshimiwa Mary Manyambo, Diwani wa Kata ya Kinaga, Jimbo la Msalala, Wilaya ya Kahama; Mzee Ichembani Ntemanye kutoka Kata ya Kinaga, nadhani pia atakuwa *basement*; na Ndugu Majuto Elias kutoka Kata ya Kinaga. Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani baadaye watapata nafasi humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dokta James Wanyancha, ambao ni Ndugu Chandi Marwa, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Serengeti karibu sana; tunaye Mheshimiwa John Ngoina, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti; tunaye Mheshimiwa Joseph Mechana, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Serengeti, karibuni sana tumefurahi mmekuja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Yusuf Makamba, Katibu Mkuu wa CCM, ambao ni vijana 12 kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, wakiongozwa na Ndugu Godwin Mwakitabu; wako wapi? Nadhani pia wamekosa nafasi, lakini mchana wanaweza kupata. Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mbunge wa Ruangwa, ambaye ni Ndugu Hamis Chitonaga, karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, ambaye ni Ndugu Machimu Magambo, rafiki wa Mheshimiwa na mpiga kura wake, kama amekosa nafasi ataweza kuingia baadaye. Tunao wageni wa Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, ambao ni Elizabeth Vedastusi, mke wake na watoto wake wawili; Mary Steven na Silvanus Steven; karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanane wa Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Jimbo la Bububu Zanzibar, ambao ni Viongozi wa CCM katika Jimbo hilo, wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT, Ndugu B. Majuto na Ndugu Juma Haji. Katika ujumbe huo, yupo pia mke wake (Mrs Masolwa); karibuni sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, ambaye ni mtoto wake, Karim Mohamed Rished, anachukua digrii ya sayansi ya jamii Kijitonyama Dar es Salaam; karibu sana. Kumbe ni binti! Karibu sana na tunakutakia masomo mema.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 48 na Walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari Kikuyu Dodoma; hawa wako wapi na walimu wao? Kwa sababu ni Dodoma wanaweza kuja wakati wowote. Tunao wanafunzi 43 kutoka Bahi Shule ya Msingi; simameni, karibuni sana tumefurahi kuwaoneni. Kuna wanafunzi 44 na Walimu 18 kutoka Shule ya Msingi St. Ignatius na wageni wao simameni; karibuni sana. Hawa wageni wanatoka Uingereza, wana uhusiano na shule hiyo ya St. Ignatius ya Dodoma. Karibuni wageni kutoka Uingereza. Shule hii kesho kutwa wanafanya sherehe yao na Wabunge wanakaribishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 30 ambao ni wanafunzi na walimu wawili kutoka Central High School Dodoma; wako wapi? Watapata nafasi baadaye. Tunao wanafunzi 40 na walimu kutoka Shule ya Sekondari Nkuhungu Dodoma; karibuni sana wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Sekondari Nkuhungu mjitahidi kusoma.

Waheshimiwa Wabunge, kama kuna wageni tumewasahau mtaniletea majina, lakini majina niliyonayo nimekwishayasoma.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa za kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dokta Abdallah Kigoda, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kuwa, leo tarehe 21 Julai, kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika Ukumbi Namba 231, saa tano asubuhi, ilikuwa iwe saa saba mchana wamefanya mabadiliko. Naomba mzingatie mabadiliko hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo kutakuwa na kikao cha Kamati, kitakachofanyika Ukumbi wa Pius Msekwa, Ukumbi Namba D; wao ni saa saba mchana.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa, kutakuwa na kikao leo tarehe 21, saa saba mchana. Kikao hiki kitafanyika katika Ukumbi Namba 227, hawa ni Kamati siyo *TAPAC*.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dokta Slaa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo tarehe 21, kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Pius Msekwa, saa saba mchana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo yote haya, naomba tundelee na shughuli nyingine.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji, inayohusu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, sasa lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nitumie fursa hii, kwanza, kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutoa umuhimu na msukumo wa pekee kwa Sekta ya Kilimo. Kama wote mtakavyokumbuka, tarehe 2 na 3 Juni, 2009, kilifanyika kikao mahususi cha Baraza la Biashara la Taifa, ambacho chini ya Uenyekiti wa Rais Jakaya Kikwete, kilitafakari sababu zinazochelewesha Mapinduzi ya Kilimo hapa nchini. Ni katika kikao hicho, kaulimbiu ya Kilimo Kwanza ilipozaliwa. Msingi wa maudhui ya dhana ya Kilimo Kwanza ni kukiri kwamba, haiwezekani kukuza uchumi wa Tanzania kwa kiwango cha kupunguza umaskini, bila kuwekeza kwa kiwango cha kuridhisha katika Sekta ya Kilimo. Aidha, Hotuba ya Rais ya tarehe 10 Juni, 2009 hapa Dodoma na uamuzi alioutoa kufidia hasara waliyoipata wanunuzi wa mazao ya kilimo msimu wa 2008/2009, yakiwemo makampuni binafsi, Vyama vya Ushirika na fidia ya bei kwa wakulima; ni hatua ya kihistoria, inayoweza tu kuchukuliwa na uongozi unaojali maslahi ya watu unaowaongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Norman Borlaug, Baba wa Mapinduzi ya Kijani huko Asia, aliwahi kusema: "Pembejeo muhimu na ya kwanza katika kuleta Mapinduzi ya Kijani (*Green Revolution*) ni utashi wa kisiasa." Kwa msukumo huu wa Rais kwa Sekta ya Kilimo na kwa msimamo wa Bunge hili wa kutaka bajeti zaidi kwa Sekta ya Kilimo, sina sababu wala wasiwasi kwamba, pamoja na matatizo tuliyonayo yakiwemo ya ukame, mikakati iliyoainishwa katika Kilimo Kwanza inatekelezeka na Mapinduzi ya Kijani yanawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, ambaye amekuwa akifanya ziara mikoani ambapo kila mara ametenga muda kuona shughuli za kilimo na kutoa maagizo mbalimbali kuhusu kilimo endelevu na kinachozingatia utunzaji wa mazingira. Maagizo na maelekezo hayo yanazingatiwa katika utekelezaji wa *ASDP* ili uzalishaji katika kilimo uwe endelevu na unaozingatia utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia, kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge, kwa kusisitiza umuhimu wa kuendeleza kilimo chenye tija; cha kisasa na cha kibiashara. Aidha, namshukuru Waziri Mkuu, kwa kuongoza mkutano wa wadau wa Sekta ya Kilimo kutoka Mikoa ya Morogoro, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Kigoma, uliofanyika Mkoani Morogoro kuanzia tarehe 16 hadi 18 Oktoba, 2008. Katika mkutano huo, wadau waliazimia kuimarisha utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, hususan Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans - DADPs*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Vilevile wadau waliweka maazimio na malengo ya kuongeza uzalishaji, ambayo yamewezesha Mikoa hiyo kuzalisha kwa wingi mazao ya chakula, hasa maeneo yanayotumia skimu za umwagiliaji. Maelekezo na maagizo anayoyatoa Waziri Mkuu, yanasaidia utekelezaji wa *ASDP* kwa lengo la kuleta mapinduzi ya kijani. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Spika, kupitia kwako, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge la Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009, Bunge lako Tukufu lilipata misiba, kwa kupotelewa na Wabunge watatu kama ifuatavyo: aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Marehemu Richard Nyaulawa; aliyekuwa Mbunge wa Tarime, Marehemu Chacha Zakayo Wangwe; na aliyekuwa Mbunge wa Busanda, Marehemu Kabuzi Faustine Rwilomba. Aidha, aliyekuwa Mbunge wa Biharamulo Magharibi, Marehemu Phares Kabuye, alifariki kabla ya shauri lake la pingamizi la kutengua Ubunge wake wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kukamilika. Ninachukua fursa hii, kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa familia za Marehemu hao. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, azilaze Roho za Marehemu hao Mahali Pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na chaguzi za kujaza nafasi zilizoachwa wazi, nachukua nafasi hii, kuwapongeza Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu katika kipindi cha mwaka 2008/2009. Wabunge hao ni Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale (CCM) Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Charles Mwera Nyanguru (CHADEMA) Jimbo la Tarime, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba (CCM) Jimbo la Busanda na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa (CCM) kutoka Jimbo la Biharamulo Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2009/2010. Naishukuru kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina, Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ya Mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2009/2010 katika kikao chake kilichofanyika Dodoma, tarehe 12 na 15 Juni, 2009. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa, yamezingatiwa katika bajeti hii. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuzingatia na kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili bajeti ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani na pongezi za pekee, kwa Wananchi wa Jimbo la Bunda, kwa ushirikiano wanaonipa na kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo. Naendelea kuwaahidi kuwa, nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kutoa mchango wangu katika kupambana na matatizo yanayotukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo, ufafanuzi umetolewa kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu kilimo, hususan dhana ya Kilimo Kwanza. Nawapongeza sana kwa hotuba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wakati wa kujadili hotuba hizo, Waheshimiwa Wabunge, wamepata fursa ya kutoa michango yao kuhusu uendelezaji wa kilimo na kushauri jinsi ambavyo usimamizi na utekelezaji wa shughuli za kilimo unatakiwa uwe. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, ushauri na maelekezo yao yatazingatiwa katika utekelezaji. Aidha, nawapongeza Mawaziri wenzangu, ambao hoja zao zimekwishajadiliwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Kilimo inatoa mchango mkubwa katika kuwapatia ajira Watanzania zaidi ya asilimia 70 na inachangia zaidi ya asilima 95 ya chakula kinachopatikana nchini. Aidha, katika mwaka 2008, Sekta ya Kilimo ilikua kwa asilimia 4.6 na ilichangia asilimia 25.7 ya Pato la Taifa na asilimia 30.9 ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pamoja na mchango mkubwa wa Sekta ya Kilimo katika uchumi wa Taifa, bado Sekta hiyo inakabiliwa na vikwazo vingi; vikiwemo uwekezaji mdogo, hususan katika miundombinu muhimu ya umwagiliaji na barabara za vijijini. Kadhalika, uhaba wa ardhi iliyopimwa na kuwekewa miundombinu muhimu kama vile maji, umeme na barabara. Vilevile uhaba wa viwanda vya usindikaji; viwanda vya kuzalisha pembejeo na zana za kilimo na uwezo mdogo wa wakulima wadogo kumudu gharama kubwa za pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, upatikanaji wa chakula haukuwa wa kuridhisha kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya chakula, hususan mazao ya aina ya nafaka yaliyozalishwa katika msimu wa 2007/2008. Katika msimu huo, uzalishaji wa mazao ya chakula ulifikia jumla ya tani milioni 10.872, ikilinganishwa na mahitaji ya jumla ya tani milioni 10.337 katika mwaka 2008/2009. Pamoja na kuwepo kwa ziada ndogo ya jumla ya tani 534,355 ya mazao yasiyo nafaka kama vile muhogo, viazi na mikunde, upungufu wa chakula ulijitokeza kutokana na pengo la uzalishaji wa mazao ya aina ya nafaka la takriban tani 860,000. Wakati mahitaji ya mazao ya nafaka kwa mwaka 2008/2009 yalikuwa tani milioni 6.45, uzalishaji wa mazao hayo msimu wa 2007/2008 ulifikia jumla ya tani milioni 5.59.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mazao kutokana na kilimo cha vuli cha msimu wa 2008/2009, haukuwa mzuri hivyo kusababisha upungufu wa takriban tani 536,134 za chakula ambacho katika hali ya kawaida kama kingepatikana, kingepunguza pengo la mahitaji ya nafaka lililotokana na uzalishaji mdogo wa msimu wa 2007/2008. Maeneo ambayo hayakupata mvua za vuli ni Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Manyara, Pwani, sehemu ya Kaskazini ya Mkoa wa Morogoro na Mikoa ya Mara, Shinyanga na Mwanza. Upungufu huo ulichangiwa pia na mvua za masika kuchelewa kuanza kunyesha katika maeneo mengi ya Mikoa hiyo na vipindi virefu vya ukame katika maeneo yanayopata mvua za msimu. Aidha,

kutokana na hali hiyo, bei za vyakula katika mwaka 2008/2009 zilipanda ikilinganishwa na bei za mwaka 2007/2008 na 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hali hiyo ya upungufu, uzalishaji wa chakula nchini msimu wa 2007/2008, ulitosheleza mahitaji ya nchi kwa kiwango cha asilimia 105. Hata hivyo, kiwango hicho ni kidogo ikizingatiwa kuwa nchi yetu imezungukwa na nchi nyingi ambazo katika mwaka 2008/2009, zilikuwa na upungufu mkubwa wa chakula. Kutokana na hali hiyo, kumekuwepo na usafirishaji wa chakula usio rasmi kwenda nchi jirani, kwa mfano, Kenya, Malawi na Zambia, hali iliyosababisha bei kubwa za vyakula, hususan katika maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kufuatilia kwa karibu, mwenendo wa hali ya chakula na uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa lengo la kuainisha maeneo, idadi ya watu walioathirika na upungufu wa chakula, mahitaji yao ya chakula na hatua za kuchukuliwa. Kati ya mwezi Julai, 2008 na Mei, 2009, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa usalama wa chakula, ilifanya tathmini za kina za hali ya chakula katika maeneo yaliyotambuliwa kuwa na upungufu wa chakula katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Lindi, Mara, Morogoro, Pwani, Mwanza, Mtwara, Iringa na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya Tathmini hizo pamoja na taarifa kutoka mikoa mbalimbali yalionesha kuwa, jumla ya watu 978,492 au asilimia 10 ya watu katika wilaya 40 walibainika kuwa na upungufu wa chakula katika kipindi cha miezi mitatu ya Mei hadi Julai, 2009. Watu hao walihitaji msaada wa chakula wa jumla ya tani 36,872.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo la kuendelea kupanda kwa bei za vyakula na upungufu wa chakula uliojitokeza, Serikali ilichukua hatua zifuatazo:-

(i) Kutenga kwa ajili ya kusambaza kwa walengwa jumla ya tani 36,872.9 za chakula kutoka Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula *(National Food Reserve Agency - NFRA).* Hadi tarehe 9 Julai, 2009 jumla ya tani 27,877.957 za mahindi zilisambazwa kwa walengwa.

(ii) Kutoa jumla ya shilingi bilioni 1.76 kutoka Mfuko wa Maafa kwa ajili ya kununua jumla ya tani 1,091 za mbegu za aina mbalimbali za mazao ya chakula kwa ajili ya kuzipatia kaya za wakulima ambazo hazikuwa na uwezo au ambazo mazao yao yalikauka na kulazimika kurudia kupanda wakati wa mvua za msimu za 2008/2009. Wilaya zilizohusika ni Arusha, Monduli, Rombo, Mwanga, Same, Lindi Vijijini, Simanjiro, Bunda, Rorya, Musoma Vijijini, Kwimba, Magu, Misungwi, Ukerewe, Nanyumbu, Bariadi, Kishapu, Shinyanga Vijijini, Singida, Manyoni, Uyui, Tabora Mjini, Bahi, Chamwino, Dodoma Manispaa, Kondoa, Kongwa, Mpwapwa, Kilombero, Kilosa, Morogoro Mjini, Morogoro Vijijini, Mvomero, Tanga, Pangani, Muheza, Mkinga, Korogwe, Lushoto, Handeni na Kilindi.

(iii) Kusitisha kwa muda utoaji wa vibali vya kuuza mazao ya chakula nje ya nchi hadi hapo itakapodhihirika kuwa hali ya chakula nchini ni nzuri. Mazao hayo ni mahindi, mchele, ngano, mtama, muhogo, maharage, kunde na viazi;

(iv) Kutoa mafunzo kwa wananchi, kuwahimiza na kuwahamasisha kutumia vyakula mbalimbali, hususan visivyo vya nafaka, pamoja na uchanganyaji (blending) wa nafaka na mazao yasiyo ya nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2008/2009, hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula hususan ya nafaka kwa ujumla haikuwa nzuri. Uzalishaji wa mazao ya nafaka usiokidhi mahitaji ya mwaka 2009/2010 ni mwendelezo wa misimu miwili iliyopita, ambapo uzalishaji wa mazao ya nafaka haukuwa mzuri. Hali hiyo inatokana na unyeshaji wa mvua usioridhisha katika maeneo yanayopata mvua za vuli na za masika na pia maeneo mengi yanayopata mvua za msimu. Hali hiyo iliathiri upatikanaji wa mavuno ya vuli ambayo yalikuwa kidogo na baadhi ya maeneo hayakupata mavuno.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mvua za masika nazo zilichelewa kuanza kunyesha ambapo katika maeneo mengi zilianza kunyesha mwishoni mwa mwezi Machi na mwanzoni mwa mwezi Aprili. Mvua hizo zilinyesha chini ya viwango vya wastani na kwa mtawanyiko mbaya ulioambatana na vipindi virefu vya ukame na pia zilikatika mapema katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Pwani na Manyara. Hali hiyo pia iliathiri ukuaji wa mazao katika mikoa inayopata mvua za msimu ya Dodoma, Lindi, Mtwara na baadhi ya maeneo ya Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwezi Mei na Juni 2009, Wizara ilifanya tathmini ya awali ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula na utabiri wa hali ya chakula kwa mwaka 2009/2010. Matokeo ya tathmini hiyo katika msimu wa kilimo wa 2008/2009, yanaonesha kwamba, uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani 10,921,536 zikiwemo tani 5,265,309 za mazao ya nafaka na tani 5,656,227 za mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2009/2010, yanakisiwa kufikia tani 10,578,196. Hivyo, Taifa linategemewa kujitosheleza kwa chakula kwa takriban asilimia 103 sawa na ziada ya takriban tani 343,340, ambayo kimsingi ni mazao yasiyo ya nafaka. Kutokana na hali hiyo, uzalishaji wa nafaka wa tani 5,265,309 ukilinganishwa na mahitaji ya nafaka ya jumla ya tani 6,578,508 utaacha pengo kubwa la mahitaji ya nafaka la jumla ya tani 1,313,139.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini hiyo imeonesha kuwa, Mikoa ya Iringa, Kagera, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Rukwa na Ruvuma, itazalisha ziada ya chakula kwa kati ya asilimia 126 na asilimia 167. Kati ya Mikoa hiyo, Mikoa ya Rukwa, Kigoma na Kagera tu, haitazamiwi kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula. Mikoa ya Iringa, Rukwa, Mbeya na Ruvuma itakuwa na ziada ya zao la mahindi. Aidha, Mikoa ya Lindi, Tabora, Morogoro na Tanga itajitosheleza lakini itakuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula kutokana na uzalishaji mdogo wa mazao ya nafaka. Mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Shinyanga, Pwani, Mwanza na Singida, itazalisha mazao ya chakula chini ya kiwango cha kujitosheleza na hivyo kuwa na upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na hali ya upungufu wa chakula, hususan nafaka unaoendelea kudhihirika katika mwaka 2009/2010, Serikali inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea na usambazaji wa chakula kwa walengwa walioathirika na upungufu wa chakula katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mikoa na Halmashauri za Wilaya inaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya chakula katika maeneo yenye upungufu wa chakula na kuainisha watu walioathirika na mahitaji yao ya chakula. Natoa wito kwa Mikoa na Halmashauri

zinazohusika, kushirikiana na Wizara yangu kuhakikisha zinawasilisha taarifa za hali ya chakula;

(ii) Hivi sasa Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(NFRA)* inaendelea na hatua za kuhamisha akiba ya nafaka iliyopo kwenye Vituo vya *NFRA* vilivyo katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, kupeleka kwenye vituo vilivyo katika maeneo yenye upungufu wa chakula. Hatua hiyo itawezesha maeneo yenye upungufu wa chakula kupatiwa chakula cha msaada kwa haraka zaidi pindi kitakapohitajika na pia itatoa nafasi ya kuhifadhi nafaka itakayonunuliwa mwaka 2009/2010;

(iii) Serikali itaimarisha akiba yake ya chakula iliyopo *NFRA* kwa kununua jumla ya tani 165,000 za nafaka zikiwemo tani 160,000 za mahindi na tani 5,000 za mtama kutoka kwa wakulima nchini;

(iv) Katika mwaka 2009/2010 *NFRA* itauza sehemu ya chakula katika soko kwa lengo la kupunguza makali ya bei katika maeneo ya nchi yatakayoonesha kuwa na bei kubwa za chakula;

(v) Wizara tayari imezungumza na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (*WFP*) na Shirika hilo chini ya Mpango wa *Purchase for Progress (P4P)* limekubali kununua mazao ya chakula katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yenye ziada ya nafaka, kwa ajili ya kupeleka katika maeneo mengine ya nchi ambayo *WFP* inaendesha miradi ya kusaidia wananchi wenye upungufu wa chakula;

(vi) Serikali itaendelea kusitisha biashara ya uuzaji wa mazao ya chakula nchi za nje mpaka hapo hali itakapokuwa nzuri;

(vii) Wizara inatoa wito kwa Mikoa kuwahamasisha wafanyabiashara kununua chakula katika mikoa na maeneo yenye ziada ili kupeleka kuuza katika mikoa na maeneo mengine ya nchi yenye upungufu wa chakula;

(viii) Wizara inatoa wito kwa Mikoa na Wilaya ziwahamasishe wakulima waliopata mavuno kuhifadhi chakula cha kutosha mahitaji ya kaya zao na kuuza ziada tu katika soko. Aidha, Halmashauri za Wilaya zidhibiti ununuzi holela wa chakula kutoka mashambani au majumbani mwa wakulima. Biashara ya mazao ifanyike tu katika maeneo rasmi yaliyotengwa badala ya mashambani au majumbani; na

(ix) Pamoja na hatua hizi, katika mwaka 2009/2010 Wizara itatekeleza mikakati ya muda mfupi, kati na mrefu ya kuongeza uzalishaji wa chakula nchini kama ilivyofafanuliwa katika Mpango wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa iliyotolewa mwezi Aprili, 2009 na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*), inaonesha kuwa kutakuwa na upungufu wa chakula katika nchi 31 duniani kote. Inakadiriwa kuwa watu milioni 17 katika nchi za Mashariki mwa Afrika, wanakabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula. Kati ya nchi hizo zimo nchi jirani za Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Uganda na Burundi. Aidha, katika baadhi ya nchi za Kusini mwa Afrika, watu milioni 8.7 wanakabiliwa na upungufu wa chakula. Baadhi ya nchi hizo ni Zimbabwe, Lesotho na Swaziland.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa, mahitaji ya chakula katika nchi hizo ni makubwa na mojawapo ya mikakati ya kukabiliana na mahitaji hayo makubwa ya chakula ni

kwa nchi hizo kununua chakula hicho kutoka nchi jirani.  Hali hiyo inaweza kuathiri upatikanaji wa chakula nchini kutokana na biashara ya kuuza mazao ya chakula nchi jirani. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Mikoa inayopakana na nchi hizo, inawahamasisha wananchi kuhifadhi mazao ya chakula kulingana na mahitaji ya kaya na kuuza ziada tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtikisiko wa uchumi duniani, umeathiri sekta mbalimbali hapa nchini, ikiwemo Sekta ya Kilimo, ambapo bei ya mazao mengi imeshuka. Mathalan, bei ya wastani ya pamba imeshuka kutoka shilingi 540 kwa kilo msimu wa 2008/2009 hadi shilingi 360 kwa kilo msimu wa 2009/2010. Bei ya kahawa ya arabica imeshuka kutoka shilingi 1,500 kwa kilo hadi shilingi 1,000 msimu wa 2009/2010 na bei ya robusta imeshuka kutoka shilingi 700 hadi shilingi 400 kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanunuzi wa mazao yakiwemo makampuni binafsi na Vyama vya Ushirika, walipata hasara kutokana na kuanguka kwa bei ya mazao hayo katika Soko la Dunia. Kwa mfano, bei ya pamba ilishuka kutoka senti 72 za Dola ya Kimarekani kwa ratili hadi senti 45 kwa ratili na bei ya kahawa ya arabica ilishuka kutoka Dola za Kimarekani 140 kwa gunia la kilo 50 hadi Dola za Kimarekani 104 na robusta ilishuka kutoka Dola za Kimarekani 96 kwa gunia la kilo 50 hadi Dola za Kimarekani 64. Kutokana na mtikisiko huo, Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali za kunusuru uchumi, zikiwemo kufidia tofauti ya bei ya mazao kwa wakulima, kufidia hasara walizopata wanunuzi, kudhamini mikopo ya mabenki, kusogeza mbele muda wa kulipa mikopo na kutoa mitaji kwa wanunuzi watakaothibitika kuathirika na mtikisiko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa Zao la Pamba kwa mwaka 2009/2010, unatarajiwa kupungua kutoka tani 368,229 za mwaka 2008/2009 hadi tani 250,000. Kupungua huko kwa sehemu kubwa kunachangiwa na msukosuko wa uchumi duniani. Baada ya wakulima kupata taarifa za msukosuko wa uchumi duniani uliosababisha bei ya pamba katika Soko la Dunia kushuka, baadhi yao ama walipunguza kiwango cha uzalishaji au kuacha kabisa uzalishaji katika msimu huo. Kwa kuwa zao la pamba ni la msimu tofauti na mazao mengine makuu ya asili ya biashara ambayo ni ya kudumu, ni rahisi kwa mkulima kuamua kulima au kutokulima kutokana na dalili za bei. Kutokana na hali hiyo, uzalishaji wa pamba umeathirika zaidi ikilinganishwa na mazao mengine. Hivyo, kwa kuwa uchumi wa dunia bado haujatengemaa, hakuna dalili za kuongezeka kwa bei ya pamba katika Soko la Dunia. Kama hatua ya muda mfupi, Serikali kupitia mpango wa kunusuru uchumi imeamua kufidia bei ya wakulima kwa shilingi 80 kwa kilo ya pamba inayouzwa katika msimu wa ununuzi wa 2009/2010. Hiyo inafanya bei ya pamba sasa kuwa shilingi 440.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuchukua nafasi hii, kuwasihi wakulima wa pamba wasikate tamaa na waendeleze juhudi za kuzalisha zao hilo, wakati Serikali inaandaa utaratibu endelevu utakaosaidia kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2007/2008 na 2008/2009, uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara, isipokuwa kwa Zao la Korosho, uliongezeka kwa viwango mbalimbali. Zao la Pamba liliongezeka kwa asilimia 83.51, tumbaku asilimia 6.04, sukari asilimia 5.43, pareto asilimia 17.14, mkonge asilimia 0.51, kahawa asilimia 44.99 na chai asilimia 4.49. Uzalishaji wa Zao la Korosho ulishuka kwa asilimia 20.22. Maelezo ya kina ya uzalishaji wa mazao hayo yako Sehemu ya III ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Ushirika nchini iliendelea kuimarishwa chini ya utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini

*(Cooperative Reform and Modernization Program – CRMP).* Vyama vya Ushirika viliendelea kufufuliwa na vingine vipya kuanzishwa ili vitoe huduma mbalimbali zinazohitajika kwa wanachama wake pamoja na wananchi kwa ujumla. Kutokana na utekelezaji huo, idadi ya Vyama vya Ushirika nchini imeongezeka kutoka vyama 8,597 mwezi Mei, 2008 hadi 9,510 mwezi Mei, 2009. Aidha, idadi ya wanachama iliongezeka kutoka milioni 1.6 hadi milioni 1.8 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilikadiria kukusanya mapato ya kiasi cha Shilingi bilioni 1.023 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi mwezi Juni 2009, kiasi cha Shilingi milioni 598.0 sawa na asilimia 58.5 ya makadirio kilikusanywa. Lengo hilo halikufikiwa kutokana na kupungua kwa mazao yaliyosafirishwa nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 157.53. Kiasi hicho kinajumuisha Shilingi bilioni 40 zilizopokelewa kutoka Mfuko wa Madeni ya Nje *(EPA)* kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo na Shilingi bilioni 3.79 zilizoongezwa kwa ajili ya mishahara ya Bodi, Taasisi na Watumishi wa Wizara. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 137.5 zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 20.03 ni fedha za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo Shilingi bilioni 2.51 zilikuwa ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 17.51 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2009, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilipokea kiasi cha Shilingi bilioni 126.57 kutoka Hazina sawa na asilimia 92.1 ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa. Matumizi hadi kipindi hicho ni Shilingi bilioni 117.35 sawa na asilimia 92.6 ya kiasi cha fedha kilichotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Shilingi bilioni 20.03 ilizoidhinishiwa Wizara kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2008/2009, jumla ya Shilingi bilioni 19.25 zilitolewa. Matumizi hadi tarehe 30 Juni 2009, ni jumla ya Shilingi bilioni 18.45 sawa na asilimia 95.8 ya kiasi cha fedha kilichotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea kutekeleza Malengo ya Milenia na MKUKUTA kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* na Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika *(CRMP).* Aidha, Wizara imeweza kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kwa kuweka kipaumbele katika kutekeleza mikakati ya kuleta mapinduzi ya kijani *(Green Revolution).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009 ulikuwa ni mwaka wa tatu wa utekelezaji wa *ASDP*. Kuanzia mwaka 2006/2007 hadi mwaka 2008/2009 fedha zilizotolewa kwa ajili ya kutekeleza *ASDP* ni jumla ya Shilingi bilioni 198.6 sawa na asilimia 34.42 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Shilingi bilioni 578.6 katika kipindi hicho. Kati ya fedha zilizotolewa, Shilingi bilioni 130.2 zilipelekwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans-DADPs)* na Shilingi bilioni 68.4 zilibaki katika ngazi ya Taifa kwa ajili ya kuimarisha huduma za utafiti, ugani, ukarabati wa vyuo vya kilimo na mifugo, mafunzo kwa wataalam, umwagiliaji, uendelezaji wa masoko na ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza Programu.

Aidha, maeneo mengine ni pamoja na kufanya tathmini ya hali ya chakula, hifadhi na kupunguza upotevu wa chakula kabla na baada ya mavuno, uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Programu. Mahitaji halisi kwa ajili ya utekelezaji wa *ASDP* hayakufikiwa

kutokana na Washirika wa Maendeleo kutotimiza ahadi za michango yao katika Mfuko wa *ASDP (Basket Fund)* unaogharamia programu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, *ASDP* iliendelea kutekelezwa katika ngazi ya Halmashauri kupitia *DADPs* ambapo miradi mbalimbali iliibuliwa na wakulima na wafugaji. Miradi hiyo ni pamoja na: ujenzi wa skimu za umwagiliaji 167 na ukarabati wa skimu 94; ujenzi wa masoko 87 ya mazao na 34 ya mifugo; ukarabati wa masoko ya mifugo 12; ujenzi wa maghala ya mazao 96; vituo 11 vya kukusanya maziwa na ujenzi wa kilometa 345 za barabara za vijijini. Aidha, Programu imewezesha ujenzi wa majosho 142 na ukarabati wa majosho 162; ujenzi wa mabwawa 129 na ukarabati wa malambo 50.

Vilevile, jumla ya machinjio 21 yalijengwa na 16 yalikarabatiwa; vituo 6 vya afya ya mifugo vilijengwa na 1 kufanyiwa ukarabati. Zana bora za kilimo zilinunuliwa ambazo ni pamoja na majembe ya kukokotwa na wanyamakazi 437, matrekta makubwa 91 na madogo 394. Aidha, maksai 301 walinunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia *DADPs* jumla ya magari 141, pikipiki 1,419, baiskeli 3,222, kompyuta 294 na mashine za kudurufu (*photocopy*) 48 zilinunuliwa. Aidha, jumla ya ofisi 5 za wagani zilifanyiwa ukarabati na nyumba 11 za wataalam wa ugani zilijengwa; Maafisa Ugani wapatao 6,479 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi, 66 mafunzo ya Shahada, 26 Stashahada na 33 Shahada ya Uzamili. Vilevile, mafunzo yalitolewa kwa wakulima 131,805 kupitia mashamba darasa 2,407, vikundi 4,057 vya wajasiriamali na Vyama vya Akiba na Mikopo. Jumla ya vikundi na Vyama vya Ushirika 2,321 vilianzishwa na kupatiwa mafunzo yatakayovisaidia kujiendesha. Aidha, jumla ya ng'ombe bora 1,444, mbuzi 1,798, majogoo ya kisasa 3,871, bata 184 na nguruwe 658 walinunuliwa na kusambazwa kwenye vikundi vya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuzijengea uwezo Halmashauri na Sekretariati za Mikoa wa kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya yenye ubora. Jumla ya Washauri wa Mikoa wa Sekta ya Kilimo 63; Wawezeshaji wa Wilaya 1,188 na Wawezeshaji wa Kata 660 walipata mafunzo kuhusu mbinu za kuibua, kuandaa andiko la miradi ya kijamii ya uwekezaji, kuandaa mipango ya *DADPs* kwenye vijiji kwa awamu (*village phased out plan)* na kutekeleza mipango bora ya *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zimeonyesha kuwa uwezo wa kuandaa na kutekeleza *DADPs* umeanza kuongezeka. Kati ya Halmashauri 132 zilizofanyiwa tathmini chini ya Mfumo wa Kuzipatia Serikali za Mitaa Ruzuku za Maendeleo *(Local Government Capital Development Grant-LGCDG)* ili kupata fedha za nyongeza, *(Top up District Agricultural Development Grant)* kwa mwaka 2009/2010, Halmashauri 125 zilifuzu ikilinganishwa na Halmashauri 110 mwaka 2008/2009. Halmashauri 3 hazikufuzu ikilinganishwa na Halmashauri 5 mwaka 2008/2009. Halmashauri ambazo hazikufuzu ni Ukerewe (DC), Kyela (DC) na Rorya (DC). Aidha, Halmashauri za Wilaya za Kibaha (DC), Kongwa (DC), Mpwapwa (DC) na Manispaa ya Ilala zilifaulu kwa kiwango cha chini (poor) kulingana na vigezo vya tathmini vilivyowekwa kwa misingi kwamba zimeandaliwa vizuri kiutekelezaji.

Kadhalika, *DADPs* za mwaka 2009/2010, zilichambuliwa na matokeo kuonyesha kuwa Halmashauri zilizoandaa *DADPs* zenye ubora zimeongezeka kutoka asilimia 20 mwaka 2008/2009 hadi asilimia 48 mwaka 2009/2010, asilimia 58 zimeonyesha kuwa na ubora wa wastani ikilinganishwa na asilimia 50 za mwaka 2008/2009 na asilimia 14 zimeonyesha kuwa na ubora hafifu ikilinganishwa na asilimia 29 mwaka 2008/2009. Halmashauri zilizokuwa na

*DADPs* zenye ubora usioridhisha ni pamoja na:- Kilolo (DC), Simanjiro (DC), Longido (DC), Muleba (DC), Serengeti (DC), Meru (DC), Shinyanga (MC), Tandahimba (DC), Shinyanga (DC), Chamwino (DC), Makete (DC), Mwanga (DC), Mafia (DC), Karatu (DC), Kasulu (DC), Morogoro (DC) na Lindi (TC).

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani *(District Agricultural Sector Investment Project – DASIP)* na Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(Participatory Agricultural Development and Empowerment Project – PADEP)* ambayo pia inatekeleza DADPs, jumla ya vikundi vya wakulima 5,846 vimeanzishwa na kufundishwa kupitia mbinu shirikishi ya shamba darasa ya kilimo bora cha mazao ya mahindi, pamba, mtama na mpunga. Aidha, miradi mbalimbali ipatayo 1,978 yenye thamani ya Shilingi bilioni 17.5 ilitekelezwa. Miradi hiyo ni pamoja na majosho, masoko, barabara, umwagiliaji, malambo, mashine za kusindika mazao na maghala.

Vilevile, jumla ya vipindi vya televisheni 13 na vya redio 26 vilitayarishwa na kurushwa. *DASIP* pia imewezesha kununuliwa kwa baiskeli 2,000 kwa ajili ya matumizi ya Maafisa Ugani na wakulima wawezeshaji wa Wilaya 28 za mradi. Menejimenti ya mradi pia ilipitia na kutathmini utekelezaji wa mradi (*Implementation review)* katika Wilaya hizo. Matokeo ya tathmini hiyo yameonyesha kuwa bado kuna tatizo la usimamizi wa matumizi ya fedha, kutoshirikisha walengwa katika kuibua miradi na kutokuzingatia ubora wa ujenzi wa miundombinu. Hatua za kurekebisha mapungufu hayo zimeanza kuchukuliwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu –Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upatikanaji wa Pembejeo na Zana za Kilimo, Mbolea, katika mwaka 2008/2009, makadirio ya mahitaji ya mbolea yalikuwa tani 385,000. Hadi mwezi Mei, 2009, jumla ya tani 237,894 sawa na asilimia 61.8 ya mbolea ikijumuisha mbolea za ruzuku zilipatikana. Katika kipindi hicho, Wizara ilitoa ruzuku ya mbolea tani 141,050 ikilinganishwa na lengo lilowekwa la tani 130,000 ambapo jumla ya vocha 1,499,000 zilitumika. Kiwango hicho cha usambazaji wa mbolea ya ruzuku kilivuka lengo kutokana na Wizara kuongezewa fedha za *EPA* Shilingi bilioni 40. Jumla ya wakulima 737,000 walinufaika na mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza ufanisi katika kufikisha pembejeo za kilimo karibu na wakulima, jumla ya mawakala 1,684 kutoka Mikoa ya Arusha (121), Kilimanjaro (178), Morogoro (102), Iringa (453), Mbeya (410), Ruvuma (127), Rukwa (108), Manyara (87), Kigoma (66), Tabora (12), Mara (19), na Tanga (1) walipatiwa mafunzo kwa kushirikiana na asasi isiyo ya KiSerikali ya *Citizen Network for Foreign Affairs (CNFA).* Hadi mwezi Aprili 2009, mawakala 223 walipata mikopo ya kununulia pembejeo kutoka benki ya NMB yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara ililenga kutoa ruzuku ya mbegu bora tani 3,000 ikilinganishwa na tani 7,180 zilizosambazwa kwa utaratibu wa ruzuku. Upatikanaji wa mbegu bora katika mwaka 2008/2009 ulifikia tani 11,056.07 kwa mbegu za mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta ambayo ni sawa na asilimia 36.8 ya mahitaji halisi ya tani 30,000. Kati ya kiasi hicho, tani 544.75 zimetokana na Taasisi za Serikali ikilinganishwa na lengo lililowekwa la kuzalisha mbegu tani 1000, na tani 300.40 zimetokana na wakulima wadogo wanaozalisha mbegu za daraja la kuazimiwa *(Quality Declared Seed – QDS)*. Aidha, makampuni binafsi ya mbegu nchini yamechangia jumla ya tani 10,511.32 ambapo tani 5,163 za mbegu ziliagizwa kutoka nje ya nchi.

Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo *(Agricultural Seed Agency-ASA),* inashirikiana na JKT na Jeshi la Magereza ili kuongeza uzalishaji na uenezaji wa mbegu bora

nchini. Hadi mwezi Mei 2009, jumla ya hekta 858 zimelimwa na kupandwa mazao mbalimbali kwa ajili ya mbegu za nafaka, mikunde, mbegu za mafuta na mboga mboga. Kati ya hizo, JKT wamelima na kupanda hekta 515 na Magereza hekta 343 ambapo jumla ya tani 1,500 za mbegu bora zinatarajiwa kuzalishwa na kusambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2008/2009, Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai *(Tanzania Smallholder Tea Development Agency –TSHTDA)* kupitia vikundi 141 vyenye wakulima 2,012 kutoka Halmashauri za Wilaya 11, vilizalisha miche bora 7,830,000 sawa na asilimia 98 ya lengo la miche 8,000,000 kwa utaratibu wa ruzuku. Taasisi ya Utafiti wa Zao la Chai *(Tea Research Institute of Tanzania-TRIT)* imezalisha na kusambaza miche bora ya chai 8,047,300. Aidha, miche bora ya kahawa 9,570,846 ilizalishwa kupitia vikundi 695 vya wakulima, Halmashauri za Wilaya, wakulima binafsi na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa *(Tanzania Coffee Research Institute -TaCRI)*, sawa na asilimia 96 ya lengo la miche 10,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Bodi ya Pamba iliendelea kutoa ruzuku ya madawa yanayohusika na zao la pamba ambapo jumla ya *acrepacks* 2,050,000 zilinunuliwa. Kati ya hizo, *acrepacks* 1,141,758 zilisambazwa kwa mawakala ambapo acrepacks 556,772 sawa na asilimia 48.7 ya kiasi kilichosambazwa zilinunuliwa na wakulima. Ununuzi huo mdogo umesababishwa na uwezo mdogo wa wakulima kununua madawa hayo ya pamba. *Acrepack* moja inatosha kudhibiti visumbufu katika ekari moja ya zao la pamba. Aidha, jumla ya lita 386,649 na tani 154 za madawa ya korosho zilisambazwa kwa wakulima chini ya utaratibu wa ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya utekelezaji wa pembejeo za ruzuku, katika msimu wa 2008/2009, jumla ya vocha 2,217,000 zikiwemo vocha 1,499,000 za mbolea na 718,000 za mbegu bora zenye thamani ya Shilingi bilioni 69 zilisambazwa kwa wakulima 737,000 katika Mikoa ya Morogoro, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Rukwa, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, na Kigoma na Wilaya za Sikonge mkoa wa Tabora na Tarime mkoa wa Mara.

Tathmini iliyofanyika mwishoni mwa mwezi Mei hadi Juni 2009 katika Mikoa ya Morogoro, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Kigoma ilibaini kuwa, wakulima walionufaika na pembejeo hizo wanatarajia kuongeza mavuno kwa ekari kutoka wastani wa magunia 5 hadi 8 na kufikia magunia 17 hadi 25 kwa zao la mahindi na kutoka wastani wa magunia 4 hadi magunia 25 kwa zao la mpunga. Uzalishaji wa mazao ya chakula katika Mikoa sita ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Morogoro, na Kigoma uliongezeka kutoka tani 4,692,411 katika mwaka 2007/2008 hadi kufikia tani 5,279,278 mwaka 2008/2009. Aidha, umbali wa kupata mbolea kwa mkulima umepungua kutoka wastani wa kilometa 40 kwa miaka iliyopita hadi kufikia wastani wa kilometa 5 kutokana na ukweli kuwa sasa mawakala wa pembejeo wanalazimika kupeleka pembejeo vijijini kufuata fedha zilizotolewa katika vocha. Hata hivyo, malengo ya uzalishaji katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara hayakufikiwa kutokana na athari za ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio niliyoyaeleza, tathmini hiyo ilibaini mapungufu yafuatayo:-

- Vocha kuchelewa kuwafikia wakulima kwa wakati;

- Bei ya mbolea kuendelea kuwa ya juu kiasi kwamba wakulima wanashindwa kumudu gharama za uchangiaji;

- Kutoeleweka vema kwa utaratibu wa vocha kwa wadau wengi; na

- Usimamizi kuwa duni katika ngazi mbalimbali za utekelezaji, hususan ngazi ya Wilaya na kijiji.

Kutokana na upungufu huo, Wizara itafanya yafuatayo:-

- Kupeleka vocha mapema kulingana na msimu wa kilimo wa eneo husika;

- Kuendelea kutoa elimu zaidi ya utaratibu wa matumizi ya vocha za pembejeo za ruzuku za kilimo kwa wadau mbalimbali;

- Kupeleka vijana 1,998 wa Cheti na Diploma kutoka Vyuo mbalimbali vya Kilimo watakaokuwa katika mafunzo kwa vitendo katika Wilaya zitakazopewa ruzuku ya pembejeo kuanzia Septemba, 2009 hadi Aprili, 2010. Hii itaboresha usimamizi na kutoa maelekezo ya kitaalamu kwa wakulima; na

- Kuanzia msimu ujao mkulima atatakiwa kuchangia malipo ya tofauti ya bei ya pembejeo kabla hajapewa vocha ili kuzuia wakulima kutumia vocha kinyume na makusudio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuhimiza matumizi ya zana bora za kilimo nchini ambapo jumla ya matrekta makubwa 472, matrekta madogo ya mkono 495 na majembe ya kukokotwa na wanyamakazi 62,194 yaliingizwa nchini na watu binafsi pamoja na makampuni. Aidha, zana mbalimbali za kilimo zilipatikana kupitia ushirikiano wa kimataifa na nchi za Korea ya Kusini na China. Zana hizo kutoka Serikali ya Korea ya Kusini zinajumuisha matrekta madogo ya mkono 30, mashine za kuvuna mpunga 2, mashine za kusukuma maji 20, mashine za kupandikiza mpunga 12, mashine za kupura mpunga 3, mashine 15 za kukata mpunga na trekta kubwa moja. Mashine hizo zimekopeshwa kwa wakulima wa mkoa wa Morogoro kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo *(Agricultural Input Trust Fund- AGITF)* kwa ruzuku ya asilimia 50 ya bei, ikiwa ni mchango wa Wizara katika kuendeleza Mpango wa “Fanya Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Taifa” (FAMOGATA). Aidha, wataalam wa zana za kilimo 10 walishiriki katika kuziunganisha na walipatiwa mafunzo juu ya matumizi yake ili watoe ushauri wa kiufundi kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zana zilizopatikana kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ni mtambo wa kukoboa mpunga ambao umefungwa katika kijiji cha Lupiro Wilaya ya Ulanga, Mkoani Morogoro. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi iliwezesha kupatikana mkopo wenye masharti nafuu kutoka India “*line of credit*” wa Dola za Kimarekani milioni 40 kwa ajili ya kununua matrekta makubwa na zana zake, matrekta madogo ya mkono na pampu za kusukuma maji kwa ajili ya umwagiliaji. Zana hizo zitakopeshwa kwa wakulima nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imefanya tathimini ya kuendeleza matumizi ya zana za kilimo na usindikaji katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ambapo jumla ya vikundi 50 vya vijana vimeainishwa kwa ajili ya kuendelelezwa. Vikundi hivyo vitapatiwa mafunzo pamoja na matrekta madogo ya mkono 35 na seti 20 za mashine za usindikaji wa muhogo na korosho ili viweze kujiendesha kibiashara chini ya Mpango wa Mashirikiano wa Umoja wa Mataifa *(One UN Joint Programme).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilitoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 176 katika Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Mara, Tabora, Singida, Dodoma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Manyara na

Arusha ili kueneza matumizi sahihi ya majembe ya palizi ya kukokotwa na wanyamakazi na zana za Kilimo Hifadhi. Kilimo Hifadhi ni mojawapo ya mbinu za kisasa zinazotumika kudhibiti mmomonyoko wa udongo, kuongeza rutuba kwa kutumia masalia ya mazao au mazao funika na kuhifadhi maji ya mvua hususan wakati wa upungufu wa mvua. Mashamba Darasa 78 yenye jumla ya wakulima 1,950 kutoka katika Wilaya za Karatu, Babati, Hanang, Mbulu, Arumeru, Same, Moshi Vijijini na Kilindi yalianzishwa kwa ajili ya kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya zana za kilimo hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maonesho kuhusu matumizi ya zana bora za kilimo na mashine za usindikaji yamefanywa kwa wakulima katika Mikoa ya Mbeya, Pwani, Arusha, Manyara, Kigoma, Morogoro, Mwanza, Tabora na Shinyanga ili kuwaongezea upeo wakulima juu ya matumizi ya zana bora mbalimbali zinazoongeza tija katika kilimo. Kutokana na mafunzo na maonesho hayo, wakulima waliweza kuibua miradi mingi ya zana na mashine za usindikaji katika *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipeperushi mbalimbali vinavyohusu matumizi ya zana bora za Kilimo Hifadhi, matrekta madogo ya mkono, matumizi ya wanyamakazi katika palizi na mashine za kusindika muhogo *(Cassava Chipper Na Grater)* vimeandaliwa na kusambazwa kwa wakulima nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulitengewa jumla ya Shilingi bilioni 3.0 kwa ajili ya kutoa mikopo ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana za kilimo. Aidha, Mfuko uliongezewa Shilingi bilioni 3.0 zilizotokana na Fedha za Madeni ya Nje *(EPA)*. Fedha hizo zikijumuishwa na marejesho ya madeni ya nyuma ya kiasi cha Shilingi bilioni 2.77 zilifanya Mfuko kuwa na jumla ya Shilingi bilioni 8.77. Mikopo ilitolewa kwa wakulima binafsi, wasambazaji wa pembejeo za kilimo na mifugo na zana za kilimo, vikundi vya wakulima, *SACCOS* kupitia Taasisi ya Dunduliza, Benki ya Biashara na Uchumi ya Mkoa wa Kilimanjaro, Benki ya Wananchi Mbinga, Benki ya Ushirika Kagera pamoja na Mifuko ya Pembejeo ya Halmashauri za Wilaya ya Newala na Tandahimba kwa ajili ya kununulia na kusambaza madawa ya zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo iliyotolewa ilitumika kununua matrekta makubwa mapya 139 ikilinganishwa na lengo la kununua matrekta makubwa 124; matrekta madogo *(Power Tiller)* 42 ikilinganishwa na lengo la kununua matrekta madogo 107; pembejeo za kilimo na mifugo na kuanzisha vituo viwili vya kukodisha matrekta katika Wilaya za Magu na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Ushauri wa Kitaalam, Wizara inatekeleza Ilani ya CCM kuhusu kuwafikishia wakulima vijijini maarifa ya kanuni za kilimo bora. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara iliendelea kutekeleza Mkakati wa Kuimarisha Huduma za Ugani ulioanza mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2008/2009, Wizara ilipeleka wataalam wa kilimo 643 wakiwemo 110 wenye Shahada, 184 Stashahada na 349 Astashahada katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Aidha, katika kutekeleza mkakati huo, ilibainika kuwepo kwa upungufu mkubwa wa wataalam wa ngazi ya Stashahada, hivyo Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ilirejesha ngazi ya Astashahada katika Muundo wa Utumishi. Kutokana na kurejeshwa kwa ngazi hiyo ya utumishi jumla ya wataalam 349 waliohitimu ngazi hiyo wameajiriwa katika mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Kuimarisha Upatikanaji wa Huduma za Ugani kwa ufanisi na kwa wakati muafaka, Wizara ikishirikiana na Wizara za kisekta imeandaa rasimu ya miongozo ya Kutekeleza na Kusimamia Huduma za

Ugani;  Kuanzisha na Kuendesha Shamba Darasa; Mashindano ya Kilimo; Kuanzisha Vituo vya Rasilimali za Kilimo na Mifugo vya Kata *(Ward Agricultural Resource Centres-WARCs)*; kutekeleza Sera ya Kilimo katika utoaji wa Huduma za Ugani na Mwongozo wa Sekta Binafsi katika kutoa Huduma za Ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia iliendelea kuhimiza matumizi ya mbinu shirikishi jamii ya Shamba Darasa katika kueneza teknolojia sahihi za kilimo chenye tija nchini kwa kutoa ushauri wa utekelezaji wa mbinu hiyo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jumla ya mashamba darasa 1,965 yenye wakulima wapatao 51,623 yameanzishwa kwa lengo la kupata wakulima wawezeshaji. Aidha, jumla ya Maafisa Ugani 751 walipatiwa mafunzo na wanaendelea kueneza mbinu hiyo. Vilevile, matumizi ya Daftari la Kilimo yameendelea kuhimizwa kwenye Halmashauri ambapo jumla ya Halmashauri 126 kati ya 132 zinatumia daftari hilo katika utoaji wa huduma za ugani. Halmashauri tano ambazo zinaendelea na maandalizi ya daftari hilo ni Kilwa (DC), Kigoma (MC), Misungwi (DC), Ukerewe (DC) na Kwimba (DC).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya iliendelea kuorodhesha watoa huduma binafsi wa ugani ambapo jumla ya watoa huduma binafsi 99 wametambuliwa, kati yao 30 wameanza kutoa huduma hizo chini ya utaratibu wa mikataba katika Halmashauri za Wilaya nchini. Pia Wizara iliendelea kuratibu maandalizi ya maonyesho yanayohusu Sekta ya Kilimo nchini. Maonyesho hayo ni pamoja na Sikukuu ya Wakulima– Nanenane yaliyofanyika Kitaifa katika viwanja vya Nzuguni, Dodoma na katika kanda mbalimbali nchini. Kwenye maonyesho hayo, wakulima walipata fursa ya kuonyeshwa na kujifunza teknolojia mbalimbali za Kilimo. Sambamba na maonyesho hayo, utekelezaji wa Mashindano ya Kilimo uliendelea kwenye kanda ya kati baada kuanzia kanda ya kaskazini mwaka 2007 ambapo wakulima waliofanya vizuri walipewa zawadi. Maadhimisho mengine yalihusu Siku ya Chakula Duniani iliyoadhimishwa Kitaifa Musoma katika mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa chai, uliongezeka kutoka tani 32,698 mwaka 2007/2008 hadi tani 34,165 mwaka 2008/2009. Ongezeko hilo linatokana na kuanza kuvunwa kwa chai iliyopandwa kutokana na mpango wa Serikali wa kusambaza miche kwa wakulima sambamba na kuboresha huduma za ugani kupitia Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai na Taasisi ya Utafiti wa Chai – *Tea Research Institute of Tanzania (TRIT).* Aidha, mikakati mingine ilikuwa ni kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima wadogo wa chai ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kuwatumia wakulima wazoefu (farmer cadre/collaborators) kutoa huduma za ushauri ili kukabiliana na upungufu wa wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa sukari, uliongezeka kutoka tani 265,434 mwaka 2007/2008 hadi tani 279,850 mwaka 2008/2009 kutokana na upanuzi wa mitambo katika kiwanda cha TPC,upanuzi wa uwezo wa usindikaji katika kiwanda cha *Kagera Sugar Ltd.* na upanuzi wa mashamba. Hata hivyo, lengo la uzalishaji wa sukari wa tani 317,000 halikufikwa msimu wa 2008/2009 kutokana na hali ya ukame, tija ndogo na ajali za mioto katika mashamba ya miwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa tumbaku, uliongezeka kutoka tani 55,357 mwaka 2007/2008 hadi 58,702 mwaka 2008/2009 kutokana na utekelezaji wa mikakati ifuatayo: kupanua maeneo ya uzalishaji, matumizi ya pembejeo, kuzingatia kanuni za kilimo bora, ujenzi wa mabani ya kukaushia, kulinda bei ya mkulima na  ushirikishwaji wa wakulima katika kuhakiki madaraja umeongeza uwazi katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa pamba, uliongezeka kutoka tani 200,662 mwaka 2007/2008 hadi tani 368,229 mwaka 2008/2009 kutokana na upatikanaji wa pembejeo

kwa wakati kwa maeneo yote yanayolima zao hilo, kuendeleza mashindano ya kilimo cha pamba, kutoa mafunzo ya kilimo bora cha pamba kwa wakulima ikiwa ni pamoja na matumizi ya wanyamakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa pareto, uliongezeka kutoka tani 2,800 mwaka 2007/2008 hadi tani 3,280 mwaka 2008/2009 kutokana na tija kubwa ya miche bora iliyopandwa misimu iliyopita, kuzingatiwa kwa kanuni za kilimo bora na kupatikana kwa soko la uhakika. Mikakati hiyo iliwezesha kuongezeka kwa kiwango cha sumu kutoka asilimia 1.4 hadi asilimia 1.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa korosho, ulishuka kutoka tani 99,107 mwaka 2007/2008 hadi tani 79,069 mwaka 2008/2009 kutokana na hali mbaya ya hewa, hususan kuwepo kwa ukungu uliofuatiwa na hali ya ukame katika Wilaya za Nachingwea, Ruangwa, Tandahimba na Newala. Aidha, madawa ya udhibiti wa visumbufu yalichelewa kuwafikia wakulima kutokana na wafanyabiashara kuchelewesha usambazaji kwa kuhofia upatikanaji wa malipo yao yaliyopitia Halmashauri za Wilaya badala ya kupitia Bodi ya Korosho tofauti na utaratibu wa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mkonge, uliongezeka kutoka tani 33,039 mwaka 2007/2008 hadi tani 33,208 mwaka 2008/2009 kutokana na mkonge uliopandwa misimu ya nyuma kuanza uzalishaji na wakulima kuzingatia kanuni bora za kilimo, hususan usafi wa mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa kahawa, uliongezeka kutoka tani 43,000 mwaka 2007/2008 hadi 62,345 mwaka 2008/2009 kutokana na miche bora iliyopandwa msimu wa 2004/2005 kuanza kuvunwa, kuongezeka kwa eneo la uzalishaji toka hekta 265,000 hadi 300,000 na tija kwa mti kutoka wastani wa gramu 250 hadi 500 na wakulima kuzingatia kanuni bora za kilimo cha kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazao mapya ya biashara (mboga, matunda na viungo). Uzalishaji wa Mazao ya Bustani, Wizara iliendelea kutunza nasaba za miti ya matunda na viungo na kuzalisha vipando bora katika bustani za Serikali za Mpiji (Bagamoyo), Bugaga (Kigoma), Songa (Muheza), Malindi na Jaegetal (Lushoto) na Igurusi (Mbeya). Aidha, Wizara ilikarabati na kukifungua tena Chuo cha Mafunzo ya Kilimo - HORTI Tengeru kilichopo mkoani Arusha ili kiendelee kuwaandaa wataalam wa ugani wa fani ya mazao ya bustani. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Serikali ya Marekani (*USAID*) kupitia Chama cha Wakulima wa Mazao ya Bustani *(Tanzania Horticultural Association – TAHA),* mnamo mwezi Desemba, 2008 ilianzisha usafirishaji wa mazao ya bustani kwenda nje ya nchi kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ambapo ndege mbili huruka kwa wiki kutoka KIA zikisafirisha mazao hayo. Aidha, mkakati mwingine ni kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam na kuhamasisha wadau kuwekeza katika uzalishaji na usindikaji wa mazao ya matunda, hususan katika maeneo yenye fursa ya kuzalisha mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ushirikiano na wadau wa sekta ndogo ya mazao ya bustani, katika mwaka 2008/2009, uzalishaji wa mazao hayo uliongezeka na kufikia wastani wa tani 557,400 za mazao ya matunda, tani 602,000 za mboga na tani 6,865 za mazao ya viungo. Mazao hayo yalizalishwa na kuuzwa katika soko la ndani na nje na hivyo kuliingizia Taifa wastani wa Dola za Kimarekani milioni 150.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzalishaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta, tathmini ya uzalishaji na usindikaji wa mbegu za mafuta kwa ajili ya chakula cha binadamu na mifugo na kwa ajili ya nishati kwa zao la mmbono ilifanyika kwa lengo la kuainisha mahitaji ya viwanda

na hali ya uzalishaji. Matokeo ya tathmini hiyo yalionyesha kuwa takriban Mikoa yote ina uwezo wa kuzalisha na kusindika mbegu za mafuta na ina uwezo wa kuzalisha mojawapo ya mazao hayo kwa viwango na aina tofauti kama ifuatavyo:-

(a) Alizeti: Singida, Dodoma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Morogoro, Kilimanjaro, Arusha , Mara na Ruvuma;

(b) Karanga: Dodoma, Tabora, Rukwa, Shinyanga, Mbeya, Iringa, Singida, Ruvuma, Mtwara na Lindi;

(c) Ufuta: Mtwara, Lindi, Pwani, Dodoma, Mbeya, Singida, Tanga na Ruvuma;

(d) Michikichi: Kigoma, Mbeya, Pwani, Rukwa, Tanga na Tabora;

(e) Pamba: Kanda ya Magharibi ni Mwanza, Mara, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Singida na Kagera na Kanda ya Mashariki ni Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Morogoro, Pwani na Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha uzalishaji wa mbegu za mafuta kati ya mwaka 2000/2001 hadi mwaka 2007/2008 ni kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 1. Kiasi cha uzalishaji kinachoweza kufikiwa kama fursa zote zikitumika ni alizeti tani 2,650,000, karanga tani 2,000,000, pamba tani 4,000,000, ufuta tani 1,500,000 na soya tani 2,166,000. Uzalishaji wa mazao hayo umekuwa ukiongezeka kidogo kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa uwekezaji mkubwa katika uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta. Ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta, mikakati itakayotumika ni pamoja na kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji, kuhimiza kilimo cha mkataba na kuwaunganisha wazalishaji na wasindikaji. Mkakati mwingine ni kuanzisha vikundi na vyama vya uzalishaji wa mazao hayo ili kurahisisha utoaji wa huduma za ugani na kuwawezesha wanakikundi kuwa na sauti moja katika kushughulikia maslahi yao.

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa mbegu za mafuta kati ya 2000/2001 na 2007/2008 (Tani).

| Mwaka | Alizeti | Karanga | Pamba | Ufuta | Soya |
|---|---|---|---|---|---|
| 2000/2001 | 80,870 | 206,800 | 123,589 | 25,707 | 1,430 |
| 2001/2002 | 104,400 | 289,500 | 148,142 | 55,100 | 1,270 |
| 2002/2003 | 112,440 | 255,100 | 187,883 | 22,485 | 2,060 |
| 2003/2004 | 106,312 | 163,360 | 139,829 | 49,163 | 1,070 |
| 2004/2005 | 88,854 | 125,311 | 341,789 | 74,989 | 1,150 |
| 2005/2006 | 373,391 | 783,775 | 376,591 | 221,421 | 5,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2006/2007 | 369,80<br>3 | 408,05<br>8 | 130,58<br>5 | 155,794 | 3,000 |
| 2007/2008 | 418,31<br>7 | 396,76<br>9 | 200,66<br>2 | 46,767 | 3,500 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea na mkakati wa kuendeleza zao la muhogo kuwa zao la biashara kwa kuzalisha vipando bora vya muhogo milioni 20 kwa kushirikisha Jeshi la Magereza na JKT ili kuwezesha upatikanaji endelevu wa vipando bora vya muhogo kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa kilimo, katika mwaka 2008/2009, huduma za utafiti zililenga kubuni teknolojia bora za uzalishaji wa mazao ili kumwezesha mkulima kupata mavuno mengi na kuongeza tija, na hivyo kumuongezea kipato na kumpunguzia umaskini. Teknolojia hizo ni pamoja na uzalishaji wa mbegu bora zenye sifa za kutoa mavuno mengi, kuvumilia visumbufu vya mimea, magonjwa na hali ya ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za utafiti zilitolewa na vituo vilivyopo katika kanda saba za utafiti na taasisi za utafiti za *Tea Research Institute of Tanzania (TRIT), Tanzania Coffee Research Institute (TaCRI), Tobacco Research Institute of Tanzania (TORITA) na Tropical Pesticide Research Institute (TPRI).* Aidha, Kituo cha Taifa cha Nasaba za Mimea *(National Plant Genetic Resource Centre – NPGRC)* kilichopo TPRI Arusha kiliendelea kutafiti na kukusanya mimea iliyopo nchini kwa lengo la kutunza nasaba hizo kwa ajili ya kuzihifadhi kwa matumizi ya watafiti katika kuzalisha aina bora za mazao. Nasaba 491 zilikusanywa katika kipindi hicho na mpaka sasa jumla ya nasaba 5,299 zinatunzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kupitia vituo vyake vya utafiti ilipendekeza aina 5 za mbegu bora za mazao kwa matumizi ya mkulima. Mbegu zilizotolewa ni pamoja na aina mbili za pamba ambazo ni UK M08 na UK 08 kutoka kituo cha Utafiti Ukiriguru, Mahindi aina ya BORA kutoka kituo cha Utafiti Ilonga, Maharage aina ya Njano Uyole kutoka kituo cha Utafiti Uyole na Nyanya aina ya Tengeru 2008 kutoka HORTI-Tengeru. Aidha, mbegu hizo pamoja na mtama aina ya Sila uliotolewa na kampuni binafsi ziliidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Mbegu *(National Seed Committee-NSC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilizalisha jumla ya tani 71 za mbegu mama *(Breeder seeds)* za mazao ya chakula na biashara kwa matumizi ya mashamba ya Wakala wa Mbegu za Kilimo *(Agricultural Seed Agency-ASA)* kama ifuatavyo: mazao ya nafaka ambayo ni mtama tani 3, mahindi tani 2.4, ngano tani 8 na mpunga tani 7.6. Mazao ya jamii ya mikunde ambayo ni maharage tani 9.2, mbaazi tani 3.1 na kunde tani 2.9. Mazao ya jamii ya mafuta ambayo ni soya tani 2.4, ufuta tani 1.5 na karanga tani 1.5. Mbegu za mazao ya biashara ya pamba tani 8.1 na korosho tani 21.3. Vilevile, vipando bora 3,761,487 vikiwemo vya muhogo pingili 3,650,000, zabibu miche 106,987 na migomba miche 4,500 vilizalishwa kwa ajili ya matumizi ya mashamba ya kuzalisha mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya mbinu shirikishi za udhibiti wa visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao na tathmini ya madawa asilia na ya viwandani yanayofaa kutumiwa bila kuathiri mazingira zilifanyika katika vituo vya utafiti vya Naliendele, Selian,

Ukiriguru, Uyole, Maruku na Ilonga. Utafiti wa funza mwekundu (*Redbollworm*) wa pamba katika Mikoa ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini umekamilika. Matokeo ya uchambuzi wa kiuchumi *(Cost-benefit analysis)* yameonesha kuwa mkulima akizalisha pamba bila ya kutumia viuadudu atapata hasara ya moja kwa moja. Hata kama atatumia viuadudu, uzalishaji wa pamba utagharimu kiasi kikubwa cha fedha bila ya kuwepo uhakika wa kurudisha gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti kuhusu magonjwa ya batobato *(Cassava Mossaic Disease)* na michirizi kahawia *(Cassava Brown Streak Disease)* katika muhogo Kanda ya Ziwa umefanyika na matokeo ya awali yanaonyesha kuwa mbegu saba zina ukinzani kwa batobato. Kati ya mbegu hizo, aina mbili zina ukinzani dhidi ya michirizi kahawia ambao ni ugonjwa mpya katika Kanda ya Ziwa. Mbegu zote saba zinaendelea kufanyiwa uhakiki (*verification*) katika mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kutoa Hakimiliki kwa lengo la kulinda aina mpya za mbegu zilizogunduliwa na watafiti wa Wizara pamoja na taasisi nyingine ambapo jumla ya Hakimiliki saba zilitolewa. Kati ya hizo Hakimiliki 5 zilitolewa kwa Wizara kwa ajili ya kulinda aina mbili za ufuta za Lindi 02 na Ziada 94 zilizotafitiwa na kugunduliwa na kituo cha utafiti Naliendele. Aidha, aina 2 za mahindi zilizotafitiwa na Kituo cha Utafiti Ilonga za TMV-1 na Staha na aina 1 ya maharage ya Uyole 04 iliyogunduliwa na Kituo cha Utafiti Uyole zilipatiwa Hakimiliki. Vilevile Hakimiliki mbili zilitolewa kwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwa ajili ya kulinda aina 2 za maharage za Mshindi na Pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa udongo na rutuba ya ardhi. Katika mwaka 2008/2009, Wizara kupitia Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Mlingano kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TaCRI), iliandaa ramani zinazoonyesha sehemu zinazofaa kwa kilimo cha kahawa katika Wilaya za Kasulu na Kibondo katika Mkoa wa Kigoma, na Wilaya za Tarime na Rorya katika Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Kituo cha Utafiti cha Mlingano kilianza kazi ya kuboresha ramani za rasilimali kilimo kwa kutumia teknolojia ya GIS kwa ajili ya kuainisha maeneo ya uwekezaji. Kazi zilizofanyika ni kuweka ramani zilizokuwepo katika mfumo wa GIS (*digitization*), katika Mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, na Tanga. Kazi nyingine iliyofanyika ni kuboresha ramani za udongo katika Wilaya za Mbarali, Njombe na Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Utafiti cha Mlingano, kilitoa rasimu ya mapendekezo ya matumizi ya mbolea kufuatana na ekolojia za kilimo kwa nchi nzima. Rasimu hiyo iliwasilishwa kwa wadau kwa maboresho. Uhakiki wa Mbolea ya Minjingu Mazao umefanyika katika Kanda ya Mashariki (Ilonga), Kaskazini (Selian) na Nyanda za Juu Kusini (Uyole). Aidha, jumla ya sampuli za udongo 3,000 zilichunguzwa na kutolewa ushauri kuhusu kiasi cha virutubisho vinavyopaswa kuongezwa kwenye udongo ili kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa mifumo ya kilimo na uchumi sayansi jamii. Katika mwaka 2008/2009, Wizara ilitoa mafunzo kwa watafiti 40 wakiwemo wanaume 30 na wanawake 10 kuhusu mbinu za kuwashirikisha wakulima katika kupanga na kufanya tafiti shirikishi *(Farming Systems Approach).*

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya tafiti nane za sayansi jamii na uchumi zilifanywa kwenye kanda tano za utafiti. Wizara pia ilitayarisha taarifa kuhusu gharama za uzalishaji *(farm budgets)* kwa baadhi ya mazao makuu katika kanda kwa lengo la kuelimisha

wakulima faida na hasara ya kuzalisha mazao hayo kitaalam. Taarifa hizo ni muhimu katika kuwaongoza wakulima kuchagua mazao ya kuzalisha, hususan chini ya utaratibu wa *DADPs*. Katika Kanda ya Kaskazini mazao yaliyohusika ni mahindi, mbaazi, ngano na maharage. Kanda ya Mashariki-mahindi, mpunga na pamba; Kanda ya Ziwa- mtama, mpunga, mahindi na pamba; Kanda ya Kusini – karanga, ufuta na korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo imeonyesha kuwa matumizi ya teknolojia bora katika mazao zinalipa zaidi. Kwa mfano, mchanganuo wa zao la mpunga katika Kanda ya Ziwa ulionyesha kuwa mkulima anayetumia mbegu bora na kanuni bora za kilimo zilizopendekezwa na wataalam anapata nyongeza ya faida ya Shilingi 2,079,500 kwa hekta, wakati kwa zao la mahindi anapata nyongeza ya faida ya Shilingi 786,100 kwa hekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha vituo na kuimarisha uwezo wa Watafiti. Katika mwaka 2008/2009, Wizara iliimarisha Mifuko ya Utafiti na Maendeleo ya Kanda *(Zonal Agricultural Research Development Fund - ZARDEFs)* pamoja na mfumo wa *Client Oriented Research and Development Management Approach (CORDEMA).* Jumla ya tafiti 64 zilipitishwa na Kamati Endeshaji za Utafiti za Kanda chini ya Mfuko wa Utafiti wa Kanda (ZARDEF). Tafiti hizo zinalenga kutoa na kusambaza teknolojia kulingana na vipaumbele vya kanda na mahitaji ya walengwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha mahusiano na usambazaji wa teknolojia kati ya watafiti, wagani na wakulima, Vitengo vya Mawasiliano vya Utafiti vya Kanda *(Zonal Information and Extension Liaison Units – ZIELU)* vilianzishwa katika kanda saba za utafiti. Wataalam 32 wa vitengo hivyo, walipatiwa mafunzo ya namna ya kuwasilisha matokeo ya utafiti kulingana na mahitaji ya wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilisambaza vitendea kazi kwa ajili ya vituo vya utafiti ikiwa ni pamoja na magari 13, pikipiki 5, kompyuta 91 na madawa ya maabara ya "*tissue* culture" kwa kituo cha Ukiriguru na Uyole. Magari yalipelekwa katika vituo vya Ukiriguru (1), Maruku (1), Makutopora (1), Hombolo (1), Selian (1), Tengeru (1), Naliendele (1), Uyole (1), Kifyulilo (1), Ilonga (1), Cholima (1) na Makao Makuu (2).

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya utafiti 11 vilikarabatiwa ambavyo ni Tumbi (kuweka umeme nyumba 55 daraja la C za watumishi pamoja na kukarabati sehemu ya mfumo wa maji), Ukiriguru (Mfumo wa maji) HORTI-Tengeru *(screen house)*, Mlingano (mfumo wa maji), Makutupora (nyumba 4 za watumishi), Hombolo (nyumba 2), Naliendele (nyumba 3 na mfumo wa maji), KATRIN (mfumo wa maji), Uyole na Mikocheni (ununuzi wa jenereta ya umeme 1) na Selian (ujenzi wa nyumba mpya daraja la A),

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya watafiti 38 waliendelea kupata mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Uzamivu (PhD.) 10, MSc. 7 na BSc. 21 pamoja na watumishi wengine 141 waliopatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani zao. Ili kukabiliana na upungufu wa Watafiti, Wizara imewarejesha kazini kwa mkataba wa miaka miwili Watafiti wastaafu wanane.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa wataalam na wakulima. Wizara iliendelea kufadhili mafunzo ya muda mrefu kwa wakufunzi nane (8) na vijana tarajali 2,327 ngazi ya stashahada na astashahada ikilinganishwa na lengo la wanafunzi 3,000 katika vyuo vya kilimo na kutoa mafunzo rejea kwa wakufunzi 40. Vilevile, Wizara iliandaa mitaala na kuboresha iliyokuwepo ili kukidhi mahitaji ya wadau mbalimbali wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilikarabati na kujenga miundombinu ambayo ni pamoja na mabwawa mawili ya umwagiliaji (Ilonga na Ukiriguru); maabara, mabweni na madarasa na miundombinu ya vitengo vya mifugo na kununua samani kwa ajili ya vyuo vya Ukiriguru, Ilonga, Igurusi, Mtwara, KATC Moshi, KATRIN Ifakara na Maruku. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wakulima katika skimu 10 za umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo cha zao la mpunga kwa njia ya umwagiliaji. Skimu hizo ni Mussa Mwinjanga (Hai), Kitivo (Lushoto), Kwemazandu (Korogwe), Mahende (Monduli), Kiroka (Morogoro Vijijini), Ilonga–Msalabani (Kilosa), Ruanda Majenje (Mbarali), Sakalilo (Sumbawanga), Titye (Kasulu) na Mahiga (Kwimba). Chini ya mpango huo, Wakulima Wakufunzi 180 (18 kutoka kila skimu) wamefuzu mafunzo ya kilimo bora cha mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imewapanga jumla ya vijana 1,998 waliopewa mafunzo maalumu ya mwaka mmoja yanayowawezesha kuwashauri na kuwaelimisha wakulima kulima kwa kuzingatia kanuni za kilimo bora. Vijana hao wamepangwa kwenye Mikoa na Wilaya kama ifuatavyo. Iringa Wilaya 8 vijana 272, Mbeya Wilaya 8 vijana 303, Ruvuma Wilaya 5 vijana 171, Rukwa Wilaya 3 vijana 117, Kilimanjaro Wilaya 7 vijana 263, Arusha Wilaya 7 vijana 234, Manyara Wilaya 6 vijana 211, Kigoma Wilaya 4 vijana 65, Tabora Wilaya 2 vijana 60, Mara Wilaya 2 vijana 52, Shinyanga Wilaya 2 vijana 45 na Morogoro Wilaya 6 vijana 205. Utaratibu huo utawezesha wakulima kutumia pembejeo kwa usahihi na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha utayarishaji wa rasimu ya awali ya Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo *(National Agricultural Land Use Planning and Management Master Plan).* Aidha, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Mikoa ya Morogoro na Pwani iliendelea kutambua maeneo yanayofaa kwa kilimo katika Mikoa hiyo kwa lengo la kupata maeneo makubwa yanayofaa kwa kilimo cha mahindi na mpunga (Morogoro) na mpunga na muhogo (Pwani) kwa ajili ya wawekezaji. Katika mkoa wa Morogoro maeneo yaliyotambuliwa yapo kwenye vijiji vya Tindiga, Malui, Changarawe, Msowero, Gongoni, Mbuyuni na Lumuma katika Wilaya ya Kilosa. Vilevile, Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Rufiji (RUBADA) ina maeneo makubwa ya ardhi yanayofaa kwa uwekezaji wa kilimo katika bonde la Kilombero Wilayani Kilombero na bonde la Rufiji katika Wilaya za Rufiji na Mkuranga. Upimaji wa mashamba ya Serikali ya mbegu yaliyopo Arusha na Kilangali, ARI na MATI Naliendele ulifanyika ili yaweze kupatiwa hatimiliki kwa lengo la kudhibiti uvamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuzihamasisha Halmashauri za Wilaya na Miji kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 katika uandaaji na utekelezaji wa shughuli za kilimo. Halmashauri hizo ni pamoja na Arusha Mjini na Vijijini, Meru, Monduli na Karatu katika mkoa wa Arusha; Musoma Mjini na Vijijini, Bunda, Tarime na Rorya katika Mkoa wa Mara; na Songea Mjini na Vijijini, Mbinga na Namtumbo katika Mkoa wa Ruvuma. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa Timu za Wawezeshaji wa Wilaya, wataalam wa kilimo wa Wilaya na wakulima katika Halmashauri za Kilombero na Kilosa Mkoani Morogoro kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, uingizaji wa shughuli za mazingira katika *DADPs* pamoja na athari za uharibifu wa mazingira zitokanazo na shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhsu usalama wa Chakula, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliboresha mfumo wa ukusanyaji takwimu na taarifa za hali ya chakula nchini. Mafunzo yalitolewa kwa wataalam katika Halmashauri za Wilaya na Miji katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kuhusu ufuatiliaji wa hali ya mazao mashambani na hali ya chakula. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilifanya tathmini za kina katika maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu wa chakula ili kutambua kaya zenye upungufu, mahitaji yao

ya chakula na kuchukua hatua kukabiliana na upungufu huo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini *(Tanzania Meterological Authority-TMA)* ilifanya savei na mafunzo ya mifumo ya ukusanyaji wa taarifa za mvua katika vituo vya kupima mvua katika Mikoa yote nchini kwa ajili ya kufufua na kuanzisha vituo vinavyokusudiwa kuunganishwa katika mfumo kisasa (*Automation*) wa ukusanyaji na uwasilishaji wa takwimu na taarifa za mvua na mazao mashambani kwa ajili ya uchambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hifadhi ya mazao na usindikaji, Wizara ilitoa mafunzo ya hifadhi bora na matumizi ya mazao ya nafaka na mikunde kwa wataalam wa kilimo 140 kutoka Halmashauri za Wilaya za Mbarali, Mbozi, Mbeya (V), Ileje, Rujewa, Nkasi, Sumbawanga, Mpanda, Kilosa, Mvomero, Ulanga, Kilombero, Iringa (V), Kilolo, Njombe na Ludewa katika Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Morogoro na Iringa ili kupunguza upotevu na kuongeza uhakika wa chakula nchini. Aidha, Wizara iliendelea kutoa mafunzo ya usindikaji wa mazao ya chakula kwa mazao ya muhogo, mboga na matunda katika Wilaya za Mbinga na Kisarawe ambapo jumla ya Vikundi 13 vyenye wakulima 160 vilipatiwa mafunzo hayo. Kwa upande wa maghala, Wizara ilitoa mafunzo ya ujenzi wa maghala bora ya kuhifadhia nafaka na mikunde katika Halmashauri za Wilaya za Muheza, Kilindi, Handeni na Mkinga katika Mkoa wa Tanga kwa mafundi ujenzi wa vijiji na wataalam wa kilimo ambapo wajenzi 25 na watalaam 10 walipatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilitoa mafunzo kwa wawezeshaji 136 kutoka Halmashauri za Wilaya za Maswa, Kishapu, Shinyanga (V), Same, Rombo, Mwanga, Makete na Njombe ili kuwajengea uwezo wataalam wa Wilaya kuwa na uwezo na mbinu za kuibua miradi inayolenga kutatua matatizo ya upungufu wa chakula katika ngazi ya kaya itakayoingizwa kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Vijiji (VADPs) na hatimaye kuingizwa kwenye DADPs. Wizara ilihamasisha uchanganyaji mazao ya nafaka na muhogo kwa wasindikaji ili kueneza teknolojia ya uchanganyaji wa mazao na kupanua wigo wa matumizi ya mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, akiba ya chakula, katika mwaka 2008/2009, *NFRA* ilipanga kununua jumla ya tani 105,000 za nafaka, zikiwemo tani 100,000 za mahindi na tani 5,000 za mtama. Hadi kufikia mwezi Juni, 2009, *NFRA* ilikuwa imenunua kutoka kwa wakulima hapa nchini jumla ya tani 62,641 za nafaka sawa na asilimia 59.7 ya lengo. Hata hivyo, lengo la ununuzi halikufikiwa kutokana na bei ya kununulia kupanda na fedha za kununulia kutopatikana kwa wakati. Kati ya tani za chakula zilizonunuliwa, tani 61,588 zenye thamani ya Shilingi bilioni 18.7 zilikuwa ni za mahindi na tani 1,053 zenye thamani ya Shilingi milioni 273.91 ni za mtama. Kiasi hicho cha ununuzi wa nafaka kikijumuishwa na akiba iliyokuwepo ghalani mwanzoni mwa mwaka ya tani 68,976 za mahindi na tani 6,886 za mtama kingeifanya *NFRA* kuwa na akiba ya chakula yenye jumla ya tani 130,564 za mahindi na tani 7,940 za mtama kabla ya mauzo. NFRA iliuza tani 36,161 za mahindi zenye thamani ya Shilingi bilioni 12.66 na tani 7,644 za mtama zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.17, na hivyo kubakiwa na tani 94,404 za mahindi na tani 269 za mtama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na wakulima ilipambana na milipuko ya visumbufu mbalimbali vya mimea na mazao. Visumbufu hivyo ni pamoja na kwelea kwelea, nzige, viwavijeshi, panya na magonjwa mbalimbali ya mimea ambayo husababisha upotevu wa mavuno wa kati ya asilimia 30 na 40. Wizara ilishirikiana pia na Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu *(International Red Locust Control Organisation for Central and Southern Africa)* kudhibiti nzige wekundu kwenye mazalio yao ya asili katika mbuga za Wembere, Malagarasi, Iku-Katavi na Ziwa Rukwa ambapo jumla ya lita 23,285 za viuatilifu zilitumika kudhibiti nzige hao kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 53,560. Aidha, udhibiti kwa njia ya kibiolojia ulifanyika katika mbuga za

Iku/Katavi katika eneo la hekta 5,300 kwa kutumia ukungu (*fungus*) uliotengenezwa kama kiuatilifu cha kudhibiti nzige kiitwacho “*Green muscle*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilishirikiana na Shirika la Kimataifa la Kudhibiti Nzige wa Jangwani *(Desert Locust Control Organisation for East Africa -DLCO-EA)* kudhibiti ndege aina ya kwelea kwelea katika Mikoa ya Mbeya, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Mara, Manyara na Kilimanjaro ambapo zaidi ya ndege milioni 152.2 walidhibitiwa kwa kutumia lita 10,440 za viuatilifu. Ndege hao wasingedhibitiwa, wangeweza kusababisha uharibifu wa takriban tani 1,522 za nafaka kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, jumla ya ekari 263.15 za mazao zilishambuliwa na fuko katika Wilaya ya Rombo ambapo vidonge 3,660 vya sumu ya kufukiza vilitumika kudhibiti fuko hao. Aidha, panya walidhibitiwa katika vijiji 7 vya Wilaya ya Mvomero kwa kutumia chambo chenye sumu kilo 2,482. Vilevile, chambo chenye sumu kilo 550 kilisambazwa katika Wilaya ya Rombo na kilo 100 zilipelekwa katika Wilaya ya Bagamoyo kwa ajili ya tahadhari endapo milipuko ingetokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuhamasisha wakulima kudhibiti visumbufu vya mimea kwa kutumia mbinu za Udhibiti Husishi *(Integrated Pest Management – IPM)* katika Mikoa ya Kigoma, Singida, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Aidha, Wizara iliendeleza shughuli za kituo cha kuzalisha wadudu wanaodhibiti visumbufu kilichoko Kibaha ambapo jumla ya wadudu 600,000 *(Forpius arisanus)* wa kudhibiti nzi wa maembe na mbawakavu 5,000,000 walizalishwa na kusambazwa kwa ajili ya kudhibiti magugu maji. Wadudu 750,000 walizalishwa kwa ajili ya kudhibiti kidung’ata wa muhogo.Vilevile, mdudu aina ya nyigu aitwaye Telenomus isis aliingizwa kutoka *International Centre for Insect Physiology and Ecology (ICIPE)* Kenya kwa ajili ya kudhibiti nzi wa maembe. Wakaguzi 18 walipatiwa mafunzo juu ya kumdhibiti nzi wa maembe kwa kutumia wadudu walawangi *(Biological Control* agents) ambapo wadudu walawangi 4,000 walisambazwa kwa ajili ya kudhibiti nzi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kukagua mazao yanayoingia nchini na yanayosafirishwa nchi za nje ili kudhibiti ueneaji wa visumbufu vya mimea. Jumla ya tani 358,607.02 za mazao mbalimbali zilikaguliwa na kusafirishwa nchi za nje na tani 300,748.4 ziliingizwa nchini ambapo vyeti 6,396 vya usafi wa mazao na vibali 292 vya kuingiza mazao nchini vilitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika *(Cooperative Reform and Modernization Program – CRMP).* Wizara iliendelea kutekeleza CRMP ambayo lengo lake kuu ni kuwa na Vyama vya Ushirika endelevu vyenye nguvu kubwa kiuchumi vinavyoanzishwa kutokana na mahitaji ya wanachama na kusimamiwa na wanachama wenyewe. Chini ya Programu hiyo Wizara imetekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuimarisha uongozi wa Vyama vya Ushirika; kuhamasisha kuongezeka kwa Vyama vya Ushirika na wanachama; kutoa elimu na mafunzo; kuimarisha mitaji ya Vyama vya Ushirika ili viweze kujimudu kiuchumi na kibiashara; kulipa madeni ya Vyama vya Ushirika, kuimarisha mfumo wa ushirika na taasisi zake; kuimarisha ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, kuimarisha mfumo wa ununuzi wa mazao kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani na kuratibu uanzishwaji wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliratibu na kusimamia chaguzi za viongozi wa Vyama vya Ushirika na kuwezesha wanachama kuchagua viongozi bora. Katika chaguzi hizo theluthi moja ya wajumbe wa Bodi wa Vyama vya Msingi pamoja na wa Vyama Vikuu vya Ushirika ambao kipindi chao cha miaka mitatu kimeisha kwa mujibu wa Sheria waliachia madaraka na katika nafasi zao wakachaguliwa viongozi wengine. Chaguzi hizo zilifanyika katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Shinyanga na Kilimanjaro.

Aidha, mafunzo ya uongozi bora na uwajibikaji yalitolewa kwa viongozi ili kuimarisha utendaji wao katika vyama husika. Jumla ya viongozi 50 kutoka Vyama Vikuu vya: KACU (Kahama), NCU (Mwanza), SHIRECU (Shinyanga), ICU (Igunga na Nzega), WETCU (Tabora), KFCB na KCU (Bukoba), KDCU (Karagwe), BCU (Biharamulo) na TTCA (Morogoro) walipatiwa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na elimu ya sheria na maadili ya uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuimarisha ukaguzi wa Vyama vya Ushirika kwa kutoa ruzuku kwa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika *(Cooperative Audit and Supervision Corporation -COASCO)* kufanya ukaguzi wa mwisho wa Vyama. Ukaguzi wa mara kwa mara hufanywa na Idara ya Ushirika wakati ambapo ukaguzi wa mwisho hufanywa na *COASCO*. Jumla ya vyama 1,772 vilikaguliwa na *COASCO* katika mwaka 2007/2008 na katika mwaka 2008/2009 Shirika lilikagua Vyama 1,461. Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa wakaguzi pamoja na baadhi ya Vyama vya Ushirika kushindwa kuandika vitabu vya hesabu kama inavyotakiwa. Katika kusaidia kuboresha uwezo wa Vyama, kwa kushirikiana na wadau wengine, *COASCO* ilitoa mafunzo kwa watendaji na viongozi wa Vyama vya Ushirika mbalimbali. Jumla ya watendaji na viongozi 306 walipewa mafunzo katika Mikoa ya Mwanza (60), Iringa (46), Dar es salaam (55), Morogoro (45), Ruvuma (40) na Dodoma (60). Aidha, Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania *(Tanzania Federation of Cooperatives-TFC)* kwa kushirikiana na *COASCO* lilitoa mafunzo kwa wahasibu 21 wa Vyama vya Ushirika nchini kwa lengo la kuwawezesha kutayarisha taarifa za kifedha zinazokidhi viwango vya kimataifa *(International Financial Reporting Standards - IFRS).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilitoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 81 wa Wilaya na Mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Arusha, Singida, Tabora, Dodoma, Kigoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam kuhusu matumizi ya miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa *SACCOS*. Mafunzo hayo ni sehemu ya usambazaji wa miongozo ya *SACCOS* iliyoandaliwa ambayo ni: Mwongozo wa Uhasibu *(Accounting and Financial Management Manual);* Mwongozo wa Ukaguzi wa mwisho *(Audit guideline);* Mwongozo wa Ukaguzi wa kawaida *(Inspection guideline)* na Mwongozo wa Mfumo wa Uongozi (MIS *guideline*). Lengo la miongozo hiyo ni kuziwezesha *SACCOS* kuimarisha uendeshaji na kuzingatia sheria husika pamoja na viwango vinavyotambulika kimataifa katika uendeshaji na usimamizi wa asasi ndogo za kifedha *(Microfinance Institutions).* Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa watumishi 42 wa ngazi za Taifa, Mkoa na Wilaya, ili kuwaongezea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara cha Moshi *(Moshi University College of Cooperative and Business Studies - MUCCoBS)*, kimeendelea kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya Vyama vya Ushirika nchini kupitia utoaji wa elimu na mafunzo kwa viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika. Chuo kinatoa elimu ya ushirika shirikishi kwa viongozi wa Vyama katika matawi ya Chuo yaliyoko Mikoani. Aidha,

Chuo kinatoa mafunzo ya mbali *(Distance learning)* kwa watendaji na viongozi ambayo yanalenga kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Chuo kinatoa kozi za Shahada katika fani mbalimbali ikiwemo Uhasibu na Menejimenti ya Ushirika. Kwa kushirikiana na Chuo, Wizara imetoa mafunzo ya ngazi ya Cheti ya uendeshaji wa asasi ndogo kwa watendaji wa *SACCOS* 16 wa Mikoa ya Mara (3), Morogoro (3), Iringa (4), Singida (3) na Mwanza (3). Lengo la mafunzo hayo ni kuboresha taaluma na stadi za watendaji wa SACCOS ili kukidhi mahitaji ya walengwa wa huduma za Vyama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na mbinu za biashara kwa viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika. Kutokana na mafunzo hayo, Vyama vya Ushirika vya mazao ya kahawa vya ACU (Arusha), KCU na KDCU (Kagera), KNCU na G32 (Kilimanjaro) na KANYOVU (Kigoma), vimeweza kufanya biashara ya tija na kujiendesha kwa ufanisi kutokana na usimamizi mzuri. Aidha, Vyama hivyo viliuza mazao nje ya nchi kwenye masoko maalum kama vile *fair trade* ambayo hutoa bei ya juu kuliko masoko ya kawaida. Jumla ya tani 3,812 za kahawa safi ya arabica na robusta ziliuzwa kwenye masoko maalum Marekani, nchi za Ulaya na Japan. Kahawa ya arabica iliuzwa kwa bei ya Shilingi 4,250 hadi 4,450 kwa kilo kwenye masoko maalum ikilinganishwa na Shilingi 1,850 hadi 2,600 kwa kilo kwenye mnada wa Moshi. Kahawa ya robusta iliuzwa kwa bei ya Shilingi 3,072 hadi 3,800 kwa kilo kwenye masoko maalum ikilinganishwa na Shilingi 1,600 hadi 1,950 kwa kilo katika mnada wa Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Ushirika vinatumia fedha za zilizotokana na mauzo ya kahawa kwenye masoko maalum kuwekeza katika miradi inayowanufaisha wanachama moja kwa moja, kama vile, kununua mashine za kukoboa kahawa katika Vyama vya Msingi na vifaa vya upimaji ili kudhibiti ubora, kusaidia ujenzi na ukarabati wa shule za msingi na sekondari, zahanati na vituo vya afya. Pia Vyama vimeajiri Maafisa Ugani 84 (Chama cha KNCU 31 na Chama cha KCU 53) kwa ajili ya kuwahudumia wanachama wake. Vyama vikuu pamoja na Vyama vya Msingi vya Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma inayozalisha korosho vilipata mikopo ya Benki ya jumla ya Shilingi bilioni 37.6 na kununua korosho tani 73,645 kutoka kwa wakulima. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko iliviwezesha Vyama vya Ushirika 175 vya mkoa wa Mtwara, 15 vya mkoa wa Shinyanga na 4 vya mkoa wa Lindi kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani katika ununuzi wa mazao. Aidha, majaribio ya kueneza matumizi ya mfumo huo kwenye zao la pamba katika Mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Mara yalifanyika. Akiba na amana za wanachama wa *SACCOS* ziliongezeka kutoka Shilingi bilioni 134 hadi bilioni 181.6 sawa na ongezeko la asilimia 35.5. Mikopo iliyotolewa na vyama hivyo iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 228.5 mwezi Mei, 2008 hadi Shilingi bilioni 383.5 mwezi Mei, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwezesha maboresho (*Restructuring*) ya Vyama vya Ushirika nchini, kwa kutambua umuhimu wa *TFC* kama chombo cha juu kinachowaunganisha wanaushirika nchini, Wizara imeliwezesha Shirikisho hilo kutayarisha Mpango Mkakati wa Biashara wa miaka mitano ambao unalenga kuleta maboresho ya muundo pamoja na utendaji wa chama hicho kulingana na mahitaji ya wanachama wake. Utekelezaji wa mpango huo utakaoanza mwaka 2009/2010 utasaidia kuboresha huduma zinazotolewa kwa wanachama wake. Aidha, Wizara imekiwezesha Chama Kikuu cha Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania *(Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania – SCCULT)* kutayarisha Mpango wa Biashara ambao nao utasaidia katika uimarishaji na modenaizesheni ya *SACCOS* nchini. Chama cha *SCCULT* pamoja na wadau wengine kina jukumu kubwa la kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo watendaji na viongozi wa *SACCOS* nchini. Katika kipindi hicho, chama cha *SCCULT* kimetoa elimu na mafunzo

kwa viongozi na watendaji wa *SACCOS* 11,052 na kimetoa mikopo ya uwezeshaji ya jumla ya Shilingi bilioni 1.9 kwa *SACCOS* 38 ambapo wanachama 10,985 wamenufaika na mikopo hiyo ikiwa ni pamoja na matrekta makubwa 3 na matrekta madogo 38 yalitolewa kwa wakulima nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulipwa kwa madeni ya Vyama vya Ushirika. Kama nilivyolifahamisha Bunge lako Tukufu la Bajeti la mwaka 2008/2009 kuhusu madeni ya wakulima wanayovidai Vyama vya Ushirika, napenda kuchukua fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa jumla ya Shilingi 1,663,945,045 zimetumika kulipa wakulima 43,149. Wakulima hao wako katika Wilaya za Mbinga, Rungwe, Kyela, Mbozi, Chunya, Igunga, Nzega, Kahama, Uyui, Sikonge, Same, Karagwe, Kilombero, Ulanga, Bunda, Musoma Vijijini, Ileje, Iringa vijijini, Mbeya Vijijini na Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Wizara inaendelea na utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambaye mapema mwaka 2008 aliagiza iundwe Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambayo itakuwa chombo maalum cha maendeleo na usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini. Wizara ilitayarisha mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya kuanzishwa kwa Tume hiyo. Aidha, kufuatia kuidhinishwa kwa Muundo wa Tume, Wizara imetayarisha mahitaji halisi ya watumishi *(Job list)* ambao watahitajika katika kutekeleza kazi za muundo huo pamoja na maelezo ya kazi *(Job Descriptions)* kwa kila nafasi ya kazi. Tume inatarajia kuanza kufanya shughuli zake katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 baada ya kupitishwa kwa Sheria husika na kuteuliwa kwa makamishina watakaoiongoza Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilikamilisha uhuishaji wa Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 ili kuwa na Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2009. Vilevile, Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria ya Mbolea *(The Fertilizer Bill, 2008)* kwa ajili ya kudhibiti ubora wa mbolea zitakazozalishwa na kuagizwa kutoka nje ya nchi. Kufuatia kupitishwa kwa Muswada wa Sheria hiyo, Mamlaka ya Kudhibiti Matumizi Bora ya Mbolea (*Tanzania Fertilizer Regulatory Authority-TFRA)* itaundwa. Aidha, Miswada mingine iliyoandaliwa ilihusu marekebisho ya Sheria Nane za Bodi za mazao, Sheria ya kuunda Bodi ya Nafaka na Mazao Mengine Mchanganyiko na kuunda Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Miswada hiyo iliwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya rasilimali watu, Wizara iliendelea kuajiri watumishi wapya ambapo watumishi 105 wa kada mbalimbali waliajiriwa, watumishi 313 walipandishwa vyeo, watumishi 130 walithibitishwa kazini na wataalam 643 wakiwemo wenye shahada 110, stashahada 184 na astashahada 349 walipelekwa katika Halmashauri za Wilaya baada ya kupata kibali cha kuajiri kutoka Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Wizara iliendelea kuwawezesha watumishi 6 wanaoishi na virusi vya UKIMWI kupata vyakula vyenye virutubisho pamoja na kuhudhuria kliniki kwa ajili ya matibabu. Pia mafunzo yalitolewa kwa wanafunzi tarajali 871 katika vyuo vya Kilimo vya Ukiriguru na Mtwara kuhusu mabadiliko ya tabia na mienendo kwa vijana ili kuepukana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Vilevile, TFC imetoa mafunzo kuhusu UKIMWI kwa Vyama vya Ushirika nchini ambayo yalitolewa mkoani Mtwara katika Maadhimisho ya wiki ya Ushirika Duniani ambapo jumla ya wanaushirika 414 walipimwa afya zao. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kutoa mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi *(Open Performance Review and Appraisal System – OPRAS)* kwa watumishi 1,438. Mafunzo yalitolewa kwa wasaidizi 18 kuhusu utunzaji bora wa kumbukumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010, ni mwaka wa tano wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Pamoja na kwamba kilimo chetu bado hakijawa cha kisasa kama

ambavyo wote tungependa, yamekuwepo maendeleo ya kuridhisha katika kipindi cha miaka minne iliyopita. Hivi sasa kuna maeneo ambako wakulima wameanza kulima kwa kutumia kanuni za kilimo bora. Maarifa yameanza kuwafikia wakulima kupitia dhana ya shamba darasa, na mahitaji ya mbolea yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka ikichangiwa na kuongezeka kwa matumizi ya matrekta makubwa na madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado tunayo safari ndefu kufikia azma ya kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa na kuwa msingi wa uchumi wa kisasa. Ili kuendeleza juhudi za kuboresha kilimo chetu, Serikali imeamua kukipa kipaumbele kilimo kwa kuimarisha nguzo kumi za kuzingatiwa katika kuharakisha Mapinduzi ya Kijani kama ilivyoainishwa katika kauli mbiu ya KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya msingi yanayozingatiwa katika dhana ya kilimo kwanza pamoja na mambo mengine ni kuongeza uwekezaji siyo tu kupitia bajeti ya Serikali, bali pia kupitia uwekezaji wa sekta binafsi na mikopo ya mabenki kwa wakulima. Suala hili la uwekezaji na mikopo ni la msingi kwa vile hakuna nchi ambayo imefanikiwa kuleta mapinduzi ya kilimo bila kuwekeza kwa njia ya mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu kwa wakulima. Dhana ya kilimo kwanza inatambua, kuwa Mapinduzi ya Kijani yanawezekana tu kwa kutumia maarifa na teknolojia za kisasa, hususan zana bora za kilimo. Teknolojia hizo hazipatikani bila gharama. Ni kutokana na ukweli huo, dhana ya KILIMO KWANZA inasisitiza umuhimu wa kuanzisha benki ya kilimo hapa nchini. Uanzishaji wa benki hiyo umepewa kipaumbele katika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kauli mbiu ya KILIMO KWANZA inatambua umuhimu wa kuwepo viwanda vya pembejeo na zana, pamoja na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na kuwapatia wakulima soko na bei nzuri kwa mazao yao. Ili kuongeza uzalishaji sekta binafsi inatakiwa kushiriki kwa kuwekeza katika maeneo hayo yakiwemo ya uzalishaji. Katika kufanikisha azma hiyo, ni lazima ardhi ipatikane na kupimwa, ili wawekezaji wanaohitaji kufungua mashamba makubwa na ya kati waweze kupatiwa ardhi ya kulima bila kuathiri mahitaji ya wakulima wadogo. Aidha, miundombinu kama vile barabara za vijijini, barabara kuu, viwanja vya ndege, reli na bandari ni lazima ziimarishwe ili mazao ya wakulima yafike kwenye masoko ya ndani na nje kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake dhana ya KILIMO KWANZA inakusudia kutilia mkazo utekelezaji wa Ilani ya CCM inayosema "Kilimo, ndiyo Msingi wa Uchumi wetu na kina nafasi ya kimkakati katika modenaizesheni ya Uchumi wa Tanzania, kilimo cha kisasa ni sharti muhimu katika kujenga uchumi wa kisasa".

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo, ni dhahiri kwamba, utekelezaji wa dhana ya KILIMO KWANZA, unahusisha sekta mbalimbali zikiwemo wizara za sekta ya kilimo kwa kushirikiana na wadau wengine kama vile sekta binafsi, mabenki, wizara zinazosimamia miundombinu ya umeme, maji, usafirishaji na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) itaendelea kuwa ndiyo Programu ya Kitaifa ya kuleta mapinduzi ya kilimo na itasaidiwa na sekta zilizotajwa hapo juu. Aidha, mipango chini ya kauli mbiu ya KILIMO KWANZA, itatekelezwa kupitia wizara zenye mahusiano (collaborators) kiutendaji na sekta ya kilimo, kama vile Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko, pamoja na watendaji na viongozi wa ngazi zote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Dhana ya KILIMO KWANZA haina tofauti na dhana ya Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Uchumi Wetu isipokuwa, dhana ya KILIMO KWANZA inaweka utaratibu wa matumizi ya raslimali

zilizopo nchini kwa kuhusisha wadau wote ili kila mmoja atekeleze sehemu yake katika kuendeleza kilimo. Kauli Mbiu hii inazingatia ukweli kwamba katika nchi maskini kama yetu, kilimo ndiyo sekta ya msingi katika maendeleo ya wananchi na uchumi endelevu, ukiwemo uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*), inatekeleza sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi *(Decentralization by Devolution – D by D)* kwa kupeleka karibu asilimia 75 ya rasilimali za Sekta ya Kilimo Wilayani na vijijini. Utekelezaji wa *ASDP* katika ngazi ya Wilaya utaendelea kutekelezwa kupitia *DADPs*. Ili kutekeleza sera hiyo, Halmashauri zilipatiwa maelekezo ya kiasi cha fedha ambazo zitatengwa kwa kila Halmashauri ili zitumie katika matayarisho ya mipango na bajeti zao kwa mwaka 2009/2010, na kujadiliwa na Kamati ya Fedha ya Halmashauri husika na hatimaye kupitishwa na Baraza la Madiwani. Hivyo, Bajeti za Mikoa zimetengewa jumla ya Shilingi bilioni 83.55 zitakazopelekwa kwenye Halmashauri kutokana na Mfuko wa Pamoja wa *ASDP (ASDP- Basket Fund)*. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 78.56 fedha za nje na Shilingi bilioni 4.998 ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya kiasi hicho cha fedha za nje, mradi wa *DASIP* utachangia Shilingi bilioni 17.4. Aidha, Sekretariati za Mikoa nazo zimetengewa jumla ya Shilingi bilioni 2.52 kwa ajili ya kusimamia, kuratibu na kununua vitendea kazi yakiwemo magari.

Wizara za Sekta ya Kilimo zimetengewa jumla ya Shilingi bilioni 52 za Mfuko wa Pamoja wa *ASDP* na kati ya fedha hizo, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika imetengewa Shilingi bilioni 21.9. Kazi zitakazotekelezwa kupitia Mfuko huo wa Pamoja wa ASDP ni kama ifuatavyo:

i. Kuimarisha na kuwezesha Timu ya Taifa ya Uwezeshaji kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa *DADPs*;
ii. Kuendelea kuzijengea uwezo Sekretariati za Mikoa na kutengewa fedha kwa ajili ya kununua vitendea kazi vikiwemo vyombo vya usafiri ili waweze kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa *DADPs*;
iii. Kuangalia uwezekano wa kuwa na Waratibu wa Programu katika Kanda saba za utafiti;
iv. Kuboresha Mwongozo wa mipango na utekelezaji wa *DADPs*;
v. Kuimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini shirikishi;
vi. Idara za Wizara na Bodi za Mazao kuainisha miradi na kazi ambazo zimewekwa katika mipango ya *DADPs* na kuiwekea utaratibu wa kuifuatilia pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam *(Technical backstopping)* ili kuhakikisha utekelezaji wa malengo hayo;
vii. Kuziwezesha Halmashauri kuandaa taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka kwa kuzingatia maeneo ya utekelezaji *(Sub-components)* wa Programu ngazi ya Wilaya ambazo ni uwekezaji, utoaji wa huduma za ugani na utafiti, kujenga uwezo wa wakulima na watendaji;

viii. Kuendelea kuzielekeza Halmashauri kuandaa mpango wa kutekeleza *DADPs* kwa awamu kwa kutoa mwongozo kwa Halmashauri jinsi ya kuchagua vijiji vichache vitakavyotekeleza *DADPs* (awamu ya kwanza, pili na kuendelea);
ix. Kuwezesha vijiji vya awamu ya kwanza kuibua miradi michache itakayowezesha kijiji kuongeza tija na uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo na miradi ya kuongeza kipato; na

x. Kuwezesha vijiji kuwa na andiko la mradi lililochambuliwa kwa vigezo vya faida kifedha, kiuchumi na kijamii na kupatiwa mafunzo ya kilimo cha kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia mradi wa *DASIP* imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Kuendelea kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya 28 wa kuibua, kupanga na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Vijiji (*VADPs*) na Wilaya (*DADPs*) yenye ubora unaokubalika;
ii. Kutoa mafunzo mbalimbali kwa Wakulima na wataalam wa kilimo na mifugo ili kuwapatia maarifa na utaalam wa kuendesha kilimo bora cha mazao na mifugo. Aidha, mafunzo ya uimarishaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo pamoja na utafiti wa masoko kwa mazao ya kilimo na mifugo yatatolewa kwa wataalam na wakulima;
iii. Kuziwezesha Halmashauri za Wilaya na jamii kuibua na kutekeleza miradi ya jamii *(village micro projects)* na miradi ya kati *(Medium Size Infrastructure Projects)*;
*iv.* Kufanya Mapitio ya utekelezaji wa Mradi *(Mid Term Review);*
*v.* Kuwezesha utekelezaji wa miradi ya vikundi *(Participatory Farmer Group Mini project);* na
vi. Kuimarisha *SACCOS* na mifumo ya masoko katika eneo la miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*PADEP*), umepanga kutekeleza majukumu muhimu yafuatayo:-

i. Kuwezesha Halmashauri za Wilaya kutoa utaalamu na mafunzo ya kilimo cha kibiashara kwa walengwa kwa lengo la kuhakikisha uendelevu wa miradi ya jamii na vikundi iliyoanzishwa;
ii. Kuwezesha mafunzo rejea kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa *DADPs* katika ngazi ya jamii;
iii. Kuwezesha timu ya wawezeshaji ya Taifa kutoa ushauri (*backstopping*) na mafunzo juu ya utekelezaji wa *DADPs*;
iv. Kuendelea kuandaa vipindi vya televisheni na redio;
v. Kuhuisha uzoefu wa utekelezaji wa mradi katika *ASDP* kupitia timu ya Taifa ya uwezeshaji ya *ASDP*;
vi. Kutayarisha na kuweka kumbukumbu na machapisho kuhusu uzoefu wa utekelezaji shughuli za maendeleo ya kilimo na mifugo kwa kutumia mbinu shirikishi;
vii. Kufanya tathmini ya mwisho *(Terminal Evaluation)* na tathmini ya manufaa ya mradi *(Impact Assessment)*; na

viii. Kuratibu shughuli za kukamilisha mradi ngazi ya Wilaya na kutayarisha taarifa ya kukamilisha utekelezaji wa mradi *(Implementation Completion Report)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na wadau wengine, katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima. Dhana ya Shamba Darasa itaendelea kuenezwa kwa kutumia Wakulima Wawezeshaji na Wagani Kazi ambayo imeonyesha kuwa na mafanikio makubwa katika maeneo ambayo inatekelezwa. Ili kufanikisha lengo hilo, wataalam wa ugani katika ngazi ya Kata watapewa jukumu la kufungua mashamba darasa katika ngazi ya Kitongoji. Halmashauri za Wilaya zimeelekezwa kuwapatia wataalam hao katika ya ngazi ya kata pikipiki na kuwapangia ratiba

ya kazi ili waweze kuwafikia wakulima katika ngazi za vijiji na vitongoji kwa urahisi. Katika mwaka 2009/2010 jumla ya magari 6, pikipiki 403, baiskeli 182 zitanunuliwa kupitia DADPs kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma kwa wakulima na wafugaji. Aidha, Vituo vya Rasilimali vya Kilimo na Mifugo *(Ward Agricultural Resource Centres)* 141 vitajengwa katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kuhakikisha wataalam wa ugani wanajengewa nyumba za kuishi kwa awamu. Katika mwaka 2009/2010 jumla ya nyumba 58 zitajengwa kupitia *DADPs*. Pia Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wakulima kupitia vijitabu, machapisho, vipeperushi na mabango kwa kuzingatia kanda za kilimo kupitia ofisi Kiungo za Mawasiliano za Kanda. Jumla ya wakulima 53,500 watapatiwa mafunzo mbalimbali kupitia utaratibu huo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko itawaunganisha wakulima na fursa za masoko zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, itasimamia viwango vya utoaji wa huduma hizo na kuajiri wahitimu kutoka kwenye vyuo vya mafunzo ya kilimo ili kukabiliana na upungufu wa wataalam wa ugani vijijini; kuratibu mashindano ya Kilimo na maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nane Nane na Siku ya Chakula Duniani na kuzishirikisha na kuziwezesha sekta binafsi na asasi zisizokuwa za kiSerikali kujenga uwezo wa kutoa huduma za ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upatikanaji wa Pembejeo na Zana za Kilimo. Mahitaji ya mbolea nchini yanakadiriwa kuwa tani 385,000 kwa mwaka. Wizara inatoa wito kwa sekta binafsi kuingiza nchini mbolea kwa wingi ili wakulima waweze kuzipata wanapozihitaji. Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Mradi wa kuongeza usalama wa chakula chini ya mkopo wa Benki ya Dunia itatumia jumla ya Shilingi bilioni 118 katika mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo ambapo Shilingi bilioni 60 ni kupitia fedha za maendeleo chini ya mradi mpya wa Kuongeza Usalama wa Chakula *(Accelerated Food Security Project – AFSP)* na Shilingi bilioni 58 kupitia fedha za matumizi ya kawaida. Wakulima watakaonufaika na mpango wa ruzuku kwa utaratibu wa vocha wataongezeka kutoka 737,000 mwaka 2008/2009 hadi 1,500,000 mwaka 2009/2010. Mpango huo wa ruzuku unakadiriwa kuhusisha usambazaji wa tani 150,000 za mbolea. Aidha wakulima 121,011 watanufaika na ruzuku ya mbegu za mtama na alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea katika Mikoa 20 inayozalisha mazao ya mahindi na mpunga. Mikoa hiyo ni Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Morogoro, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Manyara (Wilaya zote), Tabora (Wilaya za Sikonge na Urambo), Mara (Wilaya za Tarime na Serengeti), Shinyanga (Wilaya za Kahama na Bukombe), Singida (Singida Vijijini na Manyoni), Dodoma (Bahi na Mpwapwa), Tanga (Korogwe, Lushoto na Muheza), Pwani (Bagamoyo), Lindi (Lindi), Mtwara (Mtwara), Kagera ( Karagwe na Chato) na Mwanza (Geita na Sengerema). Aidha, skimu zote za umwagiliaji zitapatiwa ruzuku ya pembejeo. Ruzuku itatolewa kwa mbolea za *DAP*, Minjingu na *UREA* na wakulima watakuwa na fursa ya kuchagua aina ya mbolea ya kupandia kati ya Minjingu na *DAP*. Aidha, Wizara itaendelea kutoa ushauri kuhusu matumizi ya aina hizo za mbolea kulingana na hali ya udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaimarisha utoaji wa ruzuku ya pembejeo kwa kutumia mfumo wa vocha; kutoa mafunzo na kuimarisha mtandao wa mawakala wa pembejeo za kilimo *(Rural Agro-dealers)* ili kuongeza upatikanaji, usambazaji na matumizi ya pembejeo za kilimo. Vilevile, Wizara itakamilisha kanuni na mwongozo wa Sheria ya Mbolea na kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Matumizi Bora ya Mbolea Tanzania *(Tanzania Fertilizer Regulatory Authority).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko na Kituo cha Uwekezaji *(Tanzania Investment Centre –TIC),* inaendelea kutafuta wawekezaji watakaowekeza katika ujenzi wa viwanda vya mbolea. Jumla ya makampuni 10 yamejitokeza kutaka kujenga viwanda vya mbolea hapa nchini. Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko inaendelea na uchambuzi wa kupata kampuni iliyo mahiri katika uzalishaji wa mbolea na itakayozalisha mbolea kwa gharama nafuu.

Aidha, kiwanda cha Minjingu pamoja na kuzalisha mbolea ya *phosphate* ya chengachenga (*granulated*) kitaanza kuzalisha mbolea ya "Minjingu Mazao" ambayo imeboreshwa na viinilishe vya Naitrojeni, salfa, zinc, shaba na boron.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutoa ruzuku ya pembejeo za mazao ya pamba na korosho. Zao la pamba litapata ruzuku ya mbegu bora tani 10,000 na madawa acrepacks 3,150,000 kwa ajili ya ekari 1,000,000 za pamba. Utoaji wa ruzuku kwa zao hilo utafanyika kwa utaratibu wa vocha. Aidha, zao la korosho litapata ruzuku ya madawa lita 64,000 na tani 3,000 za madawa ya unga zitasambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutoa ruzuku ya mbegu bora za mahindi tani 13,599, mtama tani 290, mpunga tani 2,102 na alizeti tani 85.4. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha makampuni binafsi kuendelea kuzalisha mbegu bora. Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo *(Agricultural Seed Agency-ASA)* itashirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Magereza na mashamba ya Serikali kuongeza uzalishaji na uenezaji wa mbegu bora nchini kufikia tani 3,000 za nafaka, mikunde, mbegu za mafuta na mboga mboga. Wizara itaendelea kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya mbegu ya Serikali ili kuwa na uhakika wa kuzalisha mbegu hizo kwa ajili ya matumizi ya misimu yote. Aidha, Wizara itaimarisha uwezo wa wakulima wadogo kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa *(Quality Declared Seed – QDS);* kujadili na kupitisha aina mpya za mbegu kwa ajili ya matumizi ya wakulima; kuongeza matumizi ya miche bora ya kahawa kufikia miche 13,000,000 kutoka miche 10,000,000 ya mwaka 2008/2009 na miche bora ya chai 12,000,000 mwaka 2009/2010 kutoka miche 10,000,000 mwaka 2008/2009. TRIT watazalisha miche 9,150,000 kutoka miche 8,047,300 mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, inakadiriwa kuwa mahitaji ya matrekta nchini ni kati ya 1,500 na 1,800. Ili kuongeza upatikanaji wake, Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 12.8 ili kuziwezesha Halmashauri za Wilaya kununua matrekta madogo ya mkono 1,628 na matrekta makubwa 55 kupitia *DADPs*. Matrekta hayo yatatolewa kwa wakulima kwa utaratibu wa uchangiaji wa asilimia 20 ya gharama kama unavyoelekeza Mwongozo wa *DADPs*. Aidha, Serikali imesaini mkataba na Serikali ya India wa kupata mkopo wenye masharti nafuu *line of credit* wa Dola za Kimarekani milioni 40 ili kuwezesha kuingiza kutoka India matrekta 1,000 na zana zake pamoja na pampu za kusukuma maji kwa ajili ya umwagiliaji. Kadhalika, wakulima watawezeshwa kupata zana bora za kilimo kupitia mikopo nafuu itakayotolewa na Benki ya Rasilimali *(Tanzania Investment Bank).* Aidha, Shilingi bilioni 20 zitatolewa na Serikali kwa ajili ya kutoa mikopo ya riba nafuu kwa zana za kilimo kupitia mpango wa karadha *(lease financing).* Wizara itahamasisha sekta binafsi kutumia fursa zilizopo za mikopo ili kuanzisha vituo vya kukodisha zana za kilimo kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya matrekta na zana zinazokokotwa na wanyamakazi, Maafisa Ugani 50 kutoka katika Halmashauri za Wilaya 30 watapatiwa mafunzo ili waweze kutoa ushauri wa kiufundi kwa wakulima, kuwawezesha kuendesha kilimo cha kibiashara. Wizara pia itaendelea kufanya tathmini ya matumizi ya

matrekta na zana zake ili kutoa ushauri wa kifundi katika kuchagua matrekta na zana zake kufuatana na mazingira na hali ya udongo. Aidha, katika kuongeza tija ya uzalishaji wa zao la mpunga, Wizara itatoa mafunzo ya uzalishaji mpunga kwa wakulima viongozi 400 katika skimu 40 za umwagiliaji na kuzipatia matrekta ya mkono 40 ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kuhusu uendeshaji kibiashara wa huduma za kukodisha zana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pembejeo, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo utaendelea kutoa mikopo nafuu kwa ajili ya kununua matrekta makubwa 115 na matrekta madogo ya mkono 110 yenye thamani ya Shilingi bilioni 5.86. Aidha, Mfuko utatoa mikopo kwa ajili ya kusambaza pembejeo za kilimo na mifugo. Mfuko pia umepanga kukusanya marejesho ya mikopo iliyoiva yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.8 ambazo zitatumika kutoa mikopo ya pembejeo za kilimo na mifugo pamoja na zana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Kushirikisha Vijana katika Kuendeleza Kilimo, vijana ni sehemu muhimu ya jamii na wanachangia zaidi ya asilimia 60 ya nguvukazi ya Taifa. Vijana wanashiriki katika sekta nyingi kama vile kilimo, ufugaji, madini, uvuvi, ujenzi, na biashara hivyo kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa. Hata hivyo, vijana wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa ajira, mitaji ya kujiendeleza, elimu ndogo na matumizi ya zana duni. Hii inasababisha vijana wengi kukimbilia mijini kutafuta ajira na kuendelea kupunguza nguvukazi katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaviwezesha vikundi vya kilimo vya vijana katika Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Pwani, Tabora, Singida, Morogoro, Dodoma, Tanga, Mara, Mwanza na Manyara katika nyanja zifuatazo;

i. Mafunzo ya kuainisha na kuibua miradi ambayo itaweza kuingizwa katika *DADPs*.

ii. Mafunzo ya stadi na mbinu bora za kilimo, ujasiriamali, ushirika, matumizi ya zana, usindikaji, hifadhi na matumizi bora ya ardhi, utunzaji wa mazingira, uendeshaji na uimarishaji vikundi pamoja na mbinu za masoko;

iii. Kuwawezesha kupata ardhi kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo; na

iv. Kuvijengea uwezo wa kuunda ushirika imara ili kuweza kupata mitaji ya kuendesha shughuli za uzalishaji na kupata masoko ya uhakika wa mazao;

Wizara kwa kushirikiana na Mpango wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa *(One UN Joint Programme)* pamoja na Mikoa ya Lindi na Mtwara itaendeleza programu ya kushirikisha vijana katika kuendeleza kilimo cha kibiashara katika mazao ya muhogo na korosho. Kwa hatua ya awali, Wizara itaviwezesha na kuviimarisha vikundi 35 vya vijana katika Mikoa hiyo kwa kuvipatia matrekta madogo ya mkono 35 na seti 20 za mashine za kusindika muhogo *(chipper, grater, presser* na *milling* machine). Wizara inatoa wito kwa Halmashauri kuviwezesha vikundi vya vijana vya kilimo kwa kuvipatia zana bora kama vile matrekta madogo ya mkono yatakayonunuliwa kwa mpango wa kuchangia asilimia 20 ya gharama na kuwasaidia kuibua miradi mingine ya kujiendeleza kupitia *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kubuni teknolojia bora za uzalishaji wa mazao mbalimbali zinazolenga kumwezesha mkulima kupata mavuno mengi na kuongeza tija, na hivyo kumuongezea kipato na kumpunguzia umaskini. TRIT itaendelea na utafiti wa chai, *TACRI* utafiti wa kahawa, TORITA utafiti wa tumbaku na TPRI itafanya tafiti mbalimbali zikiwemo tafiti za viuatilifu. Aidha, utafiti wa zao la mahindi utafanyika katika Vituo vya Utafiti vya Uyole, Selian, Ilonga na Ukiriguru; Mpunga-

KATRIN, Dakawa, Ukiriguru na Uyole; Mtama na Uwele- Ilonga na Hombolo; Ngano, - Uyole na Selian. Vilevile utafiti wa mazao jamii ya mikunde utafanyika katika Vituo vya Utafiti vya Uyole, Selian, na Ilonga; utafiti wa mazao jamii ya mizizi utafanyika katika vituo vya Ukiriguru, Kibaha, Naliendele, Uyole na Maruku. Pia utafiti wa zao la Ufuta na Karanga utafanyika Naliendele, na Alizeti utafanyika Ilonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao mengine yatakayofanyiwa utafiti ni pamoja na minazi (Mikocheni), korosho (Naliendele), zabibu (Makutupora), mkonge (Mlingano), pareto (Uyole), sukari (Kibaha) na pamba (Ukiriguru na Ilonga). Tafiti hizo zitalenga katika kuzalisha aina bora za mbegu zenye sifa za kuzaa kwa wingi, ukinzani dhidi ya magonjwa na wadudu na kustahimili ukame, zenye sifa zinazokubalika na wadau na kukidhi mahitaji ya soko. Vilevile, Wizara inatarajia kutoa angalau aina 7 za mbegu bora kwa mazao ya nafaka, jamii ya mikunde, mboga mboga na matunda na kuendelea na utafiti wa bioteknolojia. Aidha, Kituo cha Taifa cha Nasaba za Mimea *(National Plant Genetic Resource Centre – NPGRC)* kilichopo TPRI Arusha, kitaendelea kutafiti na kukusanya mimea iliyopo nchini kwa lengo la kutunza nasaba hizo kwa ajili ya matumizi ya watafiti katika kuzalisha aina bora za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa mazao ya mboga, matunda na viungo utafanyika kwenye vituo vya Utafiti vya Tengeru, KATRIN, Maruku na Uyole kwa lengo la kupata vipando bora. Teknolojia bora zinazotokana na utafiti huo zitasambazwa kwa wadau kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, msisitizo utawekwa katika kutunza na kuzalisha mbegu mama *(breeder seed)* zipatazo tani 100 kwa mazao ya jamii ya nafaka, mafuta na mikunde. Vipingili na miche ya mbegu bora 4,000,000 vya mazao ya muhogo, viazi vitamu, viungo, migomba, zabibu vitazalishwa. Aidha, tathmini itafanyika ili kuendelea kuboresha na kutoa teknolojia angalau moja ya usindikaji na kuongeza thamani za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kubuni na kutathmini teknolojia bora za matengamano ya udhibiti visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao na kutathmini madawa ya asili ya viwandani yanayofaa kutumika bila kuathiri mazingira na kwa gharama nafuu. Kwa mfano, miti hiyo ni aina ya Dudupala *(Neorautanenia mitis)*, Girigirimo (*Crotalaria spp*) na Muarobaini (*Azadirachta Indica*).

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa udongo, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Kituo cha Utafiti cha Mlingano, itaendelea kuboresha ramani za rasilimali kilimo kwa kutumia teknolojia ya *Geographical Information System (GIS)* kwa ajili ya kuainisha maeneo yanayofaa kwa uwekezaji katika Mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Lindi, Mtwara na Tanga. Wizara kupitia Kituo cha Mlingano itaendelea kuandaa ramani za rasilimali kilimo katika Wilaya za Mvomero, Kilosa na Morogoro Vijijini ili kuainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha mpunga na mahindi. Kazi hiyo inafanyika kwa kuzingatia mkakati maalum wa kuufanya mkoa wa Morogoro kuwa ghala la Taifa (Fanya Morogoro Ghala la Taifa- FAMOGATA). Vilevile, Wizara itasambaza jarida la mapendekezo ya mbolea kulingana na ekolojia za kilimo kwa nchi nzima. Uhakiki wa matumizi ya mbolea ya Minjingu Mazao utaendelea katika Kanda za Mashariki, Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini. Aidha, jumla ya sampuli za udongo 5,000 zitachunguzwa na kutolewa ushauri kuhusu virutubisho vinavyopaswa kuongezwa kwenye udongo ili kuongeza uzalishaji. Wizara katika mwaka 2009/2010, inatarajia kutoa angalau teknolojia 2 za hifadhi ya rutuba ya udongo na hifadhi ya ardhi, teknolojia moja ya uvunaji wa maji na moja ya zana bora za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafiti wa Mifumo ya Kilimo na Uchumi Sayansi Jamii *(Farming Systems Research and Socio-economics).* Katika mwaka 2009/2010, Wizara

itaendelea kufanya tafiti za sayansi jamii na uchumi kuhusu matatizo yanayoathiri uenezaji mzuri wa teknolojia za kilimo. Tafiti hizo zitafanywa katika Kanda za Kaskazini, Mashariki, Nyanda za Juu Kusini na Ziwa. Aidha, Wizara itaendelea kutayarisha taarifa za uzalishaji wa mazao makuu (*farm budgets)* kwenye kanda zote kwa kutumia bei mpya za mazao hayo na za pembejeo mbalimbali ili zitumike kufahamisha wakulima gharama za uzalishaji na faida inayopatikana kwa kila zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itafanya tathmini ya matokeo ya tafiti *(impact studies)* kwa wakulima na pia kuchambua matatizo yao kwa kutumia mbinu shirikishi *(Participatory Rural Appraisal-PRA)* kwenye kanda zote saba za utafiti. Aidha, Wizara itatoa mafunzo ya wiki moja kwa watafiti wachumi kilimo kutoka kanda zote za utafiti ili kuboresha taaluma yao. Wizara pia itaendelea na juhudi za kuunganisha mfumo wa Utafiti wa Taifa na Mifumo ya Miradi/Taasisi zingine za utafiti nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kuboresha mazingira ya kufanyia kazi watafiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kukarabati kwa awamu nyumba za kuishi wafanyakazi wa vituo vya Maruku (4), Makutupora (2), Naliendele (2), Ukiriguru (2), Tumbi (5), Ilonga (4) na Selian itajengwa nyumba mpya 1. Aidha, ukarabati wa mifumo ya maji katika vituo vya Ukiriguru, Tumbi na Mlingano utakamilishwa. Vilevile, barabara ya kilometa 2 kutoka barabara kuu ya Dar es Salaam - Tunduma kwenda Kituo cha Utafiti Uyole itafanyiwa matengenezo. Wizara itanunua magari 8 ambayo yatasambazwa katika vituo vya KATRIN (2), Ukiriguru (2), Mlingano (2), Naliendele (1) na Ilonga (1). Vilevile kompyuta 70 zitanunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya watafiti 32 wataendelea kupata mafunzo ya muda mrefu na 6 wapya wa Shahada ya Uzamili (MSc.) wataanza masomo. Hivyo, mwaka 2009/2010, Wizara itafadhili jumla ya watafiti 38 ambao ni wa Shahada ya Uzamivu (PhD.) 10, Uzamili (MSc.) 7 na Shahada (BSc.) 21. Watafiti na watumishi wengine wapatao 300 watapatiwa mafunzo mbalimbali ya muda mfupi katika fani zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya mfumo wa usimamizi wa rasilimali na utafiti unaowalenga wadau yaani *Client-Oriented Research Development and Management Approach (CORDEMA),* Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watafiti katika vituo 16 vya utafiti ili kuwajengea uwezo wa kuandaa na kutekeleza tafiti zenye kutatua mahitaji yanayotokana na vipaumbele vya Kanda na wadau wake pamoja na kusimamia rasilimali za utafiti ili kuleta ufanisi katika uzalishaji wa teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuboresha Mifuko ya Kanda ya Utafiti *(Zonal Agricultural Research and Development Fund- ZARDEF),* kwa madhumuni ya kufanya tafiti za kilimo zinazolenga kutoa teknolojia sahihi za kutatua matatizo ya uzalishaji kulingana na vipaumbele vya kanda. Jumla ya tafiti 88 zitafanyika katika kanda zote saba ikiwa ni pamoja na kupitisha miradi mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Vitengo Unganishi vya Utafiti na Ugani *(Zonal Information Education Liaison Units – ZIELU)* vitaimarisha mbinu za kusambaza teknolojia kwa kutumia nyenzo rahisi za kufikisha ujumbe kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kutoa vipeperushi vya aina za teknolojia 28 katika kanda saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kuanzisha Kituo cha Utafiti wa Ubora wa Hali ya Juu *(Rice Centre of Excellence)* wa zao la mpunga utatekelezwa chini ya Programu ya Kilimo ya Kuendeleza Tija na Uzalishaji katika Afrika ya Mashariki *(Eastern Africa*

*Agricultural Productivity Programme).* Mradi huo utatoa msukumo wa pekee wa kubuni na kuendeleza teknolojia za mpunga na kuhakikisha kuwa zinatumiwa na walengwa kwa wingi nchini na katika nchi za Afrika Mashariki na Kati ambazo ni wanachama wa Taasisi ya Kuimarisha Utafiti wa Kilimo Afrika Mashariki na Kati (*Association for Strengthening Agricultural Research in East and Central Africa – ASARECA).* Kituo cha Utafiti cha KATRIN – Ifakara ndicho kitakachoongoza na kuratibu shughuli za utafiti kikishirikiana na vituo vyote vya utafiti katika kanda saba za utafiti, vyuo vya mafunzo ya kilimo na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Lengo ni kukipandisha hadhi kituo cha utafiti wa mpunga cha KATRIN ili kiwe na hadhi ya kituo cha utafiti wa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati *(Regional Centre of Excellence).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itatekeleza Mradi wa Kuongeza Rutuba ya Udongo *(Integrated Soil Fertility Management)* unaolenga kuleta tija endelevu katika kilimo kwenye skimu za umwagiliaji maji *(Small Scale Irrigation Schemes)* ikiwa ni mkakati wa kuongeza uzalishaji wa chakula kwa kushirikiana na Mradi wa Usalama wa Chakula *(Accelerated Food Security Project –ASFP).* Kituo cha utafiti cha Mlingano kitaratibu shughuli za mradi kwa kushirikiana na vituo vya utafiti katika Kanda na Halmashauri za Wilaya. Lengo la mradi ni kupata teknolojia zenye matengamano ya rutuba ya udongo *(Integrated Soil Fertility Management Options)* kwa kila ekolojia za kilimo zilizoko katika Wilaya 60. Wilaya hizo zimeteuliwa kwa vile zinapata ruzuku ya mbolea kwa mfumo wa vocha na ziko kwenye mpango wa kuanzisha na kuimarisha skimu za umwagiliaji maji mashambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafunzo ya Kilimo kwa Wataalam, Wizara itafundisha wanafunzi 2,400 na kufadhili wanafunzi 1,998 katika mafunzo kwa vitendo *(field attachment);* kufadhili wakufunzi 10 katika shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu ili kuinua viwango vyao vya elimu na kuandaa mafunzo ya muda mfupi *(refresher / upgrading courses)* kwa wakufunzi 40 na kuandaa mitaala mipya miwili ya programu za mafunzo. Aidha, vyuo vya mafunzo vya KATC Moshi, Igurusi, Ilonga na Ukiriguru vitawezeshwa kupanua na kutoa mafunzo ya umwagiliaji kwa wakulima katika skimu 40 za umwagiliaji katika kanda nne zenye skimu za umwagiliaji. Pia vyuo vingine vitakarabatiwa na kuboresha samani, vitendea kazi, vifaa na nyenzo za kufanyia kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao ya kilimo. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itakamilisha mapendekezo ya kuhuisha Sheria ya Visumbufu vya Mimea *(Plant Protection Act 1997)* ili kuifanya iendane na wakati. Aidha, Wizara itaimarisha uwezo wake wa kusimamia utekelezaji wa Sheria hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wakaguzi ili kutoa huduma bora kwa wakulima na wasafirishaji wa mazao kwa kuzingatia viwango vya usafi wa mazao kwa ajili ya soko la ndani na nje. Wizara pia itaendelea kushirikiana na Serikali za Mitaa na taasisi mbalimbali yakiwemo mashirika ya kimataifa ya udhibiti wa Nzige katika kukagua maeneo ya mazalio ya visumbufu na kuwadhibiti mapema ili kuokoa mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaimarisha huduma ya utabiri wa viwavi jeshi kwa kukarabati mitego 100 ya nondo na mfumo wa kompyuta unaotumika kutabiri. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kuanzisha na kuendeleza matumizi ya mbinu za udhibiti husishi wa visumbufu vya mimea ambazo ni za gharama nafuu na salama kwa wakulima na mazingira. Vilevile, uchunguzi na udhibiti wa gugumaji, ugonjwa wa migomba wa kunyauka *(Banana bacterial wilt),* batobato kali ya muhogo na nzi wa matunda utaendelezwa. Aidha, utafiti wa kutafuta wadudu walawangi ambao ndiyo njia ya kudumu katika kumdhibiti nzi wa matunda utaendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa mazao ya kilimo, uzalishaji wa mazao makuu asilia ya biashara, Wizara kupitia Bodi za Mazao ya Kahawa, Pamba, Tumbaku, Pareto, Korosho, Sukari na Mkonge itasimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia uzalishaji na biashara ya mazao hayo nchini.

Aidha, ili kuhakikisha tija na uzalishaji wa mazao hayo inaongezeka kwa mujibu wa malengo ya Kitaifa, kimkoa na kiWilaya, Wizara itashirikiana na Mikoa pamoja na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa miradi ya kuendeleza mazao hayo ikiwa ni pamoja na kuyaongezea thamani *(Rural Agro-Processing)* kupitia miradi ya usindikaji iliyoibuliwa chini ya *DADPs*. Hivyo, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara katika mwaka 2009/2010 unatarajia kuongezeka kwa viwango tofauti kama ifuatavyo:-.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa sukari unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 279,850 hadi tani 300,000. Ongezeko hilo litatokana na kuongeza uzalishaji wa sukari kupitia viwanda vidogo, kuongezeka kwa tija na uzalishaji wa miwa ya sukari kutoka wakulima wadogo na kuimarisha utaratibu wa kilimo cha mkataba kwa wakulima walio karibu na kampuni za sukari za Kagera, Mtibwa na Kilombero chini ya utaratibu wa kuunganisha mashamba yao ili yalimwe kwa utaratibu wa mashamba makubwa *(Block Farming)*. Utaratibu huo utarahisisha upatikanaji wa huduma za ugani, pembejeo, uvunaji na usafirishaji wa miwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa tumbaku unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 58,702 hadi tani 60,000. Ongezeko hilo litatokana na kuwajengea uwezo wakulima kuzingatia kanuni bora za kilimo cha tumbaku, kuwapatia wakulima mbegu bora za tumbaku, ujenzi wa mabani mapya 10,000 ya kukaushia tumbaku ili kuongeza ufanisi wa ukaushaji na kupunguza uharibifu wa majani baada ya mavuno. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wa tumbaku kuhakikisha wakulima wanapata bei nzuri ya tumbaku kwa kuhakikisha unakuwepo ushindani katika ununuzi wa tumbaku nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa chai unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 34,165 hadi tani 35,000. Ongezeko hilo litatokana na kuimarisha upatikanaji wa miche bora ya chai kupitia vikundi vya wakulima, kuendelea kwa ufufuaji wa mashamba ya chai yaliyotelekezwa, kutoa mafunzo juu ya kilimo bora cha chai, hususan kwa wakulima wadogo; kuimarisha ukaguzi katika mashamba ya chai na kuhakikisha kuzingatiwa kwa kanuni bora za uzalishaji wa chai. Aidha, utaratibu wa kuwatumia wataalam waliobobea wa huduma za ugani katika zao la chai utaimarishwa *(commodity specific extension services)* na kuhamasisha uanzishaji wa mashamba ya chai katika maeneo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa pareto unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 3,280 hadi tani 4,800. Ongezeko hilo litatokana na kuwafundisha wakulima mbinu za kilimo bora cha pareto, kuzalisha na kusambaza tani 20 za vikonyo vya mbegu bora za pareto na kuwajengea uwezo wakulima kupunguza upotevu wa maua ya pareto baada ya mavuno kwa kufundisha mbinu bora za ukaushaji wa pareto.

Mkonge

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mkonge unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 33,208 hadi tani 35,000. Ongezeko hilo litatokana na kuendelea kuongezeka kwa uzalishaji unaotokana na upanuzi wa mashamba katika misimu ya nyuma, kuanza kwa uvunaji wa mkonge wa wakulima wadogo katika Mikoa ya kanda ya Ziwa na kuwawezesha wakulima wadogo kupata mashine za kukobolea mkonge. Aidha, Bodi ya Mkonge itaendelea kusimamia usafi wa mashamba ili kuhakikisha tija na uzalishaji katika mashamba ya mkonge unaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa korosho unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 79,069 hadi tani 100,000. Ongezeko hilo litatokana na kuhimiza udhibiti wa viatilifu vya mikorosho kwa wakati unaotakiwa, kuhakisha upatikanaji wa viuatilifu vya visumbufu vya mikorosho katika wakati unaotakiwa, kuendelea kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mikorosho na kuhimiza ufufuaji wa mashamba ya korosho yaliyotelekezwa. Bodi ya Korosho itaratibu upandaji wa mikorosho mipya na kubebesha mikorosho ya zamani. Wakulima watahimizwa kuibua miradi ya mikorosho kupitia *DADPs* ikiwa ni pamoja na miradi ya uanzishwaji wa viwanda vidogo vya ubanguaji wa korosho katika Halmashauri. Aidha, mfumo wa matumizi ya stakabadhi ya mazao ghalani utatumika katika Mikoa yote inayolima korosho nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa pamba utarajiwa kupungua kutoka tani 368,229 hadi tani 250,000. Upungufu huo utasababishwa na kupungua kwa eneo lililopandwa pamba katika msimu wa 2008/2009 kutokana na baadhi ya wakulima ama kupunguza maeneo ya uzalishaji au kusitisha uzalishaji kulikosababishwa na kushuka kwa bei ya pamba katika msimu huu wa ununuzi wa 2008/2009. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuwahimiza wakulima wa pamba kuendelea kuzalisha pamba kwa kupanua kilimo cha mkataba, kutoa ruzuku ya viuatilifu na mbegu bora za pamba, kuendelea kuwafundisha wakulima kanuni bora za pamba kwa kutumia mbinu shirikishi ya Shamba Darasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa kahawa unatarajiwa kushuka kutoka tani 62,345 hadi tani 50,000. Kushuka kwa uzalishaji kutasababishwa na tabia ya mikahawa kupunguza uzalishaji katika msimu unaofuata msimu uliozalisha kahawa kwa wingi. Hata hivyo, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TaCRI) kuzalisha na kusambaza miche bora ya kahawa milioni 13, kuendelea kuhimiza matumizi ya mitambo midogo ya kumenya kahawa mbichi vijijini kupitia *DADPs*, kupanua eneo lililopandwa mikahawa bora yenye ukinzani dhidi ya visumbufu vya kahawa, na kuhimiza unywaji wa kahawa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzalisha chakula kwa wingi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya nchi na kuuza ziada nje, Wizara ikishirikiana na Mikoa na Halmashauri za Wilaya inatekeleza Mkakati wa kuzalisha mazao ya chakula kulingana na ekolojia za kilimo na fursa za upatikanaji wa masoko. Mkakati huo unazingatia kuongeza matumizi ya pembejeo za kilimo hususan mbegu bora, mbolea na zana bora. Mkakati huo unazingatia kuongeza uzalishaji wa mahindi katika maeneo yenye uhakika wa upatikanaji wa mvua kuongeza tija na uzalishaji katika skimu za umwagiliaji katika maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kuendeleza kilimo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itahimiza uzalishaji wa mazao yanayostahimili ukame, hususan mtama, muhogo, viazi vitamu na mikunde katika maeneo yanayokabiliwa mara kwa mara na upungufu wa mvua. Aidha, wakulima wataelimishwa mbinu bora za hifadhi ya mazao kabla na baada ya mavuno, kukadiria mahitaji ya chakula katika kaya na upatikanaji wa masoko ya mazao yao. Kutokana na mikakati hiyo, uzalishaji wa chakula unatazamiwa kufikia tani milioni 11.5 katika mwaka 2009/2010 kutoka tani milioni 10.9 zilizozalishwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa mazao ya bustani, hususan katika kuongeza kipato kwa wakulima katika msimu wa 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Wadau wa Mazao ya Bustani Tanzania *(Horticultural Development Council of Tanzania – HODECT)* itaandaa Mkakati na Programu ya Kuendeleza Kilimo cha Mazao ya Bustani Tanzania. Katika Mkakati na Programu hiyo, maeneo yote yaliyo na uwezekano mkubwa wa kuzalisha mazao hayo yataainishwa, fursa maalum kama ukaribu na walaji, masoko, viwanda vya usindikaji au miundombinu ya usafirishaji zitaainishwa na mpango wa

kuzalisha mazao kulingana na fursa hizo utaandaliwa kwa lengo la kutumika kuwahimiza wakulima kutumia fursa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, wakulima katika Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara watashauriwa kuendeleza kilimo cha mazao ya matunda, hususan maembe kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko na viwanda vilivyopo Dar es Salaam. Wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa watahimizwa kuzalisha mazao ya mboga na matunda kama matofaa na maparachichi kwa ajili ya soko la ndani na nje. Aidha, wakulima wa Kanda ya Kati watahimizwa kuzalisha zabibu kwa ajili ya mahitaji ya viwanda vya mvinyo au soko la zabibu tamu kwa ajili ya soko la ndani na la nchi jirani. Fursa za kuwepo kwa viwanja vya ndege kwenye maeneo hayo zitatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha wakulima wanapata vipando bora vya mazao ya matunda na bustani, Wizara kupitia Wakala wa Mbegu wa Taifa *(Agricultural Seed Agency – ASA)* itajenga maeneo maalum ya kisasa ya uzalishaji wa miche bora ya miti ya matunda kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wakulima. *ASA* inawasiliana na wataalam kutoka nchini Israel kwa ajili hiyo. Lengo ni kuijengea uwezo *ASA* wa kuzalisha miche ya matunda ipatayo milioni mbili na nusu kwa mwaka. Kwa kuanzia uzalishaji utakuwa wa miche bora ya miembe, michungwa, mapesheni na mapapai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itahimiza undelezaji na usindikaji wa mazao ya mbegu za mafuta, hususan alizeti, ufuta, michikichi, karanga na soya kupitia *DADPs* katika maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kuendeleza mazao hayo. Aidha, wakulima watafundishwa kanuni za kilimo bora cha mazao hayo kupitia mashamba darasa na watahimizwa kujiunga katika vikundi au ushirika wa uzalishaji ili kupata masoko ya uhakika ya mazao yao. Aidha, Wizara itashirikiana na Halmashauri za Wilaya 22 zilizopanga katika *DADPs* za mwaka 2009/2010 kuendeleza viwanda vidogo vya usindikaji wa mbegu za mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuhuisha vivutio vya uwekezaji katika Sekta ya Kilimo kwa lengo la kuwa na vivutio vitakavyosaidia kuongeza uwekezaji katika sekta ya kilimo; kuhamasisha uwekezaji kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji cha Taifa *(Tanzania Investment Centre- TIC)* na Baraza la Taifa la Biashara *(Tanzania National Business Council-TNBC).* Aidha, fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta zitaendelea kutangazwa kwa wawekezaji wa ndani na nje. Vilevile, Wizara itashirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Benki Kuu kuanzisha benki ya kilimo nchini kwa lengo la kusaidia wawekezaji pamoja na sekta binafsi kupata mikopo yenye riba na masharti nafuu. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Mikoa itaainisha, kupima na kusajili ardhi iliyopo kwa ajili ya kilimo cha kibiashara. Maeneo hayo yataingizwa katika Hazina ya Ardhi *(Land Bank)* kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje. Aidha, mpango wa kuzalisha mbegu za mazao mbalimbali kibiashara katika shamba la Mbozi utaanza kutekelezwa. Vilevile, Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu matumizi ya mashamba makubwa yaliyobinafsishwa kulingana na mikataba ya mauzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa chakula, katika mwaka 2009/2010, Wizara itazijengea uwezo Halmashauri za Wilaya zilizoibua miradi inayolenga kutatua matatizo ya upungufu wa chakula kupitia *DADPs* kwa kutoa mafunzo kwa timu za wawezeshaji wa Halmashauri za Wilaya na kuendelea kuhimiza uibuaji wa miradi ya aina hiyo. Jumla ya wawezeshaji 108 kutoka Halmashauri 12 za Mikoa ya Dodoma, Arusha na Manyara watapatiwa mafunzo hayo. Mafunzo mengine yatahusu masuala mchanganyiko ya Usalama wa Chakula hususan, matumizi ya teknolojia za *Geographical Information Systems (GIS)* na *Global Positioning System* (GPS) katika ukusanyaji na usambazaji wa takwimu na taarifa za mvua na hali ya mazao mashambani kwa wataalam wawezeshaji 60 kutoka katika

Halmashauri 20 za Mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara; hifadhi bora na matumizi ya mazao ya nafaka na mikunde yatakayotolewa kwa wataalam wa kilimo 180 kutoka Halmashauri za Wilaya 20 katika Mikoa ya Ruvuma, Tanga, Lindi na Pwani ili kupunguza upotevu na kuongeza upatikanaji wa chakula;teknolojia za hifadhi na matumizi ya mazao ya mizizi, mboga na matunda kwa watalaam 60 wa Halmashauri za Mikoa ya Morogoro, Arusha na Tanga na mafunzo ya ujenzi wa maghala bora ya kuhifadhia mazao ya chakula katika Mikoa ya Ruvuma na Morogoro kwa mafundi ujenzi wa vijiji na wataalam wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mafunzo hayo, Wizara itahamasisha na kuhimiza wananchi kuhifadhi chakula cha kutosheleza mahitaji ya kaya kwa mwaka mzima ili kuepukana na njaa. Halmashauri zilizoibua miradi ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhi mazao kupitia *DADPs* zitapatiwa ushauri wa kiufundi wa namna ya kutumia maghala hayo kwa ufanisi. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha na kuhimiza matumizi ya mazao yasio ya nafaka na matumizi ya teknolojia za usindikaji wa mazao ya nafaka kwa kuchanganya muhogo na nafaka kama vile mahindi na mtama na itafanya tafiti maalum zitakazochangia kuongeza uwezo wa kubuni mikakati ya kuboresha usalama wa chakula nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wake katika kuratibu hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa kufanya savei mbalimbali za utabiri wa uzalishaji wa mazao ya chakula ili kubaini hali ya chakula nchini na kupendekeza hatua za kuchukuliwa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau itafanya tathmini za kina katika maeneo yatakayobainika kuwa na upungufu wa chakula na kuishauri Serikali kuchukua hatua zinazostahili kwa kuzingatia maslahi ya wazalishaji na walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na upungufu wa chakula, Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya chakula katika maeneo yenye upungufu na itafanya tathmini ya kina mwezi Agosti 2009 na ikibidi wakati mwingine wowote ule ili kubaini kaya zitakazoathirika na upungufu na kuchukua hatua zinazostahili. Aidha, mwezi Desemba 2009, Wizara itafanya tathmini ya mavuno ya msimu wa 2008/2009 *(Final Forecast).* Tathmini hiyo pia itazingatia mwenendo wa uzalishaji wa kilimo cha vuli cha mwaka 2009/2010 ambacho kwa kawaida huchangia kati ya asilimia 20 hadi 25 ya mavuno ya msimu mmoja. Hali ya chakula mwaka 2009/2010 itategemea sana mavuno yanayotokana na mvua hizo. Tathmini ya awali *(Preliminary Forecast)* ya uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2009/2010 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2010/2011 itafanyika mwezi Mei, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Chakula Katika ngazi ya Taifa katika mwaka 2009/2010, Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) imepanga kununua kutoka kwa wakulima hapa nchini nafaka; mahindi tani 160,000 na mtama tani 5,000 zenye thamani ya Shilingi bilioni 49.40. Aidha, kazi zingine zitakazotekelezwa na NFRA ni pamoja na ununuzi wa vitendea kazi kama vile magunia, maturubai, dawa za kuhifadhia nafaka na ukarabati wa maghala. NFRA pia itahamisha nafaka zake kutoka kanda za NFRA zenye ziada na kuzipeleka kwenye kanda zenye upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, usindikaji wa mazao ya kilimo, Wizara itawajengea uwezo wataalam wa kilimo wa Halmashauri za Wilaya kwa kuwapatia mafunzo ya teknolojia za usindikaji wa mazao ya chakula, hususan yale ya nafaka, mikunde, muhogo, mboga na matunda. Aidha, mafunzo ya utayarishaji na matumizi ya mazao ya mtama, muhogo, mboga na matunda yatatolewa kwa lengo la kupanua matumizi ya mazao hayo katika kuongeza uhakika wa chakula. Ili kuongeza soko na kupanua matumizi ya zao la muhogo, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itawahamasisha wasindikaji wa mazao ya nafaka kuchanganya muhogo na nafaka kama vile mahindi na mtama.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi bora ya ardhi. Maendeleo ya kilimo nchini yanategemea sana jinsi rasilimali za ardhi, maji na bioanuai zinavyotumika. Upanuzi wa shughuli za kilimo una nafasi kubwa ya kuharibu mazingira kama kanuni za matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo hazikuzingatiwa ipasavyo. Hali hiyo tayari imejitokeza katika maeneo mengi yenye miinuko kama milima ya Uluguru, milima ya Pare na maeneo ya Mikoa yenye mifugo mingi kama Arusha, Manyara, Dodoma na Shinyanga. Ili kukabiliana na hali hiyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kusimamia na kutoa ushauri wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea na mchakato wa kukamilisha Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo *(National Agricultural Land Use Planning and Management Master Plan)* ambao unatoa dira ya matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo inayozingatia tija na hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na ASA na RUBADA itakamilisha upimaji wa mashamba matano kati ya saba yaliyo chini ya Wizara (Msimba, Dabaga, Tengeru, Mwele na Dakawa) ili kuondokana na migogoro ya ardhi inayotokana na uvamizi kwenye mashamba hayo. Kwa kushirikiana na Wilaya za Mbinga, Iringa vijijini, Kilolo, Mpwapwa, Morogoro Vijijini, Kiteto, Iramba, Sengerema, Bunda, Tarime na Same, Wizara itatoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 22 kuhusu kanuni za matumizi bora ya ardhi na udhibiti wa mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kupima na kuwekea mipaka maeneo yanayomilikiwa na Wizara kwa lengo la kupatiwa hatimiliki ili kuyalinda dhidi ya uvamizi; kuendeleza teknolojia endelevu za kilimo – mseto (za asili na za kisasa) zinazofaa kwa maeneo ya ufugaji na maeneo ya miinuko ili kuongeza tija, kuhifadhi teknolojia za asili na kuhifadhi mazingira ikiwa ni pamoja na kuchangia juhudi za kupunguza mabadiliko ya tabia nchi na kuenea kwa jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Halmashauri za Wilaya, Wizara itaandaa Mipango ya Usimamizi (management plans) kwa matumizi ya ardhi ya kilimo na ufugaji kwenye maeneo ya wafugaji *(Pastoral Ecosystems)* na wakulima *(Upland Farming Systems)*. Lengo ni kuwa na mipango shirikishi itakayotumiwa na wakulima na wafugaji wa maeneo husika katika kuhakikisha kunakuwepo na matumizi endelevu ya ardhi kwenye maeneo hayo. Wilaya zitakazohusika kwa kuanzia ni Kasulu, Kibondo na Kigoma Vijijini (Kigoma); Handeni, Mkinga na Muheza (Tanga); Ifakara, Kilosa na Ulanga (Morogoro); na Kilwa na Lindi Vijijini (Lindi) ambazo tayari zina Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Vijiji. Aidha, Wizara itatoa ushauri wa kiufundi kuhusu uendelezaji wa matumizi bora ya ardhi kwa Halmashauri za Wilaya zilizoibua miradi ya aina hiyo kupitia *DADPs* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika itaendelea kuratibu, kudhibiti na kuhamasisha shughuli za hifadhi ya mazingira katika kazi za maendeleo ya kilimo kwa kushirikisha Halmashauri za Wilaya ili kuongeza uzalishaji na kuwa na kilimo endelevu. Ili kufanikisha hayo, Wizara itatathmini athari ya shughuli za maendeleo ya kilimo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mazingira katika Halmashauri za Sumbawanga Vijijini na Mpanda (Rukwa); Urambo na Sikonge (Tabora); Iramba na Singida Vijijini (Singida); Masasi na Newala (Mtwara) na Same na Siha (Kilimanjaro) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itaelimisha jamii kuhusu Sheria ya Mazingira ya mwaka wa 2004 na suala zima la hifadhi ya mazingira katika Halmashauri zilizotajwa na

Halmashauri za Bunda, Musoma Mjini, Serengeti, Songea na Namtumbo kwa kusudi la kuwawezesha kuibua miradi inayohusisha hifadhi ya mazingira yenye kuleta tija katika kilimo na kufanya kilimo cha nchi hii kuwa endelevu. Shughuli hiyo itafanywa kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira (VPO-DoE) pamoja na Baraza la Taifa la Mazingira *(NEMC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira (VPO-DoE) pamoja na Baraza la Taifa la Mazingira (*NEMC*), itaandaa Mwongozo wa kutathmini athari za mazingira katika sekta ya kilimo kwa lengo la kuhakikisha kuwa shughuli za kilimo nchini zinafanyika kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira na zinakuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya udongo na matumizi bora ya ardhi, katika mwaka 2009/2010, Wizara itashirikiana na Halmashauri za Wilaya zikiwemo zile zinazopata mbolea ya ruzuku za Mbinga, Iringa Vijijini, Kilolo, Mpwapwa, Morogoro Vijijini, Kiteto, Iramba, Sengerema, Bunda, Tarime na Same kuwapatia mafunzo Maafisa Ugani 22. Mafunzo hayo yatahusu:-

- Kanuni za matumizi bora ya ardhi na udhibiti wa mmomonyoko wa udongo ambazo ni muhimu kuzingatiwa ili mbolea inayotumika mashambani iweze kuongeza tija kwa viwango vilivyokusudiwa.

- Matumizi ya *GPS* na upimaji wa mashamba ya wakulima utakaoambatana na ukusanyaji na utoaji takwimu za matumizi ya ardhi ya kilimo ili kuanza kujenga uwezo wa kuchangia katika maboresho ya takwimu za kilimo zinazotolewa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuandaa na kufanya mapitio ya sheria na kanuni za sekta ya kilimo ili kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya sasa au malengo ya kutungwa kwa sera na sheria hizo. Wizara itaandaa mwongozo wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kilimo ili kubainisha majukumu ya wadau mbalimbali. Aidha, kazi zingine zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Pembejeo za Kilimo ya mwaka 1994; Sheria ya Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea 2002; Sheria ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Sheria ya Hifadhi ya Mimea *(Plant Protection Act, 1997)* na Sheria ya Viuatilifu *(Tropical Pesticides Research Institute, 1979);* kuandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula. Vilevile, Wizara itaandaa Kanuni za Sheria ya Mbolea; Kanuni za Sheria za Bodi za Mazao na Kanuni za Sheria ya Bodi ya Mazao ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko na kuandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Kusimamia Rasilimali za Kilimo na Sheria ya Kilimo cha Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara za Sekta ya Kilimo kwa Tanzania Bara na Visiwani zikishirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar, zinaendelea na zoezi la Sensa ya Kilimo na Mifugo ambalo linategemea kukamilika katika mwaka huu wa fedha. Sensa ya mwaka 2008/2009, inalenga kupima mafanikio ya MKUKUTA kwenye Sekta ya Kilimo. Kutokana na sensa hiyo matokeo yatalinganishwa na sensa ya mwaka 2002/2003 ili kupima maendeleo ya utekelezaji wa malengo ya MKUKUTA na Milenia na kufanya marejeo ya viashiria vya malengo hayo. Kwa mujibu wa mpango wa kutathmini mafanikio ya MKUKUTA, sensa ya kilimo na mifugo imepangwa kuwa inafanyika kila baada ya miaka mitano. Aidha, kupitia Utafiti wa Kufuatilia Kaya *(Panel Survey)* unaoendelea nchini kote kwa kushirikisha Wizara za Sekta za Kilimo, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Washirika wa Maendeleo, utekelezaji wa malengo ya Milenia na MKUKUTA unatathminiwa ikiwa ni pamoja na kuangalia umuhimu wa viashiria vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, zinaandaa mfumo wa benki ya Takwimu za Kilimo na Maliasili unaoitwa "*CountrySTAT*" utakaowezesha kuingizwa kwa takwimu za sekta ya kilimo na maliasili katika sehemu moja na kuunganishwa na mitandao ya Wizara husika. Kwa kutumia mfumo huo, watumiaji wa takwimu za kilimo na maliasili wataweza kupata takwimu wanazohitaji kwa urahisi kupitia mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutekeleza Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenizesheni ya Ushirika *(Cooperative Reform and Modernization Program - CRMP),* Maendeleo ya Ushirika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itawakutanisha wadau wakuu wa utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika, yaani *COASCO*, MUCCoBS, TFC na SCCULT katika kutathimini utekelezaji wa Programu na kuandaa mfumo wa utekelezaji na ugharamiaji. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha utekelezaji wa CRMP kwa kufanya kazi zifuatazo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuimarisha Uongozi wa Vyama vya Ushirika, kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara itasimamia chaguzi za Vyama Vikuu pamoja na Vyama vya Msingi vya Mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Iringa, Morogoro, Tabora, Kigoma na Rukwa ambayo muda wake wa uchaguzi kwa mujibu wa Sheria umefikiwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana MUCCoBS itatoa mafunzo kwa wajumbe wa bodi wapya watakaochaguliwa pamoja na watendaji wa Vyama vya Ushirika vya mazao na *SACCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhamasisha Wananchi Kuanzisha ama Kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itahamasisha wananchi wengi zaidi kujiunga katika Vyama vya Ushirika yakiwemo maeneo ya Mbinga na Mara ambako tayari hatua za kuimarisha Vyama Vikuu vya Ushirika zilikwishaanza. Msisitizo mkubwa utawekwa katika kuongeza idadi ya wanachama katika Vyama vilivyopo ili kuimarisha mitaji yake viweze kuendeshwa kibiashara kwa manufaa ya wanachama wake. Lengo ni kuongeza idadi ya Vyama vya Ushirika nchini kwa asilimia 5 na Idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika kwa asilimia 15.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imepanga kuhamasisha vijana katika Mikoa mbalimbali wajiunge katika ushirika wa uzalishaji mali na kuanzisha Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ili waweze kupata mitaji ya kuendesha miradi yao. Katika maeneo hayo imepangwa kutilia mkazo uzalishaji wa mazao ya mboga, matunda ya muda mfupi na mazao mengine ya kilimo kutegemeana na hali ya eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kueneza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani, Wizara itashirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Tawala za Mikoa na Halmashauri za Wilaya kueneza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani katika maeneo yanayozalisha korosho na pamba, hususan katika Mikoa ya Lindi, Dar es Salaam, Tanga na Ruvuma (kwa zao la korosho), Shinyanga (Kahama), Kagera (Biharamulo), Tanga, Morogoro na Pwani (kwa zao la Pamba). Aidha, Wizara itawawezesha wanachama kuvifufua na kuviimarisha Vyama ambavyo ni sinzia ili mfumo huo uweze kutumika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufufua na kuimarisha Vyama vya Tumbaku. Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Tumbaku itafanya uchambuzi wa madeni ya pembejeo yanayodaiwa na Makampuni ya ununuzi wa Tumbaku na kuanza kuyalipa. Kufanyika kwa malipo hayo

kutaviwezesha Vyama husika kuwa na uhuru wa kuwasambazia wakulima pembejeo moja kwa moja kwa bei nafuu ikilinganishwa na bei au malipo makubwa ambayo hudaiwa na makampuni ya tumbaku kutokana na biashara hiyo. Hatua hiyo itawawezesha wakulima kutokutegemea makampuni katika kupata pembejeo za tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha uendeshaji wa *SACCOS* na Benki za Ushirika. Wizara itachapisha na kusambaza Miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa *SACCOS* kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kuviwezesha Vyama hivyo kuendesha shughuli zake kwa kuzingatia viwango vya asasi za fedha pamoja na mahitaji ya wanachama wake. Wizara itaendelea kufadhili mafunzo ya cheti kwa watendaji wa *SACCOS* yanayotolewa na MUCCoBS ili kuwaongezea uwezo. Aidha, Wizara itashirikiana na wadau wengine kutoa mafunzo kwa *SACCOS* zenye mitaji mikubwa kulinda mali za wanachama wake. Kwa kushirikiana na Benki Kuu, Wizara itaendelea kuhimiza na kufuatilia ujenzi wa mtaji wa Benki za Ushirika za Kilimanjaro na Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Kwa kushirikiana na *COASCO,* Wizara itatoa mafunzo ya ukaguzi wa kawaida wa Vyama vya Ushirika kwa wakaguzi wa Wilaya na Mikoa. Wizara itafanya ukaguzi maalum wa Vyama vya Ushirika pale inapobidi. Aidha, Wizara itafuatilia kwa karibu shughuli za Vyama ili kutoa ushauri unapohitajika kwa lengo la kuona vinaboresha huduma kwa wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itawapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu Maafisa Ushirika wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwaongezea uwezo wa kutekeleza majukumu yao. Kwa kushirikiana na mamlaka husika Wizara itateua Warajis Wasaidizi wa Mikoa pamoja na Maafisa wa Wilaya kujaza nafasi zilizo wazi. Wizara itaendelea kutoa ruzuku kwa Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika ili liweze kujiimarisha kukagua na kuwasomea wanachama wa Vyama vya Ushirika hesabu za Vyama vyao kwa wakati. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza maelekezo ya Mhe. Rais kukamilisha uanzishwaji wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa UKIMWI, katika mwaka 2009/2010, Wizara itatathmini hali ya maambukizi ya UKIMWI katika Wizara. Tathmini hiyo itaweza kutoa mwelekeo wa hali halisi ya UKIMWI katika sehemu ya kazi na kuweza kuandaa Mpango Mkakati utakaoana na Mkakati wa Taifa wa UKIMWI *(National HIV/AIDS Strategy 2008 – 2012).* Uendelezaji wa shughuli za UKIMWI utafanyika kupitia bajeti ya matumizi mengine tofauti na ilivyokuwa katika kipindi kilichopita ambapo shughuli hizo ziligharamiwa kupitia Mradi wa *Tanzania Multisectoral Aids Project (TMAP).* Wizara itaendelea kuwawezesha watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI kupata vyakula vyenye virutubisho pamoja na kuhudhuria kliniki kwa ajili ya matibabu. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa wanafunzi tarajali 800 katika vyuo vya mafunzo ya kilimo vya Ilonga na Uyole kuhusu mabadiliko ya tabia na mienendo kwa vijana ili kuepuka maambukizo ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuhaulisha masuala ya jinsia katika kuendeleza kilimo nchini, Wizara itashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kuandaa Mwongozo wa kuingiza masuala ya jinsia katika shughuli za kilimo. Aidha, elimu ya jinsia itatolewa kwa wajumbe wa Kamati ya Jinsia ya Wizara ili kuwajengea uwezo wa kuzingatia masuala ya jinsia katika kupanga na kutekeleza mipango ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Rasilimali Watu katika mwaka 2009/2010, Wizara itaajiri watumishi 174 ili kuongeza nguvu kazi katika utoaji huduma na kupandisha

vyeo watumishi 432 katika madaraja mbalimbali kwa kuzingatia sera ya menejimenti na ajira katika Utumishi wa Umma. Wizara pia itaendelea kutoa mafunzo elekezi (*orientation*) kwa waajiriwa wapya ili waweze kufahamu sheria, taratibu na kanuni zinazotumika katika utendaji wa shughuli za Serikali pamoja na maadili ya utumishi wa umma kabla ya kupewa majukumu. Aidha, ukaguzi wa watumishi *(Human Resources Audit)* utaendelea kufanyika ili kuwa na taarifa sahihi za watumishi wote wa Wizara waliopo kwenye orodha ya malipo ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutekeleza Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma, awamu ya pili *(Public Service Reform Programme II- PSRP II)* kwa kuendelea kuwajengea uwezo Wasaidizi wa Kumbukumbu kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi ili kuboresha na kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za kiutumishi na kiutendaji. Hatua hiyo itarahisisha upatikanaji haraka wa taarifa zitakazosaidia utoaji wa maamuzi kwa wakati, na hivyo kupunguza malalamiko kutoka kwa wateja. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wapya wa Wizara kuhusu Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi *(Open Performance Review and Appraisal System-OPRAS)* ili kuongeza ushiriki na umiliki wa watumishi katika kupanga malengo, utekelezaji, ufuatiliaji na kufanya mapitio ya utendaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, hususan Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ikiongozwa na Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mbunge wa Ileje iliyochambua makadirio ya matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa kina na kutoa mapendekezo ambayo yamesaidia katika kuboresha mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2009/2010. Mchango wao utatiliwa maanani na utaendelea kuwa sehemu muhimu katika kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Japan, Ireland, China, India, Israel, Indonesia, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Ubelgiji, Uholanzi na Uswisi. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, WARDA, Rockfeller Foundation na Bill and Melinda Gates Foundation*. Ushirikiano na misaada ya Nchi na Mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na mazingira magumu waliyo nayo. (*Makofi*)

Napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi; Katibu Mkuu Bw. Mohamed S. Muya; Naibu Katibu Mkuu Bibi Sophia Elias Kaduma; Wakurugenzi, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezeka kwa majukumu ya Wizara bila kukwama. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika, zinatekeleza Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi wa mwaka 2005 na Sera ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi ili washiriki kikamilifu katika kuainisha matatizo yanayowakabili, kupanga mipango ya kukabiliana nayo,

kushiriki katika utekelezaji wa mipango hiyo na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango hiyo. Aidha, Wizara kupitia Mpango wa mwaka 2009/2010 itatekeleza malengo ya MKUKUTA yafuatayo:-

i. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 9.0 mwaka 2003/2004 hadi kufikia tani milioni 12 mwaka 2010/2011;

ii. Kudhibiti mmomonyoko wa udongo na upotevu wa bioanuwai ya kilimo; na

iii. Kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo.

Kwa kuwa Sekta ya Kilimo ni mtambuka, ni matumani yangu kuwa wadau wote wenye kuchangia maendeleo ya Sekta ya Kilimo tutashirikiana katika kuyapatia ufumbuzi chini ya kauli mbiu ya KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 228,564,587,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka 2009/2010. Kati ya fedha hizo, Shilingi 135,870,333,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 92,694,254,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, Shilingi 2,516,709,000 ni fedha za ndani na Shilingi 90,177,545,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hii nimewasilisha mezani nakala ya Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2009/2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja ya Kilimo, kwanza imeungwa mkono na kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati anayehusika na hotuba hii, nafikiri kulikuwa na kasoro kidogo. Tumetambulisha watu wote waliokuja kutoka Bunda na kila mahali lakini tukaacha kutambulisha watendaji katika Wizara hii. Kwa hiyo, ninapenda kumtambua Katibu Mkuu, Ndugu Mohamed Muya, yuko kazini tayari na Naibu wake Katibu Mkuu, Bi. Sophia Kaduma. Wameongozana na Wakurugenzi mbalimbali. Tunaomba radhi hatukuwatambua kwanza lakini ninyi nyote pamoja na watendaji wenu mnakaribishwa.

Bado nasuburu *list* ya wageni walioko kwenye *Speaker's Gallery* kwa sababu wageni hawawezi kukaa *Speaker's Gallery* halafu hawajulikani kwa Spika mwenyewe. Kwa hiyo, nategemea baadaye nitaipata.

Baada ya kusema hivyo, naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Kidawa, kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. KIDAWA H. SALEHE (K.n.y. MHE. GIDEON A. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa taarifa ya Kamati, naomba kuchukua nafasi hii, kuwapongeza kina mama wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao ni wapiga kura wangu, kwa kazi nzuri wanaofanya ya kuimarisha kilimo na kuhakikisha kwamba Mkoa wetu wa Kaskazini Unguja haukumbwi na janga la njaa.

Aidha, natoa shukurani zangu za dhati, kwenu Waheshimiwa Wabunge, kwa imani mliyonayo kwangu kwa kupitisha jina langu bila la kupingwa kuwa Kamishina wa Tume ya Huduma za Bunge. Ninaahidi nitashirikiana nanyi kikamilifu na daima nitakubali ushauri wenu katika kutekeleza majukumu na kazi zangu.

Baada ya kusema hayo, sasa niwasilishe Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, kwa niaba ya Mwenyekiti naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, ilikutana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Dodoma tarehe 12 na 15 Juni, 2009. Katika vikao hivyo Kamati ilipata maelezo ya kina kutoka kwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa Fedha wa 2008/2009, mafanikio na changamoto za utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha mwaka wa 2008/2009. Aidha, Kamati ilipata maelezo ya malengo na maeneo ya kipaumbele na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa 2008/2009, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa, Wizara imeyafanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati. Utekelezaji wa baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati bado unaendelea, wakati kwa baadhi, juhudi zaidi zinahitajika. Kamati inahimiza Wizara iharakishe kutekeleza maeneo ambayo hayajakamilika. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi na Wizara ni pamoja na yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Kamati ilielezwa kwamba Wizara imekamilisha utaratibu wa uanzishaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Kikundi kazi (*Task Force*) cha kusimamia uundaji wa Bodi hiyo kimeteuliwa na mapendekezo ya Muswada wa kuunda Bodi nayo yameandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi. Kamati inaridhika na hatua iliyofikiwa na inashauri kasi hiyo iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Ushirika. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua inazochukua chini ya Mpango wa Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini wa kuimarisha vyama vya ushirika. Katika mwaka wa 2008/2009, Serikali iliamua kuviondolea mzigo wa madeni baadhi ya Vyama vya Ushirika. Vyama vya Ushirika vilikuwa na madeni ya jumla ya shilingi bilioni 26.8. Hadi mwisho wa mwaka wa 2008/2009, Serikali ilikuwa imevifutia vyama hivyo madeni yenye thamani ya shilingi bilioni 15, ilichukua madeni ya wadai mbalimbali ya shilingi bilioni 11.8 na ililipa madeni ya mabenki na ya wakulima ya jumla ya shilingi bilioni 4.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kiasi kikubwa imejitahidi kuongeza bajeti kwa Bodi za Mazao na Taasisi nyingine zilizo chini yake. Katika mwaka wa 2009/2010, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 12.98 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 9.8 zilizotengwa kwa mwaka wa 2008/2009 kwa ajili ya Bodi za Mazao na asasi nyingine, ongezeko hilo ni la shilingi bilioni 3.19 sawa na asilimia 34 ya kiasi cha fedha kilichotengwa

mwaka wa 2008/2009. Pamoja na juhudi hizo, Bodi za Mazao bado zinakabiliwa na uhaba wa fedha na Serikali inashauriwa kuziruhusu kutoza ada kwa baadhi ya huduma wanazotoa ili mradi zisiwaumize sana wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kusimamia Utafiti. Baadhi ya asasi za Utafiti wa Kilimo zinasimamiwa chini ya Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 ya Sheria za Tanzania, jambo ambalo halizingatii na kulinda haki za Serikali juu ya matokeo ya utafiti unaofanywa na asasi hizo. Kamati iliishauri Serikali ichukue hatua zitakazowezesha kutungwa kwa Sheria Maalum ya Utafiti wa Kilimo ambayo itaondoa upungufu ulioko kwenye utaratibu uliopo sasa. Kamati ilijulishwa kwamba rasimu ya Muswada wa Sheria hiyo imeshaandaliwa na inapitishwa kwenye utaratibu unaohusika ndani ya Serikali kabla ya kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pembejeo. Katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, Mfuko wa Pembejeo ulipewa shilingi billioni tatu kutoka kwenye bajeti ya Serikali na kuongezewa kiasi kingine cha shilingi bilioni tatu kutoka kwenye Mfuko wa Madeni ya Nje (*EPA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2009/2010, Wizara imetengewa shilingi bilioni nne kwa ajili ya kutoa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuupatia Mfuko fedha za kuwakopesha wakulima na inaishauri Serikali iendelee kuuongezea Mfuko fedha kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wakulima. Moja ya matatizo yanayoathiri maendeleo ya kilimo nchini, ni kutokuwapo kwa mabenki na Taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa sekta ya kilimo. Kamati ilielezwa kwamba Serikali imeshaanza mchakato wa kuanzisha Benki ya Wakulima unaoandaliwa kwa pamoja na Benki ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya China. Aidha, Serikali imeipa Benki ya Rasilimali (*TIB*) shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kuanzisha dirisha la kukopesha wakulima katika kipindi cha mpito.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2008/2009, Wizara ilitengewa Shilingi 93,704,218,000/= kwa matumizi ya kawaida na Shilingi 20,516,709,000/= kwa ajili ya matumizi ya mipango ya maendeleo. Aidha, Wizara iliongezewa kiasi cha shilingi bilioni 40 kutoka katika Mfuko wa Madeni ya Nje (*EPA*) kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo na shilingi bilioni 3.79 ziliongezwa kwa ajili ya mishahara ya Bodi za Mazao, Taasisi na Watumishi wa Wizara na hivyo kufanya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa 2008/2009, kufikia shilingi bilioni 157.53.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka tarehe 25 Mei, 2009, kiasi cha shilingi bilioni 126.57 sawa na asilimia 92.1 cha pesa za matumizi ya kawaida zilikuwa zimepokelewa kutoka Hazina na kiasi cha shilingi bilioni 18 sawa na asilimia 90 cha pesa za maendeleo nazo zilikuwa zimepokelewa kutoka Hazina. Upatikanaji wa fedha hizo uliwezesha Wizara kutekeleza kazi ilizojipangia. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Katika mwaka wa 2008/2009, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, iliendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)* kwa kuzijengea Sektretariati za Mikoa na Halmashauri za Wilaya uwezo wa kuandaa mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADP's).* Ukiwa ni mwaka wa tatu tangu kuanzishwa kwa programu hii, kiasi cha pesa ambacho tayari kimetolewa ni shilingi bilioni 198.6 sawa na asilimia 34.32 ikilinganishwa na

mahitaji halisi ya shilingi bilioni 578.6 katika kipindi hicho na hii inatokana na uwezo mdogo wa uibuaji wa miradi ndani ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pembejeo za kilimo na zana za kilimo. Katika mwaka wa 2008/2009, makadirio ya mahitaji ya mbolea yalikuwa tani 385,000. Hadi Mei, 2009 jumla ya tani 237,897 sawa na asilimia 61.8 ya makadirio ya mahitaji ilikuwa imepatikana, kati ya mbolea hiyo, tani 141,050 zilikuwa za ruzuku. Kamati inasisitiza juhudi ziongezwe katika ujenzi wa viwanda vya mbolea nchini hasa katika maeneo ambayo kuna *Phosphate* kama Minjingu, Mpanda na Mbeya na maeneo mengine yenye gesi asilia za *Nitrogen*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji halisi ya mbegu bora katika mwaka wa 2008/2009, yalikisiwa kuwa tani 30,000. Hata hivyo, upatikanaji wa mbegu bora ulifikia tani 11,056.07 tu, sawa na asilimia 54.6 ya mahitaji. Ili kilimo kiwe cha ufanisi na cha kumsaidia Mtanzania, suala la upatikanaji wa mbegu bora ni lazima liwe moja ya vipaumbele vya Taifa. Hivyo, Serikali ni lazima ijipange vyema kuhakikisha kwamba mbegu bora za kutosha zinazalishwa humu nchini ili kukidhi mahitaji ya wakulima badala ya kutegemea mbegu ambazo zinatoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miche bora ya chai na kahawa. Katika mwaka wa 2008/2009, Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai, kwa kupitia vikundi 1414, vyenye wakulima 2012, kutoka Halmashauri za Wilaya 11, walizalisha miche bora 6,603,827 sawa na asilimia 83 ya lengo la kuzalisha miche 8,000,000 kwa utaratibu wa ruzuku. Aidha, kupitia vikundi vya wakulima, Halmashauri za Wilaya, wakulima binafsi na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Nchini (*TACRI*), walizalisha jumla ya miche bora ya kahawa 9,570,846, kati ya lengo la kuzalisha miche bora ya kahawa 10,000,000, ambayo ni sawa na asilimia 96 ya lengo na kusambazwa kwa wakulima. Kamati inatoa pongezi sana kwa mafanikio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madawa ya pamba na korosho. Katika mwaka wa 2008/2009, Wizara kupitia Bodi za Korosho na Pamba, ilitoa ruzuku ya madawa yanayohusika na mazao yanayosimamiwa na Bodi hizo. Hadi mwezi Mei, 2009 jumla ya *accrepacks* 2,050,000 zilinunuliwa, kati ya hizo *accrepacks* 1,141,758 zilisambazwa kwa mawakala ambapo *accrepacks* 556,772 sawa na asilimia 48.7 zilinunuliwa na wakulima. Ununuzi huo mdogo umesababishwa na uwezo mdogo wa wakulima kununua madawa hayo ya pamba kutokana na ukosefu wa fedha. Aidha, hadi kufikia Aprili 2009, jumla ya lita 3,616,552 za madawa ya korosho zilisambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo. Katika msimu wa 2008/2009, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, ulitengewa jumla ya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kutoa mikopo ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana za kilimo. Aidha, Mfuko uliongezewa shilingi bilioni tatu zilizotokana na fedha za Mfuko wa Madeni ya Nje *(EPA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko pia ulikusanya madeni ya miaka ya nyuma yenye thamani ya shilingi bilioni 2.77 na kufanya Mfuko kuwa na jumla ya shilingi bilioni 8.77 ambazo zilitumika kutoa mikopo kwa wakulima binafsi, wasambazaji wa pembejeo za kilimo na mifugo na zana za kilimo, vikundi vya wakulima na *SACCOS*. Mfuko huu ni muhimu sana katika kutoa mikopo ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana za kilimo katika kipindi hiki ambapo hatuna Benki ya Wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za ugani. Kuanzia mwaka wa 2007/2008, Wizara ililenga kuajiri jumla ya wataalam wa ugani 2,500 kila mwaka kwa kipindi cha miaka minne. Hata hivyo, hadi mwezi Aprili 2009, jumla ya wataalam wa ugani walioajariwa na kupangiwa

vituo vya kazi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ni 573, lengo halikufikiwa kutokana na uhaba wa wataalam wenye sifa zinazotakiwa. Hata hivyo, Wizara imeamua kupeleka vijana waliomaliza Kidato cha Nne vyuoni kusomea kilimo ili kupunguza tatizo hili la Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa chakula kwa mwaka wa 2008/2009, ulikuwa ni mdogo kutokana na ukame ulioikumba nchi yetu. Uzalishaji wa mazao ya chakula ulikuwa ni tani milioni 10.87. Kati ya hizo, uzalishaji wa mazao ya nafaka ulikuwa ni tani milioni 5.59 na mazao yasiyo ya nafaka jumla ya tani 5.28. Kamati inaendelea kuhimiza kilimo cha umwagiliaji hasa katika maeneo ambayo ni kame na pia uzalishaji wa mazao uendane na hali ya hewa, udongo na mazingira ya eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujihakikishia akiba ya chakula nchini, katika msimu wa 2008/2009, Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA), ilipanga kununua jumla ya tani 105,000 za mazao ya nafaka. Hadi kufikia Mei 2009, NFRA ilikuwa imenunua tani 62,641 sawa na asilimia 59.7 ya lengo. Lengo lilishindwa kufikiwa kutokana na ukame ulioikumba nchi hasa Mikoa ya Kaskazini. Mpaka sasa kiasi cha tani 115,162 ikijumlisha na akiba ya tani 52,521 iliyokuwepo awali ghalani ndio zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa chakula. Katika mwaka wa 2008/2009, mfumo wa ukusanyaji wa takwimu na taarifa za hali ya chakula nchini uliboreshwa kwa kutoa mafunzo kwa wataalam wa ugani katika Halmashauri za Wilaya na Miji katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilifanya tathmini za kina katika maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu wa chakula ili kutambua kaya zenye upungufu, mahitaji yao ya chakula na kuchukua hatua za kukabiliana na upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa kilimo. Katika mwaka wa 2008/2009, Wizara ilitoa aina tano za mbegu mpya za mazao yenye sifa za kutoa mavuno mengi kwa eneo, kustahimili ukame, zinazokomaa haraka, zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na zinazopendwa na walaji. Mbegu hizo ni pamoja na pamba kutoka kituo cha utafiti cha Ukiliguru, Mahindi kutoka Kituo cha Utafiti cha Ilonga, Maharage kutoka Kituo cha Utafiti cha Uyole na Nyanya kutoka Kituo cha Utafiti cha Tengeru.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa visumbufu vya mimea. Katika kuhakikisha udhibiti wa visumbufu unaendelea kuimarishwa, katika mwaka wa 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Wakulima imeendelea kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao. Visumbufu hivyo ni pamoja na kwelea kwelea, nzige, viwavijeshi, panya na maradhi ya mimea ambayo husababisha upotevu wa mavuno wa kati ya asilimia 30 na 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya ushirika. Katika mwaka wa 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kutekeleza Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini. Wizara imeendelea kuviiimarisha Vyama vya Ushirika wa Pamba, Korosho na Tumbaku kwa kuviwezesha kupata mikopo kwa ajili ya ununuzi wa mazao hayo. Aidha, mafunzo kwa maafisa ushirika 18 wa Wilaya na Mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Arusha, Singida, Tabora, Dodoma, Kigoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam kuhusu matumizi ya miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa *SACCOs* yalitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa 2008/2009, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Waziri alieleza changamoto ambazo Wizara imekumbana nazo katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa 2008/2009. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Baadhi ya Wilaya kukumbwa na upungufu wa chakula kutokana na ukame na mafuriko yaliyojitokeza hasa Mikoa ya Kaskazini;

ii) Ukosefu wa Mawakala wa kutosha wenye uwezo wa kufikisha pembejeo za kilimo katika maeneo ya vijijini;

iii) Kutokuwepo kwa Maafisa Ugani wa kutosha katika ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji kunasababisha wakulima kutopata ushauri wa mbinu bora za kilimo na kuwepo kwa uwezo mdogo wa kuibua miradi ya kilimo, jambo linalosababisha wananchi kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa kilimo bora na kushindwa kutumia fursa zilizopo;

iv) Serikali za Mitaa kutokutekeleza kikamilifu majukumu yao ya kisheria ya kuhimiza na kuendeleza kilimo;

v) Shuguli za Utafiti kutengewa fedha kidogo ambazo haziwezeshi shughuli za utafiti kufanywa kwa viwango vya kuridhisha. Aidha, Watumishi wa utafiti kutopewa maslahi na motisha za kuridhisha jambo linalosababisha wengi kukimbilia nchi za nje ambako wanalipwa vizuri; na

vi) Baadhi ya Halmashauri kuwa na usimamizi hafifu wa matumizi ya fedha za *DADP's* na matokeo yake kutawanya fedha hizo kwenye miradi midogo midogo kwenye vijiji vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2009/2010, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika yenye Fungu 43, inaomba jumla ya shilingi 228,564,587,900/= kati ya hizo, shilingi 135,870,333,000/= ni kwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 92,694,254,000/= ni kwa Matumizi ya Maendeleo. Kiasi kinachoombwa ni nyongeza ya asilimia 45 ya kiasi cha shilingi 157,737,050,400/=, kilichotengwa mwaka kwa 2008/2009. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara imepanga kutekeleza kazi mbalimbali, baadhi ya kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa 2009/2010, utakuwa ni mwaka wa nne wa kutekeleza *ASDP*. Katika kuendelea kutekeleza Programu hii, kwa mwaka wa 2009/2010, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imetengewa shilingi bilioni 21.9 zitakazotumika kuboresha huduma za utafiti, ugani, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao, hifadhi ya mazingira na usalama wa chakula. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha timu ya Taifa ya wawezeshaji kwa kuwajengea uwezo zaidi wawezeshaji hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa pembejeo za kilimo. Katika mwaka wa 2009/2010, Wizara imepanga kuendelea kugharamia ruzuku ya mbolea, mbegu bora, miche bora ya kahawa, chai pamoja na madawa ya pamba na korosho. Aidha, kwa mwaka wa 2009/2010, jumla ya shilingi bilioni 58 ambazo ni fedha za ndani za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 60 kupitia Benki ya Dunia zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ruzuku ya pembejeo ikilinganishwa na shilingi bilioni 71.25 zilizotengwa mwaka wa 2008/2009. Kamati inaipongeza Wizara kwa hili kwani inatambua fika kwamba bila pembejeo hakuna Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2009/2010, Mfuko wa Pembejeo umetengewa jumla ya shilingi bilioni 4. Kati ya hizo Shilingi milioni 975 zitatumika kama gharama za uendeshaji na kiasi kilichabaki kitatumika kutoa mikopo ya pembejeo za kilimo na mifugo pamoja na zana za kilimo. Mfuko umepanga kukusanya marejesho ya mikopo iliyoiva yenye thamani ya shilingi bilioni 4.8 ambazo nazo zitatumika kutoa mikopo ya pembejeo za kilimo na mifugo pamoja na zana za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za ugani, kama ilivyokuwa kwa mwaka wa 2008/2009, katika mwaka wa 2009/2010 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili kutekeleza mpango wa kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima. Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kitaalam wa kuendesha shughuli za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama njia ya kudumisha viwango vya utoaji wa huduma. Pia itaendelea kutoa mafunzo kwa vijana tarajali na kutoa ajira kwa wahitimu hao ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za ugani vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mazao ya biashara. Katika mwaka wa 2009/2010, Wizara itaendelea kuelimisha wakulima umuhimu wa kutunza mazao vizuri mashambani na kuyapanga katika madaraja wakati wa kuuza, itahakikisha inaimarisha huduma za ukaguzi wa mazao. Vilevile itahakikisha mazao yanauzwa katika vituo vilivyoidhinishwa na itahimiza usindikaji wa mazao ya biashara kama njia ya kuongeza thamani ya mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa mazao ya bustani, mbegu za mafuta, muhogo na mazao ya nishati. Katika mwaka wa 2009/2010, Wizara itaendelea kutekeleza shughuli za uendelezaji wa mazao mapya na yenye thamani, uendelezaji wa zao la muhogo pamoja na mazao ya nishati. Aidha, uimarishwaji wa bustani sita za Serikali za Mpiji, Bugaga, Igurusi, Jaegetal, Malindi na Songa utafanyika ili kuhifadhi nasaba za mazao ya bustani kwa ajili ya utafiti na matumizi na kuwa ni vyanzo vya mbegu bora za mazao ya bustani.

Mheshimiwa Naibu Spika, zana za kilimo. Wizara imepanga katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, kushirikiana na Halmashauri za Wilaya 30 kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 50 kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha matrekta na wanyamakazi. Wizara imepanga kuvipatia vikundi 25 vya vijana katika Mikoa ya Lindi na Mtwara matrekta madogo ya mkono 25, kutoa mafunzo juu ya matumizi na matunzo ya matrekta hayo na kuendesha kilimo kibiashara kwa kutumia zana hizo za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea kupata teknolojia sahihi zinazokidhi mahitaji ya kilimo na kuhakikisha matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima, Wizara itaendelea kufanya utafiti wa mazao, rutuba na hifadhi ya udongo, kusambaza mbegu bora, kuwajengea watafiti uwezo na kuboresha mazingira ya kazi, kuboresha vitengo vya habari na mawasiliano vinavyounganisha watafiti, wagani, wakulima na wadau wengine na kusambaza mbegu zilizofanyiwa utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha usalama wa chakula unakuwepo, Wizara imepanga kuzijengea Halmashauri za Wilaya uwezo wa kuibua miradi inayolenga kutatua matatizo ya upungufu wa chakula kupitia *DADP's* kwa kutoa mafunzo kwa timu za wawezeshaji wa Halmashauri ili wasaidie wakulima kuibua miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2009/2010, Hifadhi ya Taifa ya Chakula (*NFRA*), imepanga kununua kutoka kwa wakulima wa hapa nchini nafaka zikiwemo mahindi

tani 100,000 na mtama tani 5,000 zenye thamani ya shilingi bilioni 32.39. Nafaka hizi zitasaidia kaya ambazo zimekumbwa na ukame kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya ushirika, Wizara itaendelea kufufua na kuimarisha Vyama vya Vshirika vya mazao ya Pamba, Korosho na Tumbaku hususan katika Mikoa ambayo haijafikiwa, kulipa madeni ya Vyama vya Ushirika vya Tumbaku, kuhimiza na kueneza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani katika Mikoa mingine na Kukamilisha uundaji wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza utekelezaji wa maoni ya Kamati, mafanikio na changamoto zilizoikabili Wizara katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa 2008/2009 na matarajio ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa 2009/2010 kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kutoka shilingi 157,737,050,400/= mwaka wa 2008/2009 hadi shilingi 228,564,587,000/= mwaka wa 2009/2010, ongezeko la asilimia 45. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali iendelee kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara nyingine za sekta kubwa ya Kilimo, kufikia asilimia kumi ya Bajeti ya Serikali, kama inavyoagizwa na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 na kama ilivyoamuliwa kwenye Mkutano wa Wakuu wa nchi za *SADC* uliofanyika Maputo mwaka wa 2003 na kulingana na kauli mbiu ya KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Kwa sasa jamii haielewi maana ya dhana ya Kilimo kwanza. Aidha, Baadhi ya wataalam wanapata utata kutokana na ukweli kwamba Sekta ya Kilimo ni ya nne katika kutengewa fedha katika bajeti ya Serikali ya 2009/2010 baada ya Sekta za Elimu, Miundombinu na Afya. Kamati inaishauri Serikali itafsiri Kauli Mbiu ya Kilimo Kwanza katika programu za utekelezaji na iwaelimishe wananchi ili waelewe dhana na programu hizo na nafasi za wadau wote katika kuzitekeleza. Aidha, sekta ya watu binafsi ihamasishwe kuwekeza katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Chakula (*NFRA*), Kamati inaipongeza Serikali kwa kuimarisha Hifadhi ya Chakula hasa kwa kuamua kutoa kipaumbele cha kupatiwa pembejeo za kilimo kwa Mikoa sita inayozalisha mazao ya chakula ya Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Iringa, Morogoro na Kigoma. Mapungufu yaliyojitokeza katika utaratibu wa usambazaji wa mbolea yashugulikiwe ili kuhakikisha mbolea inawafikia walengwa na hatimaye kuleta tija katika kilimo. Katika kipindi hiki ambapo nchi ina upungufu wa chakula, Kamati inashauri *NFRA* isilenge katika kuhifadhi Mahindi na Mtama pekee, mazao mengine nayo yaangaliwe. Aidha, agizo la Rais lizingatiwe ili kuhakikisha mfumuko wa bei unadhibitiwa na wakulima waruhusiwe kuuza mazao yao nje ya nchi au Serikali kama itaona kuna kila sababu ya kuwazuia, basi ihakikishe inawafidia kwa tofauti ya bei itakayojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya kilimo ina nafasi kubwa ya kutoa mchango wa kuwapatia ajira Watanzania zaidi ya asilimia 70 ambao wengi wanaishi vijijini. Kilimo kinachangia asilimia 95 ya chakula kinachopatikana nchini na asilimia 30 ya mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Pamoja na ukweli kwamba zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo kama njia ya kujiingizia kipato, ni asilimia ndogo sana ya vijana wanaofanya shughuli za kilimo. Kilimo chetu wameachiwa wazee ambao hawana nguvu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali iwatumie vijana kwa shughuli za kilimo kwa kuhakikisha inawapa maeneo na kuwamilikisha, inawapa mikopo ya kununua zana za kilimo, inawafundisha taaluma ya kilimo bora na inawahakikishia masoko kwa mazao yao. Aidha, Serikali ihakikishe kila mkulima anapimiwa na kumilikishwa eneo lake la ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo ili kuweza kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha upatikanaji wa chakula cha kutosha, Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua ambazo zitahakikisha kwamba wananchi wanazalisha mazao yanayostawi kwenye maeneo yao kwa viwango vikubwa vya kuwawezesha kujitosheleza kwa chakula, hasa tukizingatia kwamba katika ulimwengu wa sasa kuna tatizo la upungufu wa uzalishaji wa chakula, hasa nafaka, kunakotokana na wakulima wakubwa kuzalisha mazao ya nafaka kwa ajili ya nishati. Aidha, wakulima hao kutumia sehemu ya mashamba yao kwa kilimo cha kuzalisha mafuta kama Mibono na mengine. Serikali itoe mwongozo na kusimamia kilimo cha mazao ya kuzalisha mafuta ili kusiwe na athari kwa kilimo cha mazao ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pembejeo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Mfuko wa Pembejeo kwani inatambua kazi nzuri inayofanywa na Mfuko huo kwa kutoa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo. Kamati inasisitiza bajeti yake iendelee kuongezwa ili uweze kutoa mikopo kwa Watanzania walio wengi zaidi na wakati huo huo jitihada za kukusanya marejesho ya mikopo iliyoiva ziendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuhakikisha zinapatikana pembejeo za kutosha kwa wakulima. Kutokana na kuwepo malalamiko mengi kutoka kwa wakulima kwamba mbolea ya ruzuku haiwafikii, Kamati inashauri yafuatayo:-

i) Wizara isimamie kwa karibu kwa kuhakikisha inapeleka watendaji wake wakati wa zoezi la ugawaji wa mbolea ya ruzuku badala ya kuziachia Serikali za Mitaa pekee;

ii) Mbolea hiyo itolewe kwa wakati hasa ya kupandia kwani mara kwa mara imekuwa ikitolewa kwa pamoja na mbolea ya kukuzia kipindi ambacho mazao yanakua; na

iii) Tathmini ifanyike kuona mafanikio na mapungufu ya zoezi hilo ili kuweka mkakati wa kuboresha zaidi mfumo mpya wa vocha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu bora ndio msingi wa mavuno bora, Kamati inashauri Wizara iache kutegemea kuagiza mbegu kutoka nje na badala yake itilie mkazo uzalishaji wa mbegu bora hapa nchini na kuzisambaza kwa wakulima kwani katika mwaka wa 2008/2009 upatikanaji wa mbegu bora ulikuwa ni tani 11,056 kati ya 30,000 ya mahitaji ambayo ni sawa na asilimia 36.8 tu ya lengo. Taasisi za Umma na Kampuni binafsi zishirikishwe katika kuzalisha mbegu bora hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa Viwanda vya kuzalisha zana za kilimo, umesababisha wakulima kuingia gharama kubwa kuagiza zana za kilimo kutoka nje ya nchi. Kamati inashauri Serikali ifufue Viwanda vya zana za kilimo kama kile cha ZZK cha Mbeya ili kumpunguzia mkulima gharama za kununua zana hizo kwa bei ya juu. Upatikanaji wa zana za kilimo uende sambamba na mafunzo ya matumizi sahihi ya zana hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Mazao ni muhimu kwani ndio msimamizi mkuu wa zao husika. Kutopatiwa fedha za kutosha kwa Bodi hizi, kumesababisha kushindwa

kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Ingawa kumekuwa na ongezeko la asilimia 34 mwaka huu, kiwango hicho bado hakitoshelezi mahitaji ya Bodi hizo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inazipa fungu la kutosha ili ziweze kusimamia mazao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za ugani ni muhimu sana katika sekta ya kilimo. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ambazo imeanza kuzichukua za kuajiri Wataalam wa Ugani ambao watakidhi mahitaji ya wakulima hususan katika ngazi ya Wilaya, Tarafa na vijijini. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuendelea kuongeza idadi ya watalaam wa ugani, pamoja na vitendea kazi ili sekta ya Kilimo iweze kufikia matarajio yaliyokusudiwa. Aidha, Kamati inashauri huduma za ugani zitolewe kwa vikundi vya wakulima (*Farmers Groups)* ili kuleta ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua umuhimu wa utafiti kwani bila utafiti, kilimo hakitaweza kukua kwa kasi inayohitajika. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuamua kuziwezesha Taasisi za Utafiti za Naliendele, Ukiliguru, Ilonga na Uyole kufanya utafiti wa mbegu bora. Aidha, shughuli za utafiti bado zinahitaji msukumo wa kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya vituo vya utafiti wa kilimo, hali ya vituo inafanana na inasikitisha kutokana na shughuli hizi kufanywa na wataalam ambao wapo kwenye umri wa kustaafu. Hali hii ni ishara tosha kuwa nchi inaupungufu wa watafiti uliosababishwa na kutoajiri wataalam hao kwa muda mrefu. Kutokana na hali hii Kamati inashauri:-

i) Serikali ihakikishe inaajiri wataalam wengi zaidi ili kuweza kuziba nafasi zinazoachwa na wataalam ambao wamefikia umri wa kustaafu;

ii) Serikali iwajengee uwezo watafiti kwa kuboresha maslahi yao na mazingira ya kazi kwa kupatiwa vitendea kazi muhimu, usafiri na makazi bora;

iii) Serikali iandae utaratibu shirikishi na endelevu wa kufikisha matokeo ya utafiti mbalimbali kwa walengwa hususan wakulima vijijini; na

iv) Tathmini zifanyike kupima manufaa ya tafiti zinazofanyika na kuboresha ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, visumbufu vya mimea na mazao. Ili kuweza kuzalisha kwa tija, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao ni muhimu sana. Kamati inashauri Serikali ifanye tafiti kwa kutumia miti asilia kwa lengo la kupata madawa ya kudhibiti visumbufu hivyo bila ya gharama kubwa. Serikali kwa hatua za dharula, ifanye utafiti wa ugonjwa wa Mpunga kukauka ambao umeleta hasara kubwa katika mavuno ya mwaka huu, ikiwa ni pamoja na utafiti wa inzi wa maembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzalishaji wa Mazao. Mazao ya chakula Kamati inashauri jitihada zifanyike kuzalisha mazao kama Mahindi, Mpunga, Muhogo, Ngano sio tu kwa kujitosheleza mahitaji yetu ya chakula bali pia kuwa wauzaji wakubwa kwenye Soko la Dunia, kwani kuna kila dalili za mahitaji ya mazao haya kuongezeka na bei yake kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matunda. Mazao kama Parachichi (*Avocado*), Matofaa (*Apples)* na Karakara (*Passion fruit*), ni vizuri kama yatazalishwa kwa wingi kwani masoko yake yanakua haraka sio hapa nchini tu bali hata nje ya nchi, hivyo uzalishaji wake utasaidia katika kuinua maisha ya wananchi na kuongeza Pato la Taifa. Kamati inasisitiza kuandaliwe

vivutio mbalimbali vitakavyowezesha wawekezaji kuwekeza katika usindikaji wa mazao ya matunda na mboga nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mazao ya Biashara. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada inazochukua za kuhakikisha uzalishaji wa mazao ya biashara unaongezeka mwaka hadi mwaka. Kamati inashauri Serikali kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya biashara kwani ndizo zinazosaidia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao hayo. Mazao ya asili ya Pamba, Kahawa, Mkonge, Chai, Korosho, Pareto, Tumbaku, Sukari n.k yaendelee kuhimizwa na kuboreshwa. Mazao mengine kama minazi pia iendelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 20 ili kuongeza bei ya zao la Pamba kutoka shilingi 360/= hadi shilingi 440/= kwa msimu wa 2009/2010. Aidha, Kamati inashauri utaratibu wa matumizi ya vocha za stakabadhi ghalani usilenge kwenye korosho tu, bali utumike kwa mazao mengine likiwemo zao la Pamba. Kamati inashauri Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha matatizo ya wakulima wadogo wa chai wa Mufindi na Rungwe yanapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wakulima, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya uanzishwaji wa Benki ya Wakulima kwani kimekuwa ni kilio cha muda mrefu cha wakulima. Kamati imefarijika na maamuzi ya Rais ya kutenga kiasi cha shilingi bilioni 20 ili zianze kutumika na Benki ya Rasilimali (*Tanzania Investment Bank – TIB*) kutoa mikopo kupitia dirisha la mikopo la Sekta ya Kilimo. Kamati inaendelea kusisitiza kuharakishwa kwa taratibu za utoaji wa mikopo hiyo ili waombaji waweze kupata mikopo kwa riba nafuu na kwa wakati muafaka. Aidha, Serikali iendelee na taratibu za uharakishwaji wa kuundwa kwa Benki ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Kama ilivyo kwa Benki ya Wakulima, Bodi ya Mazao mchanganyiko nayo ina umuhimu wake katika suala zima la Kilimo. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara kuhakikisha Bodi hii inaundwa, bado Kamati inasisitiza uharakishwaji wa Muswada wa Kuunda Bodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria kutokana na umuhimu wa *Bio-technology*, Kamati inashauri Serikali kuandaa muongozo, sheria, kanuni na taratibu za kuruhusu na kusimamia matumizi ya teknolojia hiyo. Pamoja na uandaaji wa muongozo, Kamati inashauri Serikali ianinishe mpango wa kuendeleza kilimo cha mjini hususan mazao ya mboga na matunda *(Horticultural crops*). Aidha, Kamati inasisitiza uharakishwaji wa uandaaji wa kanuni zitakazowezesha kuanza kutumika kwa Sheria ya Mbolea ya mwaka wa 2008 ambayo ilipitishwa na Bunge hili tarehe 22 Aprili, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada inazofanya za kuhakikisha inaendelea kufufua Vyama vya Ushirika vya Mazao kama Pamba, Tumbaku na Korosho. Kamati inasisitiza Serikali kuviwezesha Vyama vyote vya Ushirika kufikia malengo yake ikiwa ni pamoja na kuendelea kuvifutia madeni vyama vinavyodaiwa. Aidha, Kamati inasisitiza ukamilishwaji wa uundaji wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini ambayo itakuwa ni chombo muhimu cha kuwaunganisha wakulima, na ambacho kitashirikiana na wadau wengine kutekeleza Programu ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na nchi yetu kutokuwa na Benki ya Ardhi, Kamati inashauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kuangalia uwezekano wa kutenga maeneo kwa ajili ya Benki ya Ardhi ili yatumike kwa shughuli za uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao maoni, ushauri na mapendekezo yao katika Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika yamewezesha Taarifa hii kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Wajumbe hao ni:

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti na Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti. Wajumbe wengine, ni Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella – Bantu, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma S. Omary, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah na Mheshimiwa Kaika S. Telele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Mohamed Muya, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Sophia Kaduma pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa juhudi wanazoendeleza kuzifanya katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika na wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge hili vizuri. Aidha shukrani za pekee, ziende kwa Ofisi ya Bunge hasa Katibu wa Bunge, ndugu Thomas Kashililah na Katibu wa Kamati hii Ndugu Pamela Pallangyo, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za Maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Fungu 43 kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, jumla ya shilingi 228, 564, 587, 000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kutamka kuwa, kwa niaba ya Kamati, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SALIM KHAMIS HEMED – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuwepo hapa, tukiwa hai wenye afya na kujadili mambo muhimu yanayogusa maslahi ya umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kukushukuru wewe binafsi na Spika, kwa kunipa fursa ya kuweza kuwakilisha mawazo ya upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na ushirika kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru kiongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na

Naibu wake Mheahimiwa Dr. Slaa, Mbunge wa Karatu,  kwa kunipa ushirikiano mkubwa mwanzo hadi mwisho wa maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila, ikiwa sitakishukuru Chama changu cha *CUF* na wananchi wote wa Jimbo langu la Chambani ambao kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na kura zao, ndio sababu ya mimi kuwepo hapa leo. Nawaahidi nitakuwa nao na nitasimama kidete katika kutetea haki zao. Pia namshukuru Naibu Waziri Kivuli, kwa Wizara hii, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Jimbo la Mtambwe, kwa ushirikiano wake katika maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijatenda haki, kama sitotambua mchango na juhudi kubwa zinazofanywa na Mheshimiwa Waziri Wasira, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu nzima ya watendaji wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, katika kujaribu kurudisha heshima ya kilimo na wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010, Waziri wa Fedha, alieleza kuwa Kauli Mbiu ni Kilimo Kwanza, ingawa fedha iliyotengwa haionekani. Serikali imetenga shilingi bilioni 667 kwa sekta ya kilimo sawa na asilimia 7.0 ya matumizi yote ya Serikali. Mwaka wa fedha wa 2008/2009, sekta ya kilimo ilitengewa shilingi 513 bilioni sawa na asilimia 7.1 ya matumizi yote ya Serikali ya bajeti hiyo. Kibajeti mchango *(share)* wa matumizi ya sekta ya kilimo umebakia pale pale kama bajeti ya mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais alieleza kuwa, Serikali itatoa shilingi bilioni 20 kwa ajili ya mkopo wa riba nafuu kwa kununua zana za kilimo. Fedha hizi hazionekani katika bajeti ya Serikali. Fungu lililotengwa kwa ajili ya "*Agricultural Mechanization*" ni shilingi milioni 700 ambazo zinazotosha kuagiza matrekta makukuu 18 na zana zake kutoka Uingereza. Waziri kaeleza kuwa:-

*"Fedha hizi zitapatikana kufuatia kusainiwa mkataba wa mkopo baina ya Serikali ya Tanzania na India."*

Je, hana uhakika na kiasi ambacho hakikuingizwa kwenye bajeti hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Rais alieleza kuwa, chini ya mkakati wa kujihami na kunusuru uchumi, Serikali itatoa shilingi bilioni 20 kwa Hifadhi ya Chakula ya Taifa kwa ajili ya kuongeza akiba ya chakula na kudhibiti mfumuko wa bei. Fedha hizo hazikutengwa katika bajeti tunayoijadili. Pia hakuna bajeti ya kuongeza maghala ya kuhifadhia chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo Kambi ya Upinzani, inaona kauli mbiu ya "*Kilimo Kwanza"* ni matamshi ya Kisiasa tu, kama vile zilivyokuwa kauli zilizopita kama vile, "Siasa ni Kilimo na Kilimo Ndio Uti wa Mgongo".

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inauliza wito au kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, imeweka vipimo vya ufanisi *(Benchmarks)*?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo unasema kwamba:-

*"Ifikapo mwaka wa 2025, kilimo chetu kiwe cha kisasa, cha kibiashara, chenye tija, chenye faida na kinachohakikisha matumizi endelevu ya maliasili zilizopo na chenye kushirikisha sekta nyingine"*.

Aidha na hili ndilo dhumuni kuu la sekta ya kilimo. Maana yake ni kwamba ifikapo mwaka 2025 kilimo chetu kitakuwa cha kisasa, chenye tija na faida. Kwa kuwa Dira hii ni ya Kitaifa, itabidi kuichambua na kuifafanua ili wananchi waitafsiri katika mazingira yao. Hivyo basi, kilimo chetu ni sharti kitimize mambo yafuatayo:-

Kwanza, ni lazima kituhakikishie upatikanaji wa chakula chetu na pia kuzalisha ziada kubwa ya chakula ambayo itatumiwa kuuza nje ya nchi;

Pili, kilimo chetu ni sharti kitupatie malighafi za viwanda vyetu vilivyopo na vitakavyojengwa. Kwa kawaida, nchi inapoanza kuendelea, hujenga viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na baadaye viwanda vya aina nyingine. Uzalishaji wetu wa mazao ya aina zote bado uko chini sana na viwanda vya kusindika mazao navyo ni vichache mno;

Tatu, tunalazimika kulima mazao ambayo tutayauza nje ili tujipatie fedha za kigeni. Kwa wastani, sekta ya kilimo huchangia theluthi mbili za mapato yetu ya fedha za kigeni; na

Nne, kwa kutekeleza hayo niliyotangulia kueleza, kilimo kitatoa ajira kwa wananchi na kuchangia kwa kiwango kikubwa katika kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji, inakisiwa kuwa Tanzania ina eneo la hekta 29.4 milioni zinazofaa kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kwa mujibu wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, hekta 405,000 zikilimwa mara mbili kwa mwaka kwa kumwagiliwa zinatosha kulisha Watanzania wote na kuuza ziada nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inauliza kama hekta hizo (405,000 x 2 = 810,000) zitagawanywa kwa Wilaya zote 130 za Tanzania Bara, kila Wilaya italima hekta 6231 tu. Au zikigawanywa katika vijiji vyote 12500 vya Tanzania Bara kila kijiji kitalima hekta 64.8 tu, je, hili nalo linashindikana?

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya matatizo ya kilimo cha Tanzania, ni kukosekana kwa uwekezaji wa kutosha kutoka ndani na nje, katika nchi za wenzetu, kazi ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji, ni ya Serikali na wala siyo ya Wawekezaji na pale ambapo kuna miundombinu, wawekezaji wa maana huvutika zaidi. Hivyo basi, katika kusaidia kilimo cha umwagiliaji, mamlaka za mabonde Tanzania zinaweza kutoa mchango mkubwa kwa kukopa fedha ili kujenga miundombinu ya maji katika mamlaka zao na kuikodisha miundombinu hiyo kwa wakulima na wawekezaji. Kambi ya Upinzani inaimani kubwa kama miundombinu itakuwepo basi Watanzania wakujihusisha na kilimo wapo wengi sana, kwa kutilia maanani kuwa zaidi ya Watanzania asilimia 80 wanaishi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapitia hotuba za Wizara hii kwa miaka ya nyuma, hotuba iliyowasilishwa mwaka 2005/2006, inaonyesha kuwa uzalishaji kwa kilimo cha umwagiliaji mashambani tangu mwaka 2001/2002 hadi 2004/2005 eneo kwa hekta limekuwa likiongezeka lakini mavuno kwa kila hekta moja yamebaki kuwa ni yale yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifanya hesabu, utaona kuwa kwa miaka yote minne uzalishaji kwa hekta moja ni tani nne. Hakuna kuzidi wala kupungua. Katika akili ya kawaida jambo hili limetutia mashaka sana kama kweli takwimu hizi tunazopatiwa na Wizara huwa ni sahihi au ni za kutengeneza tu. Kwa hali ya kawaida, jambo hili katika uzalishaji haliwezekani. Tunaomba kupatiwa ufafanuzi juu ya takwimu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tumekuwa tukitenga fedha nyingi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kila mwaka mathalan mwaka jana tulitenga kiasi cha shilingi billioni 13.2, lakini mara zote hatupatiwi ni kiasi gani cha mavuno yamepatikana kutokana na uwekezaji huo. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, ni kiasi gani kimepatika kutokana na uwekezaji huo? Ili tuone kama mavuno yanalingana na fedha iliyotumika *(value for money)* katika uwekezaji huo? Vinginevyo tunakuwa tunapoteza fedha za walipa kodi bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ASDP* ni *programme* ya miaka saba ambayo bajeti yake ni Tshs 2.7 trilioni kuanzia mwaka 2006-2013 hadi sasa takribani miaka mitatu imekwishapita, tulitakiwa kuwa tumeshatumia shilingi bilioni 578.6 sawa na asilimia 21.4, lakini tumetumia Tshs.198 bilioni tu sawa na asilimia 7.3 tu. Ni jukumu la Serikali kuwaeleza wadau wake hadi sasa mafanikio gani yamepatikana kwa programu hii iliyozinduliwa kwa mbwembwe zote ikitegemewa kuwa mkombozi mkubwa wa kilimo, au programme hii imeshindwa hata kabla ya ukomo wake kufika?

Mheshimiwa Naibu Spika, inavyoeleweka, ni kwamba fedha za *DADP's* zinatokana na Programme ya *ASDP*, na utoaji wa fedha hizo unatokana na miradi inayoibuliwa na wananchi wenyewe na pia inabidi asilimia kadhaa kuchangiwa na wale watakaonufaika na mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 29, nanukuu:-

*"...vile vile, Mkoa ya Iringa, Kigoma, Mbeya, Morogoro, Rukwa na Ruvuma, imepangiwa kupewa ruzuku ya shilingi bilioni 29.2 za mpango wa maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (DADP's) kama chachu ya kuongeza uzalishaji wa chakula katika Mkoa hiyo"*. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaomba maelezo ya kina kuhusu kama utaratibu mzima wa fedha za *programme* ya *ASDP* unafuatwa, kwani dhana nzima ya *ASDP* ni wananchi kuibua miradi yao na kuchangia asilimia kadhaa ili waione kuwa miradi hiyo ni mali yao *(sense of belonging).* Ni dhahiri wenye uwezo wa kuchangia, ni wachache sana, hivyo fedha iliyotengwa ya bilioni 29.2 inaweza isitumike kwa malengo yaliyokusudiwa. Vivyo hivyo, kwa kuwa asilimia 75 ya mahitaji yote ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, ni kwa ajili ya kutekeleza kilimo cha umwagiliaji Wilayani. Serikali si mshiriki mfuatiliaji *(active partner),* hiyo husababisha fedha zinazotolewa kutokujulikana kama zimetumika kwa malengo yaliyokusudiwa au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kushiriki kikamilifu katika kila mradi unaoibuliwa na wananchi ili tuwe na takwimu sahihi ya uzalishaji ambao unalingana na fedha zilizotumika. Tofauti na hilo, ni kwamba fedha zinatolewa sadaka na tutaendelea kupiga kwata "*mark time*" katika kilimo mpaka mwisho wa dunia, kwa kuwa sera ya *D by D,* haifiki katika utendaji wa mjasiriamali mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa chakula nchini, katika hotuba ya Mhe.Waziri kwa mwaka uliopita aliliambia Bunge kuwa watu 398,504 wa Mkoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Shinyanga walikuwa wanakabiliwa na tatizo la upungufu mkubwa wa chakula. Aidha jambo la kusikitisha, ni kuwa Mkoa wa Morogoro ambao Rais aliuteua kuwa ghala la Taifa, Mkoa wenye mito zaidi ya 140 isiyokauka kwa mwaka mzima, Wilaya zake za

Kilosa, Mvomero na Morogoro zina upungufu wa chakula zaidi ya tani 63,000. Tayari Mkoa umepokea mgao wa tani 1032,375 za mchele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa Morogoro yenye fursa za maji namna hiyo, inaomba msaada wa chakula, je, hali ikoje kwa Mkoa kama Arusha, Singida, Kilimanjaro, Manyara, Dodoma na Shinyanga ambayo ni Mkoa mikame na mwaka jana ilikumbwa na uhaba mkubwa wa chakula?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaona sasa umefika wakati Serikali kuwawekea malengo ya uzalishaji wa chakula Wakuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya kulingana na jiografia ya Mkoa na Wilaya zao. Kushindwa kwao kufikia malengo iwe ndio mwisho wao wa utumishi kwa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itumie fursa ya nguvu kazi ya vijana wanaomaliza Vyuo vya Kilimo ambao wanataaluma lakini hawana mtaji kwa kuwapa mikopo na maeneo ili wazalishe chakula kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la muhogo, ni zao linaloweza kustawishwa katika eneo lolote katika nchi yetu, zao hili ni hazina kubwa ya kupambana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo inaikumba dunia kwa sasa, lakini Serikali bado haijakuwa na mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kuwa muhogo unakuwa mkombozi wa nchi yetu kwa kuuzwa nje ya nchi na pia kwa matumizi ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vya Ukiriguru na Naliendele, vikisaidiwa kifedha, zao hili linaweza kuwa zao kubwa la biashara na hivyo kuingiza fedha za kigeni kama ilivyo katika nchi za Afrika ya Magharibi hasa Nigeria. Takwimu za uzalishaji wa zao hili hapa Tanzania kwa kipindi cha takribani miaka 21 iliyopita, kutoka 1986 hadi 2007 inaonyesha tofauti ya tani 88,000. Wakati tofauti ya idadi ya watu kwa kipindi hicho ni 4,706,612 (Kitabu cha Hali ya Uchumi mwaka 2007). Hii inaonyesha ni kwa jinsi gani kilimo hicho kisivyotiliwa mkazo. Mfano mzuri wa uzalishaji wa muhogo ni Wilaya ya Newala, wananchi wa Newala wanavyotumia zao hilo kuwanusuru wananchi wenzao wa Mkoa wa Mtwara na Lindi katika vipindi vya uhaba wa chakula. Kambi ya Upinzani, inasisitiza kuwa Serikali sasa ifungue macho na Mkoa yote iliyo na historia ya kupata mvua kidogo ilime muhogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inalenga kuwa na Wagani 12,500 ili kila kijiji Tanzania kiwe na Mgani wake. Hata hivyo, idadi hii ni vigumu kufikiwa kwa sababu wenye elimu inayotakiwa *(diploma)* hawataki kujiunga kutokana na maslahi duni, hivyo Serikali kulazimika kuchukua hata waliomaliza Kidato cha Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaona kuwa, kupunguza kiwango cha elimu, ni kupunguza ufanisi wa kazi, kwa wanataaluma wa kilimo tunasema katika tasnia nzima ya kilimo hakuna "*trial and error*" kama ilivyo kwa wanataaluma wa kutibu wanadamu. Vinginevyo utamsababishia mkulima madhara makubwa na pengine kumuua kutokana na mshtuko wa hasara ya mazao yake. Mfano mzuri, ni kitengo cha Utafiti wa Chai Tanzania *(TRIT)* ambapo Wagani 6 wanawahudumia wakulima zaidi ya 1600 tena kwa ufanisi mkubwa. Hii inatokana na ukweli kwamba wanalipwa mishahara mizuri, marupurupu na kupewa fursa mbalimbali katika utendaji mzima wa kazi zao. Hii inaonyesha kuwa wingi si hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mbolea, mwaka huu Bunge lako limepitisha Sheria mpya ya Mbolea ya mwaka 2008. Lengo kuu lilikuwa ni kuwaondolea wakulima tatizo

la mbolea ambalo limekuwa likiikabili sekta ya kilimo kwa miaka mingi. Sambamba na hilo Serikali imeanzisha matumizi ya utaratibu wa vocha katika kununulia mbolea kwa Mkoa ya Morogoro, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Rukwa na Kilimanjaro kwa majaribio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, utaratibu huu wa majaribio umeonyesha upungufu mkubwa mno na kuisababishia Serikali hasara jambo lililopelekea malengo ya uanzishwaji wa utaratibu wa mbolea ya vocha yasifikiwe. Lengo limeshindwa kuondoa tatizo la wakulima kwa sababu kubwa kuwa mbolea inashindwa kupatikana muda wote na badala yake inaletwa wakati msimu umeishaanza na pengine mahitaji yanakuwa hayapo. Mfano, mbolea ya kupandia inaletwa wakati wa palizi na mbolea ya kukuzia inaletwa wakati wa mavuno. Hii inawafanya baadhi ya wakulima kuuza vocha zao kwa bei ya kutupa badala ya kuchukua mbolea kwa *"agro dealers"* makala.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi makubwa ya mbolea za viwandani kwa muda mrefu, ni hatari kwa udongo kwani inapokosekana uzalishaji wa mazao hushuka, ili kurekebisha hali hiyo inahitajika matumizi ya mbolea za asili, kama vile samadi ya ng'ombe. Mfano wa madhara hayo inajionyesha katika baadhi ya Mikoa inayojulikana kama *"the big four"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, Kambi ya Upinzani inasikitika kuwa, ng'ombe ambao kwa kiasi kikubwa wangeondosha tatizo hilo kwa kilimo, wanashindwa kuthaminiwa kiasi kwamba kila sehemu waendako, Mpanda Mashariki, Rufiji, Lindi, Kilombero wanafukuzwa na Serikali haina jibu kwa matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha matunda na mboga mboga, Tanzania inazalisha kwa wastani tani 2,000,000 za matunda kila mwaka zenye thamani ya shilingi trillion moja. Pia inazalisha wastani wa tani 1.2 millioni za mboga kwa mwaka zenye thamani ya shilingi 600 bilioni. Lakini asilimia 40% hadi 60% ya mazao hayo yanaoza mitaani kwa ukosefu wa viwanda vya kuyasindika au kuyahifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kuelewa kama tafiti zinaonyesha hivi kuwa, mazao mengi yanaharibika kwa kiasi hicho, je, hii dhana ya kilimo kwanza imefanyia utafiti suala hili kabla ya kuingizwa kwenye mipango ya Serikali? Wakulima wanachotaka si maneno tu, wanataka kuona mazao yao yanapata soko na hivyo kuwaondolea hasara wanayoipata miaka yote. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kabla ya kuingia kwenye mipango hiyo ya vitabuni ishughulikie tatizo la mazao yanayopotea/kuharibika kabla ya kufikishwa kwa mlaji kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2000, Tanzania iliuza nje matunda na mboga mboga zenye thamani ya shilingi bilioni 10.3. Hii ni neema kubwa sana ambayo Tanzania imebarikiwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwa na hali ya hewa nzuri na inayoruhusu kilimo cha matunda na mboga mboga lakini nchi imeshindwa kutumia neema hii kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ilieleze Bunge inamkakati gani wa makusudi wa kuyatumia "*hotels* na *super markets*" kununua bidhaa hizi za matunda na mboga mboga toka kwa wakulima wetu? Kama kweli Serikali iko makini na sekta hii ni lazima ianze kuonyesha kwa vitendo mikakati ya kuwainua wakulima wanaojihusisha na kilimo cha matunda na mboga mboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mfano wa kuonyesha kuwa wakulima wanazalisha lakini soko ni tatizo, ni huko Ukerewe ambako wakulima wanauza miti iliyosheheni machungwa kwa shilingi 2000/= hadi 5000/= tena kwa wageni kwa kuwa hawana namna. Je, ni wakulima wa Mkoa mingapi wanafanya kama wale wa Ukerewe? Je, huu sio wizi wa mchana kwa mtu kununua mchungwa mti mzima kwa shilingi hizo? Kambi ya Upinzani inasisitiza tena kuwa kabla ya Kilimo Kwanza, kwanza tuangalie namna ya kuwasaidia wakulima wetu kuondokana na wizi wa mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha matunda na mboga mboga, ni mwafaka katika kanda zote za nchi hii kulingana na aina ya matunda na mboga ambazo zinazalishwa. Kambi ya Upinzani inasema kwamba, sasa Serikali iamke na kuona fursa hizi na itumie wataalamu waliopo kwa kushirikiana na wananchi ambao tayari wamo kwenye sekta hii ili kuona ni jinsi gani mapato ya nchi yanavyoweza kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna mfuko wa maendeleo *wa Africa ADF(Africa Development Fund)*, unatoa msaada wa fedha kwa Chama cha Wakulima wa Embe *(AMAGRO- Association of Mango Growers),* katika Mkoa ya Tanga, Pwani na Dar es Salaam ili kuimarisha uwezo wa chama hicho. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuongeza maeneo ya kilimo hicho kwa kanda zote zenye uwezo mkubwa wa uzalishaji (*High Potential)* kwani faida yake kiuchumi ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za mazao, kutokana na mtikisiko wa kiuchumi ulioikumba dunia, bei za mazao yetu ambayo yanaitwa ya biashara *(traditional cash crops),* zimeshuka hivyo kuhatarisha maisha ya wakulima wetu wa mazao hayo. Serikali imeahidi kwa haraka sana kufidia wafanyabiashara wa zao la pamba waliokumbwa na janga hili katika msimu uliopita. Aidha, Serikali imetoa kauli ya kupandisha bei ya pamba kutoka shs.380/= hadi 460/= kwa kilo kama fidia mojawapo. Kambi ya Upinzani, inauliza kuna mkakati gani kwa wakulima wa kahawa, chai, korosho na mkonge? Serikali itatumia utaratibu gani wa kuwasaidia wakulima wa mazao hayo ambayo nayo yameathirika na mtikisiko wa uchumi uliotokea duniani kote? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kuwa bei ya kahawa ya Tanzania ni Shs.350/= kwa kilo na ile ya Uganda Shs. 600/= kwa kilo katika soko la dunia, mahesabu yamelinganishwa kwa fedha za Tanzania toka US$. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itueleze utofauti huu unatakana na nini wakati, kahawa nyingi inayouzwa na Uganda ilikuwa inatoka Mkoa wa Kagera, Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirika katika nchi yetu ulianza toka enzi za Mkoloni na ushirika ulitumika kuendeleza jumuiya za wanaushirika katika Mkoa mbalimbali. Hili liko wazi kwa watendaji wakuu Serikali enzi hizo walisomeshwa na Vyama vya Ushirika kama vile SHIRECU, KNCU, NYANZA, BCU na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ni karibu miaka nane toka Serikali ianze mkakati wake wa kurudisha hadhi ya Vyama vya Ushirika, ambayo ilipotea na kupoteza mwelekeo kutokana na uzembe, hujuma na ubadhirifu mkubwa uliofanywa na watendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali katika kadhia yote hiyo ya kulipa madeni hayo, kueleza ni watendaji wangapi waliohusika na kusababisha hasara hizo kwa ushirika wamekwishafikishwa katika vyombo vya Sheria? Mali walizoiba zimerudishwa kwenye Ushirika? Kama bado hazijarudishwa, ni kwa nini? Kwani njia pekee

ya kurudisha imani ya wananchi kuhusu ushirika, ni kwa wahusika kurudisha mali za ushirika na wao kupata adhabu stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nawashukuru sana wote kwa kunisikiliza, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salim Hemed.

Sasa kabla sijamwita Msemaji wa kwanza, nimeelekezwa kwamba hapo kwenye *Speaker's Gallery,* kuna Mheshimiwa Mzee Peter Kisumo, ambaye alikuwa Waziri wa zamani wa TAMISEMI na sasa ni Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini la CCM. Sijui kama yupo. Nadhani kama alikuwepo ametoka. *(Makofi)*

Pia tuna *Advocate,* Sam Mapande, Mwanasheria Maarufu kutoka Dar es Salaam naye sijui kama yupo. Nadhani alikuwepo sasa hayupo. *(Makofi)*

Lakini pia nafurahi sana kusema kwamba, Mheshimiwa Mwakyembe, *at last* ameingia Bungeni hapa, baada ya kunusurika kwenye ajali ambayo ilitokea. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba aliweza kunusuru afya yake. *(Makofi)*

Lakini pia, napenda kumpa pole sana Mheshimiwa Waziri wa Sheria, Mheshimiwa Chikawe, kwa matatizo yaliyompata akiwa Geneva, alipata ajali, ndiyo maana mnamwona amefungwafungwa namna hiyo. Lakini tunaamini kwamba atapata nafuu haraka kusudi aendelee na kazi zake kama kawaida. Ahsante.

Baada ya kusema hivyo, napenda niwataje watakaozungumza asubuhi hii. Atakuwa Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Oscar Mkasa, Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Mheshimiwa George Lubeleje atafikiwa. Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe nafasi ni yako angalau wananchi wakusikie kwamba bado uko hai. *(Kicheko)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruksa yako, naomba nianze kwa kutoa shukrani na vile vile kutoa taarifa kwako na kwa Bunge letu Tukufu kwamba, kwa kweli kwa neema ya Mwenyezi Mungu, hali yangu imerejea kwa kiasi kikubwa kuwa ya kawaida.

Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu wa Bunge na uongozi mzima wa Bunge letu, kwa kunihangaikia nilipopata ajali na kunipeleka nje ya nchi kwa uchunguzi na matibabu ya ziada. Nawashukuru sana tena sana, Viongozi wote Waandamizi wa nchi yetu, kwa ubinadamu mkubwa na wa pekee wanaouonyesha wananchi wao tunapopata matatizo. *(Makofi)*

Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Kikwete na Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Pinda na Mheshimiwa Mama Tunu Pinda, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi Mbalimbali waliofika hospitalini na nyumbani kwangu kufuatilia afya yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Madaktari na Manesi wa Mkoa wa Iringa. Vile vile, Manesi na Madaktari wa *MOI,* Dar es Salaam, wakiongozwa na Profesa Joseph Kahamba, kwa msaada mkubwa walionipa. *(Makofi)*

Vile vile nawashukuru sana waumini wa dini zote kwa kuniombea. Kwa kweli ndugu zangu msingi wa mimi kupona katika ajali ile pamoja na Dereva wangu Joseph Msuya, kwa kweli ni mkono wa Mungu pekee mwenye uwezo usio na kifani. *(Makofi)*

Namshukuru vile vile Balozi Hamada Nemera na Wanadiplomasia wenzake Berlin, kwa kunipokea na kunielekeza vizuri wapi pa kwenda na kunifanyia *appointments* za Madaktari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie hii sehemu ya kwanza ya kushukuru, kwa kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Wilaya ya Kyela. Baadhi yao walisafiri kutoka Kyela, kilomita karibu 1,000, kuja Dar es Salaam kunijulia hali na wengine walifunga kwa muda mrefu kuniombea. Nasema ahsante sana, ingawaje furaha yangu inapunguzwa kwa kiasi fulani na matukio ya hivi karibuni kule Kyela ambayo yamesababisha maisha ya watu kupotea, mali kuharibiwa na baadhi ya wananchi kuumizwa kwa risasi na kadhalika. Natambua kuwa Jeshi la Polisi tayari limeunda Kamati Maalum kuchunguza suala hilo.

Lakini namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, yuko hapa, kwamba kwa sababu wananchi wa Kyela wameshalalamika kwamba baadhi ya Askari Polisi walihusika kuanzisha hizo rabsha, basi ninaomba Serikali iunde Tume Huru kuchunguza chanzo cha tatizo hilo badala ya kuliachia Jeshi la Polisi lijichunguze lenyewe. Huo siyo utawala bora wala huo siyo utawala wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba nihitimishe utangulizi wangu, kwa kuuliza swali dogo kwa sababu nimemwona Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi kweli Serikali yetu, kama kweli ni ya wacha Mungu, haijui kabisa tatizo la Wilaya ya Kyela na Mkoa wa Mbeya kiasi cha watu kupoteza maisha? Hili namwachia Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 151, inayozuia tusirudierudie kutoa pongezi na kutoa pole baada ya wewe, Mheshimiwa Spika na Waziri Mkuu kufanya hivyo, basi naomba niendelee moja kwa moja kwenye bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze, kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, kwa kuwasilisha hotuba nzuri ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yao. Nitagusia masuala mawili, matatu tu kufuatana na muda ulivyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005, inaainisha upungufu kadhaa unaoifanya sekta yetu ya kilimo, kwa kweli isikue kwa kasi. Imeeleza mambo mengi, kuhusu zana duni, vijishamba vidogo vidogo, matumizi duni ya mbolea, mbegu duni na upatikanaji wa maji kwa kudra ya Mwenyezi Mungu, yaani kutegemea mvua. Ilani inataka uwekezaji zaidi katika kilimo. Naomba niisome tu kwa kifupi, ukurasa wa 27, inasema:-

*"Kuhakikisha kuwa Sekta ya Kilimo inatengewa si chini ya asilimia 10 ya uwekezaji unaofanywa na Serikali, sambamba na lengo la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Nchi za Kusini mwa Afrika, SADC".*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na malengo ya *SADC*, nchi yetu ilishiriki katika kupitisha Azimio la Maputo. Ilikuwa tarehe 12 Julai, mwaka 2003, Azimio linaitwa Azimio

la Kilimo na Hifadhi ya Chakula, *Declaration on Agriculture and Food Security in Africa*. Azimio hilo linazitaka nchi Wanachama wa *AU*, kuhakikisha kwamba bajeti zao kila mwaka zinatenga ya asilimia 10 ya bajeti ya nchi kwa ajili ya Kilimo tu na tulipewa *dead line* mwaka jana 2008 tuwe tumetekeleza agizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona nchi zingine zote ndogo ndogo tu kama Malawi, Burkina Faso, Niger, Senegal na mwaka jana Ethiopia ikavunja rekodi, ikaweka *16 percent* ya bajeti ya nchi kwa kilimo tu. Nchi hizo zote zimeweza kutimiza hilo lakini sisi, pamoja na Kauli Mbiu ya Kilimo Kwanza, kilimo ni cha nne kwa kipaumbele na kimetengewa asilimia karibu 7 ya bajeti yetu ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo dhamira nzuri, naelewa. Nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri, dhamira kuu iko *very clear* lakini tatizo letu sisi ni utekelezaji. Tuwe wakweli, hatutafanikisha mapinduzi ya kilimo kwa kusuasua katika uwekezaji wa makusudi katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Jimbo langu linapakana na Malawi. Naweza kuona mapinduzi ya kilimo Malawi kwa sababu Malawi wameshavuka asilimia 10 ya bajeti ya nchi kwa ajili ya kilimo. Leo hii Malawi wanapata mbolea yao yote kupitia bandari ya Dar-es-Salaam, lakini mfuko mmoja wa mbolea Malawi ni shilingi 7,000/= ya Tanzania. Huko ndio kuongeza uwekezaji katika kilimo na wanatumia *voucher system* ambayo tulikuwa tunataka kutumia, kama tuna matatizo basi inabidi tutume maafisa wetu, wakakae Malawi, wakaone wenzetu wamefanikiwaje. Leo hii Malawi inazalisha mahindi mengi mpaka kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala lingine. Pengine nianze kwa kusema, jina la Tanzania sasa hivi linajitokeza kwa nguvu sana kwenye maduka makubwa ya vyakula Ulaya na Marekani. Zipo *chocolate* aghali sana kwenye *supermarkets* za Ulaya, zinazozalishwa na makampuni makubwa ya *chocolate* duniani kwa mfano *Aclear, Durig Choclatie, Luzen, Lake Shoplae Chocolate* na kadhalika ambazo wanazinadi kwamba zinatokana na kokoa ya Tanzania. Sasa kokoa hii inatoka wapi? Kokoa hii inatoka Kyela na sehemu ya Rungwe, lakini Serikali haina habari kabisa na zao la kokoa. Nilikuwa naangalia hotuba ya Waziri, hata kuigusia tu, kusema jambo, hamna!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Wassira, ni kaka yangu, tunaongea sana, mara kwa mara ananisimulia ameenda nje, amepokelewa vizuri sana. Yeye anadhani anapokewa vizuri kwa sababu Tanzania kuna Serengeti na Kilimanjaro, hayo yamepitwa; ni kwa sababu ya kokoa ya Kyela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kokoa ni zao linalohitaji uangalifu sana katika kuchagua mbegu, kuotesha, kupanda, kulea, kuvuna, kuvundika kwa siku si chini ya saba na katika kutunza kwenye maghala lakini hakuna hata mtaalamu mmoja wa kilimo ambaye Serikali imemtoa kwa ajili ya zao hili. Wakulima wa kokoa wamekuwa kama yatima Wilayani Kyela na Wilayani Rungwe, wanalelewa na makampuni ya nje, yanawanyonya kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaiomba Wizara, *for the first time* mwaka huu, naomba m-*take interest* kwenye zao la kokoa. Zao la kokoa sasa hivi limeipiku dhahabu Ghana, ndio *the biggest foreign exchange earner.* Zao la kokoa ndilo ambalo linaifanya *Ivory Coast* na Madagascar leo zijivune.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Morogoro bila kuhamasishwa na Wizara yake, umeanza kulima kokoa. Mkoa wa Tanga

umeanza kulima kokoa, lakini hawana wataalamu, wanajilimia hovyo hovyo tu. Ndugu zangu Waluguru, wanapanda utafikiri wanapanda mahindi, ile ni miti mikubwa. Kwa hiyo baadaye watakuja kulazimika kung'oa, kwa sababu inafuatana sana, mti wa aina gani unapanda *four by four,* hizo ni *metres, 3.5 by 3.5* nakadhalika? Kwa hiyo, hatuna msaada. Ninaomba sana Wizara i-*take interest* katika zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumwa na wakulima wa kokoa Kyela na Rungwe, kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kuwakumbusha kwamba nao ni watoto wao. Wanasema jamani karibuni Kyela na Rungwe mje mjionee zao hilo na muweze kujua kinachowafanya Wazungu wawafurahie sana mnapokwenda nje, sio Kilimanjaro kama nilivyosema, ni kokoa ya hali ya juu. *Chocolate* inayotengenezwa na kokoa ya kule, ni very *expensive*. Ndio maana Kyela tumeendelea kuzalisha kokoa ambayo *100%* ni *organic*, hatutumii mbolea kabisa. Lakini wenzetu Morogoro na Tanga wana maeneo makubwa sana, itabidi wao waanze kutumia mbolea ili tuzalishe kokoa nyingi. Kwa sababu hakuna msukumo wa Serikali, tunashindwa kupata kiwanda cha ku-*process* kokoa hapa kwa sababu uzalishaji wetu hauzidi tani 10,000 kwa mwaka ukilinganisha na Ghana ambao wanakwenda tani 60,000 mpaka 120,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba nivitaje vijiji vichache tu vilivyonituma nimwalike Mheshimiwa Waziri, vijiji ambavyo kwa sasa vinatangaza jina la Tanzania nje ya nchi. Kwa yeyote anayekwenda nje ya nchi, naomba tu aangalie *chocolates* ataona ninachokisema. Vijiji hivyo ni Kisyosyo, Mababu, Makwale, Mpunguti, Katela, Sebe, Mahenge, Ngeleka, Isubha, Ndobho, Lusungo, Kikubha, Lukwegho, Mpanda, Lukama, Kisale, Mabhunga, Njugilo, Bhukinga, Ikama, Kyangala, Mwambusye, Mwaya, Lugombo, Masebhe, Bhuloma, Kilwa, Kajunjumele, Isanga, Nyerere, Bangamojo, Ngonga, Lugombo, Lusasa, Ikolo, Muungano ya Ikolo, Kilasilo, Songwe, Ndwanga, Itope, Mwalisi, Busoka, Masoko na Kikusya. Nimetaja makusudi tu haya majina ya vijiji kwa sababu vijiji hivi kwa juhudi zao, vimefanya jina la Tanzania sasa linajulikana sehemu zote duniani, Marekani na Uingereza, kwa kokoa nzuri vinayoizalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu sasa niseme kwamba kwa sababu pengine nimebakia na dakika moja, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waziri atakuwa amesikia na wananchi watakuwa wamesikia ulivyomwalika Waziri.

Sasa nitamwita Mheshimiwa Oscar Mukasa, maana yeye ndio mara ya kwanza kuchangia. Naomba nimpongeze sana na nimtakie heri. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru sana kwamba umenipatia nafasi ya kutoa mchango wangu leo kwenye hoja hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Lakini pia kwa namna ya pekee nakushukuru kwa sababu, hii ni mara yangu ya kwanza kabisa kuzungumza kwenye Bunge lako Tukufu, tangu nimeapishwa tarehe 10 Julai, 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupitia kwako, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa mapokezi mazuri kabisa niliyoyapata tangu nilipofika na kwa maelekezo ya shughuli za Kibunge ndani na nje ya jengo hili, ambayo nimekuwa nikiyapata tangu nilipoapishwa na ambayo ninaendelea kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa naibu Spika, pia napenda nikishukuru Chama cha Mapinduzi, kwa kunipa uteuzi ulioniruhusu kuingia kwenye mchakato ulionifikisha hapa, nashukuru vikao vyote, vya ngazi zote vilivyoshiriki kwenye mchakato huo. Pia ninawashukuru kwa namna ya pekee Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, kwa kuniunga mkono na ninamshukuru Mungu kwamba amebariki kazi ya mikono yao, lakini ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani, kwa kutoa changamoto, ni jambo jema kabisa, ila tunawaomba sasa tushirikiane, kwa sababu wananchi wa Biharamulo wameshazungumza na wametoa ridhaa kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru kwa dhati kabisa, wapendwa wangu wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, kwa kufanya uamuzi wa kutoa imani kwa Chama cha Mapinduzi na kwangu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi yangu kwa makundi yote hayo, ni kufanya jitihada za dhati kwa uadilifu na kwa bidii kubwa ili kutoa mchango wangu kwa wananchi wa Biharamulo na Watanzania kwa ujumla. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda nitoe pongezi kwa mtoa hoja, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mzee wangu, Mheshimiwa Wassira, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara husika. Nawapongeza kwa mambo kadhaa, moja ni kazi nzuri ambayo wamekuwa wanaifanya kwenye Wizara tangu Awamu ya Nne ilipoanza. Kwa ujumla, kazi yao ni nzuri, pamoja na changamoto ambazo bado zinatukabili ya kuongeza kasi ya kuona ni namna gani tunayakaribia yale malengo tuliyojiwekea. Lakini pia ninawashukuru kwa hotuba nzuri ambayo inatupa mwelekeo wa namna gani na ni nini tunataka kufanya kwa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa namna ya pekee, ninapenda nitoe mchango wangu, nilete ujumbe niliotumwa na wananchi wa Biharamulo kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na watendaji wake. Wakulima wa Biharamulo kwa kiwango kikubwa sana, wanashiriki kwenye kilimo cha mazao ya nafaka, yakiwemo mahindi. Kata zote zile nane za Biharamulo, wanalima mahindi kwa wingi sana, maharage na mtama. Kata ya Kalenge na Nyakahura, ni mahiri sana kwenye kilimo hicho. Lakini kumekuwepo na tatizo moja ambalo linakwamisha kwa kiwango kikubwa jitihada za wakulima wa Biharamulo katika kuleta mapinduzi hasa kwenye zao la nafaka ambalo wao ndio wanajihusisha nalo zaidi, nalo ni upatikanaji wa mbegu bora na sababu zipo kadhaa, lakini ninapenda nigusie chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilitoa ruzuku ya kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora kwenye maeneo mbalimbali nchini, ambapo ni jambo jema kabisa lakini maelekezo yaliyokwenda kwa Mkoa wa Kagera, ilikuwa ni kwamba ruzuku hiyo inajikita zaidi kwenye zao la chai na kahawa, ambalo ni jambo jema ukilitazama kwa ngazi ya Mkoa, ninaliheshimu sana na ninalipongeza lakini kwa Wilaya ya Biharamulo ambayo kwa bahati mbaya, yale mazao ambayo ni ya biashara kiasilia, kama kahawa, pamba na tumbaku yamekuwa yanadorora kwa sababu nyingi, kwa hiyo wananchi hawaelekezi nguvu zao huko tena. Utaratibu ulioelekeza kwamba ruzuku iende kwenye mazo ya chai na kahawa ukawa umewatenga kwa kiwango kikubwa wananchi wa Biharamulo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, kama mnavyofahamu, wamekuwa hawana msemaji kwenye Bunge lako Tukufu kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili. Kwa hiyo, hata namna ya kujitetea, kuona ni namna gani wanaweza kukwamuka kutoka kwenye maelekezo ya utekelezaji wa baadhi ya mikakati yetu, walikuwa hawana. Kwa hiyo,

wanalazimika kutumia mbegu ambazo si bora na hii inaathiri kwa kiwango kikubwa mavuno yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri, ipo sekta binafsi, sekta ya wafanyabiashara ambayo tunatambua mchango wao na tunaiheshimu sana, inajaribu kuleta mbegu za nafaka kwa wakulima wa Biharamulo lakini kwa bahati mbaya kwa sababu ni sekta inayolenga kwenye kupata faida, mbegu hizo zinauzwa kwa bei ambayo wakulima wengi hawazimudu. Kilo moja inauzwa kati ya shilingi 4,700/= mpaka 5,000/=, kiwango ambacho wakulima wengi hawakimudu. Kwa hiyo wanabaki kwenye mzunguko ule wa kulazimika kutumia mbegu ambazo ni duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukitazama, kwanza Mpango Mkakati wa *MKUKUTA* wa Kupunguza Umasikini na Kukuza Uchumi, kupitia sekta ya kilimo, utaona kabisa miongoni mwa malengo ya utekelezaji ya Awamu hii tunayoendelea nayo, ni ya kuhakikisha kwamba tunaongeza *reserve* ya nafaka kwa kiwango kinachoweza kuiwezesha Tanzania kuwa na akiba ya kututosheleza miezi minne pale tunapokuwa tumepata matatizo. Hili ni jambo ambalo la kimkakati, ni la Kitaifa, lakini linahitaji jitihada kutoka kwenye ngazi ya chini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tuliyoisikia hivi punde, kuna pengo la takribani tani 1,000 za mbegu ya nafaka ambapo inatakiwa kuzitafutia ufumbuzi, ni namna gani zitajibiwa kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wananchi wa Biharamulo tayari wamekuwa na nafasi kwamba ardhi yao ina rutuba, inaruhusu sana kilimo cha mazao ya nafaka kama mambo yote yatakuwa yamefanyika kama yanavyotakiwa; ninapenda kusikia kauli ya Waziri, ni namna gani, pamoja na mambo haya niliyoyasema, pamoja na kwamba wananchi wa Biharamulo wamekuwa hawana msemaji kwa muda sasa na kwa hiyo, wenzetu wa lugha ya Kingereza wanasema kinahitajika kitu kinaitwa *positive discrimination* namna ya kutoa upendeleo upande mmoja kwa sababu ambazo zinakubalika na ambazo zinahitajika kuwekwa ili kuwapandisha ili nao wafike kwenye ngazi ambayo wenzao wamefika kwa sababu za kihistoria. Ninapenda kusikia Waziri wetu anasema nini kuhusu hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda kuongelea tena suala la zao la muhogo. Biharamulo tumekuwa mahiri sana kwenye kilimo cha muhogo na kwa sasa soko letu la muhogo lipo kwa kiwango kikubwa sana kwenye nchi za Rwanda, Burundi na Kongo, tunauza huko kwa wingi. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, hapo awali Serikali ilikuwa imezuia kutoa mazao ya chakula na kuyapeleka nje ya mipaka ya Tanzania, lakini kwa bahati njema ninaishukuru Wizara, kwamba Biharamulo tulipewa nafasi ya upendeleo baada ya kulalamika kwa namna ambazo hazikuwa zinapita ndani ya Bunge, lakini tukasikilizwa, tukapewa ruhusa ya kuendelea kufanya mauzo ya muhogo kwenye nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado yapo matatizo mengi yanayohusiana na zao la muhogo Biharamulo. Kuna mambo ya utunzaji bora wa mazao yetu ambapo utunzaji hauwi mzuri kiasi cha kuathiri ubora wa mazao tunayoyapata; jambo ambalo linashusha ile nguvu ya soko tunayokutana nayo kwenye nchi jirani. Lakini pia lipo suala la masoko, suala la kuhakikisha kuwa tuna mazingira yanayotoa nafasi nzuri ya kupata soko la Kimataifa. Hawa wafanyabiashara ambao ni watu wa kati, wanaochukua mazao yetu kwa wananchi na kuyapeleka kwenye masoko ya nchi jirani, wanafika moja kwa moja kwa wananchi kwa sababu hakuna mpango maalum wa nguvu ya soko ya Kimataifa ambao ungeweza kuzuia wafanyabiashara hawa kwenda moja kwa moja kwa wakulima ili tuwe na mahali ambapo

nguvu ya ushirika inaweza kufanya kazi yake vizuri, tukawa na nguvu ya kupata bei nzuri. Lakini pia tukaweka mazingira ambayo yanamwezesha mkulima kupata bei ambayo inalingana na kazi ambayo ameifanya lakini na mfanyabiashara wa katikati tukaheshimu nafasi yake ya kutengeneza bei inayolingana pia na kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kusikia Serikali, kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini hili linagusa pia Wizara nyingine ya Viwanda na Biashara, ni namna gani tunaweza kukaa na wananchi wa Biharamulo tukaona ni namna gani tunatumia hiyo fursa kwamba kuna mahitaji makubwa ya zao la muhogo kwenye nchi jirani, kuweka mazingira ambayo yatatuhakikishia tunapata bei nzuri, yatatuhakikishia kwamba wale wafanyabiashara ambao wanawaunganisha wakulima na soko la nje ya mipaka ya Tanzania wanapata mazingira ambayo wao wanapata faida, lakini hawanyonyi kwa kiwango kikubwa nguvu ya wakulima. Ukiangalia kwenye Hotuba ya Wizara, tuliyoisikia punde, utaona kwamba zao la muhogo limepewa msisitizo kabisa kwamba kuna mkakati wa kuona ni namna gani tutaendelea kulibadilisha kutoka kwenye kuwa zao la chakula pekee, ili liwe zao la chakula na biashara ili liweze kuchangia kwenye *reserve* yetu ya chakula lakini pia kwenye uchumi wa wananchi wa Biharamulo na uchumi wa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo faida nyingine nyingi ambazo tutazipata kama Taifa kama tukiweka mazingira mazuri ya soko la bidhaa ya muhogo. Tutapunguza kiwango kikubwa cha wakulima na wale wafanyabiasahara wadogo wadogo kufanya mauzo ya mazao haya kwa njia za uficho. Kwa hiyo, tutaweza kupata kujibu mambo mengi sana; kwamba takwimu za kiwango gani cha chakula ambacho tunaweza kukitoa nje ya nchi tutazipata kwa urahisi. Kwa hiyo, tunaweza kujibu mahitaji ya leo, lakini pia tutaweza kujibu mahitaji ya siku zinazofuata kwa kuweza kufanya *forecasting* na kujua kwamba kama mwelekeo ni huu, basi kinachohitajika mwaka unaofuata ni hiki na ni nini kifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kushukuru kwa kupata fursa hii, lakini ninaomba nisikie kauli ya Waziri, kwamba ni namna gani wananchi wa Biharamulo ambao kwa muda mrefu wamekuwa hawana msemaji, tutapata fursa ya kuongea, kuona ni namna gani tunaweka upendeleo maalumu, kufanya positive *discrimination* ili na sisi tuweze kukimbia walao tuone ni namna gani tutajaribu kuwafikia wenzetu walipofika. Ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwanza, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupa afya na amani na mshikamano ambao tunao mpaka sasa katika nchi yetu ya Tanzania.

Pili, napenda kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Mbinga Mashariki, kwa kazi nzuri wanayoifanya kule ya kujitolea kujenga Sekondari, shule za Msingi; sasa hivi wanajenga zahanati pale Mbinga Mjini, nawashukuru sana.

Lakini sasa, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii. Mara nyingi huwa ninajisikia kama niko nyumbani katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kunipa fursa mimi na mwenzangu, Mheshimiwa Zambi, kwenda kutembelea eneo letu la mnada pale Moshi, kujifunza zaidi juu ya zao la kahawa; ninamshukuru sana pamoja na watendaji wake hasa Katibu Mkuu, Mama Kaduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninawashukuru wenzetu wa Bodi ya Kahawa, ambao walitupokea na kuifanya safari yetu na mafunzo yetu pale kuwa mazuri sana.

Lakini pia ninapenda kuwashukuru kwa namna ya kipekee watendaji wa Wizara hiyo hiyo, ndugu Mtambo na ndugu Mama Mjawa, ambao walikwenda kule Mbinga kufanya semina juu ya usindikaji wa mihogo na pia ukaushaji wa mboga mboga katika Kata za Maguu, Langiro, Mikaranga, Kigonsera, Matili, Linda, Rwanda, Mswea na Litumbandyosi. Kazi yao ni nzuri sana na niwaombe pia waendelee hivyo kwa sababu wale watu wanahitaji *follow-up.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia zipo taasisi ambazo mimi nimefanyanazo kazi kwa karibu na zimesaidia sana katika maendeleo ya Mbinga kuhusu suala la kilimo na kumsaidia mkulima. Iko taasisi ya Mtandao wa Wakulima kule Mbinga, chini ya ndugu Menas, ambayo inafanya kazi nzuri sana ya kuwashughulikia wakulima wa kahawa na mazao mchanganyiko. Lakini pia iko taasisi ya *TACRI,* hasa kituo kile cha Ugano pale Mbinga, kinafanya kazi nzuri sana, chini ya ndugu Swai, kuendeleza zao la kahawa na hasa baada ya kuingiliwa na magonjwa ya kahawa katika Kata nne katika Jimbo la Mbinga Mashariki. Lakini pia iko Taasisi ya *INADES Formation Tanzania,* ambayo Makao yake Makuu yako hapa Dodoma, nayo inafanya kazi nzuri sana kwa wakulima, hasa hapa Dodoma lakini Mbinga pia walifika kujaribu kuwasaidia wananchi wa Mbinga. Pia ipo Taasisi ya *TAHI* inayoshughulika na kilimo cha mboga mboga kule Arusha, inayoongozwa na Ndugu Jaquiline, ambayo pia wameahidi kufika kule Mbinga, mwezi wa tisa. Mwisho ipo Taasisi ya *MKURABITA* ambayo imekubali kuja kupima mashamba kule Mbinga, ninamshukuru sana ndugu Salema, kwa uzalendo wake huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo ya ujumla katika Wizara hii, mimi ninayo mawili; kwanza tunayo kauli ya ku-*modernize* kilimo. Sasa mimi ninajiuliza, tunayo miaka 48 ya uhuru na wimbo huo *modernization* tumekuwa tukiimba toka wakati wa uhuru na hasa kumfanya huyu mkulima wa jembe la mkono aondokane na jembe hilo lakini mpaka sasa hali yake bado iko vile vile. Kuna kitu gani cha ziada ambacho tunatakiwa kufanya ili tuweze kumuondoa hapa alipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kunukuu kitabu hiki ambacho kimeandikwa na *NGO* ya *INADES Formation Tanzania;* kinasema:-

*"Kwa wakulima wadogo wengi ambao wanavuna chini ya magunia 15 ya mahindi kwa hekari..."*

**NAIBU SPIKA:** Kwa ruhusa ya Naibu Spika.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako.

*"...si rahisi kumudu gharama za mbolea za viwandani, hivyo kuchelewa kupata maendeleo.''*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo msisitizo mkubwa sana juu ya mbolea za viwandani, lakini hawa ndugu wanasema kwamba huyu mkulima mdogo anashauriwa kutumia mbolea za asili ambazo hazina gharama ya fedha na zinatumia rasilimali zinazomzunguka,
ili awe na faida kubwa na abadilike haraka kiuchumi. Hii ni mbadala mmojawapo ambao hatuusikii kabisa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na wala unapozungumza na

Wataalamu wa kilimo, mbolea ambayo ipo tu inamzunguka mwananchi, zile takataka, yale majani, ambayo anaweza kutengeneza mwenyewe, akapata mbolea na hivyo anaweza akalima kwa faida kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika mambo ya ujumla, hapa napenda pia kuongelea suala la mabadiliko ya hali ya hewa. Hali ya hewa na tabia ya nchi inabadilika hapa duniani na hapa ninayo ripoti ya kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Mazingira, ninaomba ninukuu sehemu ndogo tu, kwa ruhusa yako tena. Inasema hivi:

*"The adverse impacts of climate change are already having their turn in the lives of people and in the sectors of the economy of the country. Studies undertaken during initial National communication indicates that increase in temperature by two centigrade to four centigrade, would all turn the distribution of the agro-ecological zones, consequently areas that used to grow perennial crops will be suitable for annual crops. In addition, global warming would tend to accelerate plant growth and hence reduce the length of on going seasons.''*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabia ya nchi yanaathiri sana kilimo. Katika kijiji ninachotoka pale Rwanda, mwaka jana walipanda maharage kwa kipindi kile wanachopanda miaka yote, lakini mvua hazikunyesha na maharage yale yalikauka, kwa hiyo, walikosa maharage. Sasa nilichotaka kufahamu kutoka kwenye Wizara, ni namna ambavyo Wizara inaelimisha wananchi juu ya mabadiliko ya tabia ya nchi ili mkulima asipate hasara; hilo ni jambo kubwa ambalo pia ninapenda Wizara ilichukue.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninapenda kuhamia katika masuala yanayohusu Mbinga, Jimbo la Mbinga Mashariki; kwanza ni pembejeo, mbolea. Mwaka jana tulikuwa na *system* mpya ya ruzuku na imetusaidia sana na mwaka huu tumepata mahindi mengi, lakini tatizo ni kwamba ruzuku ile inakwenda kwa watu wachache sana. Jambo ambalo mimi ninaliomba ni hili, kwamba katika maeneo ambayo yanakabiliwa na ukame mara nyingi Serikali inatafuta chakula na inapeleka kwenye eneo lile, kwa wale wenye uwezo wa fedha wananunua, wale ambao wana uwezo kidogo wananunua katika bei ya nafuu zaidi na yale makundi ambayo hayana uwezo wa kununua chakula kile wanapewa bure. Sasa kwa vile Mbinga inalima sana mazao ya chakula na kwa sababu pia kuna wananchi ambao wanashindwa kumudu kununua hii mbolea, ni kwa nini Serikali isifikirie kuwapa hawa wananchi hiyo mbolea wakalima na ziada ikachukuliwa kuwapelekea wananchi wengine? Ni *simple economics.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa mahindi. Yako mahindi mengi kule sasa hivi, wapo wanunuzi binafsi wanapitapita kule na vikopo, wanawadhulumu wale wanachi, hawapati bei nzuri, lakini tunalo ghala la Taifa, bado hawajatangaza bei, hawajaanza biashara, watanunua lini? Mpaka mahindi yanunuliwe na hawa walanguzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, *TCB*, Bodi ya Kahawa. Bodi ya Kahawa, katika mwaka 2006 tuliondoa ule ushuru ambao ulikuwa unasaidia kuendesha Bodi hizi. Ilikuwa ni azma nzuri sana kuwasaidia wakulima wetu waweze kupata kipato kikubwa zaidi na mimi ninaunga mkono sana, lakini wateja wa kahawa, sio wakulima wa Tanzania peke yake, ni wale wanunuzi wa kahawa ambao wanatoka katika makampuni mbalimbali duniani, wanazo fedha hawataki hii takrima. Kwa kweli wamefika pale kwenye Bodi ya kahawa, wameona jinsi wanavyoendesha pale mnada, zana duni, hali duni, mpaka wakaandikia *TCB* kwamba tuko tayari kutoa fedha ili muweze kujiendesha. Ni kwa nini Serikali isirudishe ushuru kwa hizi kampuni? Tulilojifunza ni kwamba wananunua kahawa hapa kwa bei ndogo zaidi kuliko

wanavyofanya Kenya. Kule Kenya, leseni wanalipia, kila kitu wanalipia; hapa Tanzania tumeondoa, kila kitu wanapata *free of charge*. Ni kwa nini tunawapa *incentive* ya namna hiyo? Mimi ninaomba hili jambo lifikiriwe kwa hawa wanunuzi wa kahawa wanaotoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili iko Sheria ya Kahawa ambayo inataka mashamba ya kahawa yote yapimwe. Mwaka jana nilizungumza hili na Wizara iliahidi kulifuatilia; mpaka sasa jambo hili halijafanyika. Mimi ninaomba jambo hili lifanyike ili wale wakulima mashamba yao yakipimwa, yakitambuliwa wanaweza wakakopesheka vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, magunia. Wakulima wa kahawa wanatakiwa kununua magunia yale ya *export bugs* na ni lazima ili kuokoa zao la katani. Sasa mimi sidhani kama zao la katani ni la wakulima wa kahawa peke yao. Hata hapa Bungeni, hili zulia tunaloliona limetoka nje ya nchi. Ni kwa nini Bunge halikulazimishwa kutumia katani? Kwa nini walazimishwe watu wanaolima kahawa tu? Mimi nafikiri hii ni *discrimination* na ninafikiri uamuzi wa Bodi ya Kahawa, wa kuondoa hilo jambo ni mzuri na mimi ninapenda sana Wizara iunge mkono uamuzi huu. Ni kwa ajili ya manufaa ya wananchi wanaolima kahawa. Si wananchi wa kahawa peke yao ndio wanatakiwa kuinua wakulima wa katani, hapana!

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirika. Mheshimiwa Waziri alifika Mbinga mwaka jana mwezi wa 10 na kuwaahidi wananchi wa Mbinga kupitia Baraza la Madiwani kwamba Serikali itajitahidi kushirikiana na Wilaya ya Mbinga, kufufua chama kile cha *MBIFACO*, ili mwaka katika msimu wa mwaka huu ambao unaanza mwezi wa nane, *MBIFACO* iweze kununua kahawa, iweze kuwa mshindani. Nafikiri sina wasiwasi na Mheshimiwa Waziri bila ya shaka atatekeleza, nilikuwa ninamkumbusha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano ni kwenye hifadhi za mazingira, katika kitabu chake cha *page* 119, katika Mkoa wa Ruvuma kuna Wilaya ya Namtumbo na Songea Vijijini. Mimi ninapenda sana Wilaya ya Mbinga ihusishwe kwa sababu katika Wilaya ya Mbinga, walikuwa na utaratibu mzuri wa kilimo cha ngolo, sasa hivi kinaachwa. Kilimo kile kilikuwa kinasaidia sana katika mmomonyoko na kuhifadhi ardhi. Ninapenda sana Mbinga iweze kuongezwa katika programu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ninapenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na mimi ninaunga mkono hoja kwa 100%. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwanza kabisa, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi lakini najua Wizara hii wanafanya kazi katika mazingira magumu, kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, bajeti ya mwaka 2008/2009, walitengewa shilingi bilioni 157 na mwaka huu, wametengewa shilingi bilioni 228. Pamoja na kwamba, ni ongezeko la asilimia kama 45 lakini bado kuna ufinyu wa bajeti kwa sababu Wizara hii ni Wizara nyeti, ni Wizara muhimu sana kwa sababu inashughulikia chakula, ambacho ni uhai, ni maendeleo na ni uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, heshima ya nchi yoyote au Taifa lolote duniani, lazima liwe linajitosheleza kwa chakula na ndiyo maana tuna Kilimo Kwanza, kwanza tujitosheleze kwa chakula na Serikali imeshatamka kwamba hakuna mwananchi atakayekufa kwa njaa lakini kuna maeneo ambayo kuna upungufu mkubwa sana wa chakula hapa nchini. Mkoa

wetu wa Dodoma na hususani Wilaya ya Mpwapwa, ina Kata kumi na nane, zaidi ya Kata kumi, zina matatizo ya upungufu wa chakula. Kwa hiyo, kwa kuwa Serikali imeshatamka kwamba hakuna mwananchi atakayekufa kwa njaa basi Serikali iweke mkakati, kama chakula kipo, waanze kugawa kwenye maeneo hayo ambayo yana upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, hivi sasa tayari mikutano ya hadhara imeshaanza hasa katika Wilaya yangu ya Mpwapwa, ya kuelimisha watu jinsi gani ya kupata chakula cha bure, chakula cha kazi pamoja na chakula cha bei nafuu. Hivi sasa debe la mahindi ni shilingi 8,000, bei ni kubwa. Kwa hiyo, naomba kama chakula kipo basi wananchi wapelekewe chakula hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni ushirika, nakumbuka Mkoa wetu wa Dodoma tulikuwa na Chama Kikuu cha Ushirika, kilikuwa kinaitwa *CRCU*. Chama hicho kilifilisika na sasa hatuna Chama cha Ushirika. Chama cha ushirika, ni ukombozi kwa wakulima na wakulima wanapata mahali pa kuuza mazao yao lakini hivi sasa tuna utaratibu mzuri sana, kila Kata hivi sasa wameunda *SACCOS*, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, hivi kama kuna *SACCOS* zaidi ya 2003, hatuwezi kuunda Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Dodoma? Hii itasaidia sana wananchi kupata mahali pa kuuza mazao yao ili wasiweze kulangulaliwa na walaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo, hivi sasa tuna upungufu mkubwa sana wa Maafisa Ugani katika ngazi za vijiji, tuviimarishe vyuo hivi, tupeleke wanafunzi wa kutosha ili kila kijiji kiwe na Afisa Ugani. Hivi sasa Maafisa Ugani, wako kwenye Kata, kwa Kata ambazo ni kubwa sana inakuwa vigumu kwa Afisa Ugani mmoja kutembelea Kata nzima, ni vigumu. Zamani, tulikuwa na Afisa Kilimo na Afisa Mifugo kwenye vijiji. Pamoja na ufinyu wa bajeti, namshauri Mheshimiwa Waziri, tuviimarishe vyuo vyetu, tupeleke wanafunzi na wanafunzi ambao wanasoma katika vyuo hivi basi wakishamaliza mafunzo wapate ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwangu Mpwapwa kuna Chuo cha Mifugo (LITI), kulikuwa na mafunzo ya *Agro-vet* yaani watu walikuwa wanajifunza kilimo na mifugo kwa sababu huwezi kutenganisha kilimo na mifugo unapojifunza *agriculture* lazima unajifunza na *livestock*. Kwa hiyo, nashauri kwamba vyuo hivyo wanafunzi wakimaliza mafunzo basi wapewe ajira moja kwa moja badala ya kutafuta wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, Mkoa wetu wa Dodoma na Mikoa mingine, tunalima sana ufuta, karanga na alizeti na mimi nashukuru sana kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia sana kuhusu kuanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko, hili ni ombi letu la siku nyingi. Tumeshalalamika kwamba kama kuna Bodi ya Kahawa, Bodi ya Pamba, Bodi ya Tumbaku, kwa nini mazao mchanganyiko kusiwe na bodi? Hizi bodi zitasaidia sana wakulima wawe na mahali pa kupeleka mazao yao. Lakini hizi ni mbegu za mafuta, tunaweza kutumia vile vile hata kukamua mafuta kwa ajili ya matumizi ya hapa nchini. Hivi sasa tunaagiza mafuta ya kula kutoka nje lakini hizi mbegu ukiwa na viwanda vya kukamulia tunaweza kuwa na mafuta ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya hapa kwetu nchini badala ya kuendelea kuagiza toka nje. Nadhani hata kodi inayotozwa kwa mafuta ya kutoka nje, ni kidogo. Kwa hiyo, naomba hili lizingatiwe kwamba tuwe na viwanda vyetu, wakulima wetu watafutiwe masoko ili wawe na mahali pa kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo machache, sina mengi, nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii, wanafanya kazi katika mazingira magumu. Kama

nilivyosema, iko haja kwa bajeti ya mwaka 2010/2011 waongezewe bajeti. Huwezi kusema Kilimo Kwanza halafu unaitengea bajeti kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo kwenye hoja hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Eneo ambalo nitapenda kulichangia bila kupoteza wakati, ni kuhusu uanzishwaji wa Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetazama katika Kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ukurasa wa 112, pale pameandikwa mistari mitano tu na mimi kidogo ikanistua, nikasema benki hii muhimu namna hii kaiandikia mistari mitano? Lakini kwenye hotuba yake alizungumza zaidi na akaweka *commitment* kwamba itaanzishwa kwenye mwaka huo wa fedha wa 2009/2010. Katika Kitabu sikuiona lakini katika *submission paper* yake aliitaja na mimi naunga mkono hoja hii kabisa kabisa. Ni muhimu sana na nasema hivyo kwa nini?

Mheshimiwa Dr. Mwakyembe alizungumzia habari ya *cocoa* kule Kyela, nilimpelekea ki-*note* nikamuuliza inachukua muda gani kwa mche wa *cocoa* kuanzia kwenye kitalu, ukiandaa mche mpaka kuvuna, ameniambia miaka mitatu. Halafu kwa upande wangu, kwenye zao la chai, miaka mitatu mpaka minne, kwenye kahawa, korosho miaka sita na mkonge miaka mitatu. Sasa tunataka Benki ambayo inazingatia mazingira haya. Benki ambazo tunazo hapa nchini isipokuwa Benki ya Rasilimali ya Tanzania, zote ni za biashara, za mikopo ya muda mfupi. Unachukua mkopo unakwenda Malyasia kule, unanunua nguo unakuja unauza zote *wholesale.* Unarudisha fedha benki, sasa mabenki yetu yanataka watu wa namna hiyo, hakuna Benki ya Wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninasisitiza kabisa kwamba pengine tufike mahali ile Sheria ya Kuanzisha Benki hii, tujue inaletwa lini, vinginevyo hii kauli mbiu yetu ya Kilimo Kwanza, kwa kweli inaweza ikaishia kwenye makaratasi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa uamuzi wake wa kijasiri wa kupeleka fedha kwenye Benki ya Rasilimali ya Tanzania kwa njia ya Dirisha. Ametuonyesha njia, sasa tuweke utaratibu, tuweke mfumo ili benki kwa kweli iweze kuwa wazi kwa watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda nieleze historia ya benki hii maana haikuanza leo. Mwaka 1985, mwezi Januari, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa, ilikaa hapa Dodoma na kuishauri Halmashauri Kuu ya Taifa kwamba iunde Timu ya Kuchambua Suala la Kutoa Mikopo ya Kilimo na Maendeleo Vijijini na Rais akachukua jukumu lake kama Rais na mwaka huo huo, mwezi wa Juni, 1995 ikaunda Timu na Timu hiyo iliongozwa na Gavana wa Benki Kuu, Marehemu sasa hivi Nyirabu na waliokuwepo katika Timu hiyo, ni Marehemu Amon Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara, alikuwemo Mheshimiwa Magani ambaye aliwahi kuwa Mbunge hapa wakati huo akiwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini. Halafu kulikuwa na wataalam watatu kutoka Zanzibar mmoja akiwa ni Meneja Mkuu wa Benki ya Wananchi wa Zanzibar, halafu wengine wamo humu Bungeni mmoja ni Mheshimiwa Mzindakaya, wakati alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro. Walifanya kazi nzuri sana. Walimaliza kazi yao mwezi Oktoba, 29, 1985 wakamkabidhi taarifa Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa bahati nzuri mimi hiyo Taarifa ninayo hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamechambua mpaka kuweka mfumo gani utumike mpaka vijijini ili mikopo hii iweze kuwafikia walengwa, kwa sababu wakati ule Halmashauri Kuu ya Taifa...

**MBUNGE FULANI:** Ya CCM!

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Haijasema CCM, wakati ule hakukuwa na Chama kingine, kwa hiyo, ukisema Halmashauri Kuu ya Taifa maana yake ni hiyo. Halmashauri Kuu ya Taifa ilisema ni Mikopo ya Kilimo na Maendeleo Vijijini ilikuwa na maana iende huko vijijini. Timu imefanya kazi nzuri sana, hata kueleza mfumo gani utumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, nadhani hii taarifa itakuwepo ofisini kwako, ingefanyiwa kazi kwa sababu utaratibu ndiyo zaidi unahitajika. Kwa mfano, mabilioni ya Mheshimiwa Rais wetu Kikwete, Bumbuli hazikufika kwa sababu Bumbuli kwa mujibu wa utaratibu wa mfumo wa benki, matawi yanaruhusiwa kwenda kwenye kipenyo cha kilomita 20 na Bumbuli ni kilomita 40 kutoka Lushoto kuliko Benki ya *NMB*. Kwa hiyo, tawi lake linaishia kilomita 20, ni kilomita 10 kutoka mpaka wa Jimbo la Lushoto. Watu wa Soni ndiyo ambao wanaweza kunufaika na hiyo mikopo, mfumo ndiyo unaotakiwa zaidi hapa. Mheshimiwa Waziri, wakati wa kujibu hoja zetu, tunapenda kujua ni lini hasa fedha hizo zitapatikana na ziko wapi? Tungetaka tuzione hizo fedha, ziko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kumekuwa na *commitment* kama mnavyokumbuka Waheshimiwa Wabunge, nilileta mimi hoja ya kujadili taarifa ya Tanzania *Investment Bank*, tarehe 12 Novemba, 2007 na katika kujibu hoja yangu Naibu Waziri wa Fedha wakati ule Mheshimiwa Mkulo alisema hivi, nanukuu:-

*"Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunakubali tutalifanyia kazi suala hili. Nataka kuwahakikishia kwamba, tutakapokuja kwenye bajeti ya mwaka 2008/2009, nadhani mambo haya yatakuwa yamekwishashughulikiwa na tunaweza kuliambia Bunge kwamba tumeafiki, tumefika hapo".*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi wakati nafunga hoja yangu, nilisema hivi, nanukuu:-

*"Nachotaka kusema ni kwamba, suala hili sio licheleweshwe tena, nimelileta leo na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Mkulo amesema litashugulikiwa, tuseme kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha ili liingie katika mwaka wa fedha 2008/2009. Namshukuru sana, sasa tulichukue hilo kama ndiyo time frame yetu".*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kwamba kwa kweli hii kauli mbiu yetu ya Kilimo Kwanza, kama itatakiwa kutekelezwa, ni hapa kwenye kuanzisha hii kazi yenyewe na hii kwa kweli sio Waziri wa Kilimo peke yake ni ya Mawaziri wote na ni ya Bunge hili. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tulishikie bango suala la Benki ya Wakulima vinginevyo tutakwama kwenye kilimo. Mimi ni mkulima wa chai. Nani atakupa mkopo wa miaka minne mpaka kuvuna? Kwa hiyo, benki hii ndiyo mkombozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu, Mheshimiwa Kumchaya pale, korosho zake zile miaka sita nani atamkopesha huyu akalime korosho angojewe miaka sita? Lakini kama nchi tunaweza kufanya hivyo kama tungeanza kuweka msingi bora wa nchi yetu kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nilitaka kulizungumzia ni kuhusu chai hiyo inayolimwa. Katika Sheria ya Chai, *The Tea Act*, Sura ya 275, ya mwaka 2002, ilianzisha Bodi ya Chai na vilevile ikaanzisha Wakala wa Chai. Ulianzishwa makusudi na tafsiri yake nzuri zaidi ni hii ya Kiingereza-Tanzania *Small Holder Growers Agency*. Hii ilianzishwa kuwasaidia wakulima wadogo waweze kujiweka na kujiimarisha na kuendeleza zao la chai. Napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna Sheria ya Chai ya mwaka 1930 ilikuwa inakataza Wakulima Wadogo kulima chai, chai ilikuwa ni ya wakubwa tu, lakini sasa hivi tunailima. Kwa hiyo, Serikali imefanya juhudi za kuunda chombo maalum cha kuwasaidia katika kuendeleza zao la chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Chai waliopewa kazi, tukakaa nao na tukaanzisha Vyombo vinaitwa *Associations* za Wakulima wa Chai, *Associations* hizo ziko Lushoto, Rungwe, Iringa na Kagera. *Association* hizi zimeunganisha wakulima pamoja halafu tumeanzisha Umoja wa Wakulima Tanzania ili matatizo yetu tuyazungumze kwa pamoja halafu tuyapeleke Wizarani. Namshukuru sana Mheshimiwa Wasira katika awamu yake ya kwanza ya Waziri wa Kilimo, tulifanya semina pale Bagamoyo ili atufahamu na tuone vipi tutakwenda na akateua Kamati ya kuangalia ni vipi tungeweza kufanya kazi tukijua kwamba wakulima wadogo hawana viwanda, viko na wakulima wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna tatizo hapa ambalo kwa kweli tungeomba Serikali iliingilie kati, ni kuhusu bei ya majani mabichi ya chai. Bodi ya Chai inaweka bei ya chini kwamba mkulima yeyote asilipwe chini ya hapo, zaidi ya hapo, mnajadiliana. Sasa kuanzia semina ya Bagamoyo ambayo ilikuwa mwaka 2007 mpaka leo tunahangaika kufikia muafaka wa bei ya kununulia majani ya mkulima mdogo. Hao wakubwa wenye viwanda hatukubaliani, hakuna muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni wakati muafaka kwa kweli tunaiomba Serikali ifike mahali tusaidiwe kufanya mchakato kuweza kujua bei ya kuuzia chai kwenye soko la dunia ni kiasi gani halafu turudi nyuma tuangalie, majani ya chai kutoka kwa mkulima mdogo yanunuliwe kwa bei gani. Kwa njia hii, tutawasaidia sana wakulima. Sasa hivi wamehamasika sana baada ya kuunda hizi *associations*, wameongeza mashamba, mashamba ambayo yalikuwa na nafasi yamejaziwa na ubora wa chai umekuwa mzuri sana na napenda kusema kwamba chai tunayolima pale Mponde, ukienda Mombasa kwenye mnada kule utapambana na chai ya Kenya lakini chai yetu inayotoka Mponde ina ubora wa hali ya juu na tutaendelea hivyo hivyo kwa sababu ndiyo masharti tuliyopewa. Tuliuziwa kiwanda na masharti kwamba chai iwe bora isiharibu soko. Hili suala la bei ni la msingi, chai unachuma kila siku, mavuno yanapungua lakini unavuna kuanzia mwanzoni mwa mwaka mpaka mwisho. Unaanza kuvuna mwanzo wa wiki, ukifika mwisho wa shamba unarudi tena mwanzo, kwa hiyo ni kazi kubwa sana lakini bei haiendani na kazi hiyo ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo sisi kwetu linatupa matatizo, ni vitendo vya Maafisa Ushirika, Mheshimiwa Waziri, wabadilike. *Association* inafanya kazi za ushirika lakini ina taratibu zake. Sasa kuna tatizo la kupiga vita hizi *Associations.* Kwa mfano mimi nashangaa Afisa Ushirika wa Mkoa anachagiza Wakulima wa Chai katika Kata waunde Ushirika wa Chai. Ushirika wa Chai katika eneo hilo lenye *Association*, haiwezekani, ni kwenda kinyume na Sheria na vile vile kuvuruga utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili sio kwamba tunalisema tu, ninayo barua hapa, nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri, inatoka Ofisini kwake. Afisa Ushirika wa Mkoa, anatakiwa waende wakakae na wananchi wa Kata ya Mponde waone namna gani

wangeanzisha Ushirika wa Chai. Hii ni kuleta vurugu, ni fujo hii. Wanatakiwa waje watusaidie sisi tufanye kazi vizuri na siyo kuunda vitu vingine katika eneo hilo hilo. Tunarudisha maendeleo haya nyuma. Barua hii ninayo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yule Afisa Ushirika wa Mkoa pale Tanga sijui amepelekwa kufanya nini? Kama haja yake ni kuja kuturudisha nyuma, alitakiwa aje atusaidie kwenye umoja huu, tufanye vizuri zaidi sio kuturudisha nyuma, kuchombeza wananchi kwamba undeni Ushirika wa Chai katika eneo ambalo kuna Umoja na hii ni aina nyingine ya ufisadi, ufisadi si huko juu tu, hata huko chini ni ufisadi huo, hata Rungwe wana tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani muda wangu umekwisha, naomba niishie hapo lakini naunga mkono hoja na tuko pamoja, hivi vi-*study* vidogo vidogo vya kuvuruga wananchi huko, tutapambana nazo mpaka dakika ya mwisho, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru umenisemea na mimi maana tumeanza kulima chai kwa nguvu.

Waheshimiwa Wabunge, sina hakika kama kuna mtu yuko tayari kuchangia kwa dakika kumi. Kwa hiyo, tukirudi mchana wafuatao wajiaandae, atakuwepo Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Samson Mpanda na wengine, watakuwa wachangiaji kama kumi na moja.

Baada ya kusema hayo, sina tangazo lingine, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.51 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, hao ndiyo wataanza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hoja hii iliyo mbele yetu.

Kwanza, napenda kumpongeza sana mtoa hoja, pamoja na timu yake nzima, yaani Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Katibu Mkuu Msaidizi, kwa kutayarisha hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi hii kwa niaba ya Wananchi wa Chunya, niweze kuipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuleta mpango mkakati huu wa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Baraza la Biashara lilipoamua hapa Dar es Salaam kwamba, nchi yetu iwe na mkakati huu wa Kilimo Kwanza, Mheshimiwa Rais alipokwenda kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika, nao waliweka uzito kwenye mkakati huo huo katika Bara la Afrika ili Bara letu liweze kujikwamua na umaskini kupitia kilimo. Naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutambue kwamba, siyo mara ya kwanza kwa Serikali yetu kuwa na mpango mkakati juu ya kilimo. Huko nyuma tulikuwa na Azimio la Iringa Siasa ni Kilimo, lilikuwepo na lilikuwa na mikakati mizuri sana kama hii lakini halikuzaa matunda, kwa sababu moja tu ambayo nitaisema hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa sababu hii wameweka mpango mkakati na vipengele vingi vizuri sana. Naomba kwa ruhusa yako, nivinukuu vichache katika mpango mkakati wa Serikali.

Kuna Dira ambayo inaonesha kwamba, njia pekee ya kuondokana na umaskini wa Tanzania ni kilimo na kuonesha dhamira ya waziwazi ya kisiasa, kubadili mwelekeo kutokana na kilimo kuwa ni cha kujikimu tu kwenda kwenye kilimo cha biashara na cha mashamba makubwa, ugharamiaji wa kilimo kama Wabunge wengine walivyochangia asubuhi kwamba, walau ufikie 10% ya bajeti yetu; Benki ya Kilimo na Vyama vya Ushirika viwezeshwe na kuhuisha muundo wa Taasisi za Kilimo; kurekebisha Sheria ya Ardhi ili vijiji vitenge ardhi kwa ajili ya uwekezaji pia kuwe na ardhi kwa ajili ya kilimo na biashara; vivutio vya kilimo; kuondoa vikwazo vya kodi na masoko; na mageuzi ya viwanda.

La mwisho ambalo mimi nataka kuliongelea ni la uhamasishaji wa umma kuhusu Kilimo Kwanza. Kwa sababu tulikuwa na Azimio la Iringa Siasa ni Kilimo, ambalo halikuzaa matunda, kwa mtazamo wangu haukuwepo uhamasishaji wa umma kuhusu kilimo, haukuwepo uhamasishaji wa Watanzania kubadililisha mtazamo wao katika kilimo, kubadilisha *attitude* yao au mtazamo wao, *attitude* ya Mheshimiwa Rais kuhusu kilimo, *attitude* ya Makamu wa Rais kuhusu kilimo, mtazamo wa Mawaziri kuhusu kilimo, mtazamo wa Naibu Mawaziri kuhusu kilimo, mtazamo wa Wakuu wa Mikoa kuhusu kilimo, mtazamo wa Wakuu wa Wilaya kuhusu kilimo, mtazamo wa Wabunge kuhusu kilimo, mtazamo wa watumishi wote wa Serikali na wananchi wote wa Tanzania kuhusu kilimo kubadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja mfupi wa nchi jirani ya Malawi; wakati Mbunge mwenzangu alipokuwa akichangia asubuhi alisema kwamba, Malawi wao pembejeo zao zinapitia Bandari ya Dar es Salaam, lakini haupotei mfuko hata mmoja, zikifika Malawi zinauzwa kwa ruzuku shilingi saba ya Tanzania kwa mfuko mmoja. Jinsi mtazamo wao …

**NAIBU SPIKA:** Shilingi saba au shilingi elfu saba?

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Shilingi elfu saba za Tanzania kwa mfuko mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jinsi walivyo na mtazamo mzuri kwenye kilimo, Rais wa Malawi, pamoja na kwamba ni nchi ndogo, alipochaguliwa mara ya pili, juzi alimteua Waziri wa Kilimo siku ya kwanza na hiyo siku ikaisha. Kwa hiyo, ikaeleweka kwa wananchi wote wa Malawi kwamba, kateua Waziri wa Kilimo na kesho yake ndiyo akaja kuteua Mawaziri wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwetu labda kwenye Serikali ijayo, ioneshe mtazamo mpya kuhusu kilimo. Mheshimiwa Rais anamteua Waziri Mkuu, akishamteua wanateua Waziri wa Kilimo kwanza halafu kesho yake wanateua Mawaziri wengine kuonesha tu kwamba, kilimo ni kwanza na kilimo ni cha muhimu na kilimo ndiyo kitatukomboa kutoka kwenye umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia akistaafu Mkuu wa Mkoa anateuliwa Mkuu wa Mkoa ambaye ni mtaalamu wa kilimo. Akistaafu Mkuu wa Wilaya anateuliwa Mkuu wa Wilaya ambaye ni mtaalamu wa kilimo. Akistaafu Katibu Tarafa anateuliwa Katibu Tarafa ambaye ni mtaalamu wa kilimo. Akistaafu Mtendaji au Katibu Kata, anateuliwa mtaalamu wa kilimo ili tuoneshe *total commitment* kwamba, tunakwenda kwenye Mapinduzi ya Kijani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama Malawi ni nchi ndogo, lakini tukiiga kutoka kwao, inaweza ikasaidia nchi yetu kuondokana na umaskini ambao tunao hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee mambo mengine mawili mazuri, ambayo Serikali imefanya katika mkakati wao. La kwanza, kama walivyoongea Wabunge wenzangu, Benki ya Rasilimali, ambayo ina dirisha la kilimo ambapo mwaka huu kama ilivyoonesha bajeti, kuna shilingi bilioni 35, naiomba Serikali siku za usoni iweze kuanzisha Benki ya Kilimo iliyo kamili ili iweze kuwahudumia wakulima na kuwapa mikopo nafuu ili tuweze kuikomboa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Serikali imeonesha kuanzia kwenye hoja ya Waziri wa TAMISEMI na Waziri Mkuu na pia hoja ya mtoa hoja wa sasa hivi kwamba, Halmashauri zitanunua *power tillers* mwaka huu wa fedha, yaani kila Halmashauri inunue *power tillers* tano, sita au hata kumi, kufuatana na uwezo na bajeti ilivyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke angalizo hapa na napiga hata magoti, naiomba Serikali Kuu inunue *power tillers* hizi kwa niaba ya Halmashauri. Kwa sababu *this is procurement* na kwenye *procurement* ndiyo ambako hela inapotea, ukiiacha kila Halmashauri inunue *power tillers* kumi au tano, watafanya madudu ya ajabu sana huko. Naomba Serikali ichukue jukumu hilo, inunue *power tillers* iwapelekee Halmashauri, halafu mtoa hoja atuambie kwamba, kutokana na *economies of scale,* ameokoa hela kiasi gani kufuatana na zoezi hilo. Naiomba sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongea wazo zuri sana hilo la *power tillers*, naomba niongelee kidogo kuhusu Zao la Tumbaku. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa anahitimisha hoja yake, aliongelea kidogo kuhusu Zao la Tumbaku na kutoa msimamo wa Serikali kwamba, Serikali inataka Soko la Tumbaku liwe huria ili wakulima wa Tumbaku waweze kunufaika na bei nzuri, yaani kuwe na ushindani. Soko la Tumbaku liwe na ushindani ili wakulima wa Tumbaku waweze kufaidika na bei nzuri. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa msimamo huu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimnukuu Mheshimiwa mtoa hoja, katika kitabu chake leo ukurasa wa 104 kuhusu Tumbaku. Sentensi ya mwisho anasema hivi: "Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wa Tumbaku, kuhakikisha wakulima wanapata bei nzuri ya Tumbaku kwa kuhakikisha unakuwepo ushindani katika ununuzi wa Tumbaku nchini."

Kwa hiyo, naye mtoa hoja anashikilia msimamo ule ule ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu aliusema kwamba, Serikali inataka kuwepo na ushindani katika Soko la Tumbaku. Namshukuru sana mtoa hoja, kwa msimamo huu wa Serikali na ninaomba waendelee kufanya hivyo ili wakulima wetu waepukane na pingu ambazo wanafungwa, kuwa na soko ambalo ni kampuni moja tu ya Tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano tena wa nchi ya Malawi; nchi ya Malawi ilichukua mbegu za Tumbaku kutoka Urambo Tabora mwaka 1966, lakini mwaka huu nchi

hii inatoa zaidi ya kilo milioni mia moja za Tumbaku. Nchi yetu ambayo ndiyo iliwapa mbegu Malawi, kufuatana na takwimu zilizomo kwenye hoja ya mtoa hoja, tunaelekea kilo milioni 60 kwa mwaka. Waliochukua kwetu mbegu mwaka 1966 wana kilo milioni 100, sisi kilo milioni 60. Hili siyo jambo zuri.

Nakumbuka mwaka 2006, aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo, aliitisha mkutano wa wadau hapa Dar es Salaam, yaani wadau wote wa Tumbaku. Wataalamu wakamhakikishia Mheshimiwa Waziri wakati ule kwamba, ikifika mwaka 2010, nchi yetu inaweza kufikia kilo milioni 100 za Tumbaku; ndivyo walivyomuhakikishia Waziri Mkuu wa wakati huo na mkutano huo na mimi nilihudhuria. Sasa utaona kwamba, mwaka huu tunakwenda kwenye kilo milioni 60, kumetokea nini? Naomba mtoa hoja aliambie Bunge lako Tukufu kwa nini hatujafikia lengo ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidiwa na Wataalamu wakati ule?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali au Wizara, itume Wataalamu waende Malawi kuangalia wenzetu wanafanya nini kuhusu Zao la Tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee Zao la Pamba. Wilaya ya Chunya kama unavyojua, msimu wa mwaka 1994/1995, ilisimamishwa kulima Pamba kwa sababu kumetokea funza mwekundu, ambaye anaharibu sana Pamba. Kwa hiyo, mpaka leo hii Wakulima wa Chunya waliokuwa wanalima pamba, hawalimi tena. Naomba nimuulize Mheshimiwa mtoa hoja; utafiti umefikia wapi kwa sababu wale wananchi hata mkiwaambia walime ufuta wanalima kwa shingo upande, ukiwaambia limeni alizeti wanalima kwa shingo upande kwani wao wanataka kulima pamba? Utafiti umefikia wapi ili tuwaambie wananchi wajue kama ni moja kwa moja hawatalima pamba au kuna mwaka watalima pamba ambayo walikuwa wamezoea kulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika hilo hilo, naishukuru sana Wizara kwamba, tuliukwa na malalamiko kwa Wakulima wa Wilaya ya Chunya, ambao baada ya kusimamishwa kulima pamba na Chama cha Ushirika cha Pamba kufutwa, walikuwa wanakidai Chama cha Ushirika. Mwaka jana na mwaka huu mwanzoni, Wizara imetuma Wataalamu Chunya kwenda kuwalipa walikuma fedha zao walizokuwa wanadai kwa zaidi ya miaka kumi; naishukuru sana Wizara. Kwa niaba ya Wananchi wa Chunya waliopata malipo yao, nakushuru sana Mheshimiwa Waziri.

Kuna kata nyingine ambazo hazijapata. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri atatuambia kata zile ambazo hazijapata zitapata lini? Nitakutajia kata hizo. Kwa mfano, waliopata ni Kata ya Mkwajuni, Kapalala, Ngwala, Guya, Mbangala, Kanga na Kambikatoto. Kata nyingine nyingine hazijapata, ambazo ni Kata ya Ifumbo, Totowe, Mbuyuni, Namkukwe na maeneo ya Kata ya Galula. Kwa hiyo, naomba mtoa hoja atuambie wananchi wa kata hizi ambazo hawajapata hayo malipo ya pamba watapata mwaka huu au hawatapata?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, sitaki kengele inigongee, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Godfrey Zambi, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Samson Mpanda.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ili niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba na mimi niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wataalamu wote na Watumishi wa Wizara ya Kilimo, kwa kuandaa bajeti nzuri na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kama alivyosema Mheshimiwa Kayombo asubuhi kwamba, mimi na yeye tulipata fursa ya kwenda TCB pale Moshi, kujifunza namna Minada ya Kahawa inavyoendeshwa. Tulijifunza sana na ninadhani elimu ile imetusaidia sana, tunaomba fursa kama hizo zitolewe kwa Wabunge wengi zaidi ili wajue namna ambavyo minada inaendeshwa. Ninapenda nichukue nafasi hii, kutoa shukrani nyingi kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Mama Kaduma, ambaye alitusaidia sana, kwani alituongoza mpaka safari ikafanikiwa. Kama Mama Kaduma yuko hapa, naomba apokee salamu zangu za dhati. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo, naomba nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Ninaomba niungane na Taarifa ya Kamati, inayosimamia Sekta hii ya Kilimo. Kwenye taarifa, wamezungumzia suala la dhana ya Kilimo Kwanza. Wamesema dhana ya Kilimo Kwanza imekuwa haieleweki vizuri na mimi naweza kusema haieleweki kwa Watanzania wengi na inanipa tabu kuielewa. Unaposema Kilimo Kwanza, unategemea kwamba kilimo kimepewa msukumo na pengine kwenye bajeti ndiyo inayokuwa ya kwanza, lakini tumeona ni kipaumbele cha nne kwenye bajeti. Mambo yaliyoelezwa, utadhani kabisa kwamba, kilimo kimepewa kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamesema sana, sitaki nilisemee sana hili, lakini ni vizuri Mheshimiwa Waziri awaeleze Watanzania, pamoja na msukumo ambao unaonekana na mambo mazuri waliyoorodhesha chini ya dhana hii ya Kilimo Kwanza; tunaposema Kilimo Kwanza tunakusudia nini hasa wakati kimsingi kwenye bajeti tunaona kimepewa kipaumbele cha nne? Watueleze vizuri na wafafanue vizuri na kwa sababu Kamati ilishatoa hilo, mimi ningependa tu kusisitiza pale ambapo Kamati iliishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie mbolea. Sisi Mbozi nadhani hata Njombe, huwezi kuzalisha bila kutumia mbolea. Kwa hiyo, suala la mbolea kwetu ni muhimu sana na niliwahi kusema mbele ya Bunge hili kwamba, Watanzania zaidi ya 98% wanaoishi Mbozi wote ni wakulima. Kwa hiyo, mbolea inabaki kuwa jambo la msingi sana kwa Wananchi wa Mbozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha ni kwamba, tumekuwa tukipata mbolea kidogo sana. Mahitaji ya mbolea katika Wilaya ya Mbozi, tunakwenda kwenye tani 30,000, lakini tunapewa karibu tani 5,000 au 6,000. Mbozi tuna kaya karibu 120,000, lakini kaya 50,000 zilifaidika na mbolea hizo kati ya kaya 120,000 tulizonazo ndizo. Maana yake ni kwamba, kaya zaidi ya 69,000 zimebaki. Tunasema kwamba, kilimo ndiyo uti wa mgongo, lakini watu hawawezi kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri kwenye kitabu chake cha bajeti, katika ukurasa wa pili, amezungumzia suala la utashi wa kisiasa kwenye kilimo. Mimi huwa najiuliza; hivi kweli Viongozi wana utashi wa kisiasa kwenye suala la Kilimo? Nadhani hatuna utashi wa kisiasa kwenye kilimo, kwa sababu tungekuwa nao tusingekuwa hapa tulipo kwenye kilimo, tungekuwa mbali zaidi. Kama tungeendeleza yale ambayo Mwalimu Nyerere na Mungu amrehemu pale alipolala, kama kweli tungeendeleza pale alipoachia, tungekuwa mbali sana.

Ametoka kuzungumza sasa hivi, kaka yangu Mheshimiwa Victor Mwambalaswa kwamba, tulikuwa na Azimio la Siasa ni Kilimo katika miaka ya 1970, tuliona Viongozi wanahamia kabisa vijijini kufanya kazi na tulizalisha chakula kingi sana, tukatumia hata tukaweza kuuza nje ya nchi. Baada ya utawala wa Mwalimu Nyerere, mambo yakaanza kuharibika, misingi mizuri iliyowekwa wakati ule ya Azimio la Arusha, yote ikamomonyolewa na kuondolewa, tukaenda kwenye uchumi wa kibepari. Uchumi wa kibepari unatufikisha hapa tulipo. Mimi nafurahi kwamba, tunakuja na dhana ya kilimo. Sasa hili la utashi wa kisiasa ambalo Mheshimiwa Waziri amelizungumzia, tuone unakuwepo ili tuondokane na suala la kuomba chakula kwa nchi kama Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee katika hili kwani nililisema pia wakati tunapitisha Sheria ya Mbolea na pia nimewahi kuuliza swali la Mbolea ya Minjingu katika Bunge kwamba, tunaomba Mbolea ya Minjingu isiletwe Mbozi. Narejea kusema kwamba, kweli Mbozi wananchi hawahitaji Mbolea ya Minjingu mpaka Serikali ifanye utafiti wa kutosha juu ya ardhi ya Mbozi, wakiridhika kwamba inaweza ikakubali katika maeneo Fulani fulani ndipo watuletee. Nimewahi hata kuzungumza na Waziri nje nikasema mkiileta sasa hivi mtakuwa mnapoteza muda na mawakala watakaopewa mbolea hiyo watapata hasara, kwa sababu hata mbolea ya mwaka jana bado iko kwenye magodauni kwani watu wengi hawajaitumia.

Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, siyo kwamba tunaikataa, lakini fanyeni utafiti wa ardhi ya Mbozi mridhike ndipo muwashawishi wananchi. Ni kweli mbolea hiyo inakubali kwenye kahawa, lakini kwenye mahindi haikubali hata kidogo. Mwananchi anapolima mahindi, anataka matokeo ya wakati huo huo siyo matokeo ya mwaka kesho. Kwa hiyo, naomba sana hili lifanyike na wananchi watakaporidhika kwamba inafaa, basi wanaweza wakaitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunaomba mbolea iletwe kwa wakati na Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu kesho, atueleze kwa sababu huu ndiyo msimu wa kilimo. Sasa hivi watu wameanza kuandaa mashamba ili mwezi wa kumi mvua itakapoanza kunyesha wanaanze kupanda. Mbolea isije mwezi wa kumi na moja, haiwasaidii wananchi. Tunaomba mbolea inapokuja ije kwa bei ambayo wananchi wanaweza kuimudu, isiwe shilingi 100,000 kwa mbolea ya DAP na Urea, ambayo ilikuwa inauzwa kati ya shilingi 80,000 mpaka 100,000. Watanzania wangapi ambao tunawategemea wanunue mbolea kwa shilingi 100,000 halafu tunategemea wazalishe? Haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niseme kwamba, tunachoomba kwenye kupandia, tungehitaji zaidi mbolea ya DAP na Urea, ambayo wananchi wameizoea sana kwa ajili ya palizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza suala la mbolea na kabla sijatoka hapa, naomba nirejee kwenye Ripoti ya Mwaka 2007/2008 ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, inayoishia Juni, 2008. Ukienda katika ukurasa wa 45 wa Taarifa ya hiyo naomba ninukuu: "Mbolea ya ruzuku ambayo haijawafikia wakulima ya shilingi 30,402,100, katika ukaguzi uliofanyika Wilaya ya Mbozi, imebainika kwamba, kiasi kikubwa cha mbolea ya ruzuku kilichukuliwa na mawakala wa mbolea ambao si waaminifu kwa ajili ya kuwauzia wakulima. Ukaguzi umebaini kwamba, mbolea hiyo haikuuzwa kwa wakulima na haijulikani ilitumikaje."

Taarifa hii ni ya CAG, nina hakika Mheshimiwa Waziri ameisoma na ninaomba anipe majibu, kwa sababu haya ndiyo tunayosema, mbolea tumepeleka kwa wananchi kumbe

hawajapata. Hapa ninaizungumzia Mbozi tu, kwani kuna Wilaya za Mkuranga, Ruvuma na sehemu nyingine, lakini nataka maelezo kwa hii ya Mbozi.

**NAIBU SPIKA:** Mwaka gani?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Msimu wa Mwaka 2007/2008. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, atupe maelezo kwamba hiyo mbolea imekwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nizungumzie kidogo suala la kahawa. Tuna soko huria la mazao mbalimbali pamoja na kahawa, lakini soko hili limekuwa ni soko holela, ununuzi wa kahawa sasa hivi unafanywa ovyo ovyo. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ichukue hatua, tunanunua kahawa mbichi, utunzaji wake haujulikani, lakini Sheria yenyewe inayosimamia kahawa inasema wazi kabisa kwamba, utaratibu wa kununua kahawa ufanywe kwa taratibu na udhibiti wa maafisa wanaosimamia. Leo sijui kule vijijini wanasimamia akina nani kwa sababu kila mtu anachuma Kahawa nyumbani kwake, anakoboa, zinakwenda. Taratibu zote anafanya anavyotaka yeye mwenyewe, sijaona mtu anayesimamia.

Tunasema kahawa iuzwe kwenye maeneo maalum yaliyochaguliwa, lakini leo hakuna maeneo hayo, kila mtu anatoa nyumbani kwake watu wanakwenda vijijini wananunua wanapeleka sokoni. Ubora wa kahawa unashuka kwa kiwango kikubwa, kwa sababu hakuna taratibu za utunzaji ambazo zinafuatwa, lakini pia wanunuzi wanakwenda kununua kwa wananchi bila utaratibu. Kwa hiyo, naomba taratibu hizi wazifuatilie.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa tunajadili *Finance Bill* hapa, Serikali ilituambia inaahirisha VAT kwenye Chai na Kahawa. Mwaka juzi nakumbuka Serikali ilipunguza kodi nyingi kwenye mazao, leo tunataka tuweke VAT tena kwenye Chai na Kahawa. Tutakuwa tunawaumiza wakulima na wakati wote kodi zinapopanda haziendi kwa mnunuzi bali zinakwenda kwa mzalishaji. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba, tunakwenda kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, mimi nadhani yale yanayowagusa wananchi wetu tusimame nayo kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Kahawa ina hali mbaya sana, mimi nilipopata nafasi ya kwenda pale niliona wana magari chakavu, jengo lao lenyewe liko kwenye hatihati sijui kesi ya jengo imefikia wapi. Ukiuliza ni kwamba, Serikali uwezeshaji ni mdogo, wanapewa mathalani shilingi bilioni moja au bilioni mbili, lakini nusu ya pesa ndiyo wanapewa mwaka mzima. Naomba Serikali iwe *serious*. Ndiyo hayo tunayosema kwamba, tuna utashi wa kisiasa na mambo haya ni lazima Serikali itimize wajibu wake, kama tuna-*approve* shilingi bilioni moja kwa ajili ya Taasisi Fulani, basi tuhakikishe kwamba hizo bilioni moja zinakwenda, vinginevyo tutakuwa tunapiga kelele hapa lakini haya mambo hayatakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana kwamba, Serikali inaendelea kuwezesha taratibu za Mfuko wa Pembajeo wa Taifa. Naomba Serikali iendelee kuangalia Mfuko huo, kwa sababu ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu na tunaweza tukafika mahali wananchi wengi wakapata matrekta makubwa kwa madogo na kwa maana hiyo, wakaweza kuzalisha vizuri ili uwezeshaji uwe mkubwa. Niombe kwamba, Mfuko wenyewe wa Pembejeo uwe na mikakati ya kufuatilia madeni kwa wale ambao wanawakopesha na wafanye tathmini sahihi kwa wale wanaowakopesha wasimkopeshe tu kila mtu wakati hana uwezo wa kurejesha mkopo na kwa maana hiyo mfuko ukaendelea kupata hasara. Hata ukikamata trekta ulilompa mtu ambalo limekaa miaka mitano, bado utaliuza kwa thamani ndogo kuliko thamani ile ambayo ulimkopesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kwa kifupi sana suala la mahindi. Mbozi tunazalisha sana mahindi, lakini tatizo letu ni soko, inafika wakati wananchi wanafungiwa soko wanaambiwa hakuna kuuza chakula nje ya nchi kama vile ambavyo Waziri amesoma kwenye taarifa yake. Unamfungiaje huyu soko wakati hujamuwekea mazingira mazuri ya kuuza mahindi yake; atauza wapi? Mwaka jana hili lilijitokeza sana, watu wana mahindi yao karibu magunia mia tano, wameambiwa wasiuze mahali popote, humpi *alternative* unataka afanye nini? Kwa hiyo, naomba Serikali inapozuia kuuza chakula kwa wananchi kama mahindi, watoe *alternative* ili wananchi wajue wapi wanakwenda, vinginevyo tutakuwa tunawapa adhabu. Kwanza, hatujawapa mbolea ya kutosha, wamejikusanya wenyewe wakanunua mbolea yao wakazalisha na sasa wamepata mahindi unawaambia wasiuze! Tutakuwa hatuwatendei haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie kidogo kwenye Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kutuletea bajeti ambayo kama itafanikiwa kama walivyopanga, nadhani suala la Kilimo Kwanza huenda likafanikiwa kwa *percent* kubwa. Ningefurahi kama bajeti ijayo mwezi kama huu mwakani, Waziri atakuja kutueleza hiki Kilimo Kwanza tumefanikiwa *percent* ngapi? Wananchi wetu wamefanikiwaje? Wamepata tija gani? Tungeweza kujua kama kweli hii sera tuliyoitunga ni nzuri na siyo ya kisiasa; ni sera ya ukweli na uwazi na hapo ndipo watu wangu wanaweza kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nataka kulizungumzia ni mazao yetu ya asili ya kwetu Kilwa Kaskazini, ambayo ni korosho. Korosho ndiyo uti wa mgongo wa Kilwa; ukizungumzia korosho ndiyo unazungumza siasa ya Kilwa, usipozungumza korosho tunakuona kama unafanya vitu vya ajabu. Sasa hivi tumebuni zao lingine la biashara la ufuta. Ufuta ndiyo zao tunalolitegemea sana kule Kilwa, ndilo tunalojipatia mapato mengi, tunaweza kuwapeleka watoto wetu shule, tunaweza kujipatia visenti vidogovidogo kama anavyosema Mheshimiwa mwenzangu hapa, vijisenti tunavipata kwenye ufuta na korosho. Kwa hiyo, ufuta na korosho ni mazao ambayo kwa kweli Kilwa tunayategemea sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo naona ni muhimu sana ni hili la mazao mchanganyiko. Mazao mchanganyiko kwetu Kilwa kuna minazi tele, kuna kunde tele, matunda tele, yaani kila kitu. Nilipokuwa nimechangia kwa maandishi, Waziri aliyepita aliniambia kwamba, tunataka tutengeneze juisi ya machungwa halafu ndiyo tupeleke Kenya. Sawa mimi sikatai, lakini sasa umeme wenyewe unapita njia tu ndugu zangu unafuata bomba la gesi unakwenda Dar es Salaam, sisi watu wa Kilwa tutafanyaje? Hiyo juisi tutaikamua vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema kwamba, suala la mazao mchanganyiko lingeundiwa Bodi kama ilivyopangwa na Bodi ile ikawahusisha watu ambao wanalima mazao ya aina hiyo kama mananasi, mikunde, minazi na kadhalika. Hapo sasa tungeweza tukatetea mazao yetu jinsi ya kutekeleza, lakini utasikia nimepata habari kwamba, mambo yatakuwa safi, Bodi ya mazao mchanganyiko itaundwa. Mara utasikia Wamasai watawekewa bodi ya

mazao mchanganyiko, sijui watu gani wanapata bodi ya mazao mchanganyiko. Watu wanaolima mazao mchanganyiko wanaachwa na sisi ndiyo wenye uchungu wa mazao yale, kitu ambacho kinatuuma kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisije nikasahau kuhusu suala la ufuta na korosho. Ufuta na Korosho bei zake zinayumba mno, leo utasikia korosho kwa mfano kilo inauzwa shilingi mia tano, siku nyingine shilingi mia sita, siku nyingine shilingi mia tatu hamsini, hata haieleweki. Ufuta safari hii kwa mfano, walianza na shilingi 1000 kwa kilo, halafu ikaja shilingi 800, ikaja shilingi 600; nikamuuliza Mkuu wangu wa Mkoa, ufuta sasa tuuze bei gani mbona bei yenyewe inayumba namna hii? Akaniambia aah, sasa inategemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote tumeitikia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ndiyo chama chetu na ninakipenda pale kiliposema kwamba, mazao haya tuuze kwenye Vyama vya Ushirika. Kweli tunacho Chama cha Ushirika cha Ilulu kule Lindi, tunauza mazao haya yote, lakini bei ndiyo tatizo. Anakuja mtu kutoka Dar es Salaam, anakwambia mimi nanunua ufuta wako kwa shilingi elfu moja kwa kilo, Ilulu anakuja anakwambia ananuua kwa shilingi mia sita kwa kilo; sasa hapo ndipo unapokuja ugomvi. Tunawawekea mipaka ya njiani ili kuzuia mazao yasitoroshwe, sawa tunazuia ili tuuze kule Ilulu, lakini na sisi tunataka kuendelea na kuendelea kwenyewe ni kupata bei inayotufaa, ambayo kulingana na kazi yetu ionekane kwamba, tunafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tabia ya kusema kwamba, watu wa Kilwa ni wavivu eti watu wa Pwani, ndugu zangu hili suala naomba lifutwe kabisa, kwa sababu watu wa Kilwa ni watu wachapakazi sana.

Tunalima mpunga, tunalima minazi, tunalima ndimu, tunalima kila kitu, ukisema uvuvi mambo yote safi kabisa, lakini utasikia tunaletewa msaada wa mahindi. Kwa mfano, wakati huu wa njaa, baada ya ukame uliotokea Tanzania nzima, kwetu mtu anapata kibaba kimoja cha mahindi akale na familia yake. Kweli jamani kibaba kimoja na kinakuja baada ya wiki mbili, tatu au mwezi; atakula nini? Hicho kibaba ni mbegu au chakula? Maana yake nashindwa kuwajibu wananchi wangu wakati wanaponiambia sisi tumepata kikombe kimoja cha mahindi, sasa Mheshimiwa Mbunge tutafanyia nini; tupike uji au ubwabwa? Nashindwa hata kuitetea sera ya chama changu, ambacho kimenieweka madarakani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependekeza kwamba, tunapoletewa chakula, basi tuletewe chakula cha kutosha angalau madebe mawili, matatu, katika familia moja ili tuweze kupata chakula cha kujikomboa kidogo na kupata siha inayofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii kuitenganisha na Maji, kwa kweli Kilimo Kwanza hakitafanikiwa. Kule kwetu kuna Mto Matandu, unapeleka maji mengi sana baharini. Mto ule tungeweza kuuwekea *embankment* kule, halafu kidogo tukaweka *spill-way ya* kupitisha maji yatakayokuwa ya ziada, tungeweza tukavuna mavuno mengi sana kwa njia ya kumwagilia, maana mto unapita Njinjo, Mitole na kwingineko. Tungeweza kumwagilia mashamba yetu vizuri kabisa na mambo yangekuwa barabara kabisa. Suala la njaa na kuombomba kila siku kwa Waziri Mkuu, sijui kwa nani lingepungua na tabia ya kusema kwamba, watu wa Pwani ni wavivu ingekoma na kutokomea moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nilitaka kulisisitiza zaidi kwamba, tuweke makinga maji kule kwetu ili tuweze kumwagilia mashamba yetu yaliyoko katika *low land*.

Mheshimiwa Naibu Spika, matrekta na hasa *power tillers* zinakuja; ninaziunga mkono kwa sababu kuna sehemu ambazo zina *lowland, power tillers* zinafaa; lakini nenda Umatumbini, ukisema Matumbi kwa lugha yetu maana yake ni milima. Sasa *power tillers* unazoleta ukaweke kwenye vilima ambako tunalima mpunga itawezekana kweli? Tuleteeni angalau matrekta mawili, matatu; Mitole ingepata mazao ya kutosha, Njinjo ingepata mazao ya kutosha, Kikole ingepata mazao ya kutosha, yaani tungekuwa watu wa kusaidia watu wengine. Hata ndugu zetu wa Kimasai na Kisukuma wanapokuja huku kwetu Kusini, wangeweza kupata faida kidogo ya kutokuwa na ugomvi na sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalima sana mahindi na mihogo. Wakati wa Siasa ni Kilimo, nakumbuka mimi nilikuwa darasa la saba, tulikuwa tunalima mihogo ya kutosha kabisa. Tulikuwa hatuwahitaji watu wa Newala, tulikuwa na muhogo unaitwa kitangali, kKitangali maana yake ni muhogo uliokaushwa ukawa mkavu kabisa. Ule muhogo ulikuwa unatwangwa unakuwa unga wa ugali safi sana, kuliko hata hizi chapati tunazokula za kawaida na tungeweza hata ku-*export.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hotuba hii ya Bajeti ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Naibu wake na Watendaji wote, ambao najua wengi wao ni wasomi sana, kwa kuandaa hii bajeti ambayo ninaiona ni nzuri sana. Kwa hiyo, natanguliza kuiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea kusema, nataka nimpongeze Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa kutembelea Kilimanjaro hususan Jimbo langu la Vunjo na akatembelea eneo la umwagiliaji la Kahe, ambako ndiko tunao mradi mkubwa wa maji wa *Lower* Moshi *Irrigation Scheme.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Kahe ikiwa ni pamoja na wale wa Vijiji vya Mawala, walishukuru sana kwa kutembelewa na Waziri Mkuu na walimueleza tatizo lao la ukosefu wa maji ya kumwagilia mashamba ya mpunga. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni msikivu, alisikia akaagiza mfereji mkubwa wa NAFCO usafishwe ili uweze kupitisha maji mengi yafike Mawala. Kazi hiyo ilifanyika vizuri, nawashukuru Watendaji walisikia, kwa hiyo, Mawala wamepata maji ya kutosha na sasa wanavuna mpunga wa kutosha. Wanamshukuru Waziri Mkuu, wanakishukuru Chama cha Mapinduzi na Watendaji wa Serikali, kwa kuitikia wito na kufanya kazi vizuri. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishukuru Serikali kwa kutoa pesa ya kutosha kutengeneza mfereji wa Kimwangamau ambao unalisha vijiji vitano. Mfereji huo ulikuwa haujapata pesa siku nyingi, lakini alipofika Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, aliagiza wapewe pesa na wamepewa pesa na sasa imebaki ni kazi ya uongozi wa vijiji hivyo vitano kusimamia ujenzi wa mfereji huo ili waweze kupata maisha bora. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wa Kilimo Kwanza, nategemea kama Serikali ilivyoagiza kwamba, watanunua *power tillers* 50 kwa kila Halmashauri, hizo *power tillers* zikienda kwenye kilimo cha mpunga, nategemea maisha yatakuwa mazuri sana kwa

wananchi wangu wa Jimbo la Vunjo. Kwa hiyo, naishukuru Serikali na kuishauri kwamba, wafanye bidii wanunue hizo *power tillers* ili zianze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Serikali hasa Ofisi ya Waziri Mkuu, itimize ahadi yake kupitia Mradi wa Masoko wa kujenga Soko la Kimataifa Himo – Njia Panda, ambapo walishaahidi na mkataba ulishasainiwa. Kwa hiyo, tunachongoja ni ujenzi wa Soko hilo. Kwa kuwa mifereji iko sawasawa, wakulima wanalima, kilichobaki ni kupata soko ili waweze kupata bei nzuri. Kwa hiyo, ninaomba Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kushirikiana na Ofisi ya Kilimo, Chakula na Ushirika; watimize hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie kwenye Kahawa: Kahawa ni zao zuri na ni tunda zuri, lina uwezo wa kuwaletea Watanzania wanaolima zao hilo maisha bora na waondokane na umaskini kabisa. Zao la Kahawa ni zao la pili Duniani, kwa kuingiza pesa ukiacha mafuta. Mafuta namba moja, halafu inafuata kahawa; nadhani wananchi wengi walikuwa hawaelewi, hata Watanzania wengi nadhani hawaelewi kama kahawa ndio zao la pili Duniani kwa kuingiza pesa. Pesa hizo zinaliwa na matajiri wachache, ambao ndio wamejipanga Duniani kununua hiyo kahawa. Pesa hiyo haifiki kwa wakulima, mkulima anapata kidogo sana. Sasa tunachotakiwa ni kutafuta utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba, bei ya Zao la Kahawa inapangwa vizuri ili wale wakulima wapate bei nzuri, wanaonunua wapate bei nzuri na wale walaji pia wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wakubwa wa kahawa Duniani ni Colombia, Brazil na sasa hivi Vietnam inakuja kwa kasi sana na inalima *Robusta* kwa wingi sana. Sasa wakulima wa Afrika ni pamoja na Tanzania, Uganda, Ethiopia, Congo, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kahawa ya Tanzania ni kahawa ambayo inatumika kukoleza kahawa nyingine Duniani ili iweze kupata harufu nzuri ama iweze kupata ladha nzuri. Kahawa ambayo inahitajika sana katika kukoleza ni kahawa ya Kilimanjaro. Kwa hiyo, kahawa ya Kilimanjaro ambayo inafanana pia na kahawa ya Kigoma na Mbinga, *Arabica* ni sawa sawa na *Mild Arabica* ya Colombia; sasa hiyo haiwezi ikakosa soko, ndio maana inanunuliwa yote kila msimu. Tatizo, je, upangaji wa bei uko namna gani? Ndio hapo ambapo tunakosana na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningetegemea Ushirika iwe ndiyo nguzo kuu ya kuleta bei nzuri kwa wakulima, lakini cha kushangaza Ushirika ndio wanaopanga bei ndogo kuliko hata wanunuzi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimu uliopita, Ushirika kwa mfano kama KNCU, walinunua kahawa kwa shilingi 1,500 kwa kilo, lakini wakapanda mpaka shilingi 1,800. Wakulima waliouza kahawa moja kwa moja bila kupitia mnadani; kahawa safi ya Kilimanjaro Arabica walipata kilo shilingi 3,000, kahawa safi ya Kigoma walipata kilo shilingi 3,600 na kahawa safi kutoka Mbinga ilikuwa shilingi 3,100 kwa kilo. Sasa Ushirika ambao ndio tegemeo la wakulima, badala ya kuangalia mfumo wa bei unakwenda namna gani ili na wao wapange bei nzuri, wao wanapanga bei ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale matajiri ambao ndio wananunua kahawa yote Duniani, wanapokuja kununua kahawa wanauliza hivi hawa wenye kahawa yao wamepanga bei gani? Mfano, wiki iliyopita nilikuwa naangalia TV, bei elekezi ya Kagera ambao wanalima *Robuster* ni shilingi 350, lakini bei wanayonunua wanunuzi binafsi ni shilingi 450 mpaka shilingi 500, hata kule Tarime na Uganda ni shilingi 700. Huyo mkulima ataacha

kwenda kufuata bei ya shilingi 700 au 450 aende akafuate Ushirika ambao ndio tegemeo lao? Wao ndio wanaotuangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, aliwahi kusema wakati anafungua Chuo Kikuu Kishiriki cha Moshi kwamba, Ushirika wamegeuka mchwa, tena mchwa hawa wabaya wanakula mbao hadi bati lakini ndio tunawategemea! Sasa ninawashauri, pamoja na kwamba bado mchwa hao wapo, naweza nitoe mfano; angalia *Cooperative Building* pale Mnazi Mmoja Dar es Salaam, lile jengo lilijengwa mwaka 1962 mpaka leo hawajaongeza hata *room* moja! Angalia Nyanza, majengo yameuzwa sasa yana mgogoro; angalia KNCU walikuwa na magari mengi sana yote yameuzwa na Serikali bado inaendelea kuwabembeleza Ushirika na kuwapa pesa, lakini inatakiwa ipeleke wataalam vizuri kule wawasimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri, wakulima wa kahawa kwa kushirikiana na Wizara na *Tanzania Coffee Board*, wapange bei elekezi ya msimu huu; *Arabica Coffee* iwe ni shilingi 2000 mpaka 2500 kwa kilo na *Robusta* iwe ni shilingi 700/= hadi 1000/= kwa kilo.

Hawa wanunuzi wakubwa nawafahamu; wapo akina Volcafe. Mheshimiwa Zambi, alikuja kwenye mnada na mimi nilikuwepo, Volcafe, Newman na Chibu, wote wanakaa meza moja. Utakuta kwenye mnada kuna wanunuzi zaidi ya 20, lakini baba zao ni hao watatu. Kwa hiyo, wanauliza hawa wakulima wenyewe wamepanga shilingi 1200, basi sisi tufanye 1300. Wangepanga shilingi 2000 na wao wangenunua shilingi 2000 na zaidi, kwa sababu hiyo kahawa inahitajika kwa ajili ya kwenda kukoleza kahawa nyingine Duniani. Kwa hiyo, naiomba Wizara na Tanzania Coffee Board pamoja na Ushirika, wakae pamoja wahakikishe kwamba, bei ya kahawa haiwezi kushuka chini ya shilingi 2000 kwa kilo kwa Arabica na shilingi 700 mpaka 1000 kwa Robusta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kahawa iweze kuheshimika Kilimanjaro sasa na walime. Nashauri kwamba, miche ya kahawa wagawiwe wakulima na mifereji yote ya asili ya zamani ifufuliwe ili inyweshe kahawa hii mpya. Halafu na hii bei ya shilingi 2000 ipangwe na isimamiwe na Tanzania Cofee Board pamoja na Ushirika; na mbolea itolewe. Kwa hiyo, mkulima atajua kwamba analima anategemea bei ya shilingi 2000 mpaka 2500. Kwa hiyo, mkulima asipokuwa na matagemeo ya bei nzuri hawezi kulima, kwa nini asitafute biashara nyingine! Kahawa ndio zao la pili Duniani kwa kuingiza pesa, lakini kwa kukosa kusimamiwa na Serikali, bei ya wakulima inakuwa ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno hayo, nadhani ni kengele ya pili. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nianze na mimi kuipongeza Wizara, Waziri, Naibu na Watendaji kwa hotuba nzuri. Niwapongeze zaidi wakulima wangu wa Wilaya ya Ludewa, kwa juhudi zao kubwa katika kuzalisha mazao ya chakula na kuchangia kwa kiwango kikubwa sana kulisha sehemu kubwa ya Watanzania ambao wana upungufu wa chakula. Natarajia kilimo cha umwagiliaji, ambacho maandalizi yake yanaendelea kwa kasi katika Wilaya ya Ludewa, kitachangia sana kutoa chakula kingi kitakachoweza kuwasaidia Watanzania wenzetu ambako chakula hakitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ningependa nizungumzie kuhusu mpango mzima wa Kilimo Kwanza. Naomba nioneshe kutoridhishwa kwangu kwa jinsi fedha ilivyopangwa chini

ya mpango huu; ni nyingi sana, siamini kama inawafikia wakulima wa kawaida moja kwa moja. Nataka nioneshe vipengele mbalimbali ambavyo vinanisaidia kunipa wasi wasi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa 76, vifungu vya 119 na 120 vya kitabu cha bajeti kuhusu kauli ya Kilimo Kwanza, inaonesha kuwa mpango mzima wa kilimo ni nadharia au dhana, kwa vile inazungumzia vitu vinavyotakiwa kufanywa, vinavyotegemewa kufanywa na siyo kwamba tutafanya vitu vifuatavyo ili kutekeleza dhana hii. Inasema, vinavyotakiwa kufanywa na ukisoma kwenye kitabu inaeleza kabisa itatakiwa kushirikiana na watu fulani na wadau mbalimbali; inahitaji kupima mashamba yanayotakiwa kwa ajili ya wawekezaji wakubwa. Haisemi tutapima mashamba na kuvutia wawekezaji wakubwa na kuwaonesha wakulima wadogo wakalime wapi kwa utaratibu upi. Kwa hiyo, ni nadharia kuonesha inawezekana itakuwa hivi. Itakuwa hivyo lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaanza sasa. Mimi nilitegemea kwamba, mkakati wa kutekeleza dhana hii ya Kilimo Kwanza ingekuwa imejipanga vizuri na kutuonesha vizuri jinsi itakavyotekelezwa. Humu haioneshi hivyo, inaonesha bado ni dhana kwamba, inatakiwa ifanywe kwa utaratibu kama unavyooneshwa kwenye kitabu katika kifungu kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika katika kifungu cha 121, nilitarajia Programu ya ASDP ioneshe uhusiano kati ya wadau mbalimbali, watakaohusika katika Mpango huu wa Kilimo Kwanza, kwa kuonesha mafungu ya pesa watakazopewa wadau mbalimbali au walizotengewa wadau mbalimbali na kazi zao watakazozifanya katika kuchangia Kilimo Kwanza na kuonesha mategemeo ambayo tunategemea kila mdau atachangia kwenye uzalishaji; uwe wa kilimo cha chakula au kilimo cha mazao ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitarajia bajeti itaonesha mchanganuo kama ni watu wa Magereza, huko tumepeleka kiasi gani, kama ni *National Service*, tumepeleka kiasi gani, kama ni watu wa mbegu, kuna fedha kiasi gani kwa ajili ya kuzalisha mbegu kiasi gani. Mimi nilitaka mchanganuo unaoonesha mafungu ya fedha tumeyaweka wapi, hawa wote watafanya kazi zipi na watachangia vipi katika mpango mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hayo mimi sikuyaona, kwa hiyo, mkakati mzima na upangaji wa dhana nzima haukunifurahisha hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata matumizi ya fedha za ASDP, kurasa za 79 na 123 zinazungumzia uratibu na usimamizi na manunuzi ya vyombo vya kutumia watendaji na wataalamu mbalimbali, haisemi ni vipi kama alivyosema Mheshimiwa Zambi. Je, kule chini watachacharika vipi wataalamu hawa na wagani wataishi vipi na wananchi wanahamia vijijini na kuwasaidia moja kwa moja katika kilimo na kuhakikisha kwamba kilimo kinakuwa endelevu na tunapata mazao ya vyakula tunavyotaka? Utakuta fedha nyingi zinaelekea zitatumika kununua magari, mikutano, mafunzo na kadhalika, lakini mtu wa kawaida, mkulima mwenyewe, atafikiwa kwa mbali sana, yaani kama matone ya mvua haimgusi sana. Kwa hiyo, matokeo yake katika mpango mzima huu, unanipa wasiwasi sana kama kweli mwisho wa mwaka kesho tutakapozungumzia, tutaona kumekuwa na *impact* kubwa ya dhana hii ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kuelekeza Halmashauri kuwapatia pikipiki wataalamu ngazi za Kata na kuwapangia ratiba za kazi kwenye vijiji na vitongoji ni mzuri, ndio vitu ambavyo nilitaka nivione zaidi. Hata kama vocha za ruzuku zimeongezeka sana safari hii, haitasaidia kitu kuongeza hizo vocha kama hatukuzingatia mapema maandalizi ya mashamba, kuteua hawa mawakala mapema, kuwapa mafunzo mapema na mawakala

wamepatikana wapo tayari, mbolea zinapelekwa mapema tunasimamia kilimo kinaanza mwezi gain. Sisi Ludewa tunaanza kutayarisha mashamba mwezi wa Septemba. Ratiba iko wapi inayoonesha kwamba kwa ujumla wakulima wa mahindi katika Nyanda za Juu labda kwa mfano waanze mwezi gani kuandaa mashamba na ifikapo mwezi gani mbolea ziko kwenye *site* na wananchi wanaanza kutumia mbolea ya kupandia? Sasa nilidhani vitu vidogo vidogo kama hivi ndio vya kawaida vya kucheza navyo wagani na wataalamu na wakulima kwenye vijiji na vitongoji. Nilitaka fedha ielekezwe kwenye mambo hayo ili tufanye mabadiliko, kuliko kuzungumzia nadharia kwa ngazi za juu, lakini kule vijijini *impact* hatuioni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimependezwa sana na suala la matumizi bora ya ardhi na hifadhi ya mazingira, kwa maelezo marefu tu ya kuridhisha katika bajeti ya Waziri, imenitia moyo sana hasa ukurasa wa 116 namba 183. Hata hivyo, nasikitika kuona kwamba, Mheshimiwa Waziri anasema Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itafanya kazi ya kusimamia na kutoa ushauri wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo. Mimi nilitegemea watueleze, kwa mfano, watazuiaje kilimo ambacho hakikubaliki kwenye maeneo ambayo hayafai kwa kulima. Wametoa mifano ya Wilaya na maeneo ambayo wanalima kwenye miteremko mikali, kuna mgogoro kati ya wakulima na wafugaji. Sasa mimi nilidhani waseme watatumia mbinu gani kuzuia mambo haya yasiendelee kufanyika, kwa sababu nchi nzima sasa hivi tunafungua mapori kwenye miteremko mikali *everywhere*, lakini hakuna mtu anayejali pamoja na Wizara ya Kilimo. Nilidhani katika kuzungumzia matumizi bora ya ardhi na kupanga matumizi, wangeweza kutusaidia kusema moja kwa moja kwa uwazi ni nini kinatakiwa kufanywa na nini kisifanywe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimewahi kulalamika mara nyingi hapa Bungeni kwamba, sisi kule Ludewa kuna mpango mkubwa wa kuchimba madini ya chuma na makaa ya mawe na kujenga viwanda pamoja na Kiwanda cha Umeme Mchuchuma. Nikasema kwamba ili matatizo yanayotokea Kaskazini yasitupate sisi kule, kuwe na *land use plan* nzuri na matumizi bora ya ardhi yapangwe. Nimeona kwenye Wizara hii wanazungumzia Wilaya kadhaa kutakuwa na fedha kwa ajili hiyo. Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, mbona nimepiga kelele sana hapa Bungeni kwa nini Wilaya ya Ludewa mnaipuuza ambako kutakuwa na matatizo kabisa ya mgongano kati ya kilimo na mifugo na viwanda na uchimbaji wa madini, tufanye *land use plan* kule tuwe na uchimbaji endelevu, viwanda endelevu, kilimo endelevu na ufugaji endelevu. Eneo hili linalima sana mahindi kwa wingi, linauza mahindi kwa wingi; kwa nini hatusaidii eneo lile likawa na maendeleo endelevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika katika ukurasa wa 119 kifungu cha 188, Wizara inazungumzia kufanya tathmini ya kimkakati ya mazingira ya mpango huu wa Kilimo Kwanza na imetoa mfano wa Wilaya ambako hii itatokea na mambo haya nimesema hata kule Ludewa tunahitaji kitu kama hicho, baada ya *land use plan* ile itahitajika kufanya tathmini ya athari ya mazingira, itusaidie kujua tutapata matatizo gani huko mbele. Hili ni eneo ambalo linalima sana mahindi, lakini humu wanazungumzia kuhusu mabadiliko ya tabia nchi. Maeneo yatakayoathirika sana hapa nchini ni maeneo ya Nyanda za Juu. Ukisoma kwa mfano mabadiliko ya *temperature* wakati maeneo mengine yanakuwa yamefikia 0.2 *degrees* milimani kule kama Ludewa iko 0.6 *degrees*. Kwa hiyo, maeneo ya Nyanda za Juu yanaathirika zaidi, ningetegemea hata hizi tathmini pamoja na matumizi bora ya ardhi, vile vile mngezingatia maeneo ya Nyanda za Juu pamoja na Wilaya ya Ludewa, ambayo nasema kwamba kutakuwa na matatizo sana ya matumizi ya ardhi. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, hebu iangalieni kwa jicho la pekee Wilaya ya Ludewa, imeachwa kwa muda mrefu sana, lakini tunazalisha chakula kingi kwa ajili ya nchi hii. Wananchi wa nchi hii tusaidieni matumizi bora ya ardhi kule, pamoja na tathmini ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anazungumza alisema kuna zaidi ya shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya watakaokosa chakula. Mimi katika Kata yangu ya Makonde, Mwambao wa Ziwa kule, kulikuwa na *land slide* kubwa sana, ikazoa chakula chote cha wananchi. Tumepeleka maombi mpaka kupitia RCC yamepelekwa kwa Waziri Mkuu, hivi ninavyozungumza wanahangaika na chakula hamna kimepelekwa kule. Mheshimiwa Waziri, tusaidie chakula hiki mnachokizungumza na fedha hizi tunazopitisha ziwasaidie Wananchi wa Makonde. La mwisho kabisa, mwaka jana mlinunua mahindi asilimia karibu 60 chini ya ilivyotarajiwa, kwa sababu fedha hazikutosha bei zikapanda sana. Mmejipanga vipi kwa mwaka huu ambapo bei zita-*fluctuate* sana kwa kuwa shida ya chakula itakuwa kubwa kuliko ilivyokuwa mwaka jana? Je, mmejifunza nini kutokana na matatizo ya mwaka jana ili tuhakikishe kwamba hayo hayatokei katika msimu huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nashukuru kwa kunipa fursa, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa nitamwita Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Cynthia Ngoye ajiandae, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura ajiandae na Mheshimiwa Mpina pia.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, kwa hiyo, inawezekana nisizungumze sana lakini ninayo machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda niipongeze sana Serikali kupitia Wizara hii, kwa kuongeza maeneo ya mbolea ya ruzuku, lakini vile vile na kuongeza fedha kwenye mbolea hii ya ruzuku. Kwa hiyo, sasa hivi tutakuwa na fedha nyingi lakini na maeneo vile vile yameongezeka. Nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kutuongezea tena Wilaya nyingine kwenye Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Urambo. Mwaka jana, Wilaya ya Sikonge tulifanya vizuri, mwaka huu tunaendelea na Wilaya ya Urambo. Mimi nina hakika hatua kwa hatua basi azma ya kuendelea kwa maeneo mengi sana nchini juu ya suala hili la mbolea ya ruzuku basi litapatiwa ufumbuzi. Ninachoomba, vocha ziwahi lakini vile vile mbolea nazo zifike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nianze moja kwa moja na suala la watumishi. Hali ya Watumishi wa Kilimo ni mbaya sana. Kama huna watumishi wazuri kule vijijini, huna wataalam, huna mabwana shamba na mabibi shamba, kusema kwamba tutapata Mapinduzi ya Kijani, mimi nasema tutapata Mapinduzi Mekundu, maana hakuna mkulima ambaye anaweza akalima bila maelekezo mazuri na kufuata kanuni bora za kilimo kama wataalam hawapo. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali, tukiendelea tu kuwalaumu wataalam kwanza ni wachache na sidhani kama jitihada za kuendelea kuwatoa kwa wingi katika vyuo kuwapeleka vijijini zinafanyika kikamilifu. Mimi mwaka huu nimepata mmoja, Wilaya yenye vijiji 43, walioko vijijini wanaofanya kazi wako watano ukiacha wale walioko ofisini. Hawa watano unaweza ukafikiri kwamba, unaweza ukafanya mabadiliko ya kuleta kilimo kiwe kizuri kweli, unaongezewa mmoja, kwa hiyo wanafika sita, pale tunacheza.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba turejee huko nyuma. Tulikuwa na mabadiliko makubwa sana ya kilimo, tukazalisha sana mazao ya biashara na mazao ya chakula kwa sababu zifuatazo: Mimi nilikuwa nasomasoma sana vitabu vya zamani nina kitabu hapa cha Siasa ni Kilimo, sasa nitakapokuwa nasema Mheshimiwa Naibu Spika, utaniruhusu kunukuu baadhi ya vifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuna sehemu hiyo ya kwanza ya wataalamu, nilikuwa niombe sana Serikali ijikite kadiri ya uwezo wake, kuhakikisha kwamba, wataalam wanapatikana kwa wingi na wakienda vijijini kama ilivyotuahidi, ijitahidi kuwajengea nyumba. Ukienda vijijini leo unakuta nyumba ya mwalimu, mganga, lakini kukuta nyumba ya bwana shamba ni nadra sana. Unamtoa kijana aliyemaliza chuo anakwenda pale kijijini nyumba ya kufikia hakuna, hakai pale ataondoka. Kwa hiyo, nalo nilikuwa naomba Serikali ilizingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka hiyo ya nyuma, kilimo kilipata msukumo mkubwa sana, maana tusifike mahali tukawalaumu wataalam peke yao; kwanza ni wachache. Kilipata msukumo mkubwa sana kwa viongozi nao kushirikiana na kilimo na kukihamasisha. Tunao viongozi wachache sana wenye mashamba, hata hapa Bungeni. Kwenye Siasa ni Kilimo ukurasa wa 22, naomba ninukuu ibara ya 36 ilikuwa inasema: “Lazima wao wenyewe viongozi wajifunze kanuni za kwanza za kilimo bora na kwa mazao yao na ardhi ya sehemu yao. Vile vile kilimo bora hakifundishwi kwa kuhutubia mikutano ya hadhara tu, kinafundishwa kwa mazungumzo na kwa kushirikiana kazi. Vinavyohitajiwa ni vitendo, kilimo bora sio maneno katika jukwaa. Wako wapi viongozi wa aina hii kwa leo hii ni wachache na inawezekana hawapo kabisa.”

Mimi nina hakika tukirejea yale mambo mazuri yaliyofanywa katika kipindi kile cha nyuma, kilimo kitapata msukumo na wananchi wetu pengine maeneo mengine wanawaamini sana viongozi wa siasa kuliko wataalam. Kwa hiyo, wakichukua ya wanasiasa na ya wataalam, nina hakika kilimo kitapata mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende katika suala la zao langu la biashara la tumbaku. Kwanza, mimi naomba niendelee kusema wazi, mengine nitakayokuwa nayasema hapa, inawezekana yakawa yanagusagusa Bodi yangu. Mimi ni Mbunge, lakini vile vile ni Mjumbe wa Bodi ya Tumbaku; ni Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku Tanzania. Mwenyekiti wangu ni Mheshimiwa Vita Kawawa. Zao la Tumbaku limepitia misukosuko mikubwa sana hapa katikati, lakini inatoka moyoni kabisa, niishukuru na niipongeze sana Serikali; kumefanyika mabadiliko makubwa sana na Wizara hii imeshiriki. Bodi ya Tumbaku imeshiriki, wadau mbalimbali wa ushirika wameshiriki kikamilifu kuhakikisha kwamba, wananchi wetu wanaoshiriki katika kilimo hiki cha tumbaku, wanapata bei nzuri lakini vile vile wanauza mazao yao kwa uhakika, kwa wakati na ndiyo ambayo yamefanya sasa hivi zao liendelee kupanda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka tu niiombe Serikali, nilikuwa naangalia mazao mengine yanapatiwa ruzuku, kwa mfano pamba, korosho, iwe ya madawa au mbegu, lakini sisi kwenye tumbaku hakuna ruzuku. Tungehitaji angalau kuwapunguzia mzigo kidogo wakulima wetu, hasa kwenye suala zima la mbolea, maeneo machache kama tunavyofanya kwenye mazao ya chakula. Tumbaku ina uzalishaji mzuri na inaongeza pato kubwa sana la Taifa letu, kwa hiyo, nina hakika wakiongezewa jambo hili, wanaweza wakafanya jambo zuri sana katika kuendeleza kilimo hiki cha tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengine ni suala la baadhi ya wakulima wasio waaminifu, kutorosha tumbaku kutoka chama kimoja cha msingi kwenda kuuzia chama kingine cha msingi. Mimi nilikuwa naishauri Serikali katika kipindi hiki ambacho tunaelekea sasa kuwapa uwezo wanaushirika wa kupata pembejeo na kuwasambazia wakulima, lile jambo tulililokuwa tumelizoea huko nyuma la vyama vya msingi kukatwa asilimia mia moja deni, halafu wale wakulima waaminifu na wale wasio waaminifu, wakae wasubiri ndiyo baadae waanze kugawana yale mafungu yatakayokuwa yanafuata baadaye. Mimi nilikuwa naomba katika kipindi hiki ambacho tunaelekea huko, dhana hii iachwe kila mkulima aweze kujidhamini yeye mwenyewe afe na chake. Katika kipindi hiki, tumeshuhudia baadhi ya wakulima wameshindwa kuendelea kulima tumbaku, kwa sababu ya kuendelea kuwalimia wakulima ambao si waaminifu. Kwa hiyo, nina hakika katika kipindi kijacho yanaweza yakabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la kujitosheleza kwa chakula. Niliuliza swali juzi juzi hapa, nikaambiwa karibu mikoa 17 itakuwa na upungufu wa chakula. Hali hii si nzuri ni mbaya, suala la njaa si mchezo; njaa haina CHADEMA, CCM wala CUF. Nilikuwa naomba sana, tuna matatizo kadhaa mengine hayo nimeyataja ya uhaba wa wataalamu, uhaba wa zana, lakini vile vile tunayo matatizo ya kutumia nguvukazi. Tulikuwa na Sheria ya Nguvukazi hapa sijui ilifutwa namna gani. Walaji ni wangapi na wanaozalisha ni wangapi, hii hesabu nayo ni jambo la msingi sana katika vipindi hivi. Watu wengi hawafanyi kazi ya kuzalisha chakula, wanasubiri chakula kizalishwe na watu wachache wao wale; huwezi ukategemea ziada katika hali ya namna hiyo. Kwa hiyo, nilichokuwa naiomba Serikali sijui tunatumia utaratibu gain, lakini ni lazima tuwawezeshe watu wanaoamua kwenda kushiriki katika shughuli za kilimo, maana vijana wengine wanatoka mashambani kwenda mijini kwa sababu ya kukosa mitaji. Huwezi ukakaa ukaanzisha tu kwa jembe la mkono ukategemea utailisha familia yako na ukapata na mtaji wa kufanya shughuli nyingine. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali kwa makusudi ihakikishe kwamba, inawawezesha vijana na inawawezesha watu ambao wameamua kufanya shughuli za kilimo mashambani ili waweze kuleta tija katika shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia dhana ya Kilimo Kwanza kwamba ni lazima ardhi ipatikane na kupimwa na ndiyo sababu ukishapima ardhi ukapata hati, taratibu hizo zinaweza zikakupelekea kwenda Benki kukopa. Maelezo haya ambayo yapo kwenye ukurasa wa 77, bado yamenitisha kidogo kwamba, ardhi ipatikane na kupimwa ili wawekezaji wanaohitaji kufungua mashamba makubwa na ya kati, waweze kupatiwa ardhi ya kulima bila ya kuathiri mahitaji ya wakulima wadogo. Mimi nasema wanaohitaji kupimiwa ardhi sio wawekezaji, hata wakulima wetu wa kawaida sasa hivi wanahitaji kupimiwa ardhi ili waweze kupata hati, waweze kwenda kukopa kwenye Mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, narudia kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, nawashukuru sana kwa kunisikiliza ahsante. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninyi wenyewe mnatutaka sisi tufuate utaratibu. Orodha yetu tunavyoiandika tunaanza na asiyechangia, aliyechangia mara moja, aliyechangia mara mbili, aliyechangia mara tatu na tunakwenda namna hiyo kwa kuwaita watu. Sasa mkileta barua kwa Kiti kwamba, mnaomba mkachangie kesho, sawa mimi nitawachukua wale waliochangia mara tatu wataitwa, kwa sababu wale wengine wanahesabu wanajua hawafikiwi leo. Kwa hiyo, nalo ni tatizo nitawaita wale waliochangia mara tatu, wewe kesho utakosa nafasi, ndiyo itakavyokuwa. Kwa hiyo, naomba kama unataka

kubadilisha ukubaliane na mtu kwamba, wewe uzungumze leo na mimi nitazungumza kesho leteni barua, lakini vinginevyo haiji.

Sasa Mheshimiwa Cynthia Ngoye, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura.

**MHE. CYTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache kwa Wizara yetu hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Napenda vile vile kumshukuru sana Waziri wa Kilimo, Naibu wake na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhimiza kilimo hapa nchini. Mimi ni Mjumbe wa Kamati, kila siku tumezoea kuwapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya na mambo mazuri wanayotuandalia, lakini kwa sababu mimi ni mtoto wa mkulima na ninakipenda kilimo na ninalima, ninayo machache ya kuzungumza ili kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwepo katika Mkutano ule ulioendeshwa na *Tanzania Business Council* pale Kunduchi. Nilikuwa mmoja wa washiriki, nilifuatilia sana dhana ile ikizungumziwa na wadau mbalimbali, mwisho tumekubaliana kwamba dhana hii ni nzuri. Kwa kuwa dhana hii ilikuwa inazungumziwa wakati mipango ya bajeti imeanza, tukaambiwa utekelezaji wake hautakuwa *reflected* sana katika kipindi hiki cha mwaka 2009/2010, isipokuwa kwa mwaka ujao. Hata hivyo, nampongeza Waziri kwamba, kuanzia sasa ameshatuweka Wabunge tuelewe ni nini Serikali imedhamiria. Kwa hiyo, tuna nafasi nzuri ya kuchangia mawazo mazuri na vile vile tunaipongeza Serikali kwa kuongeza kiwango cha bajeti ya kilimo kwa asilimia 45, ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana. Kwa hiyo, kazi imeanza kufanyika na ninaamini kabisa hii mipango ambayo imezungumziwa katika hotuba yake Waziri kama itasimamiwa vizuri na watendaji wote, tutafika mahali pazuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 77, Waziri alikuwa anazungumzia mipango hii chini ya kaulimbiu ya Kilimo Kwanza kwamba, itatekelezwa kupitia Wizara zenye *collaboration* na Wizara ya Kilimo. Nafikiri bila kukusudia, amesahau kutaja Wizara ya Maji na Umwagiliaji na vile vile Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira. Ninasema hivyo kwa sababu ni kweli kabisa na Wabunge wote wamesema hapa kilimo hiki hakiwezi kuwa kilimo chenye mafanikio kama hatutajiingiza kikamilifu katika kilimo cha umwagiliaji. Hata kama tumewakaribisha wawekezaji na watakuja, wengi wao watapenda aina ya kilimo ambacho wana uhakika nacho, yaani kilimo cha umwagiliaji. Hata mkulima mdogo naye vile vile atapenda kuwa na uhakika wa kilimo kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji. Hivyo ni lazima tuwe na uhakika kwamba, tunayo maji ya kutosha. Lazima kuwe na mipango mizuri ya hifadhi ya mazingira, kwa maana ya kulinda vyanzo vya maji vyote ambavyo hivi sasa watu wanaviharibu sana. Lazima tuhakikishe kwamba, kuna mipango mizuri ya upandaji miti kwa wingi sana ili kupambana na hili tatizo kubwa la kiulimwengu la mabadiliko ya hali ya hewa, tusije tukajikuta tunahimiza kilimo na Kilimo Kwanza katika jangwa haitawezekana hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nizungumzie suala la mbolea, ni kweli kabisa hatua viwanda vya mbolea. Ninaipongeza Serikali, Wizara hii imetamka wazi kwamba, kuanzia sasa itafanya juhudi kubwa katika kuwaomba na kuwakaribisha wawekezaji mbalimbali kuja kujenga viwanda vya mbolea, hilo ni wazo zuri sana. Maeneo yote yanayolimwa hivi sasa yamechoka yanahitaji mbolea, Kiwanda pekee tulichonacho ndiyo hiki cha Minjingu. Sasa kwa sababu ni kimoja tu, basi Serikali ikubali kukilea vizuri kiwanda hiki, kilelewe namna gani? Kwanza, sasa hivi kumetokea tafsiri mbalimbali kwamba, mbolea ile haifai maeneo mengine na maeneo mengine inafaa. Sasa ni lugha tofauti tofauti. Mimi ambaye ni Mjumbe wa Kamati, nimekitembelea kiwanda kile nimeshuhudia wakulima waliotumia vizuri mbolea

hii; ni mbolea nzuri sana. Kwanza, kwangu naiona ni nzuri kwa sababu ni *organic*, kwa hiyo ni rafiki kwa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kuna utata wengine wanasema nzuri; kule Makete nilipita wanasema mbolea ya Minjungu ni nzuri, kule Kyela nilipita nikaona baadhi ya wakulima wa mboga wanasema ni nzuri, ndugu yangu wa Mbozi anasema sio nzuri! Sasa kwa sababu kuna mkanganyiko wa mawazo haya, ushauri wangu ni kwamba, utafiti wa udongo uendelee, lakini vilevile tujitahidi kama Serikali, kueneza haya mashamba darasa, tueneze walau hata kila kijiji basi wakulima wapate nafasi ya kujifunza vizuri matumizi mazuri ya mbolea. Kwa hakika kabisa, Wizara itajikuta kwamba, siku moja watu wengi wanasimama hapa wanasema naam mbolea hii nzuri. Sikatai kwamb, kuna baadhi ya udongo si mzuri, ambao tunahitaji kusaidiwa labda kwa mbolea ya aina nyingine. Hii isiwe inaleta maana kwamba, mbolea inayozalishwa pale ni mbaya, hapana. La sivyo, Viongozi wote wa Kitaifa kuanzia Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, wameikubali mbolea hii na ndiyo maana Serikali nzima sasa hivi inakubali hata kuipa dhamana katika mikopo ili iweze kuzalisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ya kukilea kiwanda hiki ni pamoja na kulipa madeni ya watu ambao wanachukua mbolea pale. Hivi sasa naambiwa kiwanda kinaidai TFC zaidi ya shilingi bilioni mbili, huyu mwenye kiwanda atazalisha namna gani? Hawa wanazalisha phosphate, nafikiri hiki kiwanda kingewezeshwa zaidi kikalipa madeni yake na tukakiunga mkono, kingekuwa ni moja ya viwanda ambavyo vingeweza kuzalisha hata mbolea nyingine. Tunapofika mahali kukikatisha tamaa kwa kutowalipa madeni, mbolea iliyopo pale imerundikana, nimeambiwa sasa hivi kuna tani zisizopungua 15,000 zipo pale hazijasombwa. Sasa hawa wanazalisha namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubali kwamba ni kiwanda kitakachosaidia basi tukisaidie, hizi tani 15,000 ambazo hazijasombwa zilitakiwa sasa hivi ziwe katika malori kuelekea kwenye Wilaya lakini hazijakwenda. Tunangoja nini na wakulima wengi wameshavuna wana hela wanangoja kununua mbolea haijafika; wafanye nini? Mwisho, tunangoja mpaka inapokutana na msimu wa mbolea ya kupandia; hii haisaidii hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni wazo ambalo linapigiwa kelele kila wakati, unajua nchi hii misimu inatofautina, kwa mfano, ukienda kule Wilaya ya Rungwe, msimu wao wa kupanda mahindi unaanza mwezi wa tisa na mwezi wa nane, wakati wanapohitaji mbolea haipo kabisa. Mbolea hiyo itakuja Novemba wakati Mbozi, Chunya, Mbeya Vijijini na Wilaya nyingine zote ndiyo wanapanda, sasa watu wa Rungwe hawawezi kutumia mbolea ndiyo maana ni nadra sana kukuta wanapandia mbolea kwa sababu haipo kabisa. Naomba Wizara ijitahidi kujua maeneo haya au mikoa fulani; mfano Kilimanjaro wanapanda lini, Arusha wanapanda lini, Tanga wanapanda lini na hivyo hivyo kwa Wilaya zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni suala la kilimo. Ningependa chombo kinachotumika (TFC), Wizara ingeanza kuzungumza na Serikali kwa ujumla kwamba, TFC iwe chini ya Wizara ya Kilimo badala ya kuwa ya Viwanda na Biashara. TFC ni chombo ambacho kinatumika kwa kusambaza pembejeo na mbolea zote; kwa nini kisiwe chini ya Wizara ya Kilimo, hebu anzeni kulifikiria hilo lina madhara gani, mimi nafikiri halina madhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nizungumzie Zao la Chai; Zao hili linalimwa sehemu zenye mvua nyingi sana kama Lushoto, Rungwe, Njombe, Mufindi na maeneo mengine ya *high altitude,* ndiyo maeneo ambayo chai inastawi. Tatizo chai inasombwa kila

siku na kwa kuwa inasombwa kila siku na mvua ni nyingi barabara zinaharibika sana. Kwa hiyo, utakuta kila siku kwa kuwa barabara ni mbaya magari yanakwama, yakikwama maana yake chai ile imeharibika tayari. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana tuangalie nyuma wakati wa *Tanzania Tea Authority*, wakati ule barabara zilikuwa safi sana kwa nini tusichukue mfano ule, barabara zikawa safi na chai isije ikawa inamwagwa na kadhalika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala hili litiliwe mkazo sana, barabara za vijijini zinazosomba Zao la Chai kila siku ziimarishwe. Vipaumbele vya Halmashauri ni vingi mno. Kwa hiyo, naomba fedha hiyo iwe chini ya Wizara ya Kilimo na ielekezwe moja kwa moja kwa ajili ya mashamba hayo ya Chai. Chai ni mali inatuletea uchumi nchi hii, tena uchumi mzuri kabisa na wakulima wangu ninaowawakilisha, Wanawake wa Mkoa wa Mbeya, hasa Wilaya ya Rungwe, wengi wanajitokeza kuvuna chai lakini mwishoni wanashtukia chai yenyewe imemwagwa na hawapati hela. Ninaomba sana suala la barabara lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngoye. Sasa namwita Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Mpina ajiandae na Mheshimiwa Maida Abdallah ajiandae.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza kabisa, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na vile vile niwashukuru sana na kuwapongeza wakulima wote wa Wilaya ya Tunduru, kwa namna walivyojikita mwaka huu, licha ya hali mbaya ya hewa ya ukosefu wa mvua, lakini wamejitahidi kuzalisha kwa kiasi kikubwa zao la mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naishukuru Kampuni ya TFC kwa kujitahidi kusambaza pembejeo ya Zao la Korosho, sulphur, kwa bei nzuri ambayo haijapata kutokea katika historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Vita Kawawa, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku, kwa kulipokea ombi langu la kutuwezesha Wilaya ya Tunduru kuanza kulima tumbaku katika Kata za Matemanga, Ligunga, pamoja na Mchoteka. Kwa niaba ya wananchi wa eneo hilo, tunakushukuru sana na tunakuombea ili uendelee kuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu, uchaguzi wa mwaka 2010 upite kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunduru tunalima Korosho kama zao kuu la biashara na tutafarijika sana kama pembejeo za Zao la Korosho, zitawafikia wakulima mapema iwezekanavyo. Tunduru kKorosho zinachipua kuanzia mwezi wa nne kwa yale maeneo ya joto na mwezi wa tano mpaka wa sita kwa maeneo ambayo yana hali ya hewa ya baridi. Kwa hiyo, tutafarijika sana kama pembejeo hizi zitakuwa zinawafikia wananchi mapema iwezekanavyo. Vile vile tunaishukuru sana Serikali kwa kuimarisha masoko na bei ya korosho na ni matumaini ya Wananchi wa Tunduru na maeneo mengine yote yanayozalisha korosho kwamba, bei ya korosho mwaka huu itaongezeka ili kuongeza tija ya wakulima hawa. Vile vile tunaiomba Serikali iendelee kuweka msisitizo wa kubangua korosho zote hapa nchini badala ya kusafirisha zikiwa ghafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza kwamba, Tunduru tunalima korosho, lakini korosho si chakula, chakula kikuu cha Wananchi wa Tunduru ni mahindi, mchele na mara nyingine huwa tunakula ugali wa muhogo. Kwa hali hiyo ni matarajio makubwa sana kwa

Wananchi wa Tunduru kupata mbolea mapema iwezekanavyo, kama Wabunge wenzangu waliotangulia walivyoeleza. Mwaka jana mazao ya wananchi wengi yalipungua kwa sababu ya mbolea, pamoja na mbegu bora zilifika wakati ambao siyo mufaka. Kwa hiyo ni imani ya Wananchi wa Tunduru, mwaka huu mbolea pamoja na mbegu zitawafikia mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, nchi yetu mara zote tunaambiwa kwamba ni nchi ambayo uti wake wa mgongo ni kilimo na takriban asilimia 85 ya wananchi wanategemea kilimo katika kujikimu katika maisha yao ya siku hadi siku. Cha kushangaza, nchi hii miaka ya 1970 tulikuwa na kiwanda cha mbolea kule Tanga, kile kiwanda sasa hivi ni historia hakipo tena. Tukabahatika hapa katikati tukapata Wawekezaji kiwanda cha kutengeneza mbolea ya kupandia na kukuzia kule Arusha Minjingu. Mwaka jana Serikali iliwahamasisha sana hawa wawekezaji wazalishe mbolea ya kutosha wakawezeshwa na wakafanya walivyoweza wakazalisha mbolea nyingi sana.

Katika hotuba ya mwaka jana, tuliambiwa katika Bunge hili kwamba, Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kununua mbolea ile takriban shilingi bilioni 30; sina hakika kama zile fedha zilitolewa ili kuweza kununua mbolea ile?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yetu kwamba, Bunge hili Tukufu litaarifiwa kwamba, zile fedha zilitolewa. Ninasema hivyo kwa sababu vyombo vya habari hivi karibuni vimeripoti kwamba, kiwanda kile kimefungwa kwa sababu mbolea ile haijanunuliwa imerundikana. Haiingii kichwani mwetu, Serikali imeahidi kutoa shilingi fedha bilioni 30 kwa ajili ya kuwezesha TFC wanunue ile mbolea, wakati huo huo tunaambiwa kwamba, kiwanda kinafungwa kwa sababu mbolea ile haijanunuliwa, sasa tuwaamini akina nani. Matarajio yetu ni kwamba, Bunge hili Tukufu litaarifiwa zile fedha zilitolewa au lah na hatua zipi za haraka zinachukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba, kiwanda kile mazao yake yananunuliwa ili yasambazwe kwa wakulima na kiwanda kile kiendelee kuzalisha, kwa sababu kinatoa ajira kwa Watanzania wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, si haki na si vyema kiwanda pekee kilichopo nchini mwetu cha kuzalisha mbolea kifungwe eti tu kwa sababu mbolea ile tumeshindwa kuitumia. Ninafahamu kwamba, mbolea ile kwa baadhi ya maeneo haikufanya vizuri hususan baadhi ya maeneo katika Mkoa wa Mbeya, lakini maeneo mengine mbolea ile imefanya vizuri na imekubalika hatujapata malalamiko, kwa nini isitumike? Mbolea ambayo imerundikana katika kiwanda kile, nchi jirani wanaimezea mate na wanaitaka. Afrika Kusini wanaitaka mbolea hiyo hiyo, sisi ambao tunainunua tena kwa bei rahisi hapa nchini mwetu hatuitaki ila tuagize mbolea kutoka Afrika Kusini!

Mheshimiwa Naibu Spika, nitanukuu maneno ya hekima yaliyowahi kuzungumzwa na Mwanafalsafa wa Kimataifa aliyesema kama huwezi kuruka basi ni vyema ukimbie; kama huwezi kukimbia basi ni bora utembee; kama huwezi kutembea ni vyema utambae; lakini kwa namna yoyote ile utakayofanya, hakikisha kwamba unaelekea katika mwelekeo wa kutimiza majukumu mliyojipangia. Sisi kama nchi katika eneo hili la kilimo tupo katika hatua ipi; tunaruka; tunakimbia; tunatembea; tunatambaa au tumelala? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri watendaji ambao tumewapa dhamana ya kutuongozea nchi yetu katika Sekta hii ya Kilimo, basi wahakikishe kwamba, Watanzania tunakimbia ili baadae tuweze kuruka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelazimika kuyasema hayo yote, kwa sababu nchi hii ni yangu, lazima niwe na uchungu nayo. Sitafurahi kabisa kuona yale yaliyotokea Tanga katika

kiwanda kile cha Mbolea, yanatokea katika kiwanda hiki cha Minjingu. Kama kuna upungufu wowote wa ubora wa mbolea ile, urekebishwe ili tuweze kupata mbolea katika nchi yetu, tuweze kuhifadhi fedha za kigeni chache tulizonazo katika nchi yetu, badala ya kutumia fedha hizo za kigeni kuagiza mbolea nje ya nchi wakati mbolea tunayo katika nchi yetu hii hii.

Kitendo cha kuendelea kuagiza mbolea ilhali tunayo, itafikia siku tutaagiza hata samadi. Nchi yetu tuna idadi kubwa ya ng’ombe, tutasema kwamba ngombe hawa nyasi zake hazina *protein* ila wa Afrika ya Kusini wana *protein,* kwa hiyo, tuagize samadi kutoka huko. Hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na Kiwanda cha UFI cha kuzalisha majembe. Kiwanda hiki kimeuzwa na sasa hivi kinazalisha mabomba. Moja ya masharti ambayo waliwekeana na Serikali ni kuhakikisha kwamba, inazalisha vilevile majembe ya kukokotwa na ng’ombe, lakini cha kushangaza mpaka leo kiwanda hiki hakijazalisha jembe hata moja. Hivi kweli nchi ambayo inategemea kilimo kama uti wa mgongo, asilimia 85 ya wananchi wake ni wakulima, nchi hiyo hiyo ilivyo kubwa yenye watu zaidi ya milioni 40 haitengenezi jembe hata moja la mkono ndani ya nchi; tunaipeleka wapi nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili tuliangalie kwa makini sana. Tutengeneze majembe, mapanga, majembe ya kukokotwa na ng’ombe ndani ya nchi yetu, kwa sababu fedha nyingi sana za kigeni zinatumika kuagiza majembe kila mwaka, ambazo zingeweza kuokolewa kama majembe yale yangekuwa yanatengezwa ndani ya nchi yetu. Ninahofu kama tunaendelea kuagiza majembe kutoka nje, ipo siku tutaagiza hata mipini Msumbiji, hapo ndipo tutafikia hatua mbaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini dakika zangu zilizobaki ni chache, nimeambiwa kama mbili hivi; sijui wamepata wapi taarifa hiyo! Nasema naunga mkono hoja hii, nawatakia kila la kheri Mawaziri wangu hawa wawili, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii ya Kilimo. Namwomba Mheshimiwa Mathayo, kwa sababu hajawahi kufika Tunduru, safari hii afike ili ajionee mabanio ambayo ametuletea kule Tunduru ili aweze kufanya hamasa. Mheshimiwa Waziri, Tunduru ni kama nyumbani kwake na kwa Mkuu wa Wilaya kuna kikombe kabisa tunaambiwa hiki ni cha Mheshimiwa Wasira, kwa sababu ni mtu ambaye amekuwa akiitembelea sana Tunduru. Mheshimiwa Mathayo, karibu sana Tunduru ututembelee ili utoe hamasa kubwa kwa wananchi na wakulima wa eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nasimama hapa nikiwa na majonzi makubwa ya kufiwa na Mwalimu Emmanuel Mahembo, ambaye alikuwa pale TSD, alipata ajali ya pikipiki jana na akafariki dunia. Nipeleke salamu za rambirambi kwa Viongozi na Watumishi wote Wilaya ya Meatu na Walimu wote, kwa msiba huu mzito na Mungu aendelee kututia nguvu katika kipindi hiki kizito, bila kuisahau familia yake, ndugu zake na marafiki zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwa sababu muda wangu ni mfupi mno; Tanzania na Kilimo. Nchi yetu kwa miaka 32 sasa kulingana na takwimu ambazo zimeoneshwa kwenye Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa ya Mwaka 2008, inaonesha toka mwaka 2007 hatujapiga hatua kubwa. Pamoja na hatua hizi tunazojivunia, lakini ukiangalia ongezeko la watu, haliendi sambamba na mafanikio yale ambayo tunajivunia. Idadi ya watu wakati wa uhuru walikuwa milioni tisa, leo tupo milioni 40. Sasa ukienda kwenye takwimu za kilimo cha pamba msimu wa mwaka 1977 na mwaka 1978, tulipata tani 67,000. Mwaka

2007/2008 tumepata tani 70,000. Kwa hiyo, ukiangalia takwimu hizo 67,000 kwa mwaka 1967 na 70,000 kwa mwaka 2007/2008, unakuta kwamba, tunapiga *mark time* hutendi mbele, licha ya ongezeko la watu, semina mbalimbali zinavyoendeshwa, mabadiliko ya teknolojia, gharama za uzalishaji, lakini bado hatujaweza kupiga hatua za makusudi katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kwamba, hata ukiangalia kwenye ukuaji wa Pato la Taifa, utakuta kwamba, mwaka 2002 tulikua kwa 5.6, mwaka 2003 tulikua kwa 3.2, mwaka 2004 tulikua kwa 6.6, mwaka 2005 tulikua kwa 4.4, mwaka 2006 tulikua kwa 4.0, mwaka 2007 tulikua kwa 4.5 na mwaka 2008 5.1. Kwa hiyo, vielelezo hivi vyote ni ushahidi kwamba, hatupigi hatua katika kilimo. Sasa tunajifunza nini? Je, jitihada zinazochukuliwa na Serikali zinaleta matunda gani? Je, wakulima wanapungua au wanaongezeka na kama wanapungua wanakwenda kujiajiri wapi? Wana kazi maalum au wako kwenye uzururaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa napitia hotuba hii, sikuona sehemu ambayo imeeleza katika takwimu zote nilizozipitia kwenye Hotuba ya Waziri mwenyewe, pamoja na hali ya uchumi nchini. Hakuna sehemu iliyoonesha idadi ya wakulima na hakuna sehemu iliyoonesha kwamba ni hekta ngapi ambazo zinalimwa nchini. Kwa sababu ukosekanaji wa Takwimu hizo ndiyo unaotupelekea sasa tusijue kwamba, tunapiga hatua ama hatupigi hatua. Vikwazo ambavyo vinatusababisha, tusipige hatua kwenye kilimo ni bei ya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mazao imebaki ile ile licha ya mfumko wa bei kuongeza, licha ya gharama za maisha kupanda lakini wakulima wamekuwa wakipewa bei ile ile ya mazao. Wananchi wanafanya jitihada zao za uzalishaji, lakini Serikali haijajipanga kuwasaidia wananchi wake katika kupata bei nzuri ya mazao. Mkulima yeyote anaangalia bei ndiyo anazalisha. Ukiangalia kwenye *trend* yote ya uzalishaji, mkulima anaongeza uzalishaji kulingana na bei anavyopanda. Je, hapa tunajifunza nini kama wananchi wana-*opt* bei nzuri? Mwaka 2003/2004 bei ya pamba ilipopanda kutoka shilingi 180 mpaka 280, ukulima wa pamba ulitoka kutoka tani 139,000 na kufikia tani 340,000.

Bei iliposhuka kutoka shilingi 280 mpaka 220, uzalishaji wa pamba kwa mwaka uliofuata ulishuka kutoka tani 376,000 na kufikia tano 130,000. Kwa hiyo, ipo siku wakulima hawa watajitoa kabisa kwenye ukulima wa pamba kama hatuwezi kuchukua hatua za makusudi za kuhakikisha wakulima wetu wanapata bei nzuri ya mazao yao.

Aidha, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuongeza bei ya pamba ya shilingi 80 kwa wakulima kufidia bei, lakini pia na kufidia hasara ya wafanyabiashara; ingawa bei hii bado ni ndogo sana kwa wakulima ukilinganisha na gharama zao za uzalishaji. Kwa hiyo, bado zinahitajika jitihada za makusudi za kuhakikisha kwamba, wakulima hawa wanapatiwa bei nzuri ya Zao la Pamba pamoja na mazao mengine ya Kahawa, Korosho Tumbaku na Katani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili ni kukosekana kwa huduma za kibenki katika maeneo ya vijijini. Hili ni tatizo kubwa sana, wakulima wanalima mazao na mimi kule kwangu Kisesa wakulima wangu ni walimaji wakubwa sana wa pamba, mahindi, mtama, dengu na choroko na wanapata fedha. Sasa hawana mahali pa kuziweka fedha hizi, wengi wanavamiwa wanaibiwa na pengine kuuawa kabisa na majambazi, kwa sababu hawana pa kuhifadhi fedha. Serikali inatakiwa itoe msukumo wa haraka kuhakikisha kwamba, *financial institutions* zinaanzishwa katika *potential area* kama Kisesa pale Mwandoya. Kwa mfano, watu wa *Postal Bank* wanaweza wakashawishiwa wakaenda kuwekeza pale. NMB wanaweza wakapeleka kule. Watumishi ni wengi na watu wana kipato kizuri cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la tatu ni umeme vijijini. Ili uweze kuanzisha viwanda vya kusindika mazao, pamoja na kuongeza thamani ni lazima uhitaji umeme. Wananchi wangu wa Kisesa, wanalo tatizo kubwa la kukosa umeme huo na hivyo hawawezi kupata viwanda na inawezekana *financial institutions* zinachelewa kwa sababu ya umeme. Naamini Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, keshokutwa atawasilisha Bajeti yake na atawaeleza Wanakisesa, hatima ya umeme wao ule wa Ng'oboko, Semu, Balagane, Lubiga, Mwandoya hadi Igobe kwamba, utakuja lini na wanamsubiri kwa hamu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine kubwa ni migogoro ya wakulima na wafugaji. Hili nalo linachangia sana katika uzalishaji. Tatizo la migogoro ya wakulima na wafugaji linasababishwa na Serikali yenyewe. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu wafugaji waliopo Shinyanga ...

**SPIKA:** Umesema migogoro ya wakulima na wafanyakazi?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni migogoro ya wakulima na wafugaji. Migogoro ya wakulima na wafugaji, inasababishwa na Serikali yenyewe. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu Serikali imeshindwa kujenga mahusiano kati ya wafugaji na wakulima. Wafugaji waliopo Shinyanga, Tabora, Mwanza hawagombani; kwa nini wafugaji walioko Morogoro wanagombana? Wanagombana kwa sababu mwingine hajazoea kufuga na mwingine hajazoea kulima.

Kwa hiyo, kazi ya Serikali itakiwa kujenga mahusiano tu kati ya hao watu wawili. Watu wa Morogoro wanataka ghala la chakula huku wanafukuza mifugo wakati ng'ombe hao sasa wangezitumia kama zana za kilimo. Badala yake imekuwa ugomvi mkubwa, halafu utaratibu huu wa kumhukumu mfugaji mmoja kwa sababu ya kosa la mfugaji mwenzake, nao si utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfugaji aliyetenda kosa alitakiwa achukuliwe hatua yeye mwenyewe *independently*. Najua tabu kubwa wanayopata wafugaji wangu wa pembezoni hasa wa Vijiji vya Semu, Mbaragane, Lubiga, Tindabuligi, Butuli na Malwiro; hii Sheria ya Malisho ingewahi ili muafaka wa malisho ya mifugo uweze kupatikana. Wafugaji wanateseka, kwa sababu ya kukosa maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza, nizungumzie Sheria na Kanuni zilizopitwa na wakati. Serikali bado imeendekeza Sheria na Kanuni zilizopitwa na wakati. Kwa mfano, haina mantiki ya kwa nini leo mpaka wewe unazungumza kwamba, Mwananchi haruhusiwi kuuza mazao nje ya nchi, kwa mantiki gani? Mwananchi kalimi kwa gharama zake, kateseka sana sasa unataka auze kwa bei ya kutupa! Unataka auze kwa bei ya hisani! Mantiki yake nini? Kwanza, unaposema auze kwa bei ya kutupa amuuzie nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni wafanyakazi, wengine ni wafanyabiashara; mfanyakazi analipwa mpaka na ruzuku lakini Mkulima huyu halipwi hata ruzuku, mkulima huyu halipwi hata kiinua mgongo anapostaafu. Sasa unapolazimisha kwamba, auze mazao yake kwa bei ya hapa nchini na ukamkataza kusafirisha mazao yake kwenda nje; mantiki yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ingekuwa na maana nzuri ya kumsaidia mkulima huyu, ingenunua mazao hayo ya ziada kwa bei inayolingana na ile inayotolewa nchi za nje. Pale ingeleta tija na ingeleta mantiki, lakini kufanya hivi ni kuwaonea wananchi.

Serikali inawapiga pingu wananchi wake huku ikiwasisitiza kwamba, inataka kuleta Mapinduzi ya Kilimo. Sasa kama nazalisha mazao na mazao yangu hayawezi kununuliwa kwa bei kubwa, nitazalisha chakula hicho cha ziada nikipeleke wapi wakati hapa nchini nakataliwa kusafirisha na bado hakuna bei nzuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima huyo mazao nayo yanakosa soko la nje ya nchi, mazao ya chakula nayo haruhusiwi kuuza nje ya nchi, bali anatakiwa auze kwa bei yoyote iliyopo ndani ya nchi, huo ni unyanyasaji mkubwa na hata Mheshimiwa Waziri, mwaka jana tulimshauri juu ya hili, lakini inaonekana kuwa msimamo huu hauwezekani kuondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia Sheria nyingine ambayo ningehitaji kwamba, Wizara iifanyie uchunguzi. Sheria hiyo ni ile inayomzuia mkulima kuchanganya mahindi na pamba. Najua tatizo ni dawa, lakini hivi kweli mpaka sasa hivi hakuna utafiti unaowezesha kupatikana kwa dawa nzuri itakayoruhusu uchanganyaji wa mahindi na pamba kwa sababu sasa hivi kwanza, ardhi inapungua, lakini vilevile gharama za uzalishaji ni kubwa na bado sheria hii haitekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda hautoshi, nasema nitaunga mkono hoja pale tu ufafanuzi utakapotolewa.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabisa, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuweza kunijalia kusimama jioni hii ya leo ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hotuba yake nzuri, ambayo inaleta matumaini makubwa kwa Watanzania wote nchini. Pia napenda nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji mbalimbali wa Wizara hii, kwa jinsi wanavyojituma na kufanya kazi ndani ya Wizara hii ngumu na kufanya kazi katika mazingira magumu katika miaka iliyopita na hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Serikali kwa kuweza kuweka kipaumbele cha Kilimo Kwanza kwa mwaka huu wa 2009/2010 na kuongeza fedha za bajeti katika Wizara hii ili kuweza kufikia lengo la Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka kuwa, miaka ya nyuma, Sekta hii ya Kilimo ilikuwa inashuka siku hadi siku, pia ulizalishaji wa Kilimo nao ulikuwa unashuka siku hadi siku. Katika kipindi hiki ambacho Serikali imejielekeza katika Kilimo Kwanza, tuangalie ni maeneo gani kwa miaka ya nyuma Sekta hii ilikuwa inashuka ili tuweze kujirekebisha vizuri katika mwaka huu wa kutekeleza Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia suala la Wataalamu wa Ugani, mara nyingi walikuwa wanakaa maofisini walikuwa hawaendi katika maeneo ya mashamba, lakini sasa hivi Serikali imeandaa maboresho kwa ajili ya Wataalamu wa Ugani kwa kutoa pikipiki na fedha ambazo zitawawezesha katika kuendeleza Kilimo. Ufuatiliaji unatakiwa ufanyike ili wataalmu hawa waweze kuwafikia wakulima kule waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pamoja na kuweka viwango au idadi ya Wataalamu wa Ugani katika kipindi hiki, bado idadi ya Wataalamu hao ni ndogo kutokana na wakulima tulionao katika nchi yetu. Serikali ni lazima ijiweke vizuri katika kuongeza Wataalamu wa Ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia masuala ya mbegu.  Kwanza niyapongeze mashirika au makampuni binafsi, kwa kuweza kuingizia mbegu na kuwagawia wakulima katika maeneo mbalimbali. Serikali nayo pia inajitahidi katika nyanja hii ya kuwaelimisha wataalamu mbalimbali ili waweze kuzalisha mbegu zilizo bora ili tuweze kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningeiomba Serikali kwa sababu katika hili ambalo inasisitiza kuhusu suala la mbegu, mara nyingi tumekuwa tunaagiza mbegu kutoka nje; Tanzania tunategemea sana kilimo; kwa nini tuwe tunaagiza mbegu kutoka nje kila mara? Sisi ni wakulima na ni lazima wataalamu wetu tulionao tuwaelimishe katika masuala ya uzalishaji wa mbegu bora ili tuweze kupata mbegu zinazoendana na kilimo chetu na zinazoendana na mahitaji ya walaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wataalamu wa Kilimo; kwa nini serikali isiangalie namna ya kuanzisha Vyuo vya Wataalamu wa Kilimo katika kila Wilaya au Mkoa katika nchi yetu? Nasema hivyo kwa sababu tumevuka lengo kwa upande wa Elimu kwa kujenga shule mbalimbali katika kila Kata; kwa nini tusiweze kuelekeza suala hili kwa upande wa Kilimo na kuweza kujenga au kuweka vyuo katika kila Wialaya au Mkoa na kuweza kuwafundisha wakulima japo 50 kwa kila Wilaya au Mkoa na kuweza kufikia lengo lililokusudiwa la Kilimo Kwanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali ni lazima ijiweke tayari katika kuliimarisha hili suala ili na sisi tuwe na wingi wa vyuo vya kilimo katika kuwaimarisha wakulima wetu na kuweza kuzalisha kwa wingi zaidi.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pembejeo za kilimo; wakulima wengi hawana utaalamu hivyo elimu inahitajika zaidi kwa wakulima ili waweze kujua namna ya kutumia pembejeo za kilimo. Pembejeo za kilimo nyingine zinaendana na udongo, wengi hawajui udongo huo unaendana na mbolea gani, kwa hiyo, lazima Serikali ijiandae vizuri kuwapatia elimu wakulima au wataalamu ili hatimaye waweze kufanya kazi ya ziada katika maeneo mbalimbali na kuwafikia wakulima katika juhudi za kuendeleza kilimo chetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kufikia lengo la Kilimo Kwanza kama hatutaangalia maeneo hayo, kwa sababu kila mara kilimo kilikuwa kinashuka katika miaka ya nyuma, lakini mwaka huu ambao tumejielekeza katika Kilimo Kwanza, ule upungufu wote ambao ulitokea miaka ya nyuma, basi tuweze kuurekebisha katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umwagiliaji; hadi sasa nchi yetu suala la umwagiliaji ni dogo sana.  Kilimo cha umwagiliaji hakijakua ipasavyo ndani ya nchi yetu, lazima Serikali ijiweke vizuri na tayari kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Wakulima wengi wanahitaji kilimo cha umwagiliaji, lakini uwezo hauruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka kuwa, fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya Wizara ya Kilimo na sisi kama Bunge huwa tunaidhinisha fedha hizo kwa ajili ya matumizi, yakiwemo ya kawaida na ya maendeleo. Fedha za maendeleo zinakuwa hazitoki kama Bunge tulivyokusudia, fedha hizi zinatoka polepole na matarajio yaliyokusudiwa yanakuwa hayafikiwi. Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Hazina, iweze kuliona hili ili fedha hizi ziwafikie Wizara mapema, ziwafikie Halmashauri mapema kama zilizoidhinishwa siyo kwenda nusunusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia fedha ambazo zimekusudiwa katika maeneo mbalimbali katika Wizara, zielekezwe kule ambako zimekusudiwa na siyo kutumika vibaya. Mara nyingi katika Bunge letu, huwa tunaidhinisha fedha lakini huwa zinatumika vibaya kutokana na uwajibikaji mbaya ndani ya Wizara. Naiomba Serikali na Wizara, watimize wajibu wake ili tufikie lengo la Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa kuwa katika kilimo cha Zao la Mkonge faida ni asilimia 98 na asilimia mbili zilizosalia ndiyo hubaki kuwa makapi. Naiomba Serikali kuweza kukikuza zaidi Kilimo hiki, kwa sababu mwaka 2007 Zao la Mkonge katika uchumi wa Dunia liliingiza kiasi cha Dola za Marekani 928.4 na Dola za Marekani 1050 na kuendelea kwa mwaka 2008. Kwa hiyo, kutokana na pato hili na ili kuwakuza wakulima wetu wa kilimo cha mkonge ni vyema Serikali ikaweza kuliangalia hili, kwa sababu wakulima wengi wa mkonge wameacha mashamba yao kutokana na bei ya zao hili hushuka katika miaka ya nyuma na kuamua kuingia katika kilimo cha mazao mengine. Nashauri kuwa sasa tuweke mkazo zaidi hasa katika kipindi hiki cha Kilimo Kwanza ili Zao hili la Mkonge liweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuwaelimishe wakulima katika zao la mkonge kwamba, wanaweza kulima mazao mengine ndani ya mashamba yao ya Mkonge. Kwa hiyo, wanaweza kulima mazao ya chakula na vilevile wakalima Zao hili la Mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie kuhusu suala la mikopo. Nilipokuwa nachangia Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilitoa msisitizo kuhusu mikopo kwa wakulima. Mara nyingi tunaposema mikopo, tunakuwa hatuwapi wakulima elimu ipasavyo, kwa hiyo, naiomba Serikali katika kipindi hiki iweze kuwapa wakulima utaratibu kamili wa mikopo ili waweze kujiweka tayari kuhusiana na mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka kuwa fedha za JK tulipoziidhinisha hapa Bungeni na tukasema kuwa, kila mkoa utapata shilingi bilioni moja, wananchi walijitokeza kwa wingi na kwenda katika Halmashauri na benki mbalimbali kwa ajili ya mikopo, matokeo yake ni kwamba, mpaka sasa hivi kuna wajasiriamali hawajapata mkopo wa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mikoa mingine ambayo hata mtu mmoja hajawezeshwa mkopo wa aina yoyote; kwa hiyo na hili nalo katika kuangalia zaidi suala la Kilimo Kwanza ni vyema kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mikopo na wao wakajiweka tayari kuhusu suala la mikopo, kwa sababu tukiangalia suala la kilimo mara nyingi ni suala la msimu kwa vile katika nchi yetu hakuna kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo ni vyema Serikali ikawapatia wakulima elimu zaidi kuhusu taratibu nzima za mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa Mheshimiwa Waziri hahusiki kuhusiana na suala hili ambalo ninataka kulizungumza, naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo lakini wasaidizi wake wapo; kipengele cha mikopo kwa upande wa Zanzibar hakijawekwa kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini tuna miradi ambayo inajumuisha Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, kama Miradi ya MACEMP, TASAF na PADEP. Naiomba Serikali iweze kuielekeza kwa wingi kule Zanzibar ili wakulima wa Zanzibar nao waweze kufaidika kupitia miradi hii katika kuimarisha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa wewe ulitaka kesho kufanya nini mbona umejadili vizuri? Alikuwa ameomba achangie kesho nikamwambia hakuna uwezekano, lakini amejadili vizuri.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia jioni ya leo. Nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Kilimo, kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika Wizara hii na hususan hivi karibuni walipokuwa wanawafidia wakulima bei ya mazao waliyokuwa wanalima ambayo iliteteleka katika Soko la Dunia iliteteleka. Jambo lile nikupongeze sana kama Waziri, Wizara na Serikali, kuweka ruzuku pale ambapo bei ya mazao ya bidhaa mbalimbali kama pamba, korosho, inapotokea kuteteleka katika Soko la Dunia, kuwajali wakulima wetu ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natokea Mkoa wa Iringa, kwa hiyo, vile vile nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wanyalukolo wa Iringa, kwa kuwa Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa Mikoa michache nchini ambayo imejikita sana katika suala zima la kilimo. Wilaya zake zote saba katika Mkoa wa Iringa zinashughulika sana na masuala ya kilimo. Kwa hiyo, niwapongeze sana na hivi sasa tumekubaliana kwamba, Kilimo Kwanza, sisi watu wa Iringa tunasema Siasa ni Kilimo, ukitaka utengeneze siasa vizuri, basi hakikisha kilimo kimekaa vizuri. Si hivyo tu, ninatambua kwamba, hakuna nchi ambayo inaweza ikajutia pale ambapo inakuwa imewekeza katika kilimo, kwa sababu ukishawekeza katika kilimo, kwanza watu wa nchi hiyo wanakuwa wana afya, wanapata maisha bora. Pia ukishawekeza kwenye kilimo si rahisi malighafi za kilimo zikashindwa kuuzika hasa kwa kutambua kwamba, kutokana na utandawazi *(Globalization)*, kumekuwa na upungufu wa chakula Duniani, maeneo mengi sana yanahitaji chakula. Yako maeneo katika Afrika kwa mfano; Somalia, Ethiopia, wananchi wao wanakufa kutokana na Kwashakoo na matatizo mbalimbali. Tunapowekeza kwenye Kilimo Kwanza tunajitosheleza, lakini zaidi sana ni rahisi pia kupata Pato la Taifa. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo ni nyeti sana na ni uti wa mgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri kwa kazi nzuri, lakini nina maswali machache ambayo ningependa tushirikiane kuyatafakari kwa pamoja. Tunaposema Kilimo Kwanza na mambo mazuri ambayo tumekuwa tukiyajadili, pamoja na kuweka Sera imara katika nchi yetu, yako mambo mengine ambayo kimsingi ni muhimu sana yakaendelea kuzingatiwa. Mambo hayo ni kama haya yafuatayo:-

Kuna kitu kinaitwa Benki ya Mazao, wakulima wetu wengi wanafanya kazi kubwa sana na wakati mwingine wanapata mazao mengi sana. Benki ya Mazao, wengine wangependa kuiita Benki ya Kilimo, kitu hiki katika nchi yetu bado hakijakaa vizuri. Baadhi ya maeneo baada ya kuzalisha yale mazao waliyozalisha watu, kwa mfano, mahindi katika Mkoa wangu wa Iringa, tunaweza kwenda kwenye eneo tuka-benki yale mahindi. Pale ambapo wananchi wanahitaji kubadilisha mazao yale katika *cash*, basi ni jukumu la vyombo husika kusema ndugu huyu ameweka magunia 10, magunia 100, magunia 200 na magunia haya yana thamani ya kiasi fulani. Linakuwa jukumu la Serikali za Mitaa ama Serikali Kuu, kubadilisha mazao yale katika pesa. Maana yake ni lazima tuwahakikishie wananchi wetu kwamba, ukishawekeza katika kilimo ni hakika hujapoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na Benki ya Kilimo, Benki ya Mazao, ni jambo ambalo lazima tulizingatie sana. Maeneo mengi ya nchi yetu na wakulima wetu tunafahamu, utakuta *storage* ya yale mazao eneo lile bado halijakaa vizuri. Wengine wanaweka mazao katika maeneo tunaita kule kwetu vihenge, mvua ikija mazao yale yanalowana. Sasa vitu kama hivyo ni vizuri tukaanza kuvifufua kupitia Vyama vya Ushirika kama SACCOS na

kadhalika. Lazima iwe ni Sera kamili ya Wizara kwamba, Benki za Mazao zifanye kazi. Nikiamua kuwekeza kwenye mahindi, nisiseme kwa nini nisiende kufanya biashara, kwa sababu nina hakika kabisa nitakapopata mazao, kupata pesa ni kitu ambacho kinawezekana, mtu anakuwa hajiulizi mara mbili mbili. *Otherwise,* inakuwa ni rahisi sana mtu kuacha kujikita katika kilimo na kusema ngoja nikafanye biashara, ngoja nikaajiriwe. Wote wakienda kwenye biashara au wakienda kuajiriwa, kilimo kitabaki na nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la kuwa na Benki ya Kilimo, Benki ya Mazao; ni jambo la msingi sana. Jambo hili linataka lifanane na ile Stakabadhi ya Mazao, lakini Benki ya Mazao ni zaidi ya pale. Watalaam wanajua, ningeomba sana Sera ya kuwa na Benki ya Mazao na wakati wowote inapowezekana kubadilisha mazao yale katika pesa, liwe ni jambo ambalo halina kikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mazuri mengi ambayo yamefanyika katika kilimo katika nchi yetu, bado suala la bei ya mbolea ni jambo ambalo lazima tuliangalie sana. Juzi wakati nipo Iringa, nilikuwa na vikao na Waheshimiwa Madiwani wa Wilaya mbalimbali; Iringa Manispaa, Njombe, Mufindi, walikuwa wananiuliza maswali na mimi naomba nimuulize Waziri kama ifuatavyo; je, bei ya mbolea kwa mfano DAP inapofikia zaidi ya 100,000/= hivi mlengwa wa kununua mbolea hii ni mkulima, mfanyabiashara au ni wawekezaji wa aina gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbolea hiyo hiyo wakati wa msimu wa kilimo tunaita Masika, inakuwa shilingi laki moja na wakati wa msimu wa Kiangazi ambapo si msimu wa kilimo, inashuka kwa asilimia 50, ndipo hapo maswali yanakuwa mengi, kulikoni? Je, wakati wa msimu wa kilimo usafirishaji unakuwa ni ghali sana wakati wa Kiangazi unakuwa si ghali au hapa katikati kuna wahusika kama maajenti na *transporter* ambao wanasababisha bei hii kuwa tofauti? Baadhi ya maeneo nilikuwa ni shahidi, kwenye maduka ya *Tanzania Farmers Association* pale Iringa, hakika bei ilikuwa imepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vitu gani ambavyo vinasababisha bei hiyo hiyo wakati wa Kifuku inakuwa juu na mbolea hiyo hiyo wakati wa Kiangazi inakuwa imeshuka ghafla *(rapidly)*? Sasa hapo tungeomba sana jambo hili liangaliwe, bei iwe ya kukidhi wakulima wetu, kwa sababu kama gunia la mahindi kwa mfano ni shilingi 30,000 au 25,000, lakini gunia la mbolea ni zaidi ya shilingi laki moja; hivi kweli huyu Mtanzania ataweza kukidhi? Hii ina maana kwamba, atanunua mbolea kidogo; na akinunua kidogo atazalisha kidogo. Kwa hiyo, eneo hili ni lazima tuliangalie; tunafahamu na kutambua kwamba, wakati mwingine bei ya mbolea inakuwa *regulated* katika masuala ya Kimataifa zaidi, lakini tujaribu kutafakari tunawasaidiaje wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni masuala ya vitendea kazi kama majembe. Lazima tuwe na viwanda katika nchi yetu vya kuweza kukidhi mahitaji ya majembe. Vipo vitendea kazi vingine si vyema sana tukiagiza kutoka nje. Kwa mfano, tunapozungumza majembe, labda jembe la mkono, kweli huu ni wakati wa ku-*mechanize* kila kitu kiwe *automatic*, huyu mwananchi toka asubuhi anatumia jembe la mkono, baadae akapalilie, baadae akavune na kupukucha, hata mashine za kupukucha mahindi hatuzioni sana katika maduka yetu ya pembejeo. Kwa hiyo, hivi ni vitu muhimu sana vikawepo wakati wote ili viweze kutumika. Leo hii mwananchi kutumia nguvu ya mwili ni kazi sana na afya zenyewe ndio hivyo. Kwa hiyo, lazima tuangalie sana. Hivi unatarajia alime kiasi gani kwa kutumia afya ya mwili bila kutumia mota?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, yako maeneo katika nchi yetu ambayo yanafanya kazi sana, kwa mfano, maeneo ya Iringa na Mbeya yanazalisha sana. Mimi nilidhani yale maeneo ambayo yanazalisha sana, basi ndiyo yapewe mbolea zaidi maana mwenye nacho ataongezewa na ile ni *promotion*, hata kazini mtu ukifanya kazi sana na cheo kinapanda. Kwa hiyo, maeneo ambayo yanazalisha sana kilimo, pembejeo, ruzuku, mbolea, wapelekewe zaidi na ile itawavutia maeneo mengine ambayo yanazalisha kiasi basi yakavuta ile kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunapozungumzia suala zima la kilimo, tunao vijana wetu kwa mfano, wanakuwa wanauza mazao ya kilimo; kama Chalinze kuna matunda, ukienda Ilula kuna nyanya, kuna vitunguu na kadhalika. Hivi wale wanaouza vile vitu, watalaam wetu wa masuala ya kilimo wako wapi mbona hatuwasaidii? Tunahitaji *packing materials*, tunahitaji utunzaji. Pale Chalinze, watu wanapita, mazao yamewekwa chini, Ilula pale Mabwana Afya wako wapi tuwasaidie vijana wetu? Unakuta *apples* za *South Africa*, watu wanaweka kwenye friji, lakini matunda ya Tanzania ndio tumeweka chini. Basi tunaomba *Council* na Miradi ambayo iko kwenye Halmashauri, ASDP, DADPs, tubuni, maana wakati mwingine wananchi si rahisi kubuni kwamba, kuna jambo hili na pesa hizi zipo kwa ajili ya wananchi ili waweze kuwasaidia. Kwa hiyo, ningeomba sana Halmashauri ziwasaidie wale wanaozalisha viazi kule Njombe, tuone *packing materials* nazo huwa zinasaidia sana kuongeza hadhi ya mazao yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tuna chai na kahawa kiasi cha kutosha katika nchi yetu. Kwa hiyo, bidhaa hizi tunapokuwa tuna-*import*, basi *Import Tax* iongezeke ili kumlinda huyu mkulima wa ndani. Tuna chai ya kutosha, tuna mchele wa kutosha, sasa si sawa bei ya mazao yanayotoka nje inakuwa ni chini kuliko mazao ya Mtanzania. Mchele wa *Basmat* wakati mwingine unakuwa bei ya chini kuliko mchele wa Mbeya. Kwa hiyo, ningeomba sana *Import Tax* iwekwe vizuri kumlinda mkulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya Vocha yametusaidia sana kipindi kilichopita. Ningeomba ugawaji wa Vocha uzingatie sana ushirikishwaji wa wadau wote katika maeneo mbalimbali. Waheshimiwa Madiwani ni watu muhimu sana katika maendeleo ya nchi; Madiwani wa Kata, Madiwani wa Viti Maalum na kuielezea Sera za Nchi; ni kama Wabunge walivyo. Wabunge wanafanya kazi katika *National Level*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii leo kuwa mchangiaji wa mwisho, kuchangia Wizara yetu ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa vyema hotuba ya bajeti yao na Waziri leo ameiwasilisha kwa ufasaha mkubwa sana. Pia naomba niishukuru Serikali, kwa kuiongezea Wizara hii bajeti, kwani sote tunafahamu umuhimu wa Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niipongeze Serikali kwa kuja na kaulimbiu hii ya Kilimo Kwanza. Kama Waziri alivyosema katika ukurasa wa 77, Kilimo Kwanza kitatekelezwa kupitia Wizara zenye mahusiano *(Collaborators Ministries)* kama vile Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Miundombinu,

Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Viwanda ya Viwanda, Biashara na Masoko, pamoja na Watendaji na Viongozi wote wa ngazi zote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona nianze na hili kwa sababu haya mahusiano katika hizi Wizara, sijaona Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika hili na pembejeo ya kwanza kabisa ya kilimo ni maji, naomba Waziri waiunganishe hii Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya semina na mkutano wa Kilimo Kwanza pale Kunduchi, mimi nilishaanza mazungumzo ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Naibu Waziri Mheshimiwa Chiza, alikubali kutembelea katika maeneo yangu ya umwagiliaji yote ya Nambecha, Vibanio vya Umwagiliaji vya Msanjesi, Kitanda, Mchomoro, Mtonya, Liuni, Amani na Maoka, Msindo na Likuyu, kuna miradi mikubwa sana ya kilimo, ambayo inatolewa fedha pia na Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji. Pia barabara inatusaidia sana kufika katika maeneo ya kilimo cha umwagiliaji, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aiunganishe Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuishukuru Serikali katika utaratibu wake mpya wa mbolea za ruzuku kwa maana ya Vocha. Utaratibu huu umetusaidia sana ingawa ulikuwa na matatizo yake nitayaelezea, lakini mazao hasa mahindi yamepatikana ya kutosha. Ninachoomba, kwa sasa hivi watu wa Namtumbo, kituo cha kununulia mazao kile cha *Food Security* kifunguliwe mapema. Mazao wameshavuna na wananchi wanababaika watauza wapi na Serikali imezuia kuuza mazao yale nje ya nchi. Kwa hiyo, tunaomba sana; vinginevyo yatachukuliwa na walanguzi watayahifadhi halafu wao ndiyo wata-*maximize profit*. Tunaomba sana wakulima waweze kuuza na kurudisha gharama zao za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kueleza kwamba, waratibu wa mpango wa Vocha waelewe matatizo yalitojitokeza mwaka jana. Mfano; katika Mkoa wetu wa Ruvuma, mpango huu ulianza kwa *package* nzima, kwa maana ya mbolea ya kupandia, mbegu na mbolea ya kukuzia kwa gharama isiyopungua shilingi 162,000 kwa mbolea mifuko miwili ya *DAP* au mbolea ya Minjingu, *UREA* na mbegu. Tulianza kwa kuwalazimisha wakulima wanunue yote kwa pamoja, lakini tatizo lililojitokeza ni kwamba, wakulima walikuwa hawana uwezo wa kununua mbolea yote kwa pamoja, lakini pia mbegu ilichelewa kufika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliushauri Uongozi wa Wilaya ya Namtumbo kwamba, wanunue mbolea ile kwa wakati; kwa maana wanapopanda wanunue mbolea ya kupandia halafu wakati wanasubiri mahindi yakue watie mbolea ya kukuzia, ndiyo watafute hela nyingine, kwa sababu wananchi wetu bado ni maskini hawana hela ya kununulia Vocha ya mbolea ya kukuzia. Tulifanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, kuna watu wengine katika maeneo mengine, walikuwa hawana uwezo, kwa sababu tuliwakusudia watu wasio na uwezo wapatao kaya 22,000 kati ya wale wasio na uwezo, wapo ambao hawakuwa na uwezo kabisa wa kununua ile mbolea. Kilichokuwa kinafanyika pale, mawakala waliwarubuni Watendaji wa Vijiji wakaenda kuwachukua wale wenye Vocha, wengine walikuwa wananunua wanapewa shilingi elfu tano halafu yule wakala anaichukua ile Vocha anakwenda kui-*submit* katika benki ili arudishiwe fedha za ruzuku ya Serikali kama ameiuza ile mbolea. Hili ni tatizo kubwa ambalo lilijitokeza kule kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine walikuwa wanarubuniwa watoe shilingi elfu kumi na nne kwa mfuko mmoja, halafu anapewa mfuko mmoja, ile mifuko mitatu mingine yote anasainishwa na wakala anakwenda kuipeleka benki analipwa mfuko mmoja shilingi elfu ishirini na nne. Kwa hiyo, hela nyingi sana za Serikali zimepotea kwa mtindo ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kazi rahisi sana kulidhibiti hili; unaangalia ni tani ngapi alizopewa wakala na akazifikisha kule, unalinganisha na Vocha anazorudisha benki, tutagundua nani mwizi na nani amepeleka mbolea ile kwa mhusika. Kwa hiyo, naomba sana eneo hili waratibu waliangalie vizuri sana katika msimu huu unaokuja. Naomba pia kama walivyosema wenzangu, mbolea ifikishwe kwa wakati hasa wakati huu mwezi wa nane na wa tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile itolewe elimu ya kutosha kupitia vyombo vya habari, kwa mfano, redio ndiyo inafika kwa wakulima wetu wote vijijini. Umuhimu wa Vocha zile thamani yake, sisi kama Wabunge wa maeneo yale tulieleza, lakini hatukuweza kufika katika maeneo yote. Tunaomba sana redio zitumike kuwaelimisha wakulima kwamba, Vocha ile thamani yake ni kiasi gani na imelipiwa na Serikali si ya kuiuza. Ukiuza Vocha mbili za elfu arobaini na nane ukauza kwa shilingi elfu tano ni hasara kubwa sana, kwake yeye mkulima na kwa Serikali, kwa hiyo, naomba sana Serikali pia itumie vyombo vya habari kuelimisha wakulima thamani ya vocha na nini maana yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Serikali ilitutambulisha mbolea inayoitwa Mijingu Phosphate na mbolea hii ilitumika katika Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Rukwa, Mbeya na kadhalika. Naibu Waziri wakati anajibu swali lake jana alisema, naomba nimnukuu: "Utafiti wa Mbolea ya Mijingu ulifanyika katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini. Utafiti ulibaini kuwa, Mbolea ya Mijingu inafaa katika maeneo yenye udogo ambao una kiwango cha tindikali cha chini, PH 5.5 na pia kiwango kidogo cha madini aina ya Phosphorus na Chokaa hususan Calcium. Mkulima akitumia mbolea ya Mijingu katika maeneo hayo, anaweza kupata matokeo ya haraka na mazuri. Utafiti ulifanyika pia katika maeneo ya Wilaya ya Mbinga, Njombe, Mbozi na Nkasi, matokeo yalionekana ni mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea hii imeonesha inafaa na hata Waziri Mkuu alipopita katika ziara zake, aliambiwa na watalaam na wananchi aliwauliza kuhusiana na matokeo ya mbolea hii walisema inafaa. Katika eneo hili, naiomba sana Serikali kwa sababu iliipigia sana debe mbolea hii kwa maana tatu; moja baada ya tafiti iliyofanyika kuonekana inafaa; pili ni kwa kuwa inazalishwa hapa nchini na bei yake itakuwa nafuu; tatu, tutampunguzia mkulima gharama kwa sababu bei yake ni nafuu na ambayo ni kubwa sana kwa mkulima. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iliangalie sana eneo la mbolea hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzangu wamesema sana kwamba, tusiiache mbolea hii peke yake ikaenda ikashindana na DAP. Tutoe *allocation* kabisa ya mbolea ya ruzuku na tuseme tani fulani ndizo zitalipiwa ruzuku mbolea ya Mijingu Phosphate. Tukifanya hivyo pia tuta-*encourage* kile kiwanda kiweze kuendelea, tunataka kile kiwanda kiendelee ili baadaye tutakapokuja kuzalisha mbolea ile ya *DAP* na *CAN* kwenye kiwanda ambacho tunategemea *raw material* yake ambayo yatatokana na makapi ya gesi itakayokuwa Lindi, basi iwepo wakati kiwanda kifanye kazi. Naomba sana Waziri aliangalie eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuongelea Zao la Tumbaku. Naomba ni-*declare interest* kwamba, mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku Tanzania, kwa mujibu wa kanuni ya 61.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali na wadau wa tumbaku, kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, kwa kukubali na kusikiliza ushauri wa Bodi ya Tumbaku, mpaka leo hii Tumbaku imepanda chati. Leo hii wakulima wote waliokuwa wameacha kulima tumbaku, sasa wanakimbilia kulima tumbaku. Tumbaku imepanda bei, kwa ushirikiano wake tumetatua na tumeshirikiana kutatua kero karibu zote zilizokuwa zinalikabili Zao la Tumbaku na sasa tunategemea lile lengo la kufikia tani laki moja tutalifikia, lakini siyo mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na matatizo mengi, mapato pia katika ile Bodi ya Usimamizi yalikuwa madogo, tulikuwa tunapata karibu *19 percent* ya usimamizi wa uendelezaji zao, lakini mwaka huo Serikali imetupa mara tatu zaidi. Kwa hiyo, tunaamini kabisa usimamizi wetu utakuwa ni mzuri na tutaendeleza zao hili. Ninachopenda pia kuwakumbusha wakulima wa tumbaku wanaonisikiliza ni kwamba, mwaka huu wamepata fedha nyingi sana, fedha hizo waziingize katika kununua *power tillers* ili kupunguza muda wa kulima na kuongeza uwezo wa kusafirisha pembejeo na kuchukulia pembejeo na kuongeza uzalishaji. Lazima pia tufuate kanuni bora za uzalishaji bora wa zao la tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nipokee shukrani nyingi sana walizotoa wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na tunakupongeza pia kwa kushirikiana na wenzio kunyanyua zao la tumbaku.

Waheshimiwa Wabunge, pale niliposema kwamba, mnapojiorodhesha kuongea sisi tuna-*categorize* aliyeongea, ambaye hajaongea, aliyeongea mara moja na kadhalika. Unaposema naomba niongee kesho ile orodha ya wachangiaji inabandikwa pale, sasa unakuta Mbunge anayeona jina lake lipo mbali haji humu ndani. Sasa wewe unasema unataka kuongea kesho, matokeo yake inakuwa hata wale wa kuongea hawapo, ndiyo maana nasema kama unabadili basi mwambie mwingine mbadilishane inakuwa rahisi kwetu. Naomba sana hili lizingatiwe kwa sababu linatuchanganya sana na matokeo yake hatufuati orodha, inabidi tufuate kwa kuangalia aliyemo humu ndani. Kwa hiyo, akishakuwemo humu ndani basi matokeo yake wale waliotangulia watakosa nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, kesho asubuhi tutaanza na Mheshimiwa Charles Keenja, ingawa katika orodha hakuwa wa kwanza, kwa sababu hapa niliomba awe tayari kama watakuwa hakuna wa kuchangia na watu wengi walisema watachangia kesho; yeye atapata *previledge* ya kuanza kesho. Atafuatiwa na Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o, Mheshimiwa Dokta Mzindakaya, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Janguo na nitajitahidi kesho tuwatambulishe wageni kwa muda mfupi ili wengi waweze kufikiwa katika kujadili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kesho saa saba mchana, Kamati ya Uongozi ya Bunge itakuwa na kikao. Wenyeviti wa Kamati mbalimbali tutakuwa na kikao saa saba mchana, kwa hiyo, msisahau, tutakumbusha pia kesho asubuhi.

Mheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana kwa kazi tulizofanya kwa siku ya leo nzima, michango yenu ilikuwa mizuri na penda mkapumzike ili mjiandae kwa ajili ya kesho.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.42 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 22 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*